

16 MEI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 16 Mei, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Nduga) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge Kikao cha Ishirini na Saba kinaanza. Mkutano wetu wa Kumi na Moja.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:-

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA UCHUKUZI):

Taaqrifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Uchukuzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama kawaida yetu siku ya Alhamisi tunakuwa na Kipindi cha Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na swali la kwanza la siku ya leo linaulizwa na Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kunipa chakula cha msaada kule kwenye jimbo langu. Swali linalokuja ni hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Maafa ni Kitengo ambacho kiko chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi nzima kinajua jinsi unavyosaidia wananchi.

Je, ni kwa nini inapotokea matatizo kwa mfano maafa inachukua muda mrefu sana kufika sehemu inayohusika?

16 MEI, 2013

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Ngonyani kwa maelezo yake ya awali. Kwa nini Kitengo hiki yanapotokea maafa hakifiki kwenye tukio kwa muda ambao wananchi wanategemea.

Kwa utaratibu ulivyo kila Wilaya imetengenezewa utaratibu wa kuwa na Kamati ya Maafa na hivyo hivyo katika ngazi ya Mkoa. Kwa hiyo yanapotokea maafa matarajio ya Serikali ni kwamba Kamati ya Maafa ya Wilaya ambayo Mkuu wa Wilaya ndiyo Mwenyekiti wake ndiye anaye-*take charge* kwanza au ndiyo anayeshughulikia hilo tatizo kwa mara ya kwanza.

Mara nyingi sisi Ofisi ya Waziri Mkuu tunategemea taarifa kutoka kwenye hiyo Kamati ambayo mara nyingi imekuwa imethibitishwa na Kamati ya Mkoa kabla hatujachukua hatua nyingine yoyote ya ziada. Ndiyo maana unaona hatuna ule utaratibu wa namna hiyo kwa kuwa tunajua vyombo kwa mfumo ulivyo vipo.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana kwa majibu yako mazuri, ila tu nataka kuuliza swali moja la nyongeza.

Kumekuwa na tatizo katika jimbo langu hasa kwenye Kata ya Magamba kwa Lukonge, Kata ya Mombo katika kijiji cha Mwisho wa Shamba na Kata ya Magoma katika kijiji cha Makangara karibuni miezi 5 nyumba zao zimebebwa na upepo na nyumba zingine zimeungua moto na mashule ya kule Kwilasa yamebebwa na upepo na mpaka sasa hivi wananchi hawajapata msaada wa aina yoyote.

Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki wananchi wa Korogwe Vijijini?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema maafa yoyote yanapotokea Ofisi ya Waziri Mkuu inategemea taarifa ya Wilaya na Mkoa itawasilisha maombi ya namna gani. Ni vizuri vilevile kujua kwamba yanapotokea hivyo si kwamba kila kitu kitahudumiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Yako mambo mengine ambayo tunayategemea jamii yenyewe ambayo inaishi na wale waliopata maafa na yenyewe itasaidia katika kujaribu kuchukua hatua fulani fulani za awali.

Kwa hivyo mimi nafikiri kwa upande wa tatizo lako pengine nikusihii tu kwamba hebu pata taarifa za kutosha kutoka kwenye Wilaya yako. Cheki na mkoa halafu tuone taarifa gani iliwasilishwa kwetu na sisi tulichukua uamuzi gani. Wakati huo na mimi nitamwomba Mheshimiwa Lukuvi aangalie kwenye kumbukumbu zetu pale Ofisini ni mambo gani ambayo yaliletwa kwetu na sisi tulichukua hatua ya namna gani kutokana na hali unayoieleza. *(Makofi)*

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi hii kumwuliza Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, najua Serikali ipo kwenye mchakato wa kuanzisha ama kuleta Muswada ndani ya Bunge juu ya uanzishwaji wa Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi yetu. Je, ni lini Muswada huo utaletwa ndani ya Bunge hili?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nitoe maelezo kwa ufupi tu kwamba ni kweli tulishatoa kauli hiyo na tayari sisi tumeshaanza kulifanyia kazi katika hatua zile za awali kwa maana ya kupitia sheria iliyopo lakini vilevile kupata maoni mbalimbali ya awali kabla hatujatengeneza mfumo wenyewe wa sheria hiyo iweje na mambo gani yazingatiwe ili baadaye tutakapouleta hapa Bungeni tuweze kupata tu nyongeza za mawazo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Sasa lini pengine si rahisi sana kujibu hiyo sehemu ya swali kwamba ni lini, lakini tutakapokuwa tayari tutaleta. *(Makofi)*

16 MEI, 2013

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa Serikali ipo kwenye mchakato huu wa sasa wa kuanzisha hiyo sheria. Ninaamini kwamba taasisi za Serikali pamoja na Mashirika ya Serikali yatahamia Dodoma mara sheria hii itakapoanzishwa. Zipo taarifa sahihi kwamba Mfuko wa *LAPF* ambao upo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu hivi sasa wanajiandaa kuhamia kutoka Dodoma kuelekea Dar es Salaam.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu upo tayari kuwazulia wasiondoke Dodoma ili kuonyesha kweli Serikali ina nia ya dhati kuhamia Dodoma?

NAIBU SPIKA: Kwa niaba ya Wabunge wote wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba majibu ya swali hilo. *(Makofi/Kicheko)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhamia Dodoma ni jambo la msingi na ndiyo maana unaona muda wote tunasema lazima jitihada hizo zifanyike na katika hatua hizi tunazokwenda nazo zote ni jitihada za kujaribu kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya Ofisi, watu, Makampuni kuhamia Dodoma, sababu changamoto zake zilikuwa ni nyingi, maji hayatoshi, lakini sasa angalau maji yameweza kupatikana kidogo. Kwa hiyo, kunahitajika vivutio vingi zaidi ili kuweza kufanya mahali hapa paweze kuvutia watu wengi zaidi. Sheria hiyo ndiyo itabainisha mambo mengi zaidi ya kiutaratibu na sheria ili kuweza kuvuta Makampuni mengi.

Sasa umetoa rai juu ya chombo chetu kimoja ambacho na wewe kwa taarifa unasema unasikia hivyo lakini si kusikia tu ni jambo ambalo na sisi tullipata lakini linatokana na mazingira fulani ambayo yanafanya chombo hiki kwa hapa Dodoma kwa sababu shughuli zake nyingi za kibiashara zinahusiana zaidi na Jiji la Dar es Salaam ndiyo maana wakaomba kibali waweze kushiriki katika mazingira yale ya kibiashara lakini si kwamba wamehama na hawatarudi tena Dodoma hapana. Ndio sababu kubwa iliyotufanya tukajaribu kuliona kama ni jambo jema katika mazingira, tuliyonayo sasa. *(Makofi)*

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Bunge hili ni chombo cha wananchi, ndani ya Bunge hili kumetokea kauli za kushtusha kwa sisi Wabunge lakini kwa wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mbunge wa Mwibara alitoa kauli akisema kwamba wako baadhi ya Mawaziri wetu walijishughulisha na biashara haramu za madawa ya kulevya. Tunajua kwamba tunalindwa na ibara 100 ya Katiba lakini pamoja na ibara hiyo kauli hii ni nzito na inaipaka matope Serikali yetu.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu unawaambia nini Wabunge na wananchi kwa ujumla?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja wa watu ambao nichukulie Wabunge tuliopo hapa ni watu wazima na kwamba kauli wanazozitoa zimepimwa vizuri kabla hujasema jambo lolote. Sasa ninachoweza kusema tu ni kwamba Mawaziri hawa kabla hawajachaguliwa mchakato wake ni mrefu kidogo, Rais lazima ajiridhishe kwa mambo mengi.

Sasa kama mwenzetu Mbunge wa Mwibara aliyasema hayo kazi yangu mimi ni kusema kwamba si kweli. Sasa sijui maana jambo hili wakati lilipotokea pengine lilikuwa wakati muafaka wa kulisema, lakini kwa sababu umeliuliza na mimi nataka nikubaliane kabisa na wewe kwamba pengine tumwombe tu Mheshimiwa Lugola sasa atuletee maelezo, ushahidi wa Waziri yeyote ambaye anajishughulisha na madawa ya kulevya, sisi tutapeleka maelezo hayo kwa Rais hatua stahiki zitachukuliwa.

Lakini nirejee kusema tu mimi naheshimu sana kauli za Wabunge, lakini ni vizuri zikapimwa vizuri na uone unataka kusema nini na kwa nini. Kwa hiyo mimi nadhani kwa hili ndiyo sana sana tunachoweza kufanya.

16 MEI, 2013

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu kutokana na kauli yako inathibitisha kwamba Spika au Naibu Spika atoe kauli ya kumtaka Mbunge huyu athibitishwe kwa mujibu wa kanuni zetu. Je, unasema nini kuhusu suala hilo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Rashid mimi utakuwa umenisaidia sana maana sina hakika kauli yangu kiutaratibu kama itakubalika. Lakini ilitokana na swali lako mwenyewe ndiyo maana nikasema jambo ninaloweza kimsihi mwenzetu Mheshimiwa Lugola ni hilo tu kutokana na hili swali. Lakini Naibu Spika akilitoa sasa Kibunge hiyo ni bora zaidi maana najua mwenzangu tena hatanipiga chenga.

Kwa hiyo, mimi nafikiri nakubaliana na wewe kabisa na Mheshimiwa Naibu Spika, kama unaona inafaa basi utoe kauli ili tuone mwishowe itakuwaje. (*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kutokana na matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne mwaka 2012 Serikali kwa kupitia kauli yake hapa Bungeni wiki iliyopita imeamua kufuta matokeo yale kwa maelezo kwamba mojawapo ya sababu ya matokeo yale mabaya yalisababishwa na Serikali kufanya mabadiliko ya upangaji wa alama yaani madaraja ya ufaulu bila kuwaandaa wanafunzi wale.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili sio jambo dogo ni jambo kubwa sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, elimu ni kitovu cha maendeleo ya Taifa lolote na taasisi au Kiongozi yoyote au Mtendaji yoyote hawezi kuja na mfumo mpya au utaratibu mpya akauingiza kwenye *system* ya elimu bila ya kushirikisha wadau wakiwepo Maafisa elimu, Walimu wafundishaji kuwaandaa wanafunzi na wadau wengine.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ni Kiongozi mkubwa wa Serikali hapa Bungeni unaliambiaje Bunge hili na Taifa hili nini kuhusiana na udhaifu huu wa Serikali ulioonyeshwa kwenye sekta hii muhimu ya elimu hapa nchini? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kama linataka jibu au alikuwa anatoa rai kwa Serikali kwa ujumla tu. Ninachoweza kusema ni kwamba hilo analisema Mheshimiwa Sakaya ni moja kati ya mambo mengi ambayo tulitaka Tume iyatazame.

Sasa kwa sababu Tume ile bado inakamilisha hili zoezi pengine nikusihhi tu Mheshimiwa Sakaya kwamba hebu ngoja tukamilishe lile zoezi ili tuje na maelezo fasaha juu ya nini kilichotokea, athari zake zimekuwa nini na baada ya yale mawazo tuliyokuwa nayo nini sasa tunafikiri itakuwa hali halisi ya matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne maana kwa sasa nikijaribu kulieleza bado mchakato ule haujakamilika vizuri. Tafadhali sana.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, matokeo haya yalitikisa Taifa na yameleta madhara makubwa kwa Taifa na kwa jamii.

Mheshimiwa Waziri Mkuu wapo watoto waliopoteza maisha kutokana na matokeo haya, wapo watoto wamekimbia familia zao kutokana na matokeo haya, wazazi wamefedheheka na wengine wamepata *Blood Pressure* kwa ajili ya matokeo haya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu Serikali sasa haioni umuhimu wa kuwawajibisha Watendaji wote waliohusika na masuala haya ukianza na Waziri mhusika kwenye Wizara hii ambaye ameonyesha udhaifu mkubwa kuongoza Wizara hii muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu? (*Makofi*)

16 MEI, 2013

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kulieleza hili Mheshimiwa Sakaya maana yake unataka niendeleo kuonekana kama napiga chenga swali lako na mimi si nia yangu.

Ninachosema tu kwamba unayoyasema ni mambo ambayo tunaamini kabisa baada ya kukamilisha lile zoezi tutapata maelezo ya kina yanayotokana na uchunguzi kuweza kujibu maeneo karibu yote ambayo tulikuwa tunayahisi, mengine tulikuwa na uhakika nayo.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi ukiniuliza nasema pengine tusingi kidogo muda si mrefu tutakuwa tumeshakamilisha ile kazi halafu tutaona namna ya kuitoa mbele ya umma ili waweze kuona kilichotokea ni nini na kama wako watu waliosababisha jambo hili wala halitakuwa tatizo hata kidogo kuchukua hatua za kuwawajibisha kwa sababu ni dhahiri kabisa kwamba jambo lile sio dogo na lilitikisa karibu nchi nzima. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge tunakushukuru sana kwa majibu ya kipindi hiki.

Waheshimiwa Wabunge leo tulikuwa na Wabunge wanne tu waliokuwa wamejiorodhesha kwenye kuuliza maswali kwa Kipindi cha Mheshimiwa Waziri Mkuu. Baada ya shukrani hizo Katibu tuendeleo.

MASWALI YA KAWAIDA

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali ya kawaida na swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mbunge wa Mbarali.

16 MEI, 2013

Na. 219

Mradi wa Maji Katika Wilaya ya Mbarali

MHE. MODESTUS D. KILUFI aliuliza:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka kuondoa tatizo la maji kwa matumizi ya watu wa Mbarali?

(b) Je, Serikali ipo tayari kufanya Mradi wa Maji wa kutegwa kutoka Mto Mpeng'o uliopo Wanging'ombe uwe wa kitaifa ili uweze kusaidia vijiji vya Wilaya mbili (2) Mbarali na Njombe badala ya kutegemea mradi wa *World Bank* ambao umekwama?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabili na matatizo ya maji yaliyopo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 iliidhinishiwa shilingi milioni 684.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji vya Ubaruku na Chimala.

Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2013/2014, Halmashauri hii imeidhinishiwa shilingi bilioni 1.4. kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji na shilingi milioni 72.9 kwa ajili ya uhamasishaji wa shughuli za usafi wa mazingira. Ujenzi wa miundombinu hiyo ya maji utafanyika katika vijiji vinne ambavyo ni Udindilwa, Igurusi, Mkunywa na Simike. Hivyo ni wazi kwamba Serikali imedhamiria kuwaondolea wananchi wa Mbarali adha ya maji inayowakabili ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa matumizi ya kila siku.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pendekezo la kutoa maji katika chanzo cha Mto Mpeng'o ambacho kinaweza kuhudumia Wilaya mbili za Mbarali na Njombe, Serikali tayari imekamilisha usanifu wa mradi huu ambapo makisio ya gharama za kutekeleza mradi huu ni bilioni shilingi 17. Aidha kutokana na gharama kubwa zinazohitajika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali iliomba maombi maalum katika Wizara ya Maji ili kupata fedha hizo zitakazowezesha mradi huo kutekelezwa kwa manufaa ya Wilaya zote mbili. Wizara ya Maji imepanga kutumia sehemu ya fedha zilizoongezwa katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 ya shilingi bilioni 184 ili kuanza utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuona mradi huu unatekelezwa ili kukabiliana na matatizo ya maji yanayowakabili wananchi wa Wilaya ya Mbarali na maeneo jirani.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mbarali naomba kuishukuru sana Serikali kwa jitihada ambazo inafanya kuwawezesha wananchi wa Mbarali kupata maji safi na salama. Napenda kujua utekelezaji wa mradi huu mkubwa ambao ungewakomboa sana Wanambarali na Wilaya jirani ya Njombe utaanza lini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Kilufi kwa sababu swali kama hili lilijibiwa hapa Bungeni tarehe 22 Juni, 2012 na katika Bunge hili tumelijibu kwenye swali la nyongeza. Hii inaonyesha umuhimu wa mradi huu kwa wananchi na kwamba mradi huu umeiva kwa sababu usanifu wake umeshafanyika ndiyo maana umeingizwa kwenye miradi itakayotekelezwa katika zile fedha ambazo tumeziomba na Bunge limeidinisha bilioni 184.5/-.

Kwa hiyo, huu mradi ni mmojawapo ukiwemo huo wa Njombe, Mbarali ukiwemo wa Lugenge kwa Mheshimiwa Spika, ikiwemo ya Ludewa na mingine itaanza utekelezaji wake mara bajeti hii mwezi wa saba tukiitoka hapa.

MHE. MOZA ABEID SAIDY: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa Mamlaka ya Mji ya Mji wa Kondoa iliunda Bodi ya Maji ili iweze kufanya kazi na majina tayari yalishafika kwa Mheshimiwa Waziri.

Je, ni lini utateua majina hayo ili Bodi hiyo iweze kufanya kazi ipasavyo kuliko kupoteza hela mpaka sasa hivi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, jibu hili ni kwa ajili na wale wengine wote ambao wameleta majina kwa ajili ya mamlaka. Kwa kawaida majina yakishaletwa kwetu hapa sisi hatuna tatizo mapendekezo hayo tunayapeleka kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwa hiyo nimhakikishie kwamba kama wameleta mapendekezo kwa ajili ya watu ambao wanaingia katika bodi sisi tunakwenda kuangalia na nitahakikisha kwamba nitapeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ili afanye *endorsement* kwa sababu yeye ndiye mamlaka husika.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Kwa kuwa Serikali ya CCM imetekeleza mradi mkubwa sana wa maji Singida Mjini yaani maji kutoka Mwankoko kuja mjini; na kwa kuwa pale mjini mabomba yaliyoko ni machache.

Je, Serikali itakuwa tayari kusaidia fedha za kwenda kusambaza maji Singida Mjini na vijiji vinavyopitiwa na bomba hili ili wananchi wengi wapate maji kwa urahisi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo Serikali itakuwa tayari kuona kwamba wananchi wanaopitiwa na hilo bomba wanapata maji kutoka kwenye hilo bomba.

16 MEI, 2013

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Tatizo la maji ni la nchi nzima na ndiyo sababu Bunge lako Tukufu liliona umuhimu wa kuitaka Serikali iongeze pesa kwa ajili ya kutatua tatizo la maji katika nchi yetu.

Lakini kuongeza zile bilioni 184/- kwenye Bajeti ya Wizara ya Maji ni jambo moja, lakini upatikanaji wa fedha hizo kwa ajili ya kwenda utekelezaji wa miradi ni jambo jingine.

Je, Serikali inatuhakikishia kwamba pesa zilizoongezwa bilioni 184/- kufikia karibu Bajeti ya bilioni 500/- zitapatikana zote ili ziende kwenye kazi ya utatuzi wa tatizo la maji katika nchi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani sisi wote hapa ndani tulisikia mazungumzo yaliyotembea hapa kuhusu suala la maji katika Wizara ya Maji. Hapa tuka-*postpone* kikao cha Bunge ili kujua kwamba tunafanyaje katika jambo hili.

Wakati unaangalia zile *labs, lab* mojawapo ambayo tumeunda ni lab ya maji imewekwa. Kwa hiyo nimwambie Mheshimiwa Zamboni mimi siwezi kukaa hapa nikai-*doubt* Serikali kwamba haitafanya hivyo. Juzi Serikali imenituma nimekwenda Dar es Salaam, tumekutana na wadau wa maji wote tumezungumza pale, aliyefungua mkutano ule alikuwa Waziri wa Maji mimi nikafunga mkutano ule. Tukasema pale waziwazi hizi hela tunazihitaji kwa ajili ya kufanya kazi iliyozungumzwa hapa.

Bajeti ni mpango wa Serikali inaokuonyesha hela zitakavyopatikana na hela zitakavyotumika. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, kwenye suala la maji wala hatutaki kufanya utani na kama wapo watu kwenye Halmashauri wanafikiri tutafanya utani hapa, hapahapa ndipo tutabanania hapahapa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha majibu ya nyongeza.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa niaba ya Serikali nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge nyongeza ya Bajeti ya bilioni 184.5/- niliyoitamka hapa Bungeni kwa niaba ya Serikali kama nilivyotamka itatekelezwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kutuhakikishia hilo. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi swali linaulizwa na Mheshimiwa Sara Msafiri Ally Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 220

Hitaji la Kituo cha Polisi Kata ya Mlali – Mvomero

MHE. SARAH M. ALLY aliuliza:-

Kata ya Mlali katika Wilaya ya Mvomero - Morogoro kumekuwepo na ongezeko la matukio ya uhalifu ukiwemo wizi wa mifugo na kuvunjwa kwa nyumba na kuibiwa vitu kwenye maduka.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi ili kulinda maisha ya watu na mali zao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sarah Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kujenga vituo vya Polisi na nyumba za askari wasiopungua tisa kwa kila Kata/Shehia nchi nzima ikiwemo Kata aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Mpango huu unatekelezwa kwa

kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wananchi na TAMISEMI. Kwa sasa siwezi kusema ni lini hasa kituo cha Kata ya Mlali kitajengwa. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hali ya usalama wa raia na mali zao katika Kata ya Mlali sio mbaya ikilinganishwa na Kata nyingine za Wilaya ya Mvomero katika Mkoa wa Morogoro. Hii inatokana na juhudi zinazofanywa na Polisi kwa kutumia dhana ya Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi na jitihada za Mheshimiwa Mbunge Makala. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tusaaidiane kuwahamasisha wananchi na wadau wengine katika utekelezaji wa Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi ili nchi yetu iwe salama zaidi. (*Makofi*)

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa sababu wananchi wa Kata ya Mlali wanatumia kituo cha Polisi cha Mzumbe ili kupata huduma za kipolisi.

Lakini kile kituo kimejengwa ndani ya Chuo Kikuu cha Mzumbe na kuna mgogoro wa kihistoria pale ambapo wananchi wanalaumu wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe kwamba wanatoka nje ya chuo chao na wanawabaka watoto wa kike na wanawapa mimba jambo ambalo limechangia watoto wa mtaani wengi sana. Lakini wanachuo nao wanawalaumu wananchi kwamba ni wezi wanakwenda kwenye maeneo yao na huko nyuma ilishatokea mgogoro mkubwa tu kati ya wananchi na wanachuo.

Je, kwanini sasa Serikali isikitoe kile kituo cha Polisi Mzumbe kiwe nje ya eneo la chuo ili kuimarisha utawala bora kati ya wananchi na wanachuo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, Kituo cha Polisi Mzumbe kinatumia pikipiki moja tu kama usafiri kwa hiyo inahudumia Kata mbili ya Mzumbe na Mlali kwa kutumia pikipiki. Kwa hiyo inapelekea panapotokea matukio ya kihalifu polisi wanashindwa kuji-*mobilize* vizuri na kufika eneo la tukio kwa wakati.

Je, kwanini Serikali isitoe sasa usafiri wa gari ili kwenye migogoro ile ya makundi kama ya wakulima na wafugaji ambao wanahitaji polisi wengi zaidi wafike kwa wingi na kwa wakati?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kutolewana na kulaumini kati ya wananchi na wanafunzi tunalielewa na wazo na wazo la Mheshimiwa Mbunge la kufikiria kukitoa kituo hiki nje tunaweza tukalifikiria.

Hata hivyo nitoe taarifa kwa Mbunge kwamba Mbunge wa Jimbo la Mvomero ameshafuatilia suala la namna hii na tumeshamruhusu anaweza akajenga vituo vingine vitatu na katika hivi vituo vitatu kimoja ni katika kata ya Mlali eneo la Ludingu. Kwa hiyo, nafikiri hili tatizo halitakuwa kuwa kubwa na pengine matatizo haya yatakaa sawa, kikubwa Mheshimiwa Sara washirikiane na wenzake ili kuanza ujenzi huu ili na sisi tushiriki vile ambavyo tunaweza kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kuhusu pikipiki. Kweli tuna tatizo la usafiri na kama tulivyosema kwenye bajeti yetu ni jambo ambalo tunalielewa na kubwa na lina kwaza utekelezaji wa kuhakikisha kwamba ulinzi unakuwa kamilifu kila eneo. Jitihada nyingi zipo na namwahidi Mheshimiwa kwamba yeye pamoja na wenzake ambao wenye tatizo hili tumo mbioni kulitatu na *inshallah* itakaa sawa.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa wananchi wengi wameshapoteza imani na Jeshi la Polisi kwa matukio yanavyotokea mara kwa mara na Polisi wanakuwa hawafiki kwa wakati mwafaka na kujihusisha kwenye vitendo vya rushwa.

Je, Serikali ina mikakati gani kuimarisha Jeshi la Polisi ili kurudisha maadili ya Polisi na wananchi kuwa na imani na Jeshi hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda nimthibitishie kwamba kweli kuna matatizo ya kukiuka kwa maadili kwa baadhi ya askari lakini Jeshi kama Jeshi na ukubwa wake bado liko imara na wapo wengi ambao wanatimizi maadili. Kuhusu suala la rushwa ni kwamba Jeshi la Polisi lenyewe lina kitengo cha maadili, limeanzisha na jitihada zinafanywa katika kuwatambua na kuwaadhibu wale ambao wanakiuka taratibu hizi. Pia kuna mradi maalum ambao unafadhiliwa na *DFID* katika kusimamia suala la rushwa peke yake na kazi hii inaendelea nafikiri tusivunjike moyo na wananchi niwasihii kwamba wao ndio ambao wanaweza kusaidia Jeshi likawa zuri zaidi na la maadili. Tushirikiane kwa sababu Polisi anapokiuka maadili mara nyingi hasa kwa rushwa na mambo mengine anashirikiana na wananchi. Nafikiri ni vyema wananchi wakashirikiana na sisi ili tuhakikishe kwamba maadili yanakuwa mazuri na wasishiriki katika kuvunja Sheria ambazo zilizopo na Polisi wanatakiwa wazisimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Wabunge wote kwamba sisi tunahakikishia kwamba Jeshi linabaki na taswira nzuri na linafanya kazi kwa ajili ya Watanzania.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na upungufu mkubwa uliopo katika Mkoa wetu wa Iringa wa vituo vya Polisi.

Kuna vituo vya Polisi Ifunda, Idodi, Isimani vinajengwa kwa nguvu ya wananchi. Je, Serikali ipo tayari kusaidia vituo hivyo ili viweze kwisha haraka ili kusaidia wananchi wasiweze kupata adha wanayoipata mpaka sasa hivi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi mtu unapoombwa kwanza ujue unachoombwa ni nini kabla hujatoa kauli ya kukubali; na kwa sababu vituo ambavyo amevisema Mheshimiwa sijui mahitaji yake labda niseme tu tutavitembelea ili tushauriane na hapo ndipo tutatoa kauli ya maana.

16 MEI, 2013

Na. 221

Mbinu za Kukabiliana na Wavuvi haramu

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA (K.n.y. MHE. SELEMAN S. BUNGARA) aliuliza:-

Wavuvi haramu wanaotumia mabomu hutumia zana kubwa za kujihami, kiasi kwamba vikosi vya usalama katika ukanda wa Pwani ya Kilwa ambako uvuvi mkubwa wa aina hiyo hufanyika havina zana za kisasa za kukabiliana na wavuvi hao:-

(a) Je, Serikali inatenga kiasi gani za kununua Boti ziendazo kasi zenye uwezo wa kukabiliana na wavuvi haramu?

(b) Je, ni maeneo gani yamechaguliwa kwa kuanzia kupatiwa Boti hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutumia Bajeti yake *program* ya miradi mbalimbali ilitenga fedha na kununua boti za doria za mwendo kasi ishirini na sita (26) na Vifaa mbalimbali vya doria.

Aidha, Shirika la *WWFlina* boti moja na kupitia program ya Rufiji, Mafia na Kilwa (*RUMAKI*) imetoa boti 4 kwa *BMUs* katika Halmashauri za Mafia, Kilwa na Rufiji ili kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kupitia jamii za wavuvi. Kwa ujumla eneo la kusini mwa Tanzania katika bahari ya Hindi lina boti ziendazo kasi 30 ambazo zinafanya kazi za doria.

16 MEI, 2013

Pia, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, vyombo vya ulinzi na usalama (dola), *BMUs* na wadau wengine inaendelea kutoa fedha za uendeshaji ili kudhibiti uvuvi haramu ukiwemo wa mabomu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyochaguliwa na kupatiwa boto hizo ni Wilaya ya Kilwa(2) Lindi (1), Mafia (4) na Rufiji (2).

Ili kukabiliana na uvuvi haramu Wizara inazishauri Halmashauri na Majiji, Manispaa, Wilaya na Miji nchini, kutumia kiasi cha fedha wanazokusanya kutokana na shughuli mbalimbali za uvuvi ili kuwezesha kazi ya kudhibiti na kusimamia rasilimali za uvuvi ifanyike kwa ufanisi katika maeneo yao.

Pia, Halmashauri zitenge fedha kwa ajili kununua boti za mwendo kasi na vifaa vya doria na kutoa fedha kwa ajili ya doria. Vilevile zisimamie na kuziwezesha *BMUs* zitekeleze majukumu yao ili kupunguza kasi ya uvuvi haramu wa mabomu na iana nyingine za uvuvi haramu hapa nchini. (*Makoff*)

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Naibu Spika nina maswali madogo ya nyongeza baada ya jawabu lililotolewa na Mheshimiwa Waziri, Kwa kuwa maeneo haya yana ukanda mrefu sana wa bahari kijiografia na kwa kuwa Boti zilizotajwa ambazo zilitolewa na Serikali ni kidogo mno ukilinganisha na maeneo hayo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza hizi Boti walau kumi kwa kila mwaka ili kukabiliana na haya majanga wanayoyapata ya kuharibiwa samaki na uvuvi haramu unaofanyika katika maeneo hayo?

Suala la pili, kwa kuwa Boti hizi ni ghali sana ukilinganisha na uwezo wa Halmashauri zetu na kwa kuwa hata kama zitatengwa au kukusanywa fedha na Halmashauri hizo, Manispaa na Miji zitakuwa hazifikii lengo la kupatikana boti hizo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha katika Halmashauri hizi ili waweze kuongeza na wao mfuko mdogo wanaokusanya kwa kununua Boti zingine zitakazosaidia katika maeneo yao ya uvuvi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa tuna Pwani ambayo ni ndefu sana zaidi kilomita 1424 na ni kweli kwa ulinzi tu kama huu wa Boti na kutegemea doria hatutaweza kudhibiti uhalifu ulimo katika maeneo haya, na mpango mzima umekuwa ni wananchi wanaishi katika maeneo yale wajione kuwa wao ndiyo wamiliki wa rasilimali na wao ndiyo walinzi wa kwanza wa rasilimali. Kwa hiyo sehemu ya mkakati imekuwa moja ni kuunda vikundi hivi shirikishi ambavyo ni vya wavuvi maslahi ya wavuvi ni hao.

Sisi kama Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri zetu kujaribu kuwezesha vikundi hivi ili view na utaratibu na mkakati wa kulinda rasilimali na doria ya kutumia hasa boti hizi aghali iwe ni sehemu tu ya kujazilisha nguvu zinazofanywa na hawa wamiliki wa rasilimali.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ughali wa Boti ni kweli kuwa hizi boti ni ghali na ununuzi wake ni ghali maana moja ina gharimu mpaka shilingi milioni 400, ukiweka vifaa vingine vya *electronic* vinavyohitajika kama rada, *sensors* na vitu vingine. Gharama inaongezeka, lakini ninaomba nitumie nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kuomba Halmashauri zetu zione kuwa uvuvi ni shughuli muhimu kiuchumi na ya kuwapatia watu wetu ajira. Hivyo ni lazima tuchukue kama kipaumbele kutengea fedha za kutosha na inapokuwa kwamba Halmashauri katika mipango yao imepanga vizuri na kupanga fedha za kutosha Serikali ni hakutakuwa na tatizo la kuunga mkono jitihada hizo za Halmashauri zetu. (Makofi)

16 MEI, 2013

NAIBU SPIKA: Swali la nyongeza nilikuona Mheshimiwa Ignas Malocha na Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja dogo la nyongeza. Ziwa Rukwa linakabiliwa sana na tatizo la uhaba wa samaki kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira, nini jitihada ya Serikali kurejesha hali ya ziwa hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunakiri kuwa kuzunguka Ziwa Rukwa kuna uharibifu wa mazingira na *HABITAT* inapoharibika hata na viumbe wanaoishi mle wakiwamo samaki na wenyewe wanakuwa katika tishio la kutoweka, kinachofanyika kwa upande huo hivi sasa kuna *program* inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo inashirikisha Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika.

Japo mradi unatazama mazingira kwa upana wake uvuvi na shughuli za samaki ni moja kati ya shughuli zinazowezeshwa na program hiyo ama mradi huo ili kuhakikisha moja watu wanapata uelewa wa kutosha watunze mazingira yao na kwa mazingira yanapotunzwa *habitat* ya samaki itaboreka na kumbe idadi ya samaki katika ziwa Rukwa itarudi katika level iliyokuwapo hapo mwanzoni. *(Makofi)*

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii sekta ya maendeleo ya uvuvi ikisimamiwa vizuri ni chanzo kimojawapo cha mapato na kwa mwaka huu wa fedha sekta hii ingesimamiwa vizuri tungeweza Serikali ikapata takribani milioni 821 na kwa kuwa Ukanda wa Bahari ya Hindi ni wa kilomita 1424 na mapato yanapotea zaidi kwenye *deep sea* na kwa kuwa Wizara haina uwezo wa kutosha.

Je, Serikali haioni ni busara kushirikisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania na vyombo vingine vyenye uwezo zaidi ili Serikali kupata mapato ya kuhudumia miradi mingine? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa nyingi zipo katika Bahari Kuu na ndiyo maana kuna Sheria na kuna Mamlaka iliyoundwa kusimamia uvuvi katika bahari kuu Makao yake Makuu yako Zanzibar na kwa pamoja huwa wakifanya doria na doria hizi hawafanyi wao kama wao maana hawana *manpower* ya kuweza kutumia vyombo vya moto inapobidi, na jeshi letu la wananchi limekuwa moja kati ya watu wanaofanya hasa kikosi cha *Navy* wamekuwa wakishiriki katika shughuli hii.

Mikakati pia ipo kama unavyosema tuna fursa nyingi katika bahari kuu lakini mikakati ipo ya kujaribu kutafuta namna ya kuwa na uwezo wa kujenga bandari ya uvuvi na baada ya kuwa na bandari kutafuta meli zinazoweza kufanya uvuvi kwa ajili ya watu wetu ili lkiasi kikubwa tunachopata cha samaki kitoke kule zaidi ya kutegemea maji baridi katika maziwa na katika mito yetu. (*Makofi*)

Na. 222

Ujenzi wa Barabara ya Ndundu- Somanga

MHE. JUMA A.NJWAYO aliuliza:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha ujenzi wa barabara ya Ndundu - Somanga baina ya Serikali na *Kharafi & Sons Ltd.* kutokamilishwa?

(b) Je, ni hatua gani ambazo Serikali imechukua dhidi ya kutokamilika huko?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo Mbunge wa Tandahimba lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

16 MEI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga urefu wa KM 60 kwa kiwango cha lami ulitarajiwa kukamilika kama ilivyopangwa kwa sababu mbalimbali. Hii ni pamoja na mvua nyingi zilionyesha kuliko kiwango kilichotarajiwa kimkataba katika kipindi cha Desemba, 2009 hadi Mei 2010, udhaifu wa *menejiment* ya Mkandarasi na kuongezeka kwa kiwango cha kazi zaidi ya ile zilizoainishwa kwenye mkataba. Kutokana na matatizo haya na kulingana na matakwa ya mkataba Mkandarasi aliomba na kupewa muda wa nyongeza wa siku 607 hadi tarehe 12 Septemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi ambazo ni kuimarisha usimamizi wa kazi, kumwelekeza Mkandarasi kuongeza mitambo yenye uwezo mkubwa, kumtaka Mkandarasi kuongeza masaa ya kufanya kazi na kumweleza Mkandarasi kuongeza uwezo wake wa kifedha kumwezesha kuendelea na kazi wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara imetenga shilingi bilioni 5.288 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.

MHE. JUMA A.NJWAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali kama ifuatavyo:-

(a)Serikali imempa adhabu gani mkandarasi huyu kwa kukiuka Mkataba na hata muda wa nyongeza aliopewa.

(b)Ahadi isiyotimizwa siku zote husumbua fikra na hivyo kuwa kero katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri hapa amesema mwenyewe kuwa muda ulipaswa kuwa Septemba 2002, ni kariibu miaka miwili sasa. Juzi akiwa anahitimisha bajeti yake alitoa maelezo kuwa barabara hii itakamilika Desemba 2013, mimi ninavyoona eneo lilobaki ni zaidi ya kilomita 20 na muda huu ni mdogo.

Je, anaweza kulihakikishia Bunge hili na Watanzania kwamba ahadi hii ya Serikali ya kumalizika kabla ya Desemba itakuwa mwisho wa kila kitu na itatimizwa kweli?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nilitegemea Mheshimiwa Njwayo baada ya kujibu swali hili tarehe kumi mwezi wa nne mwaka huu asingeuliza tena na pia katika bajeti yetu ambayo tumewasilisha juzi tumeelezea kuhusu barabara hii mipango ya Serikali kwamba tutaimaliza kabla ya Desemba mwaka 2013. Nilitegemea kabisa Mheshimiwa Njwayo angeishukuru Serikali katika kilomita 317 kutoka Kibiti mpaka Lindi kilomita 260 zimekamilika na katika hizo Ndundu – Somanga kilomita 60 na kilomita 30 tayari ni lami na madaraja yote yamejengwa pamoja na kujenga daraja kubwa la Mkapu ambalo ni kubwa kuliko yote nchi hii, Mikoa ya Lindi na Mtwara yote imefikwa kwa lami kuna Mikoa ambayo hata lami haijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningetemea angeishukuru sana Serikali kwa juhudi ambayo inafanyika, nikuhakikishie kuwa wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi Barabara hii tutaimaliza.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninapenda kumwambia Naibu Waziri kuwa watu wa Kusini hawezi kushukuru kwa sababu ni takribani ni miaka minane tunaongelea kuhusu barabara hii. Lakini katika mwaka 2011/2012 waliahidi barabara hii itakamilika walitenga bilioni 4, Mwaka 2012/2013 walitenga hiyo bilioni 4 tena, Mwaka 2013/2014 bilioni 5.

Mheshimiwa Waziri, watu wa Kusini wamechoka kusikia habari ya barabara hii tunataka *commitment* ya Serikali mwaka huu isipokamilika tufanye nini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthum, kama ifuatavyo:-

16 MEI, 2013

Kwanza nimesema kuwa tutajitahidi kwa sababu unajua Mkataba una tarehe ya kuanza na tarehe ya kumaliza na pia Mkandarasi anapokuwa hakumaliza tarehe ile iko adhabu ambayo iko kimkataba, kuna *requidated damages*.

Kwa hiyo anakatwa malipo yake, hiyo ndiyo njia tunayoweza kufanya na ndiyo maana ninakuhakikishia ndugu yangu ni vizuri uendelee kushukuru kwa sababu tayari Serikali imeweka mtu anayefanya kazi kuliko maeneo mengine ambako hata Mkandarasi hayupo. Sasa pale Mkandarasi yupo na wewe umepita pale umeona magreda yanafanya kazi. Sasa hakuna kingine ambacho Serikali inaweza kufanya zaidi ya kuweka mtu anafanya kazi na Serikali inasema fedha zipo kwa hiyo tumesha ji - *commit*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, walikuwa wanasema isipokamilika wakufanyeje wewe mwenyewe? Haya jibu swali, Mheshimiwa Joseph Selasini. (*Makofi/Kicheko*).

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ngonjera za hii barabara ni za miaka mingi na siyo siri kuwa Serikali inadaiwa mabilioni ya shilingi kama tozo kutokana na ucheleweshaji wa kuwalipa wakandarasi, mimi ninataka kujua Mkandarasi huyu kwa nini analelewa au Serikali ituambie kuwa ilisha mtoza kiasi gani kama na Serikali yenyewe inavyotozwa inapochelewesha kuwalipa wakandarasi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, tozo kwa Mkandarasi huwa tunaifanya mwisho wa Mkataba anapokuwa amemaliza kazi ndiyo tunafanya tathimini na kumtoa tozo huwezi kumtoa tozo kabla vinginevyo hawezi kuendelea kujenga. Kwa hiyo, akimaliza kazi ndiyo tutamtoa tozo.

NAIBU SPIKA: Swali la mwisho kwenye eneo hili Mheshimiwa Jenista Muhagama.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo lakini muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho. Kwa kuwa tatizo la ujenzi wa barabara lililosemwa na Mheshimiwa Njwayo lina fanana kwa namna nyingine na ujenzi wa barabara kutoka Songea Mjini kwenda Mpakani mwa Tanzania na Msumbiji katika Kijiji cha Mitomoni Muhukuru.

Kwa kuwa upembuzi yakinifu umeshakamilika na *design* imeshakamilika na sasa hivi tunachohofia muda mrefu ukishapita inawezekana haya mambo yote yasiendane pia na wakati.

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ikiwa ni miongoni mwa ahadi za Mheshimiwa Rais za kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Shemeji yangu, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa ni kweli hiyo barabara anayoizungumza ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na ni kweli Serikali tayari imeshafanya upembuzi yakinifu. Kwa hiyo, hatua itakayofuata baada ya kumaliza upembuzi yakinifu ni kutafuta fedha ili tuweze kujenga kwa kiwango cha lami.

Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie kuwa barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami mara fedha zitakapo patikana.

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mkapu swali la mwisho kabisa la nyongeza.

16 MEI, 2013

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninavyoona Serikali haina dhamira kabisa ya kumaliza hii barabara ya Dar es salaam mpaka Lindi, kuna kipande cha Nangulukulu mpaka Mbwemkulu kilijengwa hovyoy na tayari imeshafumuliwa upya sasa anaponiambia Naibu Waziri kwamba barabara hii itaisha Desemba Mwaka huu. Siyo kweli, mimi ninaomba tu aseme dhamira ya kweli kwamba barabara hii itaisha labda 2020 lakini siyo mwaka huu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, dhamira ya kweli ni ipi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkapa kama ifuatavyo:-

Kwanza swali la msingi linahusu kipande cha kutoka Ndundu-Somanga siyo barabara nzima huko anakokusema tunazungumzia Ndundu- Somanga na Ndundu- Somanga tumeshamaliza 83% ya kazi inayotakiwa kufanywa pale bado 17% tu nikuhakikishie kuwa 17% Serikali haiwezi kushindwa kumaliza.

Na. 223

Ujenzi wa Ring Roads Dar es Salaam

MHE. HALIMA J. MDEE aliuliza:-

Wakati Serikali ikijibu swali lililoulizwa na Mbunge wa Kibaha, Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka kuhusu ujenzi wa njia nne toka Dar es Salaam – Kibaha ilisema haina mpango wa muda mfupi wa kupanua barabara hiyo kutokana na ukosefu wa fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani mpaka sasa wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara za ndani *ring roads* ili kupunguza adha hii?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee Mbunge wa Kawe kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam hadi Kibaha kuwa njia sita kupitia mradi wa *Dar es Salaam Chalinze Express way* kilomita 110 kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi, *Public Private Partnership (PPP)* au utaratibu mwingine utakaofaa. Serikali kupitia wakala wa Barabara *TANROADS* imeshatangaza zabuni *request for expression of interest* za ujenzi wa barabara kutoka Dar es Salaam Chalinze *express way* na makampuni 19 yamewasilisha nyaraka kuonesha nia ya kufanya ujenzi wa barabara hiyo.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa *ring roads* kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam. Baadhi ya barabara hizo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi ambayo ujenzi unaendelea ni *Ubungo Bus Terminal - Kawawa road roundabout* kilomita 6.4, *Kawawa roundabout - Msimbazi Valley Jangwani/Twiga, Junction* kilomita 2.7 na *Jet Corner - Vituka - Devis Corner* kilomita 10.4

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ambayo zabuni zimetangazwa kwa ujenzi kwa mwaka 2012/2013 ni Mbezi Malamba mawili, Kinyerezi Banana kilomita 14, *Tegeta Kibaoni - Wazo Hill - Goba*, Mbezi Mwisho *Morogoro Road* kilomita 20, Kimara Baruti Msewe Changanyikeni kilomita 2.6, Ubungo Maziwa *External* na Tabata Dampo Kigogo kilomita 2.25, Kimara *Kilungule External* kilomita tisa na Tangi bovu - Goba kilomita 9.

16 MEI, 2013

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa *outering road* ya Bunju *Victoria Morogoro Road* na Pugu kilomita 54 kwa kiwango cha lami, barabara hiyo itakuwa na njia nne yaani njia mbili kwa kila upande. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Waziri kwa majibu yake lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza linahusiana na kutaka Waziri aniambie hususani barabara za Jimboni kwangu wka sababu mwaka jana tulitenga bilioni kumi kwa ajili ya *ring roads* lakini katika barabara za Jimbo la Kawe kulikuwa hakuna matengenezo yeyote ya maana yaliyofanyika.

Mwaka huu tumetenga bilioni 28, nilitaka hususani kwenye barabara za Tegeta Kibaoni Wazo Hill kwenda Goba na Mbezi Mwisho zitajengwa kilomita ngapi na hali kadhalika barabara za Tangi Bovu na Goba zitajengwa kilomita ngapi kutokana na hizi fedha za mwaka huu kwa sababu hizi barabara zote kiujumla zina kilomita zaidi ya 60 na bilioni 28 haiwezi kutosha kujenga kilomita zote kwa kiwango cha lami nzito.

Ninataka kujua sasa barabara hizi *specifically* za Kawe ambazo zimeshatangazwa zitajengwa kilomita ngapi ili tuweze kuzifuatilia.

Lakini swali la Pili, kuna hizi barabara muhimu sana ambazo zinaunganisha Manispaa ya Kinondoni na Ilala kwa mantiki ya Jimbo la Ubungo la Mnyika na Jimbo la Segerea, hii ni barabara ambazo zilitolewa ahadi na Rais mwezi Mei 2010.

Barabara ya Kimara Bonyokwa kwenda Segerea na ni barabara ya kilomita sita tu wala haizidi kilomita sita na tayari makisio ya kujenga yameshafanywa na inahudumiwa na *TANROAD* ni kati ya barabara zinazopunguza foleni, nilitaka nijue hii barabara itajengwa lini kwa kiwango cha lami? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mwaka wa fedha huu ambao tunao tulitenga bilioni kumi na mwaka huu wa fedha tumetenga bilioni 28 kwa ajili ya barabara mbalimbali ambazo nimezielezea kwenye jibu la msingi katika kupunguza msongamano wa Jiji la Dar es Salaam. Ni kilomita ngapi zitajengwa ni kwamba fedha hizi barabra nyingi temeshatangaza tayari tenda za kuanza kujenga. Hizi bilioni 28 zinatoshia kuanza kujenga hizo barabara.

Kwa hiyo, kwa mwaka itategemeana na namna wakandarasi watakavyo-*bid*, maana ukitangaza tenda unaweza ukakuta pengine utapata *offer* ambayo ni tofauti na ile ambayo wewe umetenga kwenye Bajeti. Kwa hiyo, kama fedha zitakuwa zimezidi Serikali itatafuta fedha ili kuweza kukamilisha miradi ambayo imepangwa kutekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie tu nia ya Serikali ni kwamba miradi yote hii ambayo nimeielezea itatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara zile za Manispaa kama tulivyoielezea kwenye Bajeti yetu ya mwaka huu kwamba kuna karibu barabara 25 ambazo zimekasimiwa kutoka barabara za Jiji kuingia kutengenezwa na *TANROADS* kwa hiyo barabara zile tutazishughulikia katika matengenezo kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, mimi naipongeza Serikali kwa kujenga barabara, napongeza Magufuli na Naibu wake hasa kwa

16 MEI, 2013

barabara ya Kunduchi Ununio, tunajua wote ile barabara inavyunguza msongamano kwa watu wanaotumia *New Bagamoyo Road*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipande cha Kunduchi Mtongani kimeharibika sana na pale sasa hivi ajali nyingi zinatokea na barabara hizo unajua, mbaya zaidi kipande kile kimeharibika kabla hata barabara haijakabidhiwa, nilitaka kupata kauli ya Serikali kuhusiana na barabara hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa Kunduchi Mtongani.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kuipongeza Serikali kwa kazi ambayo inaendelea kuifanya katika kujenga barabara katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipande hicho ambacho unakielezea na kwamba kina Mkandarasi na inaonekana kwamba kazi haijakabidhiwa na imeanza kuharibika, nikuahidi tu kwamba tutachukua hatua ili kuhakikisha kwamba Mkandarasi anairudia hiyo kazi kwa gharama zake mwenyewe. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umeisha na maswali yamekamilika nawashukuru sana kwa hatua hiyo.

Waheshimiwa Wabunge matangazo ya kazi, Mheshimiwa Mwambalasa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo saa saba na robo leo mchana wakutane katika Ukumbi wa Msekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Profesa Msolla anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji wakutane saa Saba na Robo leo mchana Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Katibu wa Wabunge wa CUF anawaomba Wabunge wa Chama hicho wakutane leo saa Saba Mchana ukumbi wa *Basement* baada ya kuahirishwa kwa Bunge saa Saba Mchana.

Waheshimiwa Wabunge, katika ziara za Mafunzo tuna kundi la Waheshimiwa Madiwani wote Wilaya ya Iringa Vijijini pale mlipo naomba msimame, karibuni sana Madiwani mjifunze kuhusu Bunge na mnapoendesha Halmashauri zenu basi mzingatie sana namna gani Bunge linaendeshwa na ninyi muendeshe mambo yenu kama Bunge linavyoendeshwa. Wageni hawa ni wageni wa Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa William Agustao Mchimwa, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge lakini vile vile kuna Walimu wangu 18 kutoka Kongwa, karibuni sana Walimu mmekuja kujifunza kuhusu Bunge, mnaona Mbunge wenu ninavyoshughulika hapa, pelekeni salaam kule. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge wageni wengine wa mafunzo ni Wanafunzi 63 kutoka shule ya sekondari ya Ibihwa Wilayani Bahi karibuni sana. Wanafunzi 32 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma karibuni sana wanafunzi wa *UDOM* mjifunze kuhusu Bunge, muelewe linavyofanyakazi, naamini baadhi yenu mtakuwa Wabunge siku zijazo.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni 35 ambao ni washauri wa VVU UKIMWI kutoka Kanisa la Waadventisti Wasabato Tanzania, huenda watakuwa *Basement*. Tunao wanafunzi sita kutoka Chuo cha Hombolo Dodoma, karibuni sana pale mlipo. Tunao wafanyakazi 10 kutoka *TRL* Dodoma ambao wamekuja kujifunza na kusikiliza kuhusu Wizara yao ya Uchukuzi, karibuni mahali mlipo.

16 MEI, 2013

Waheshimiwa Wabunge, wapo wanafunzi 73 na Walimu wanne kutoka shule ya msingi Montensori, Kaloleni karibuni sana wanafunzi na walimu wa Kaloleni mjifunze kuhusu Bunge. Wanafunzi 65 kutoka Chuo cha Biashara (CBE) natumaini watakuwa *basement* leo tuna wageni wengi sana, lakini pia tunawakaribisha wale Maafisa 89 kutoka Wizara ya Uchukuzi karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni 13 kutoka Siha waliokuja kujifunza Mambo ya Bunge, wageni wa Mheshimiwa Mwanri karibuni sana wageni kutoka Siha. Vilevile wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, watakuwa wamefika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tuendeleo, Katibu tuendeleo.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali Mwaka 2013/2014 Wizara ya Uchukuzi

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi Dkt. Harrison Mwakyembe, karibu sana kwa hotuba yako.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi; Baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi, kuweka mezani taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kukutana tena leo kujadili maendeleo ya Sekta ya Uchukuzi, Hali ya Hewa na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile nimpongeze kwa namna ya pekee Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Kuchaguliwa kwake, tena kwa kishindo, ni ushahidi tosha wa imani kubwa waliyonayo wana CCM kwake kutokana na kazi nzuri aliyofanya miaka mitano ya kwanza ya uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha, nawapongeza Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM (Zanzibar), Mheshimiwa Philip Mangula kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM (Tanzania Bara) na Mheshimiwa Abdulrahman Kinana kuwa Katibu Mkuu wa CCM. Binafsi nina imani kubwa kuwa safu hii mpya ya uongozi yenye rekodi ndefu ya utendaji uliotukuka nje na ndani ya Chama cha Mapinduzi itatusogeza karibu zaidi na malengo tuliyojiwekea kama Taifa ya kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu vilevile nitumie fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wao imara na wa mfano ambao umeisaidia sana Wizara ya uchukuzi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa pongezi zifuatazo: Kwanza kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Naibu wako, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mbunge) na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa staha, uvumilivu mkubwa na bila kuyumba katika kusimamia Kanuni tulizojiwekea.

Pili, Mawaziri wenzangu na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa ushirikiano mzuri wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu kama Waziri wa Uchukuzi. Tatu na mwisho, familia yangu na wapiga kura wa Jimbo la Uchaguzi la Kyela ambao wameendelea

16 MEI, 2013

kunionyesha upendo na ushirikiano mkubwa hata pale ninapokuwa nimebanwa na majukumu ya Kitaifa nje ya Jimbo langu la Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imezingatia kikamilifu maudhui yaliyomo kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mbunge wa Katavi, iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu tarehe 10 Aprili, 2013. Naomba kumshukuru na kumpongeza kwa hotuba nzuri iliyotoa ufafanuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013 na mwelekeo wa shughuli za Serikali na dira ya Bajeti ya Serikali katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi nayo imefanya kazi nzuri na kubwa ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Sekta katika mwaka 2012/2013 na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014. Pamoja na kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri, Wizara itazingatia maoni na ushauri wa Kamati katika kuboresha utendaji wa Sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa.

Mapitio ya Utekelezaji wa mpango wa Wizara kwa mwaka 2012/2013 na malengo ya mwaka 2013/2014; baada ya maelezo hayo ya awali, niruhusu sasa nifanye mapitio ya utekelezaji wa mipango ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2012/2013 na kutoa maelezo kuhusu Malengo na Makadirio ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2012/2013 ulizingatia: Dira ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Malengo ya MKUKUTA II, Ahadi na Maagizo ya Serikali pamoja na Sera za Kisekta, Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Uchukuzi kwa njia ya Nchi Kavu; Usafiri na Uchukuzi kwa Njia ya Reli; Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuboresha na kukuza kiwango cha utoaji wa huduma ya usafiri wa reli nchini. Pamoja na jitihada hizo, utoaji wa huduma katika sekta hii kwa kipindi kirefu umekuwa hauridhishi kutokana na kuchakaa kwa miundombinu ya reli, uchakavu na uchache wa vifaa vya uendeshaji kama vile vichwa vya treni, mabehewa, mashine na mitambo ya kufanyia kazi. Hali hiyo imelazimu, katika sehemu mbalimbali za njia ya reli, treni kupunguza mwendo hadi wastani wa Kilometa 15 tu kwa saa ili kuzuia ajali, na hivyo kulinda usalama wa abiria na mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia taasisi zake zinazohusika na uchukuzi kwa njia ya reli, imechukua hatua kadhaa ili kudhibiti hali hiyo. Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli nchini (*RAHCO*) iliendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uimarishaji wa miundombinu ya reli: kuondoa reli nyepesi na chakavu na kutandika reli mpya na nzito zaidi; kuimarisha madaraja yaliyopo na kujenga mengine mapya; kuimarisha tuta la reli na kuendelea na ujenzi wa vituo vya upakiaji na upakuaji wa makontena.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kullifanyia kazi eneo kati ya stesheni za Kitaraka na Malongwe lenye urefu wa Kilometa 89 ambalo lina reli kuukuu na nyepesi za ratili 56.2 kwa yadi (sawa na kilo 28 kwa mita), hivyo kuwa chanzo cha ajali za treni za mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kazi ya kutandika reli mpya na nzito za ratili 80 kwa yadi (kilo 40 kwa mita) ambayo tuliimbea fedha hapa Bungeni na tukapewa, ilianza Septemba, 2012 kwa kutumia mikono (*manual relaying*) badala ya kusubiri mashine maalum kwa kazi hiyo. Utaratibu huo umetuwezesha kung'oa reli zisizohitajika na kutandika nyingine kwa umbali wa Kilometa 13 na kutoa ajira ya moja kwa moja kwa vijana 250 wa Ki-Tanzania.

16 MEI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mkandarasi, Kampuni ya ujenzi kutoka China iitwayo China *Civil Engineering Construction Company (CCECC)*, ameshafikisha kwenye eneo la mradi mashine maalum ya kutandikia reli yenye uwezo wa kutandika Kilometa 1 ya reli kwa siku, kreni 2 za kupakia paneli zilizokwisha unganishwa kwenye mabehewa na viberenge vikubwa viwili kila kimoja kina uwezo wa kuvuta mabehewa 4 yenye reli na mataruma, na mitambo midogo ya kushindilia kokoto baada ya kutandika reli. Tunatarajia mradi huu kukamilika mwezi Oktoba 2013 kwa gharama ya Shilingi bilioni 29.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maombi yetu ya fedha kwa mwaka 2012/2013, tulieleza Bunge lako Tukufu kuhusu uharibifu mkubwa wa miundombinu uliotokea kwenye maeneo 32 ya Reli ya Kati, kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe kutokana na mvua kubwa zilizonyesha mwaka 2009 na 2010 na maeneo 13 kati ya Gulwe na Godegode kutokana na mvua za mwaka 2011.

Pia tulieleza jitihada zilizofanyika za ukarabati wa reli, madaraja na ujenzi wa kingo za tuta la reli kwenye maeneo hayo. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mbali na ujenzi wa madaraja unaoendelea, kazi zingine zote za ukarabati wa mindombinu ya reli na udhibiti wa mto Mkondoa, zimekamilishwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililobaki katika eneo hilo na ambalo tunalifanyia kazi ni la mchanga kujaa kwenye makalavati kila mvua inaponyesha. Mathalan, makalavati yaliyopo stesheni ya Gulwe, pamoja na kwamba yalisafishwa kikamilifu, kwa sasa yamejaa mchanga kwa karibu asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishadokeza awali, kazi kubwa inayoendelea eneo hilo hivi sasa ni ujenzi wa madaraja mawili makubwa kati ya Kilosa na Gulwe na daraja moja kati ya stesheni za Bahi na Kintinku. Kazi ya awali, ambayo inaendelea ni ujenzi wa nguzo za madaraja hayo

na udhibiti wa uimara wake. Juu ya nguzo hizo, patafungwa madaraja ya vyuma (*Bridge Steel Girders*) ambayo kwa sasa yanamaliziwa kutengenezwa nchini China. Mkandarasi, CCECC, anatarajia kuwa ifikapo mwishoni mwa Juni, 2013 tayari madaraja hayo ya vyuma yatakuwa yameshawasili nchini tayari kwa kazi ya kuyafunga. Gharama za ujenzi wa madaraja hayo matatu ni Shilingi bilioni 14.45.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilipokuwa nawasilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2012/2013, nilielezea kuwa pamoja na mabadiliko makubwa ya tabia nchi ambayo husababisha mvua kubwa kunyesha bila matarajio, shughuli za binadamu hususan ufugaji na kilimo kinachoambatana na ukataji miti milimani na uedeshaji wa kilimo na ufugaji karibu kabisa na tuta la reli, ni miongoni mwa sababu kuu zinazosababisha mvua zinazonyesha maeneo hayo kuwa na athari kubwa kwenye miundombinu ya Reli ya Kati hasa kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe. Natumia fursa hii kuwaomba wananchi walio karibu na njia za reli nchini kutunza mazingira na kuepukana na shughuli zozote ndani ya eneo la hifadhi ya reli ambalo kwa mujibu wa sheria ni mita 15 pande zote za reli kwa sehemu za miji na mita 30 kila upande nje ya miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuwahamasisha wananchi kuendelea na shughuli zao za uzalishaji mali lakini kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na sheria ili kulinda miundombinu ya reli. Mathalan, tarehe 14 Septemba, 2012, Wizara kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa na Wilaya za Morogoro na Dodoma, Waheshimiwa Wabunge, Madiwani na Makatibu Tarafa wa maeneo kutoka Kilosa hadi Gulwe walishiriki mkutano mkubwa wa hadhara uliofanyika Gulwe kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi na viongozi wao juu ya athari zitokanazo na shughuli za kilimo na ufugaji zisizozingatia masharti ya sheria na kuzembea utunzaji wa mazingira.

16 MEI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kuwakumbusha wananchi kuwa, kutokana na shughuli za binadamu zisizofuata sheria wala utaratibu, mvua zikinyesha husomba magogo, udongo na mchanga mwingi kutoka milimani.

Mzigo wote huo huishia kwenye tuta la reli na kusababisha makalvati na madaraja kuziba hivyo kulazimisha maji kupita juu ya tuta la reli na hatimaye kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya reli. Vilevile, maji huathiri uimara wa tuta la reli na hivyo kusababisha ajali za mara kwa mara ambazo zinalisababishia Taifa hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanya tathmini ya hali na mahitaji ya kufufua na kuboresha miundombinu na utendaji kazi wa Reli ya Kati, *RAHCO* iliajiri Mshauri Mwelekezi (Kampuni ya *CPCS Transcom* kutoka Canada) kufanya kazi hiyo. Katika taarifa yao iliyowasilishwa Serikalini mwezi Machi 2013, *CPCS* wameshauri kufanyika kwa tathmini ya kina kuhusu namna ya kupata ufumbuzi wa kudumu katika maeneo yanayoathirika mara kwa mara na mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na eneo hilo korofi kati ya Kilosa na Gulwe, Wizara vilevile imeelekeza macho kwenye maeneo mengine korofi kati ya Kaliua na Mpanda kwa kuondoa reli kuukuu na nyepesi za ratili 45 kwa yadi (kilo 22 kwa mita) na kutandika reli nzito zaidi za ratili 56.2 kwa yadi (kilo 28 kwa mita).

Njia ya reli yenye urefu wa Kilometa 9 kati ya Lumbe na Mto Ugala na kati ya Mto Ugala na Katumba, ilionekana na wataalam wetu kuhitaji ukarabati wa haraka. Tumeweza, hadi sasa, kukarabati Kilometa 5.5 kati ya Kilometa 9 kutokana na kukosekana kwa vifungio vya reli na mataruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hilo litapata ufumbuzi kutokana na utekelezaji wa mradi wa reli niliouelezea awali wa kutandika reli mpya za uzito wa ratili 80 kwa yadi kutoka Kitaraka hadi Malongwe ambao utazalisha vipuri, reli na mataruma ya kutosha. Hivyo, Kilometa 3.5 zilizosalia katika reli ya Kaliua-Mpanda zitakamilishwa ndani ya mwaka 2013/2014. Aidha, ukarabati wa tuta la reli linalokatiza mto Ugala na ukarabati wa daraja lake utaanza muda wowote kuanzia sasa baada ya mkandarasi kupatikana kwa gharama ya Shilingi milioni 430.6. Mkandarasi ameshaanza maandalizi (*mobilisation*) na anatarajiwa kukamilisha kazi Agosti, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia *RAHCO* ilikamilisha mchakato wa kuwapata Washauri Waelekezi watakaofanya usanifu wa kina wa uboreshaji wa njia ya reli ya kutoka Tanga hadi Arusha na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli mpya ya kutoka Arusha hadi Musoma kwa kiwango cha Kimataifa (*standard gauge*). Kutokana na ukosefu wa fedha mikataba ya kazi hizo haikuweza kusainiwa katika kipindi hicho. Wizara imetenga fedha zinazohitajika kwa kazi hii katika bajeti ya mwaka 2013/2014. Utiaji saine wa mikataba hii utafanyika mara tu baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha makadirio ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014. Aidha, kama sehemu ya mradi huu wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma, Wizara kupitia *RAHCO* na kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mkoa wa Tanga imekamilisha taratibu za kulipa fidia kwa wakazi wa eneo la Mwambani, Tanga ili kupisha ujenzi wa sehemu ya kupanga mabehewa (*marshalling yard*). Zoezi la kulipa fidia lilianza mwishoni mwa Aprili, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara ilitarajia kufanya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha reli kati ya Tabora na Kigoma, Kaliua na Mpanda na Isaka na Mwanza kwa kiwango cha Kimataifa (*standard gauge*). Kazi hii ambayo haikuweza kutekelezwa katika mwaka 2012/2013 kutokana na ukosefu wa fedha, inatarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 51.14 kwa ajili ya kuendeleza miradi mbalimbali ya miundombinu ya reli. Miradi hiyo ni pamoja na ile niliyoigusia awali ya: kukamilisha utandikaji wa reli nzito za ratili 80 kwa yadi kati ya stesheni za Kitaraka na Malongwe; kukamilisha ujenzi wa madaraja mawili kati ya Kilosa na Gulwe na daraja moja kati ya stesheni za Bahi na Kintinku; na ujenzi wa Kituo cha Kupakua na Kupakia Makasha (*ICD*) cha Mwanza. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia itagharamia mradi wa kuinua uwezo wa madaraja yaliyo chini ya tani 15 kwa eksele (*axle*) kufikia tani 25 kati ya Dar es Salaam na Isaka. Katika mwaka 2013/2014, kazi itakayoanza kutekelezwa ni pamoja na kufanya tathmini ya madaraja (*bridges rating*) madaraja yote katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na: ukarabati wa mtambo wa mgodi wa kokoto ulioko Tura; kuendelea kulifanyia kazi eneo korofi la njia ya reli kati ya stesheni ya Kilosa na Gulwe, hasa kazi ya kufukua mchanga kila baada ya mvua kubwa ikinyesha; kushirikiana na Serikali za Rwanda na Burundi katika kuendeleza mradi wa ujenzi wa reli kutoka Dar es Salaam hadi Isaka na kutoka Isaka kwenda Kigali (Rwanda) na Musongati (Burundi) kwa kiwango cha Kimataifa; kufanya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha reli ya Tanga - Arusha na kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa reli kati ya Arusha na Musoma kwa kiwango cha Kimataifa. Aidha, Serikali inatarajia kuunda mfumo wa kusimamia na kufuatilia mizigo na vyombo vya uchukuzi (*Cargo Tracking & Management Sytem*), kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Mtwara – Songea – Mbambabay na michepuo ya kwenda Mchuchuma na Liganga na usafiri wa treni ya abiria katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma ya uchukuzi kwa njia ya reli, Serikali vilevile imekuwa ikitenga fedha katika bajeti zake ili kuboresha na kuimarisha huduma hiyo inayotegemewa sana siyo tu ndani ya nchi bali na nchi jirani tunazopakana nazo. Mathalan, bajeti ya mwaka 2012/

2013, ilienga kuongeza uwezo wa Kampuni ya Reli Tanzania (*TRL*) wa kubeba abiria na mizigo kwa kununua vichwa vipya vya treni, mabehewa mapya ya abiria na mizigo, kukarabati vichwa vya treni vilivyochakaa na mabehewa chakavu ya abiria na mizigo, na kuiongezea *TRL* uwezo zaidi wa kuifanyia njia ya treni matengenezo ya kawaida pale inapolazimu. Ndani ya mwaka 2012/2013, *TRL* imeweza kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuingia mikataba kwa ajili ya kujenga upya vichwa vya treni nane (8), kununua mabehewa 22 ya abiria, mabehewa ya breki 34, mashine moja (1) ya kutandika reli, mabehewa 274 ya mizigo na 25 ya kokoto na seti moja ya mashine ya kushindilia kokoto;

(ii) Kuingia mkataba kwa ajili ya kununua vichwa vipya 13 vyenye uwezo mkubwa wa kubeba mizigo. Mkataba huo ulisainiwa tarehe 4 Aprili, 2013 na vichwa hivyo vinatarajiwa kuanza kuwasili nchini mwezi Desemba, 2014;

(iii) Kununua vipuri kwa ajili ya ukarabati wa vichwa vya treni vinne (4) na mabehewa 125 ya mizigo na kazi za kukarabati mabehewa hayo katika karakana za *TRL* zinaendelea;

(iv) Kuendelea na ukarabati wa injini moja aina ya 89xx. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika Juni, 2013;

(v) Kuendelea na matengenezo ya kawaida ya miundombinu ya reli;

(vi) Kuanza kazi ya kufufua magenge ya Reli ya Kati na kufanikiwa kukamilisha ujenzi wa genge la kwanza kati ya stesheni za Pugu na Mpji. Ukarabati wa magenge mengine manne ya Kigwe, Malongwe, Goweko na kati ya Kwala na Msua uko kwenye maandalizi;

(vii) Ukarabati wa majengo ya karakana za Morogoro na Dar es Salaam na stesheni za Kigoma, Mwanza na Kaliua umeanza na unaendelea;

(viii) Kununua seti tatu (3) za mashine ya kunyanyulia mabehewa yaliyopata ajali; na

(ix) Kurejesha huduma za treni ya abiria kati ya Dar es Salaam na Mwanza tarehe 7 Desemba 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012, *TRL* ilisafirisha tani 198,024 za mizigo ikilinganishwa na tani 267,008 zilizosafirishwa mwaka 2011, ikiwa ni pungufu kwa asilimia 25.8. Kwa upande wa abiria, katika mwaka 2012, *TRL* ilisafirisha abiria 505,223 ikilinganishwa na abiria 519,036 waliosafirishwa mwaka 2011. Huu ni upungufu wa asilimia 2.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu huo wa mizigo na abiria umetokana na uhaba na uchakavu wa injini za treni na mabehewa; kushindwa kutekelezwa kwa Mpango wa Biashara wa *TRL* kutokana na uhaba wa fedha; uharibifu wa njia ya reli tuliouongelea awali kati ya stesheni za Kilosa, Godegode na Gulwe; uchakavu wa njia ya reli hasa katika maeneo ya kuanzia stesheni ya Kitaraka na kuelekea Malongwe; uwezo mdogo wa njia ya reli iliyopo na madaraja yake (*axle load*) katika kubeba mizigo; uhaba wa vipuri vya injini na mabehewa na uchakavu wa mashine mbalimbali za kufanyia kazi za reli; uhaba wa vifaa vya karakana na kushindwa kufanya kazi ipasavyo kwa mgodi wa kokoto wa Tura ambao unahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya reli na utoaji wa huduma zake. Juhudi hizo ambazo zimegusa pia maeneo ya ukarabati na ununuzi wa vitendea kazi vipya, zimeanza kuzaa matunda. Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza kwa dhati kampuni ya Kitanzania ya S. S. Bakhresa kwa kuitikia haraka mpango huo na kutoa Dola za Kimarekani laki nane ambazo zimetumika kukarabati vichwa viwili (2) vya treni aina ya 73xx. Vichwa hivyo vya treni vinatumika, pamoja na kazi zingine, kusafirishia ngano kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza kwa ajili ya soko la S.S. Bakhresa la Uganda. Vilevile Kampuni ya *TICTS Ltd* imeonyesha nia ya kutoa kiasi hicho hicho cha fedha kukarabati vichwa viwili (2) vya injini aina ya 64xx na

mabehewa 20 kwa ajili ya kusafirishia makasha kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Kituo cha Makasha cha Ubungo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzo huu mzuri wa ushiriki wa sekta binafsi katika kuboresha huduma za treni haujaishia kwenye ununuzi na ukarabati wa vichwa vya treni na mabehewa tu, bali umehusisha hata ununuzi na umiliki wa mabehewa ya mizigo, mabehewa ya mafuta na makasha. Aidha, napenda kutambua ushiriki wa Kampuni zifuatazo: *Prime Fuels* yenye mabehewa ya mafuta 6; *East African Railway Hauliers* yenye mabehewa 139; *Mohamed Enterprises Ltd* yenye mabehewa 19 na *S. S. Bakhresa & Co. Ltd* yenye makasha 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, *TRL* imetengewa shilingi bilioni 113.12 kwa ajili ya kukamilisha ununuzi wa vichwa vya treni 13, mabehewa 22 ya abiria, mabehewa 274 ya mizigo, mabehewa 34 ya breki, mashine ya nyakua, toroli 30 na vifaa mbalimbali pamoja na kulipa madeni ya Kampuni. Kazi nyingine ni kujenga upya vichwa vinane (8) vya treni, kukarabati mabehewa 123 ya mizigo, kukarabati majengo ya karakana, stesheni na matengenezo ya njia ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma za uchukuzi wa mizigo na usafirishaji wa abiria kati ya Tanzania na Zambia na nchi zingine jirani za ukanda wa *SADC* kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Malawi. Katika kutekeleza majukumu yake, TAZARA imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali katika utendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili Mamlaka hii, Baraza la Mawaziri la TAZARA limeunda Kamati ya pamoja ya Ukaguzi na Udhhibiti wa Hesabu za Mamlaka. Aidha, Bodi imeunda Kamati za Ufundi, Fedha na Utawala. Kamati hizo zimekwishaanza kazi ya mapitio ya kero mbalimbali za Mamlaka hiyo. Pia, mchakato wa kurekebisha Sheria ya TAZARA Na. 23 ya mwaka

1975 kama ilivyohuishwa na Sheria Na. 4 ya mwaka 1995, Sura ya 143 unaendelea. Kamati mbili za wataalam wa sheria zimeundwa, moja upande wa Tanzania na nyingine upande wa Zambia. Hadidu za rejea pamoja na mpango kazi wa Kamati zimekamilishwa na kazi ya kuainisha maeneo ya sheria yenye upungufu imeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi, 2012, Serikali za Tanzania, Zambia na China zilisaini makubaliano ambapo Serikali ya China ilikubali kutoa msaada wa fedha kwa ajili ya kufanya utafiti na upembuzi yakinifu kuhusu maboresho ya reli ya TAZARA. Kampuni ya *Third Railway Survey and Design Institute (TSDI)* kutoka China iliteuliwa kufanya kazi hiyo. Taarifa ya utafiti huo inatarajiwa kukamilika mwezi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Aprili, 2012 hadi Machi, 2013, TAZARA ilisafirisha jumla ya tani za shehena 208,695 ikilinganishwa na tani za shehena 394,117 zilizosafirishwa katika kipindi cha Aprili, 2011 hadi Machi, 2012. Utendaji huu ni pungufu kwa asilimia 47. Katika kipindi cha Aprili, 2012 hadi Machi, 2013, TAZARA ilisafirisha abiria 695,609 ikilinganishwa na abiria 851,959 waliosafirishwa Aprili, 2011 hadi Machi, 2012. Hii ni pungufu kwa asilimia 18. Utendaji huu usiotabirika na kuridhisha ni moja ya masuala yanayoangaliwa kwa undani na Kamati za Bodi nilizoziongelea awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Itifaki ya 14, TAZARA ilitekeleza miradi mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na ununuzi wa vichwa vipya sita (6) vya treni; ununuzi wa vipuri vya kukarabati vichwa vingine sita (6) vya treni; ukarabati wa vichwa vitatu (3) vya sogeza; ukarabati wa mashine nne (4) za kunyanyua makasha na ununuzi wa vipuri 9,600 kwa ajili ya mabehewa. Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013, TAZARA ilibadilisha jumla ya mataruma ya zege 6,862 na mataruma ya mbao kwenye madaraja 476, kwenye sehemu za kawaida 1,138 na kwenye vibaadilisha njia 213.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2012/2013, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Machi, 2012, Serikali ya

Watu wa China na Serikali za Tanzania na Zambia zilisaini Itifaki ya 15 ya mkopo wenye masharti nafuu wa thamani ya Shilingi bilioni 67.2. Napenda kutoa taarifa kuwa, utekelezaji wa Itifaki hiyo utaanza katika mwaka 2013/2014. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ununuzi wa vichwa vipya vinne (4) vya treni; vichwa vipya viwili (2) vya sogeza; ukarabati wa mabehewa 42 ya abiria; mashine mbili (2) za okoa, mitambo na vifaa vya uokoaji. Miradi mingine ni kufanya upembuzi wa kina wa ujenzi tawi sasa jipya la reli kutoka Kiwira - Uyole (Kilometa 50), tawi la reli kutoka Tunduma – Bandari ya Kasanga - Sumbawanga - Kigoma (Kilometa 700) na tawi la reli la Mlimba - Liganga - Mchuchuma (Kilometa 260); ukarabati wa madaraja 265 na kuweka mawasiliano yanayotumia Mkongo wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za usafiri wa reli Jijini Dar es Salaam. Katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, nilitoa ahadi ya Serikali kuanzisha huduma za usafiri wa abiria kwa njia ya reli Jijini Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari na adha ya usafiri Jijini Dar es Salaam. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa huduma za usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam kati ya stesheni za Dar es Salaam hadi Ubungo Maziwa na Mwakanga hadi Kurasini zilianza Oktoba, 2012. Huduma hizo zinatolewa na *TRL* kutoka stesheni ya Dar es Salaam hadi Ubungo Maziwa (Km 12) na TAZARA kutoka Mwakanga hadi Kurasini kupitia stesheni kuu ya Dar es Salaam (Km 34.5) kwa siku sita (6) za wiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwikio wa wananchi kutumia huduma za treni ya abiria Jijini Dar es Salaam umekuwa mkubwa ikilinganishwa na uwezo wa kutoa huduma yenyewe, hususan nyakati za mahitaji makubwa ya usafiri yaani (*peak hours*). Kwa upande wa TAZARA, wastani wa idadi ya abiria wanaosafiri kwa treni kwa siku umefikia abiria 9,000 baada ya kukamilika kwa ukarabati wa mabehewa mengine saba (7) na kichwa kimoja (1) cha treni na kuanza kutumika rasmi hivi majuzi tarehe 9 Mei 2013 na kufanya treni zianze kupishana. Aidha, kwa upande wa *TRL* wastani wa abiria wanaosafiri kwa siku ni 5,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa usafiri wa treni katika Jiji la Dar es Salaam kumesaidia kupunguza idadi ya magari barabarani. Abiria 14,000 wanaobebwa kwa treni kwa siku hivi sasa wangehitaji kutumia mabasi zaidi ya 467 yenye uwezo wa kubeba abiria 30 kila moja. Aidha, kuanza kwa usafiri huu kumeshawishi baadhi ya wananchi waliokuwa wanatumia magari binafsi kuja katikati ya Jiji la Dar es Salaam, kuanza kutumia usafiri wa treni. Baadhi ya faida zinazotokana na usafiri huu ni pamoja na kupungua kwa matumizi ya mafuta, muda unaotumika barabarani na hivyo kusaidia wananchi kufika kwa wakati katika shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na usafiri wa treni ya abiria kuanzishwa katika Jiji la Dar es Salaam, Wizara inaendelea kufanyia kazi changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utoaji wa huduma hii. Changamoto hizo ni pamoja na kutokuwa na mfumo thabiti wa ukusanyaji wa mapato, uchakavu wa miundombinu na uhaba wa injini na mabehewa. Mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo ni pamoja na kuhakikisha kuwa mfumo wa ukusanyaji wa mapato unaboreshwa ili kila abiria anayepanda treni alipe nauli na hivyo kusaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa huduma hii. Wizara pia inaendelea na ukarabati wa vichwa vya treni na kukamilisha ujenzi wa miundombinu iliyopo ili iweze kutumika kutoa huduma endelevu na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuongeza huduma ya usafiri wa treni ya abiria katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam ni suala mtambuka linalogusa taasisi nyingi. Kwa kutambua hilo, Wizara imeunda Kamati Maalum, chini ya Uenyekiti wa Naibu Waziri wa Uchukuzi kwa ajili ya kuchambua, kuainisha na kushauri mipango na mikakati ya kuboresha na kupanua huduma ya usafiri wa treni ya abiria Jijini Dar es Salaam. Wajumbe wengine wa Kamati hii ni Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam; Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke; Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam; *TANROADS*; *RAHCO*; *TRL*; *TAZARA*; Jeshi la Polisi - Kikosi cha

Usalama Barabarani, *SUMATRA* na Halmashauri za Wilaya za Kibaha, Mkuranga, Bagamoyo na Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maandalizi ya kuboresha usafiri wa treni Jijini Dar es Salaam, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia *RAHCO* itakamilisha mchakato wa kumpata mwekezaji na mwendeshaji wa huduma ya usafiri wa treni ya abiria katika Jiji la Dar es Salaam atakayetumia miundombinu ya reli iliyopo na vichwa vya treni na mabehewa maalum (*Diesel Multiple Units - DMUs*) kwa ajili ya usafiri wa abiria katika miji. Wazabuni nane (8) wanategemewa kuwasilisha maandiko (*proposals*) kabla ya mwisho wa mwezi Mei, 2013. Aidha, Wizara kupitia *RAHCO* itafanya upembuzi yakinifu wa kupanua huduma hii ya treni ya abiria kwenda maeneo ya Luguruni, Bunju, Chamazi na Pugu. Pia, Wizara inaangalia uwezekano wa kuanzisha huduma maalum ya treni kati ya Stesheni ya Dar es Salaam na Gongo la Mboto kwa ajili ya kuhudumia abiria wanaopita kuelekea Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa huduma za usafiri wa nchi kavu na majini. Katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, niilitaarifu Bunge lako Tukufu juu ya *SUMATRA* kufungua ofisi zake katika mikoa mbalimbali ili kusogeza huduma zake karibu zaidi na wananchi. Katika mwaka 2012/2013, *SUMATRA* ilifungua ofisi zake katika Mikoa ya Pwani, Singida, Shinyanga, Lindi, Manyara na Ruvuma. Kwa sasa, Mamlaka ina ofisi katika Mikoa 21. Katika Mikoa iliyobaki ya Geita, Katavi, Njombe na Simiyu, *SUMATRA* inaendelea kutoa huduma zake kupitia ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa. Katika mwaka 2013/2014, *SUMATRA* itaendelea kusogeza huduma za udhibiti karibu zaidi na wananchi kwa kuendelea kufungua ofisi katika Mikoa ya Geita, Katavi na Simiyu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa huduma za usafiri wa reli. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, *SUMATRA* ilifanya ukaguzi wa miundombinu, vifaa, utendaji na huduma zitolewazo na Kampuni ya Reli ya Tanzania (*TRL*) na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (*TAZARA*). Kuhusu *TRL*, ukaguzi

ulifanyika katika maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko kati ya Morogoro na Dodoma na njia ya reli kwa ajili ya usafiri wa treni Jijini Dar es Salaam. Kwa upande wa *TAZARA*, ukaguzi huo ulifanyika katika eneo la kutoka Dar es Salaam hadi Tunduma na usafiri wa treni Jijini Dar es Salaam. Ukaguzi ulibaini kasoro kadhaa ikiwa ni pamoja na uchakavu wa miundombinu, mabehewa na mawasiliano hafifu. *TRL* na *TAZARA* ziliagizwa kushughulikia kasoro zilizobainika.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya ajali za treni yameendelea kuwa ni changamoto katika sekta ya reli. Tarehe 17 Septemba, 2012, ajali mbaya ya treni ilitokea kati ya Makambako na Kangaga katika reli ya *TAZARA* na kusababisha kifo cha dereva wa treni, kuanguka kwa vichwa viwili (2) vya treni na mabehewa yote 29 ya mizigo. Uchunguzi wa awali uliofanyika kuhusu ajali hiyo ulibaini kuwepo kwa udhaifu wa ukaguzi katika kituo cha Makambako. Wizara imeunda Kamati inayofanya uchunguzi wa kina kuhusu ajali hiyo na inatarajiwa kukamilisha kazi yake Juni, 2013. Aidha, *TAZARA* imeelekezwa kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa taratibu za uendeshaji salama wa treni.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa huduma za usafiri kwa njia ya barabara. Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni mbalimbali ili kusaidia katika udhibiti wa biashara ya usafiri wa pikipiki ambayo imekuwa ni chanzo kikubwa cha ajali za barabarani na pia kuhusishwa na uhalifu kwa kushiriki moja kwa moja ama kuwezesha uhalifu kutokea. *SUMATRA* iliendelea kuingia mikataba ya Uwakala na Halmashauri za Wilaya nchini ili zisimamie utekelezaji wa kanuni za usafiri wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu katika maeneo ya Halmashauri hizo. Hadi kufikia Machi, 2013, *SUMATRA* ilikuwa na makubaliano na Halmashauri 126 kati ya Halmashauri 133 zilizokuwa zimelengwa. *SUMATRA* inaendelea kuzifuatilia Halmashauri saba (7) ambazo hazijasaini mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kusimamia agizo la kuzuia abiria wa mabasi ya masafa marefu kujisitiri katika maeneo yasiyo rasmi, maarufu kama

kuchimba dawa. Utekelezaji wa agizo hili ulianza tarehe 1 Septemba, 2012. Katika kufanya utekelezaji wa suala hili kuwa shirikishi, Wizara kupitia *SUMATRA* ilikutana na wasafirishaji ili kuweka mikakati ya pamoja ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na kuainisha vituo vyenye staha vitakavyotumika kwa ajili ya huduma za abiria ambavyo vilitangazwa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari mwishoni mwa Agosti, 2012. Aidha, *SUMATRA* imeandaa michoro mahsusi ya kuwasitiri abiria wakiwa safarini ambayo inazingatia tofauti za kijinsia na mahitaji ya walemavu. Michoro hiyo inapatikana katika ofisi za *SUMATRA*. Serikali inatoa wito kwa Halmashauri na wananchi kwa ujumla kujitokeza ili kuwekeza katika huduma hii muhimu. Wananchi pia wanaombwa kutokukubali kuendelea kujisitiri katika vichaka kwani kufanya hivyo kuna madhara makubwa kiafya, kimazingira na kiutamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kukabiliana na changamoto ya ajali nyingi za barabarani. Ajali hizi zimekuwa zinasababisha vifo, ulemavu, upotevu wa mali na matatizo ya kisaikolojia kwa waathirika wa ajali na wategemezi wao. Katika mwaka 2012, ajali za barabarani zilipungua hadi 23,578 kutoka ajali 23,986 zilizotokea mwaka 2011; huu ni upungufu wa asilimia 1.7. Kuanza kupungua kwa matukio ya ajali za barabarani ni ishara njema kuwa juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali pamoja na wadau wengine zimeanza kuleta matunda. Wizara kupitia *SUMATRA* na kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kuchukua hatua zote za tahadhari ili kupunguza zaidi ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SUMATRA* imeendelea kuhakikisha kwamba wenye mabasi na magari ya mizigo wanakuwa na nyaraka muhimu ikiwa ni pamoja na hati ya ukaguzi wa gari (*vehicle inspection report*) kutoka Jeshi la Polisi - Kikosi cha Usalama Barabarani na hati ya bima kabla ya kupewa leseni. Lengo likiwa ni kukabiliana na tatizo la ajali za magari barabarani. Ili kuimarisha uzingatiaji wa masharti ya leseni za usafirishaji, *SUMATRA* kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi – Kikosi cha Usalama Barabarani ilifanya kaguzi katika mikoa yote Tanzania Bara. Katika ukaguzi huo, jumla ya magari 1,935 yalikuwa na makosa mbalimbali kama kutoa huduma bila ya kuwa na leseni, kutumia leseni bandia,

kukatisha safari, kuzidisha nauli na kutofuata ratiba. Aidha, mabasi 42 yalibainika kufanya makosa ya kujirudia na hivyo yalifungwa kwa muda kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za usafirishaji wa abiria kwa njia ya barabara ziliendelea kuimarika. Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013, leseni 25,215 za usafirishaji wa abiria zilitolewa ikilinganishwa na leseni za usafirishaji 23,119 zilizotolewa katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Machi, 2012. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 9.0. Pamoja na ongezeko hilo la leseni za usafirishaji wa abiria, Wizara imepokea malalamiko mengi kutoka mikoa kadhaa juu ya hatua ya *SUMATRA* kuzuia magari madogo aina ya *NOAH* kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria. Sababu zinazotolewa na *SUMATRA* ni za msingi kwamba magari hayo hayakuundwa kubeba abiria kibiashara kwani: hayana uwezo mkubwa wa kubeba abiria wengi, hivyo kwa nauli elekezi za *SUMATRA*, hayawezi kamwe kupata faida mpaka kwa kukiuka masharti ya leseni, na hayana madirisha yanayofunguka sehemu ya nyuma ya gari. Hoja hizo, kama nilivyosema awali, ni za msingi lakini kwa kuzingatia hali ngumu ya usafiri iliyopo nchini ambayo imelazimu Serikali iruhusu pikipiki za magurudumu mawili na magurudumu matatu kubeba abiria, Serikali inaiagiza *SUMATRA* kuchukua hatua zifuatazo mara moja:-

(i) landae utaratibu wa kutoa leseni kwa magari hayo ya *NOAH* kwa sharti la kurekebisha madirisha yake ya nyuma, kubeba idadi ya abiria itakayotajwa na *SUMATRA* na kwa nauli elekezi ambayo *SUMATRA* itatangaza baada ya kuwashirikisha wamiliki wa magari hayo.

(ii) Kuhakiki leseni za udereva siyo tu kwa madereva wa *NOAH*, bali pia kwa madereva wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu.

(iii) Kutoruhusu biashara ya *NOAH* ndani ya Majiji ambayo tayari yamechukua hatua mahsus kuzuia matumizi ya magari madogo, mbali na teksi, yasiyoweza kubeba zaidi ya abiria¹⁸.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa usalama wa vyombo vya usafiri majini. Wizara kupitia *SUMATRA* iliendelea kusimamia udhibiti wa usalama wa vyombo vya usafiri majini kwa kuzingatia Sheria ya Usalama wa Vyombo vya Majini ya mwaka 2003 na Kanuni zake pamoja na itifaki na mikataba mbalimbali ya Kimataifa iliyoridhiwa na nchi yetu. Katika kutekeleza jukumu hilo, *SUMATRA* ilikagua vyombo vidogo na vikubwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Pwani, Kagera, Kigoma, Mara, Rukwa, Mtwara na Tanga. Jumla ya vyombo vidogo vya usafiri majini (vyenye uzito chini ya tani 50) vipatavyo 4,634 vilikaguliwa katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013 ikilinganishwa na vyombo 2,594 vilivyokaguliwa katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Machi, 2012; kwa ujumla asilimia 36.7 ya vyombo vilivyokaguliwa vilipewa vyeti vya ubora vilivyoruhusu vyombo hivyo kuendelea kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013, idadi ya ajali za majini zilizoripotiwa Tanzania Bara zilikuwa 19 ambapo jumla ya watu 231 waliokolewa na 59 kupoteza maisha ikilinganishwa na ajali 13 zilizoripotiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2011/2012 ambapo watu 574 waliokolewa na 17 kupoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kupunguza ajali za vyombo vya majini, hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kusimamia vyombo vya usafiri majini ili kuhakikisha kuwa ni salama na vimepakia abiria na mizigo katika uzito unaotakiwa kabla ya kuondoka bandarini. *SUMATRA* inaendelea kushirikiana na uongozi wa bandari katika kusimamia usalama. Aidha, *SUMATRA* inaendelea kukamilisha utaratibu wa kuwa na mwakilishi wa usalama katika bandari ndogo na mialo.

Mwakilishi atakayeteuliwa anaweza kuwa ni mmiliki wa bandari ndogo au mwalo, kiongozi wa Serikali ya Mtaa husika au kiongozi wa *Beach Management Unit*.

(ii) Kuhamasisha utamaduni wa usalama kwa watumiaji wa huduma za usafiri wa majini na wavuvi kupitia mikutano, mabango, vipeperushi, matangazo ya radio na televisheni.

(iii) Kuhakikisha taarifa za hali ya hewa zinawafikia waendesha vyombo vya majini kupitia wawakilishi wa usalama.

(iv) Kujenga utamaduni kwa wamiliki wa vyombo kutekeleza sheria bila shuruti kwa kufanya ukaguzi wa kawaida wa vyombo mara moja kwa mwaka na wakati wowote vyombo vinapokuwa kazini.

(v) Kuhakikisha vyombo vinaendeshwa na wafanyakazi wenye sifa kulingana na mitaala ya mafunzo na kusimamia utoaji wa vyeti kwa wafanyakazi hao. Aidha, idadi na sifa za wafanyakazi melini pia hukaguliwa.

(vi) Kuendeleza ushirikiano wa kikazi uliopo kati ya *SUMATRA* na *Zanzibar Maritime Authority (ZMA)* katika ukaguzi wa pamoja na kusimamia sheria na kanuni zilizopo za usalama wa vyombo vya usafiri majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri na uchukuzi majini. Huduma za uchukuzi katika maziwa. Kampuni ya Huduma za Meli (*MSCL*) imeendelea kutoa huduma katika maziwa makuu ya Viktoria, Nyasa na Tanganyika. Changamoto inayoikabili *MSCL* katika utoaji wa huduma ni uchakavu wa meli zake. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeendelea kutenga fedha katika bajeti na kuwasiliana na wahisani mbalimbali ili kukarabati meli hizo. Aidha, Serikali imeendelea kuwasiliana na Serikali ya Shirikisho la Ujerumani ambayo ilikubali kuikarabati meli ya *MV Liemba* kupitia sekta binafsi. Kulingana na makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Ujerumani, Serikali ya Jimbo la Lower Saxony ambako ndiko meli ilikojengwa, Kampuni ya Saruji ya *Twiga Cement* ambao ni wawekezaji kutoka Ujerumani, marafiki wa Liemba na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitachangia ukarabati wa meli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaguzi kutoka Ujerumani walitarajiwa kufanya ukaguzi wa *MV* Liemba kuanzia tarehe 22 - 27 Aprili, 2013. Hata hivyo, ukaguzi huo haukufanyika kutokana na wakaguzi hao kutoa taarifa kuwa kwa tarehe hizo wasingeweza kupatikana kutokana na ratiba zao za kazi; Wakaguzi hao wameahidi kufanya kazi hiyo kuanzia tarehe 22-28 Juni 2013. Madhumuni ya ukaguzi huo ni kujua hali ya meli ilivyo kwa ujumla (mwili, mkuku wa meli, mitambo na sehemu zingine zote) na kubaini gharama za matengenezo zinazohitajika. Tunatarajia kuwa ukarabati wa *MV* Liemba utaanza baada ya ukaguzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya kujenga meli mpya tatu katika maziwa ya Viktoria, Tanganyika na Ziwa Nyasa na ukarabati wa meli za *MV* Viktoria, *MV* Umoja na *MV* Serengeti unaendelea. Serikali ya Denmark imekubali kufadhili mradi huu kwa kutoa mkopo nafuu (*mixed credit funding*) ambao Serikali ya Tanzania itagharamia asilimia 50 na Serikali ya Denmark asilimia 50. Tathmini ya uhifadhi wa mazingira wa mradi huu ilikamilika Aprili, 2013. Mradi huu unatarajiwa kuanza kutekelezwa mwishoni mwa mwaka 2013 na kukamilika mwaka 2018; Mradi huu utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani milioni 60. Aidha, Serikali inawasiliana na Serikali ya Korea Kusini kupitia benki ya *Exim* ili kupata mkopo wenye masharti nafuu wa kujenga meli tatu (3) za abiria na mizigo katika maziwa ya Viktoria, Tanganyika na Nyasa. Lengo la mradi ni kuhakikisha kwamba, ifikapo mwaka 2015 meli hizo ziwe zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, hadi kufikia Desemba, 2012, jumla ya tani za mizigo 124,319 zilisafirishwa ikilinganishwa na lengo la kusafirisha tani 150,000. Hii ni sawa na asilimia 83 ya lengo. Aidha, jumla ya abiria 217,799 walisafirishwa katika kipindi hicho ikilinganishwa na lengo la kusafirisha abiria 355,736. Hii ni sawa na asilimia 61 ya lengo. Aidha, katika mwaka 2013/2014, Kampuni ya Huduma za Meli inategemea kusafirisha jumla ya abiria 316,134 na tani za mizigo 166,846.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Uchukuzi Baharini. Kampuni ya *SINOTASHIP* inayojishughulisha na usafiri wa masafa marefu baharini inamilikiwa kwa ubia na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Watu wa China kwa asilimia 50 kila mmoja. Katika mwaka 2012/2013, Kampuni ilitumia meli yake moja yenye uwezo wa kubeba tani 57,000 kwa wakati mmoja kufanya safari saba badala ya nane zilizopangwa na kusafirisha jumla ya tani 334,000 ikilinganishwa na tani 406,000 zilizosafirishwa katika mwaka 2011/2012. Utekelezaji huo ni pungufu kwa asilimia 17.7. Hii ni kutokana na meli ya Kampuni kufanya safari za masafa marefu zaidi; katika mwaka 2013/2014, Kampuni ya *SINOTASHIP* inatarajia kusafirisha jumla ya tani 350,000 za shehena.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2012/2013, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu utafiti uliokuwa ukifanywa na *SINOTASHIP* kuangalia uwezekano wa kutoa huduma ya usafiri katika maziwa yetu matatu (3) kwa kuanzia na Ziwa Viktoria. Utafiti huo ulianza mwezi Juni 2012 na ulikamilika mwezi Desemba, 2012. Taarifa ya utafiti huo, ambayo inathibitisha uwezekano wa kufanya biashara kwa faida katika Ziwa Viktoria kwa kuanzia, inafanyiwa kazi na uongozi wa *SINOTASHIP* kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za bandari. Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*) iliendelea kuhakikisha kuwa bandari zinakuwa miongoni mwa miundombinu muhimu katika kuchocheo ukuaji wa biashara, uchumi na ustawi wa Taifa. Lengo la kuboresha miundombinu na huduma za bandari ni kuweza kuhudumia shehena ya Tanzania na ya nchi jirani za Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Uganda kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, *TPA* ililenga kuhudumia shehena tani milioni 12.65 yakiwemo makasha 576,300. Katika kipindi cha miezi tisa (Julai, 2012 hadi Machi, 2013), jumla ya tani milioni 9.067 zilihudumiwa, kiasi hiki ni sawa na asilimia 72 ya lengo la mwaka. Shehena iliyohudumiwa katika kipindi cha miezi kumi na miwili yaani kuanzia Aprili, 2012 hadi Machi, 2013 ni jumla ya tani milioni

12.92 ikilinganishwa na tani milioni 11.51 zilizohudumiwa katika kipindi kilichopita cha miezi kumi na miwili, yaani Aprili, 2011 hadi Machi, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Makasha chini ya *TICTS* katika mwaka 2012/2013 kililenga kuhudumia jumla ya makasha 406,300; katika kipindi cha miezi tisa cha kuanzia Julai, 2012 hadi Machi, 2013, Kitengo hicho kilihudumia jumla ya makasha 305,208, sawa na asilimia 75.1 ya lengo kwa mwaka. Makasha yaliyohudumiwa katika kipindi cha miezi kumi na miwili yaani kuanzia Aprili 2012 hadi Machi 2013, ni jumla ya makasha 399,614 ikilinganishwa na makasha 353,267 yaliyohudumiwa katika kipindi kilichopita cha kuanzia Aprili 2011 hadi Machi, 2012. Hili ni ongezeko la makasha 46,347 sawa na asilimia 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya mwaka jana nilitoa taarifa juu ya Wizara kuunda vikosi kazi viwili kikiwemo kile cha kuangalia maeneo ya ushirikiano kati ya bandari, reli na wadau wengine (mfano *TRA*). Lengo la kuanzisha kikosi hicho ni kuharakisha uondoshaji wa mizigo bandarini. Wizara imefanyia kazi mapendekezo ya Taarifa ya Kikosi Kazi hicho na matokeo yake yameanza kuonekana. Muda wa Makasha kukaa bandarini (*Dwell time*) umepungua kutoka wastani wa siku 11.5 mwaka 2011 hadi wastani wa siku 9 mwaka 2012. Aidha, muda wa meli kukaa bandarini (*Ship Turnround Time*) umepungua kutoka wastani wa siku 7.3 mwaka 2011 hadi wastani wa siku 6.3 mwaka 2012. Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013, jumla ya shehena za tani 3,261,209 zilizohudumiwa kwenda na kutoka nchi jirani kupitia bandari ya Dar es Salaam. Hili ni ongezeko la tani 478,445 sawa na asilimia 17 ikilinganishwa na tani 2,782,764 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2011/2012. Ongezeko hilo la shehena limechangiwa kwa kiasi kikubwa na jitihada za *TPA* kwa kushirikiana na wadau wengine kuvutia wateja kutoka nchi jirani kutumia bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa shehena katika bandari za mwambao umeendelea kuwa wa kuridhisha. Katika kipindi cha miezi kumi na miwili yaani kuanzia Aprili, 2012 hadi Machi, 2013, aina ya shehena iliyohudumiwa

ikilinganishwa na kipindi kilichopita cha miezi kumi na miwili yaani kuanzia Aprili, 2011 hadi Machi, 2012 iliendelea kukua katika viwango mbalimbali; ukuaji wa shehena ya makasha ulikuwa asilimia 11.4, mafuta asilimia 11.8, kichele asilimia 14.5 na shehena ya kawaida ikijumuisha magari (*break bulk*) ilikua kwa asilimia 19.3. Kutokana na ongezeko hili, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali iliyoainishwa katika Mpango Kamambe wa Mamlaka (*Ports Master Plan, 2009 – 2028*) ili kuongeza uwezo na ufanisi wa bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, nilitoa taarifa kuhusu utekelezaji wa baadhi ya miradi iliyoainishwa kwa ajili ya kuongeza uwezo wa bandari ya Dar es Salaam kuhudumia shehena. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa boya jipya la mafuta (*SPM*) ambao awamu ya kwanza ya ujenzi ilikamilika Novemba, 2012. Awamu ya pili ya mradi huo inahusu ujenzi wa matanki ya kuhifadhia mafuta ambapo kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza Julai, 2013. Uwezo wa boya jipya ni kuhudumia meli za mafuta zenye uwezo wa kubeba hadi tani 150,000 kwa wakati mmoja. Uwezo huu ni zaidi ya mara tatu ya uwezo wa *KOJ* ambao ni tani 45,000. Kuanza kufanya kazi kwa boya jipya la mafuta kumepunguza msongamano wa meli bandarini, uliokuwa unachangiwa na meli nyingi ndogondogo lakini zenye uwezo mdogo wa kubeba mafuta. Kwa sasa meli yenye tani 100,000 inahudumiwa kwa wastani wa siku sita (6) katika boya jipya (*SPM*), kiasi hiki kama kingehudumiwa na *KOJ* zingetumika meli tatu (3) ambazo zingehudumiwa kwa wastani wa siku 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*) ilipanga kuanza utekelezaji wa mradi wa gati Na. 13 na 14. Kutokana na Kampuni ya *China Construction Communications Company Limited (CCCC)* ya China iliyokuwa inaendelea na mradi huu kufungiwa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma (*PPRA*), Wizara ya Uchukuzi iliwasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kuiomba Serikali ya Watu wa China iteue Kampuni

mbadala ya kuendeleza mradi huu. Desemba, 2012 Kampuni ya *China Harbour Engineering Company Ltd (CHEC)* iliteuliwa na Serikali ya Watu wa China kuendeleza mradi huu. Mazungumzo kati ya *TPA* na *CHEC* kwa ajili ya kukamilisha kazi iliyokuwa imebaki ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina (*study and detail engineering design*) yamekamilika; Kampuni hiyo inatarajiwa kuanza kazi Juni, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine iliyotekelezwa ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu wa kuimarisha na kuongeza kina cha gati Na. 1 hadi 7 katika bandari ya Dar-es-Salaam. Kazi ya upembuzi yakinifu ilianza Mei, 2012 na kukamilika Machi, 2013. Kazi hii iligharamiwa na *Trade Mark East Africa (TMEA)* na Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (*Development Bank of South Africa - DBSA*). Mradi huu ni moja ya miradi ya bandari iliyotangazwa na *TPA* kwa ajili ya kushirikisha sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wake chini ya utaratibu wa *Design, Finance and Build*. Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kituo kikubwa cha kuhifadha mizigo katika eneo la Kisarawe kwa ajili ya mizigo ya kwenda Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Uganda na Rwanda unatarajiwa kukamilika Septemba, 2013. Jumla ya ekari 1,468 zimetengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kwa ajili ya mradi huo. Aidha, taratibu zinakamilishwa ili Bandari Kavu ya Mbeya (*Mbeya Dry Port*) ianze kazi ndani ya mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na juhudi za kupunguza msongamano wa makasha bandarini. Aprili, 2013, *TPA* ilikamilisha ujenzi wa eneo la kuhifadha makasha yanayohudumiwa na kitengo chake ndani ya bandari, lenye ukubwa wa mita za mraba 22,601. Kukamilika kwa mradi huu kumeongeza ufanisi katika kuhudumia shehena ya makasha na magari. Aidha, Septemba, 2012, *TICTS* walikamilisha ujenzi wa reli katika gati Na. 8 na kununua mtambo mkubwa wa kuhudumia makasha (*ship to shore gantry crane*). *TPA* imenunua kreni tatu (3) zenye uwezo wa kubeba tani 100 kila moja kwa ajili ya kuhudumia shehena ya makasha. Hatua hii itapelekea kuongeza ufanisi wa utendaji katika utoaji wa huduma za makasha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, ujenzi wa bandari ya Bagamoyo ni moja ya vipaumbele vya Serikali katika kuendeleza bandari nchini. Ujenzi wa bandari ya Bagamoyo ulipewa kipaumbele katika Mpango Kamambe wa Mamlaka (2009 – 2028) ili kuongeza uwezo wa kuhudumia ongezeko kubwa la shehena inayotarajiwa katika bandari ya Dar-es-Salaam. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uwekezaji (*EPZA*) imetenga ardhi yenye ukubwa wa hekta 1,000 kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo. Tarehe 25 Machi, 2013, Serikali ilisaini makubaliano (*framework agreement*) na Serikali ya Watu wa China kwa ajili ya kuendeleza bandari ya Bagamoyo na eneo lake la *EPZ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bandari ya mwambani, kazi ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa mradi ilikamilika Desemba, 2012. Jumla ya eneo lenye ukubwa wa hekta 174 limenunuliwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo. Lengo la Serikali ni kujenga bandari hii ili itumike katika kusafirisha shehena za Uganda na maeneo mengine inakopita reli ya Tanga - Arusha hadi Musoma. Aidha, Wizara kupitia *TPA* imetangaza mradi huu ili kumpata Mwekezaji kwa ajili ya kuendeleza bandari hiyo kwa mpango wa ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ya Mtwara ni kiungo muhimu katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara na uendelezaji wa shughuli za uwekezaji hasa za uchimbaji wa mafuta, gesi, makaa ya mawe na chuma zinazoendelea katika ukanda huo. Kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Mtwara ilikamilika Oktoba, 2012. Taarifa ya upembuzi yakinifu imependekeza kuwa upanuzi wa bandari ya Mtwara ufanyike kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza itahusu kuendeleza eneo la bandari lenye ukubwa wa hekta 70, ujenzi wa gati nne na uanzishwaji wa bandari huru (*free port zone*) kwa ajili ya kuhudumia shughuli za utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi. Awamu ya pili itahusisha ujenzi wa magati kwa ajili ya kuhudumia mizigo mchanganyiko (*multi purpose bulk terminal*) na uendelezaji wa shughuli za *EPZ* zinazohusiana na bandari; Wizara

inaendelea kutekeleza mapendekezo ya utafiti huu. Kwa sasa, Wizara kupitia *TPA* imetangaza mradi huu ili kumpata Mwekezaji kwa ajili ya ujenzi wa magati manne (4) na uendelezaji wa bandari huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa bandari katika maziwa, Wizara kupitia *TPA* imeendelea kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kushirikiana na Manispaa ya Kigoma - Ujiji kufanya kazi ya uthamini kwa ajili ya kulipa fidia eneo la ujenzi wa gati la Kibirizi. Taarifa ya uthamini inatarajiwa kukamilika Juni, 2013.

(ii) Kazi ya kumpata Mtaalamu Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu wa kuendeleza bandari ya *Mwanza South* inaendelea na inatarajiwa kukamilika Juni, 2013.

(iii) Ujenzi wa gati katika bandari ya Kiwira unaendelea na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2013.

(iv) Ujenzi wa gati katika bandari ya Mafia unaendelea na unatarajiwa kukamilika Juni, 2013.

(v) Ujenzi wa gati katika eneo la Kagunga unaendelea na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine iliyoendelea kutekelezwa katika mwaka 2012/2013 ni pamoja na ujenzi wa magati katika Ziwa Tanganyika maeneo ya Kipili, Karema, Lagosa na Sibwesa. Ujenzi wa magati hayo umeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na matatizo ya kimkataba kati ya Mamlaka ya Bandari na Mkandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi. Mkandarasi huyo ameshindwa kukamilisha miradi kwa wakati kutokana na usimamizi mbovu wa Mamlaka ya Bandari. Uongozi mpya wa Mamlaka ya Bandari umechukua hatua zifuatazo kurekebisha kasoro hizo:-

(i) Kuajiri Mshauri Mwelekezi kupitia upya Mkataba ili kubaini udhaifu katika masharti na taratibu za utekelezaji wa mradi.

(ii) Kufanya mapitio (*review*) ya michoro ya magati hayo manne (4) na kuiboresha pale itakapolazimu.

(iii) Kuwahamisha Wahandisi Ujenzi wawili (2) kutoka Makao Makuu Dar es Salaam kwenda Kigoma kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa miradi katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, TPA imelenga kuhudumia jumla ya tani milioni 13.84 ikijumuisha tani za makasha yatakayohudumiwa katika kitengo cha TICTS. Aidha, bandari itahudumia makasha (TEUs) 635,400. Kati ya makasha hayo, Kitengo cha TICTS kimepanga kuhudumia makasha (TEUs) 430,600 na TPA inatarajia kuhudumia makasha (TEUs) 204,800.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2013/2014 ni pamoja na kuboresha miundombinu ya bandari na maeneo ya kazi kama ifuatavyo: Uboreshaji wa gati Na. 1-7 katika bandari ya Dar es Salaam; kuanza ujenzi wa magati manne (4) katika bandari ya Mtwara; kuanza ujenzi wa awamu ya pili wa SPM, kuanza ujenzi wa gati Na. 13 na 14 katika bandari ya Dar es Salaam; ununuzi wa chelezo (*floating dock*) katika bandari ya Dar es Salaam; kufanya maandalizi ya ujenzi wa bandari ya Bagamoyo; mradi wa kuwaweka pamoja watoa huduma wote (*single window system*); kuweka mfumo wa usalama bandarini (*port integrated security system*); kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya uendelezaji wa kituo cha mizigo cha Kisarawe (Kisarawe *Freight Station*) na ununuzi wa vifaa mbalimbali kwa bandari zote. Serikali kupitia TPA imetenga jumla ya Shilingi bilioni 343.223 kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 137.973 zitatolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari na Shilingi bilioni 205.25 zitatoka kwa wahisani, mikopo yenye riba nafuu na wawekezaji binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri na uchukuzi kwa njia ya anga. Udhhibiti wa usalama wa usafiri wa anga. Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (*TCAA*) imeendelea na jukumu lake la udhibiti wa usalama wa usafiri wa anga hapa nchini. Aidha, Mamlaka imeendelea kutoa huduma ya uongozaji ndege katika anga letu na la nchi za Rwanda na Burundi (kuanzia futi 24,500 kwenda juu). Jukumu la uongozaji ndege katika nchi hizi lilikasimiwa kwa Tanzania na Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga (*ICAO*). Katika mwaka 2012/2013, Mamlaka ilipata cheti cha ubora cha *ISO 9001:2008* na kufanyiwa ukaguzi wa jinsi inavyosimamia sekta ya usafiri wa anga nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukua kwa usafiri wa anga kwa kiasi kikubwa kunachangiwa na kasi ya ukuaji wa pato la Taifa na katika sekta ya utalii. Idadi ya abiria wanaotumia usafiri wa anga kwa safari za ndani na nje ya nchi yetu imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga iliongezeka kutoka abiria 4,034,152 mwaka 2011/2012 hadi kufikia abiria 4,327,977 mwaka 2012/2013, sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Idadi ya abiria waliosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi iliongezeka kutoka abiria 1,873,476 mwaka 2011/2012 na kufikia abiria 2,191,967 mwaka 2012/2013, sawa na ongezeko la asilimia 17. Aidha, idadi ya abiria wa ndani waliosafiri iliongezeka kutoka abiria 2,160,676 mwaka 2011/2012 hadi kufikia abiria 2,506,384 mwaka 2012/2013, sawa na ongezeko la asilimia 16. Kuongezeka kwa idadi ya watumiaji wa huduma za usafiri wa anga kulichangiwa na kuongezeka kwa ushindani hasa baada ya Kampuni ya *Fly 540 (T) Ltd* ambayo inajulikana kama *Fastjet* kuongeza huduma za usafiri, ATCL kurejesha huduma zake na upanuzi wa huduma za safari za ndege kwa Kampuni ya *Precision Air*. Katika mwaka 2013/2014, idadi ya abiria inakadiriwa kuongezeka hadi kufikia abiria 4,847,334, sawa na ongezeko la asilimia 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu safari za ndege nchini (*aircraft movements*), katika mwaka 2012/2013 kulikuwa na safari 240,195 ikilinganishwa na mwaka 2011/2012 ambapo kulikuwa na safari 214,460, hii ni sawa na

16 MEI, 2013

ongezeko la asilimia 12. Safari za Kimataifa zimeendelea kuongezeka kutoka safari 37,088 mwaka 2011/2012 hadi safari 42,280 mwaka huu wa 2012/2013, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10. Ongezeko hili limetokana na mashirika ya ndege ya ndani na nje ya nchi kuongeza safari zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeendelea kuingia mikataba ya usafiri wa anga (*Bilateral Air Services Agreements - BASA*) na nchi mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya soko na hali halisi ya sekta ya uchukuzi wa anga. Aidha, mikataba ya zamani iliboreshwa ili kukidhi matakwa ya soko huria na pia mikataba mipya ilisainiwa. Mikataba hiyo ilihusisha nchi za Ujerumani, Uholanzi na Ethiopia. Katika mwaka 2013/2014, Tanzania inatarajia kuingia mikataba mipya au kupitia upya mikataba iliyopo na nchi tano (5). Nchi hizo ni Sudan ya Kusini, Australia, Italia, Syria na Mauritania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeendelea kuingia makubaliano ya usafiri wa anga na nchi mbalimbali. Katika mwaka 2012/2013, tulikuwa tumesaini makubaliano na nchi arobaini na nane (48) ambapo kati ya makubaliano hayo ni mikataba ishirini na moja (21) tu ambayo kampuni za ndege za nchi husika zinatoa huduma kuja Tanzania. Mwaka 2012/2013 tulikuwa na safari za ndege 196 kwa wiki na katika mwaka 2013/2014, tunatarajia kuwa na safari za ndege 210 kwa wiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeweka mikakati mbalimbali ili kukuza sekta ya usafiri wa anga. Mikakati hiyo ni pamoja na kuruhusu safari mpya za ndege kutoka nchi husika kuwa kati ya safari kumi na nne (14) hadi arobaini na mbili (42) kwa wiki kutegemeana na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, jumla ya Kampuni za ndege 16 mpya zilisajiliwa. Aidha, kampuni za ndege 12 zilipewa leseni mpya na hivyo kufanya jumla ya kampuni za ndege zilizosajiliwa nchini ili kutoa huduma ya usafiri wa ndege ndani na nje ya nchi kuwa 54.

Katika mwaka 2013/2014, tunatarajia kutoa leseni mpya sita (6) za kampuni za ndege na hivyo kufanya idadi ya makampuni yenye leseni kufikia 60. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za uongozaji ndege katika kiwanja kipya cha ndege cha Songwe kilichopo Mkoani Mbeya zilianza kutolewa kuanzia tarehe 13 Desemba, 2012 hii ni baada ya kufunga redio za mawasiliano na mtambo wa kuongozea ndege zinazotua (*Non Directional Beacon - NDB*) eneo la Iwambi, Mbeya. Kazi ya ukamilishaji wa mifumo na ramani ya taratibu za utuaji wa ndege kwa ajili ya matumizi ya marubani (*Instrument Approach Procedure*) kwa viwanja vya ndege vya Arusha na Songwe zinaendelea na zitakamilika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeboresha mawasiliano kati ya waongoza ndege na marubani kutoka kiwango cha asilimia 85 katika mwaka 2011/2012 hadi asilimia 95 katika mwaka 2012/2013. Kituo kipya (*VHF area cover relay station*) cha kuboresha mawasiliano kati ya waongoza ndege na marubani kimefungwa Moroninya, Kasulu mkoani Kigoma ili kuimarisha mawasiliano na ndege zinazoruka katika eneo la Magharibi ya Tanzania. Katika mwaka 2013/2014, mtambo kama huo unatarajiwa kufungwa Mkoani Tanga eneo la Mnyusi, ili kuimarisha mawasiliano na ndege katika kanda ya Mashariki na juu ya eneo la Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, niliahidi kuwa Wizara itaoanisha mfumo wa upashanaji habari wa safari za ndege uliopo na mifumo ya Kimataifa ya safari za ndege (*ICAO new flight plan*). Napenda kutoa taarifa kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga ilikamilisha kazi ya kuoanisha mfumo huo na ile ya Kimataifa ya upashanaji habari wa safari za ndege ilipofika tarehe 15 Novemba, 2012. Hii ilikuwa tarehe iliyopangwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*ICAO*) kwa nchi zote duniani kukamilisha utaratibu huu mpya. Hatua hii imeifanya Tanzania kuwa moja ya nchi zilizotekeleza

mpango huu kwa wakati na hivyo kuiletea heshima nchi yetu katika nyanja za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa anga duniani unasimamiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*ICAO*) ambalo lina wanachama 191. Shughuli za *ICAO* husimamiwa na Baraza Kuu (*ICAO Council*) lenye wajumbe kutoka nchi 36. Serikali imeamua kuwa katika Mkutano Mkuu ujao wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*ICAO Assembly*) utakaofanyika huko *Montreal*, Canada mwezi Septemba, 2013, Tanzania igombe nafasi ya kuingia kwenye Baraza Kuu. Tunashukuru kuwa nchi za *SADC* na nyingine barani Afrika zimeahidi kutuunga mkono wakati wa uchaguzi. Nchi za *SADC* zilituunga mkono tangu mwaka 2012 na katika mkutano wake uliofanyika Aprili, 2013, Accra, Ghana, Kamisheni ya Afrika ya Usafiri wa Anga (*Africa Civil Aviation Commission*) pia imetamka kutuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya ajali za ndege imepungua kutoka ajali mbili (2) mwaka 2011/2012 hadi ajali moja (1) mwaka 2012/2013. Ajali hiyo ilitokea mwezi Aprili, 2013 huko Arusha kwa kuhusisha ndege ndogo aina ya Maule. Katika ajali hiyo, mtu mmoja ambaye ni rubani alipoteza maisha na ndege kuharibika. Aidha, katika mwaka 2012/2013 idadi ya matukio (*incidents*) ilifikia 12 katika miruko ya ndege (*air traffic movements*) 179,543.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa anga imeanza kazi ya kuboresha mtandao wa utoaji na upashanaji habari wa safari za ndege. Mradi huu unahusu kuhama kutoka katika mfumo wa sasa wa analogia katika kuunganisha viwanja vya ndege (*aeronautical Fixed Telecommunication Network-AFTN*) kwenda mfumo wa digitali wa mawasiliano (ATS Message Handling System (*AMHS*)). Utekelezaji wa mradi huu utakamilika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za viwanja vya ndege. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*) iliendelea kusimamia,

kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege nchini kwa kuzingatia miongozo na kanuni za Kitaifa na Kimataifa. Mamlaka imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege vya Mafia, Tabora, Kigoma, Bukoba na Mwanza. Katika kipindi hicho, mawe ya msingi yaliwekwa kwenye viwanja vya ndege vya Tabora na Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 13 Desemba, 2012, kiwanja kipya cha ndege cha Kimataifa cha Songwe kilianza kutoa huduma za safari za ndege za abiria za ratiba (*scheduled flights*). Aidha, Mkatoba wa ujenzi wa Jengo jipya la Tatu la Abiria (*terminal 3*) katika Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere ulisainiwa tarehe 18 Aprili, 2013 na ujenzi unatarajiwa kukamilika Novemba, 2015. Kukamilika kwa miradi hii kutachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa huduma za usafiri wa anga nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, mnamo tarehe 13 Desemba, 2012 kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Songwe kilianza rasmi kutoa huduma za uendeshaji wa ndege. Kuanzia tarehe 16 Januari, 2013 Kampuni ya ndege ya *Precision* ilianzisha safari kati ya Dar es Salaam na Mbeya. Safari hizi za ndege ni za kila siku na wananchi wa Mbeya na mikoa ya jirani sasa wanafurahia kwani wanatumia muda wa dakika 90 tu kusafiri kwenda/kutoka Dar es Salaam hadi Songwe. Hadi kufikia mwishoni mwa Aprili, 2013, jumla ya abiria 12,201 walisafirishwa kupitia Kiwanja cha ndege cha Songwe. Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea na taratibu za upatikanaji wa uhakika wa huduma ya mafuta ya ndege. inatarajiwa kwamba, taratibu hizo zitakamilika ifikapo Juni, 2013. Pamoja na kiwanja hiki kuanza kutoa huduma za safari za ndege, kazi za ujenzi wa maegesho ya ndege (*apron*) zimekamili kwa asilimia 60 na ni matarajio yetu kuwa zitakamilika ifikapo Juni, 2013. Ujenzi wa majengo mengine ya abiria na uzio kuzunguka maeneo yote ya uendeshaji wa kiwanja zinategemea kukamilika mwishoni mwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeendelea kukamilisha awamu ya kwanza ya kazi za uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Tabora na Kigoma. Kazi za ujenzi wa matabaka yote ya lami katika viwanja vya Tabora na Kigoma imekamilika. Kwa sasa kazi zinazoendelea ni ukamilishaji wa ujenzi wa mfumo wa maji ya mvua, upakaji rangi kwenye barabara ya kuruka na kutua ndege (*runway*) na uimarishaji wa sehemu za kiusalama katika viwanja hivyo. Aidha, kazi za ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Bukoba kwa kiwango cha lami zinaendelea na ni matarajio yetu kwamba zitakamilika katika mwaka wa fedha wa 2013/2014. Kazi zinazofanyika katika kiwanja hicho ni ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege (*runway*), barabara za viungio (*taxiways*) na maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami, ujenzi wa jengo la abiria na usimikaji wa taa za kuongozea ndege kutua na kuruka usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanikiwa kupata mkopo kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), kiasi cha *Euro* milioni 50 zaidi ya Shilingi bilioni 100. Fedha hizo zitatumika kuendelea na awamu ya pili ya ukarabati na uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Kigoma na Tabora. Mkopo huu pia utatumika kukarabati miundombinu ya viwanja vya ndege vya Shinyanga na Sumbawanga kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine itahusu ujenzi wa majengo mapya ya abiria na usimikaji wa taa za kuongoza ndege kutua na kuruka usiku. Kukamilika kwa awamu hii ya pili kutawezesha viwanja hivyo kuwa vya kisasa na kutumika kwa saa 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepata nyongeza ya mkopo kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 26 kutoka Benki ya Dunia. Fedha hizi zitatumika kurefusha barabara ya kutua na kurukia ndege katika kiwanja cha ndege cha Kigoma kutoka urefu wa mita 1,800 hadi kufikia mita 3,100 na hivyo kuwezesha ndege kubwa za abiria zaidi ya 150 kutua na kuruka. Tayari Serikali imeshalipa fidia za mali kwa eneo litakalohusika na upanuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Mafia kwa kiwango cha lami zinaendelea ambapo tabaka la kwanza la lami (*binder course*) limekamilika. Kwa ujumla kazi za upanuzi wa kiwanja hiki zimekamilika kwa asilimia themanini (80%). Mradi huu unagharamiwa na Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Changamoto za Millenia (*MCC*). Tunatarajia kwamba kazi hizi zitakamilika ifikapo Juni, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuboresha viwanja vya ndege nchini, Serikali imepata mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 2.0 sawa na Shilingi bilioni 3.2 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa viwanja kumi na mbili (12). Viwanja hivyo ni Iringa, Kilwa Masoko, Lake Manyara, Moshi, Musoma, Lindi, Njombe, Songea, Singida, Ngungungu (Mkoa wa Manyara), Bariadi (Mkoani Simiyu) na Tanga. Baada ya hatua hii, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kazi ya ukarabati na upanuzi wa viwanja hivyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeendelea kuboresha ulinzi na usalama kwa viwanja vya ndege nchini. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka ilinunua vifaa maalum vya ukaguzi wa abiria na mizigo (*x-ray machines*) kwa viwanja vya ndege vya *JNIA*, Mwanza, Arusha, Songwe na Mpanda. Mamlaka imeagiza gari jipya la zimamoto kwa ajili ya kuimarisha usalama katika kiwanja cha Songwe na kununua vifaa mbalimbali vya zimamoto na uokoaji katika viwanja vingine ili kuzingatia viwango vinavyowekwa na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (*ICAO*). Vilevile, mipango ya usalama wa viwanja vya ndege ilihuishwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za usalama wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya viwanja vya ndege ikiwemo:

16 MEI, 2013

(i) Kuimarisha na kuboresha Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (*JNIA*) kwa kujenga jengo jipya la abiria na majengo mengine ya huduma za ndege ambapo Shilingi bilioni 89 zimetengwa na Serikali;

(ii) Kukamilisha ujenzi wa kiwanja kipya cha Kimataifa cha Ndege cha Songwe (Mbeya) ambapo Shilingi bilioni 8.5 zimetengwa;

(iii) Kuendelea na uboreshaji wa kiwanja cha ndege cha Mwanza ambapo Shilingi bilioni 11.483 zimetengwa;

(iv) Kukamilisha ukarabati wa Kiwanja cha ndege cha Bukoba ambapo Shilingi bilioni 11.297 zimetengwa;

(v) Kukamilisha ukarabati wa Kiwanja cha ndege cha Kigoma ambapo Shilingi bilioni 31.3. zimetengwa;

(vi) Kukamilisha ukarabati wa Kiwanja cha ndege cha Tabora ambapo Shilingi bilioni 15.6 zimetengwa;

(vii) Kuanza ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Shinyanga ambapo Shilingi bilioni 17.34 zimetengwa;

(viii) Kuanza ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Sumbawanga ambapo Shilingi bilioni 13.3 zimetengwa; na ix. Ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mtwara ambapo Shilingi milioni 500 zimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaendelea kufanyia matengenezo viwanja vingine vya ndege na kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia mapato yake ya ndani ili kuboresha utoaji wa huduma. Hii ni pamoja na ufungaji wa mitambo ya umeme wa dharura katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Mafia na Mtwara; kuweka madaraja mapya ya kupandia na kushuka abiria (*aerobridges*) katika kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere, kuboresha mitambo na mfumo wa kufuatilia mienendo ya shughuli za usalama na uendeshaji wa kiwanja (*CCTV*) kwa

kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere, kufanya ukarabati na upanuzi wa jengo la II la abiria kwa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere na kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuwaongezea ujuzi na weledi katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuendelea kutekeleza majukumu yake, TAA inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Kutokuwa na miundombinu yenye ubora wa kuwezesha ndege kutua na kuruka salama katika viwanja vya ndege vya mikoa na hivyo kufanya mashirika ya ndege kushindwa kufika katika mikoa hiyo;

(ii) Kutokuwapo kwa taa za kuruhusu ndege kutumia viwanja kwa saa ishirini na nne (24) na hivyo kufanya mashirika ya ndege kutotumia ndege zao kwa ufanisi; na

(iii) Kutokuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege ambavyo havizalishi (*public service obligation*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Kampuni ya KADCO inayosimamia uendeshaji wa shughuli za uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) katika juhudi zake za kuboresha na kuongeza biashara katika uwanja huo ilifanikiwa kuyashawishi mashirika ya ndege makubwa matatu (3) kuanza kutumia uwanja wa KIA kutoa huduma zake. Mashirika hayo ni Kenya Airways (Julai, 2012), Qatar Airways (Julai, 2012) na Turkish Airline (Desemba, 2012) ambayo yamepelekea kuongezeka kwa idadi ya abiria kufikia 665,147 mwaka 2012 ikilinganishwa na abiria 641,167 waliohudumiwa mwaka 2011. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 3.7. Ongezeko hili pia lilichangiwa na Kampuni ya Fly 540 (T) Ltd kuanza kutoa huduma zake katika uwanja wa KIA mwishoni mwa Novemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, KADCO itaendelea na maandalizi ya mradi mkubwa wa

ukarabati wa uwanja unaokadiriwa kugharimu Euro milioni 35. Mradi huu utahusisha ukarabati na upanuzi wa maeneo ya maegesho ya ndege (*aprons*), ukarabati wa njia za viungio (*taxiways*), ukarabati wa jengo la abiria (*terminal building*), ukarabati wa sehemu ya njia ya kurukia na kutua ndege (*runway*) na ujenzi wa mfumo mpya wa maji taka. Mradi huu utakapokamilika utaongeza uwezo wa *KIA* kuhudumia ndege nyingi na kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za usafiri wa ndege. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Serikali iliendelea na juhudi za kuiboresha Kampuni ya Ndege Tanzania. Juhudi hizo ni pamoja na kufanya mazungumzo na mashirika ya ndege ya Kimataifa kutoka Dubai, Uturuki, Misri, China na Urusi, kwa lengo la kuingia nayo ubia. Lengo la majadiliano hayo ni kushawishi kampuni hizo kuwekeza katika *ATCL* kwa ubia. Aidha, Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi za fedha za ndani ya nchi inaendelea na majadiliano kuhusu kuboresha Shirika hili kwa kuzishirikisha Taasisi za Umma na baadaye sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, *ATCL* iliendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga katika maeneo ya Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Kigoma na Moroni nchini Comoro. Safari za Dar es Salaam - Kigoma kwa kutumia ndege aina ya Dash-8 zilianza tarehe 11 Januari, 2013; Dar es Salaam - Mtwara zilianza tarehe 8 Februari, 2013 na zile za kwenda Comoro kwa kutumia ndege aina ya *Boeing 737-200* zilirejeshwa Februari, 2013 baada ya kusimama tangu Agosti, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013, idadi ya abiria waliosafirishwa na *ATCL* ilikuwa 23,030 ikilinganishwa na abiria 8,342 waliosafirishwa katika mwaka 2011/2012. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 176. Ongezeko hili limetokana na kutosimamisha safari, kufunguliwa kwa kiwanja cha ndege cha Kigoma, kufanyiwa matengenezo ndege aina ya *Dash-8* na kuanzishwa kwa safari za Mtwara zilizokuwa zimesimama. Aidha, *ATCL* imeboresha hanga lake lililopo *JNIA* na hivyo kufanya

matengenezo ya ndege zake hapa nchini. Pia, katika jitihada za kupunguza matumizi, tangu Desemba, 2012, Kampuni inatoa huduma za uwanjani kwa ndege zake (*self ground handling*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, ATCL itaendelea kuboresha usalama na ulinzi wa usafiri wa anga katika ndege zake; kuanza safari za kwenda Afrika Kusini, Bujumbura, Mombasa, Songwe; pia kurejesha safari za Mwanza, Tabora, Arusha na Zanzibar. Kazi nyingine inayotarajiwa kutekelezwa na ATCL katika mwaka 2013/2014 ni kurejesha uanachama katika Chama cha Usafirishaji wa Anga Kimataifa (*IATA*) na kukarabati jengo la ATC (*ATC House*) ili kuchangia katika mapato ya Kampuni. Katika mwaka 2013/2014 huduma za ATCL zitaendelea kutolewa kwa kutumia ndege yake aina ya Dash 8-Q300. Aidha, Serikali inaangalia uwezekano wa kununua kwa mkopo (*lease purchase*) ndege moja (1) mpya ya abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wakala wa Ndege za Serikali (*TGFA*) umeendelea kutoa huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wakala huo umekuwa ukitumia ndege zake nne (4) katika kutekeleza jukumu hilo. Aidha, katika kuhakikisha kuwa ndege hizo zinakuwa salama wakati wote, Wakala ulifanya matengenezo makubwa na ya kawaida hapa nchini na nje ya nchi. Katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia *TGFA* itaendelea kuzifanyia matengenezo ndege zake kwa kufuata ratiba ya matengenezo ya ndege hizo ili kuhakikisha usalama wake. Aidha, Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa marubani na wahandisi ili kuhuisha leseni zao za kuhudumia ndege hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za hali ya hewa. Huduma za hali ya hewa zimeendelea kuboreshwa ili zifikie matarajio ya watumiaji wa huduma hizo. Katika mwaka 2012/2013, Mamlaka ya Hali ya Hewa (*TMA*) kwa kushirikiana na Kampuni ya Simu ya *Vodacom* imeanza kutoa huduma za hali ya hewa kupitia ujumbe wa simu za mkononi (*sms*).

Mazungumzo kati ya Mamlaka na Kampuni ya *Tigo* kwa ajili ya kuanza kutoa huduma za hali ya hewa kwa wakulima yanaendelea. Zoezi hili litasogeza huduma za hali ya hewa kwa watumiaji na kuwa na uhakika wa kupata huduma wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Mamlaka ilianza kutoa huduma za hali ya hewa katika kiwanja kipya cha ndege cha Kimataifa cha Songwe, kufunga mtambo wa kuchambua data na taarifa za hali ya hewa (*computer cluster*) katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (*JNIA*) na ufungaji wa mitambo saba ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe (*automatic weather stations*) umekamilika. Taratibu za ununuzi wa mitambo mingine saba (7) ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ilifanyiwa tena ukaguzi wa Kimataifa kwa utoaji wa huduma bora za hali ya hewa kwa ajili ya usafiri wa Anga mnamo Desemba, 2012 na kuthibitishwa tena kuendelea kukimiliki Cheti cha ISO 9001:2008. Aidha, maandalizi ya ufungaji wa rada ya hali ya hewa ya pili Mkoani Mwanza yanaendelea. Mkataba wa kutengeneza rada hiyo ulisainiwa Aprili, 2012 na katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Serikali imelipa asilimia 90 ya malipo ya uundaji wa rada hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, *TMA* itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake ili kuwaongezea uwezo wa kutoa huduma bora. Aidha, *TMA* itaanza kufanya upembuzi yakinifu na kuanza ujenzi wa Kituo Kikuu cha Utabiri (*central forecasting office*) kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa taarifa za huduma za utabiri wa hali ya hewa kwa uhakika na kwa wakati ili kuepukana na madhara yatokanayo na hali mbaya ya hewa. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa kitaanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Hali ya Hewa (*BSc. Met*). Kuanzishwa kwa mafunzo hayo hapa nchini kutaipunguzia Serikali gharama ya kusomesha wataalamu wa hali ya hewa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki katika Jumuiya mbalimbali. Katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kushiriki katika mikutano, semina, kongamano na warsha mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa. Mikutano hiyo ilifanyika kwa lengo mahsusi la kukuza mashirikiano ili kuendeleza miundombinu ya uchukuzi na huduma zake. Mikutano hiyo ni pamoja na ile ya ushirikiano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*) na Maziwa Makuu (*great lakes*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano wa SMT na SMZ, Wizara imeendelea kufanya vikao vya mara kwa mara katika ngazi ya Mawaziri na Watendaji wa Wizara ya Uchukuzi (SMT) na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano (SMZ). Aidha, tumekuwa tukishiriki pamoja katika mikutano mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa inayohusu sekta ya uchukuzi na hali ya hewa. Tutaendelea kukutana mara kwa mara ili kuondoa kero mbalimbali katika sekta ya uchukuzi na hali ya hewa. Namshukuru sana Mheshimiwa Hamad Masoud Hamad, Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – SMZ kwa ushirikiano anaoendelea kunipa katika kutekeleza jukumu hilo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia taasisi zake zinazosimamia usafiri wa majini zimeendelea kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuimarisha usalama wa usafiri majini. Aidha, vyombo vya udhibiti na usimamizi wa usafiri majini yaani *SUMATRA* na Mamlaka ya Bahari Zanzibar (*Zanzibar Maritime Authority-ZMA*) vimeendelea kushirikiana katika masuala yanayohusu ukaguzi na uhakiki wa ubora wa vyombo vya usafiri majini, taratibu za utafutaji na uokoaji na kubadilishana taarifa muhimu. Taasisi hizo zimekubaliana kuwa na Hadidu za Rejea za pamoja kwa ajili ya ukaguzi wa vyombo vya usafiri majini utakaofanywa na mawakala wa Mamlaka hizi; kuwianisha kanuni za ukaguzi wa vyombo na kufanya kaguzi za pamoja zilizopangwa na za kushtukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*EAC*). Wizara imeendelea kushiriki kwenye miradi ya pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika sekta ya uchukuzi wa nchi kavu, majini, anga na hali ya hewa. Katika sekta ya usafiri wa anga, nchi wanachama zinaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Uwekezaji na Ufadhili wa Viwanja vya Ndege vya Kipaumbele katika nchi Wanachama kwa lengo la kuvutia utalii. Hadidu za Rejea za kufanya utafiti wa kuandaa mkakati imekamilika. Tanzania imependekeza viwanja tisa (9) vya Arusha, *Lake Manyara*, Loliondo, Mafia, Kilwa, Iringa, Mpanda, Kigoma na Pemba kuingizwa katika mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea kuandaa Mkakati wa Uendelezaji wa Usafiri Majini chini ya ufadhili wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA*). Mkakati huo utainisha vipaumbele vya miradi ya uendelezaji wa Usafiri Majini na Bandari katika Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili ya mradi wa utunzaji na Usimamizi wa Mazingira katika Bonde la Ziwa Viktoria unaendelea kutekelezwa. Awamu ya kwanza ya Mradi huo ilitokelezwa katika nchi za Kenya, Uganda na Tanzania kuanzia mwaka 1997 hadi 2005 kwa kufanya utafiti wenye lengo la kubaini hali halisi ya uharibifu wa mazingira na hali ya maisha ya jamii inayozunguka Ziwa Viktoria. Matokeo ya utafiti huo yaliibua programu ya kudhibiti uharibifu mkubwa wa mazingira katika Ziwa Viktoria ili kurejesha mazingira ya ziwa hilo katika hali yake ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchukuzi na usafirishaji wa mizigo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi za Tanzania, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Uganda kwa umoja wao zilianzisha Wakala wa Uwezesaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati (*Transit Transport Facilitation Agency - TTFa*) Agosti, 2009. Lengo likiwa ni kuratibu shughuli za uchukuzi na usafirishaji wa mizigo inayopitia Bandari ya Dar es salaam ili kuongeza ufanisi na kiwango cha mizigo, kupunguza muda

wa usafirishaji na kuongeza usalama wa mizigo inayosafirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta ufanisi katika kufikia malengo, Wakala wa *TIFA* unatayarisha takwimu muhimu za ufanisi kama vile usimamaji wa magari ya mizigo njiani, muda wa kusimama katika vituo na idadi ya vituo. Wakala umekamilisha kazi ya kutengeneza *transport observatory software* itakayorekodi mwenendo wa gari kupitia teknolojia ya *Global Positioning System (GPS)* na baadaye kutoa takwimu mbalimbali kuhusu utendaji. Warsha ya kuwahamasisha wadau kutoa taarifa zao ilifanyika Oktoba, 2012 nchini Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki katika Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*). Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya uoanishaji wa viwango na mifumo ya Sekta ya Uchukuzi kwa njia ya barabara, reli, anga, majini na hali ya hewa kwa kuzingatia makubaliano ya Itifaki ya Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa. Aidha, nchi wanachama zinaendelea na maandalizi ya kuwa na mikakati ya pamoja ya uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi hususan miradi ya barabara, reli, viwanja vya ndege na bandari itakayoweza kupunguza gharama za usafirishaji na pia kuunganisha nchi yetu na nchi zingine wanachama wa *SADC*. Lengo kuu likiwa ni kuibua fursa za uwekezaji na uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maendeleo kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya nchi wanachama wa *SADC* kupitisha Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa Miundombinu (*Regional Infrastructure Development Master Plan – RIDMP*) Agosti, 2012 mikakati mbalimbali imeandaliwa kwa ajili ya kuuza miradi iliyoko kwenye mpango huo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuandaliwa kwa Mkutano wa wawekezaji uliofanyika tarehe 13 Machi, 2013 nchini Uingereza. Miradi ya Tanzania iliyowasilishwa katika Mkutano huo ni Ujenzi wa Reli ya DSM – Isaka Kigali/Keza – Musongati, Mpango wa Uboreshaji wa Reli ya Kati (*Revival of TRL*), Ujenzi wa Reli ya Mtwara –

16 MEI, 2013

Mchuchuma/Liganga na Ujenzi wa Kituo cha Shehena eneo la Kisarawe (Kisarawe *Freight Station*). Ni matarajio yetu kuwa wawekezaji watajitokeza ili kuwekeza katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo na mafunzo ya watumishi. Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi wake katika nyanja za kitaaluma na kijamii kwa kutambua umuhimu wa kuwa na wafanyakazi wenye weledi na ufanisi katika utendaji kazi. Katika kutimiza azma hiyo, mwaka 2012/2013, Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake zimegharimia mafunzo ya jumla ya watumishi 812. Kati ya hao, watumishi 240 walipatiwa mafunzo nje ya nchi na watumishi 572 walipatiwa mafunzo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwaongezea watumishi wake ujuzi, ufanisi na tija katika utendaji kazi, katika mwaka 2013/2014, Wizara pamoja na Taasisi zake zitaendelea kugharamia mafunzo ya watumishi kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, kwa kuzingatia Mipango ya Mafunzo, Wizara inakusudia kuwapeleka kwenye mafunzo wafanyakazi 850 ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za mafunzo. Wizara inathamini mchango unaotolewa na vyuo vyetu vya mafunzo katika kukuza na kuendeleza taaluma na wanataaluma wa sekta ya uchukuzi na hali ya hewa nchini. Wizara imeendelea kuvihudumia vyuo vilivyo chini yake kulingana na uwezo wa kifedha. Vyuo hivyo ni Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (*NIT*), Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Chuo cha Hali ya Hewa - Kigoma, Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam, Chuo cha Bandari Dar es Salaam na Chuo cha Reli Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji. Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kilipata ithibati kamili kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*) katika ngazi ya Nane (*NTA level 8*) ya Muundo wa Tuzo mwaka 2008/2009. Hatua hii ilikiwezesha Chuo kuanza kutoa taaluma katika ngazi ya Shahada ya Kwanza na kufuta utoaji wa taaluma katika ngazi ya Stashahada ya Juu. Chuo

kimeendelea kutimiza majukumu yake ya kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi katika sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Chuo kimeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wake wa miaka mitano (2011/2012–2015/2016). Hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza Mpango huu ni pamoja na kupanua wigo wa programu za mafunzo ya muda mrefu ili kuweza kutoa mafunzo katika sekta ndogo za uchukuzi na usafirishaji. Mafunzo haya yanagusa maeneo ya usafiri wa majini, barabara, reli, anga na mfumo wa usafiri kwa njia ya mabomba. Katika kipindi hiki, Chuo kimeendesha jumla ya programu 21 ikilinganishwa na programu 14 zilizotolewa katika mwaka 2011/2012. Hili ni ongezeko la programu saba sawa na asilimia 50. Ongezeko la programu limekwenda sambamba na ongezeko la udahili wa wanafunzi. Jumla ya wanafunzi 945 walidahiliwa katika mwaka 2012/2013 ikilinganishwa na wanafunzi 393 waliidahiliwa katika mwaka 2011/2012. Hili ni ongezeko la wanafunzi 552 sawa na asilimia 140. Katika mwaka 2013/2014, Chuo kimepanga kuongeza udahili kwa asilimia 27 kufikia wanafunzi 1,200.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uchukuzi wa barabara inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo uwepo wa magari chakavu barabarani, ajali za barabarani, msongamano wa magari mijini pamoja na uchafuzi wa mazingira. Katika kukabiliana na changamoto hizi, Chuo kiliendesha jumla ya kozi fupi 12 zilizoshirikisha washiriki 8,872 kuhusu matumizi ya vyombo vya moto barabarani. Aidha, Kampuni ya *British Gas* ilidhamini mafunzo ya uendeshaji pikipiki na usalama barabarani kwa wanafunzi wa shule za msingi mkoani Mtwara. Jumla ya waendesha pikipiki 600 na wanafunzi 14,611 kutoka shule 30 walishiriki katika mafunzo hayo. Madhumuni ya kozi hizo ni kupata wataalamu waliobobea na kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kujipanua na kusogeza huduma zake Mikoani, Chuo kimefungua vituo vyake katika Mikoa ya Mbeya, Arusha, Dodoma, Mwanza na

Kigoma. Katika mwaka 2013/2014, Chuo kwa kutumia vituo hivyo, kitatoa mafunzo kwa waendesha pikipiki 2,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya usafiri wa anga inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa wataalamu. Kwa kulitambua hilo, katika mwaka 2012/2013, *NIT* imeanzisha programu mpya ya Stashahada ya Uzamili katika Menejimenti ya Usafiri wa Anga na mafunzo ya ufundi wa ndege na utoaji huduma ndani ya ndege. Aidha, Chuo kinatarajia kuanza kutumia viwanja vya ndege vya Dodoma na Tanga kwa ajili ya mafunzo ya marubani wa ndege. Maandalizi ya mafunzo hayo yanaendelea ambapo kwa sasa mitaala imekamilika na inasubiri ithibati kutoka kwenye mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Chuo kinatarajia kuanzisha programu ya Stashahada ya Uzamili katika Uhandisi wa Usafirishaji (*Postgraduate Diploma in Transportation Engineering*). Lengo ni kuwa na wataalamu wa kutosha katika sekta ndogo za bandari, viwanja vya ndege, reli na usafirishaji kwa njia ya mabomba. Kazi nyingine inayotarajiwa kutekelezwa ni kukarabati majengo ya Chuo ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam. Mafunzo ya uongozaji ndege, ufundi wa mitambo ya kuongozea ndege, utoaji taarifa na usalama na upekuzi wa ndege (*aviation security*) yameendelea kutolewa nchini na Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam. Katika mwaka 2012/2013, jumla ya wanafunzi 551 walihitimu mafunzo yao katika Chuo. Kati ya wahitimu hao, wahitimu 500 ni kutoka Tanzania na wahitimu 51 ni kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na mwaka 2011/2012 ambapo wanafunzi 146 walihitimu mafunzo. Kati ya hao, wanafunzi 117 ni Watanzania na 29 ni kutoka nje ya nchi. Aidha, Chuo kimekamilisha taratibu za usajili na kinatarajiwa kupata usajili wa kudumu kutoka *NACTE* Juni, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Chuo kitaendelea na juhudi za kupata eneo la kutosha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo kipya. Aidha, Chuo kitaendelea kuhakikisha kwamba viwango vya mafunzo vinaendelea

kuboreshwa ili kukidhi matakwa ya Kitaifa na Kimataifa. Lengo ni kukiwezesha Chuo kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali za usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI). Chuo cha Bahari Dar es Salaam kimeendelea kutoa huduma za mafunzo, utafiti, ukarabati wa vifaa vya kuokolea maisha na uwakala wa ajira kwa wafanyakazi melini. Mafunzo yaliyotolewa yalilenga katika kuendeleza rasilimali watu katika sekta ya usafiri majini. Katika mwaka 2012/2013, Chuo kilidahili wanafunzi 7,510 wa kozi fupi, wanafunzi 165 wa diploma ya uendeshaji meli, wanafunzi 95 maafisa waendesha meli na wahandisi na wanafunzi 234 wa diploma ya miundombinu ya upokeaji na utoaji wa mizigo bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kimeendelea kukuza taaluma ya watumishi kwa kuwapeleka kwenye mafunzo walimu wanne (4) ili kuhuisha vyeti vya wataalam hao katika ukarabati wa maboja ya meli. Aidha, kupitia ushirikiano kati ya Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Usafiri majini cha *Dalian* cha China, *DMI* imepata ufadhili wa Dola za Kimarekani milioni 20 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa tawi la Chuo Kikuu cha *Dalian Maritime University (DMU)* hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara imetenga fedha Shilingi bilioni 2.87 katika bajeti yake kwa ajili ya kuchangia gharama za ujenzi wa tawi la *DMU* ndani ya *DMI* kwa madhumuni ya kuboresha miundombinu ya madarasa, maabara, karakana, ofisi za waalimu pamoja na kuandaa eneo patakapojengwa kituo kwa ajili ya mafunzo ya nidhamu na ukakamavu (*cadetship training*) Wilayani Mkuranga. Aidha, Wizara itaendelea kutenga fedha na kukisimamia Chuo cha *DMI* ili kuhakikisha kinaendelea kutunza sifa za ubora za *IMO*, *NACTE*, *SUMATRA* na Jumuiya ya Afrika Mashariki zilizotolewa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma. Katika mwaka 2012/2013, Chuo cha Hali ya Hewa

Kigoma kiliendelea kutekeleza majukumu yake licha ya kukabiliiana na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa bajeti na uhaba wa vifaa vya kisasa vya kufundishia. Mikakati iliyopo ya kukabiliiana na changamoto hizo ni pamoja na kununua mitambo, vifaa na kuendeleza mpango wa kufundisha wataalam wapya na waliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Chuo kilipatiwa vitendea kazi mbalimbali vikiwemo kompyuta 16 na mashine moja (1) ya kudurufu (*photocopier machine*). Aidha, Wanafunzi 28 wa mafunzo ya kati walihitimu masomo yao Desemba, 2012. Kati yao wanawake ni saba (7) na wanaume ni 21. Wahitimu hao wamepangiwa kazi katika vituo mbalimbali vya hali ya hewa hapa nchini. Kuhusu mafunzo ya awali, jumla ya wanafunzi 39 wamehitimu mafunzo Machi, 2013. Kati ya hao wanawake ni wanne (4) na wanaume 35. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kujenga uwezo wa Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma kwa kujenga mabweni na uzio na kukamilisha taratibu za usajili wa *NACTE*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Reli Tabora. Chuo cha Reli Tabora kimeendelea kuwa ni Chuo muhimu katika kutoa mafunzo yenye lengo la kuboresha huduma za usafiri wa reli. Chuo hiki kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 135 kwa upande wa Tabora na wanafunzi 80 kwenye tawi lake la Morogoro. Chuo cha Reli Tabora kinaendesha kozi za usafirishaji, wakaguzi wa mabehewa, miundombinu ya reli, ishara na mawasiliano na rasilimali watu. Tawi la Morogoro linatoa kozi za ufundi makanika wa kutengeneza vichwa vya treni, ufundi umeme wa vichwa vya treni na udereva wa treni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuendelea kuwasilhi Watanzania kujiunga katika Chuo hiki ili kustawisha na kuboresha sekta ndogo ya reli nchini kwa upande mmoja na kupata ujuzi wa huduma za reli kwa ajili ya kutafuta ajira kwa upande mwingine. Sifa za kujiunga na Chuo ni kuhitimu kidato cha nne au cha sita kwa baadhi ya kozi au kuhitimu kozi za *VETA* kwa wanaotaka kusomea

ufundi wa kutengeneza vichwa vya treni. Chuo kina usajili wa Baraza la Vyuo vya Ufundi (*NACTE*). Chuo cha Reli Tabora kinapokea wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi wakiwemo wafanyakazi wa *TRL* kwa lengo la kuwaendeleza kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mtambuka. Utunzaji wa mazingira. Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa miradi yote ya miundombinu ya uchukuzi inatekelezwa kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira kwa kutumia sera, sheria, kanuni na mikataba ya Kimataifa iliyoridhiwa na Serikali. Katika mwaka 2012/2013, Wizara iliandaa kanuni zenye lengo la kuzuia uchafuzi wa mazingira ya bahari unaosababishwa na umwagikaji wa mafuta, kemikali za sumu, shehena hatarishi na aina zingine za visababishi vinavyoharibu mazingira ya bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imeandaa kanuni za namna ya kujiandaa na kukabiliana na uchafuzi wa mazingira uliosababishwa na kumwagika mafuta baharini. Kanuni hizi zimeandaliwa kwa kuzingatia Sheria ya Usafiri Majini ya mwaka 2003 ambayo inazingatia Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari Unaosababishwa na Meli (*The International Convention for the Prevention of Pollution from ships 'MARPOL 1973/1978'*) ambao Tanzania ni mwanachama. Kiambatisho I cha Mkataba huo inahusu kanuni za kuzuia uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na mafuta (*Annex I - Regulations for the Prevention of Pollution by Oil*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuimarisha utunzaji wa mazingira katika mwambao wa nchi yetu na katika maziwa makuu kwa kuhakikisha kwamba vyombo vinavyoruhusiwa kufanya kazi ni salama. Kanuni kuhusu usalama wa meli za mwambao na vyombo vidogo zimetengenezwa ili kuhakikisha kuwa viko salama na havichafui mazingira ya uchukuzi majini. Kanuni zote zilizotajwa zilisainiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 23 Novemba, 2012.

16 MEI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa utunzaji wa mazingira katika njia ya reli ya *TAZARA* ulifanyika ambapo changamoto mbalimbali ziligundulika. Changamoto hizo ni pamoja na uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na ajali za treni kumwaga shehena zenye sumu hivyo kuhatarisha maeneo yaliyohusika na ajali hizo. Ili kutafuta ufumbuzi wa namna ya kushughulikia changamoto hizo, Serikali kupitia *TAZARA* wanashirikiana na Kampuni ya Puma ambayo ina uzoefu mkubwa katika usafirishaji wa shehena hatarishi, kufanya utafiti na kushauri namna ya kurejesha hali ya awali ya maeneo yaliyoathiriwa na shehena hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa bandari zetu zinakuwa rafiki wa mazingira, Wizara ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini imeendelea kutekeleza Sera ya Usalama, Afya na Mazingira Katika Sehemu ya Kazi ya mwaka 2008. Kupitia sera hii zimeundwa Kamati za kusimamia mazingira katika bandari zote nchini ambapo kila Mkuu wa Bandari ndiye msimamizi wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kusimamia uimarishaji wa vitengo vinavyohusika na utunzaji wa mazingira kwenye Taasisi zilizo chini yake. Aidha, Wizara kupitia *SUMATRA* inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utunzaji wa mazingira kwa huduma na miundombinu ya uchukuzi. Huduma na miundombinu ya uchukuzi ikiwa rafiki wa mazingira itavutia watu wengi zaidi kuwekeza kwenye huduma za uchukuzi hapa nchini na hivyo kuongeza pato la Taifa. Rai yangu kwa Watanzania ni kutunza mazingira tukiwa ndani na nje ya vyombo vya uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia *SUMATRA* imeendelea kuimarisha usalama na uhifadhi wa mazingira ya uchukuzi majini. Hatua zilizochukuliwa ili kukabiliana na uchafuzi wa mazingira ni pamoja na kutoa mafunzo na zoezi la namna ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira ya bahari unaotokana na umwagikaji wa mafuta. Mafunzo na zoezi hilo yalifanyika Novemba, 2012 katika gati ya mafuta bandarini Dar es Salaam (Kurasini *Oil Jetty - KOJ*) ambapo wadau mbalimbali

walishiriki kupata mafunzo ya nadharia na vitendo. Vifaa vilivyotumika katika mafunzo haya vilitolewa kama msaada kwa Serikali chini ya mradi wa *GEF – Western Indian Ocean Marine Highway Project (WIOMHP)*. Mradi huu unasimamiwa na Kamisheni ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Commission – IOC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa UKIMWI. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, *TACAIDS* na wadau wengine imeendelea na juhudi za kupambana na janga la UKIMWI kwa kuendesha semina na warsha kwa lengo la kutoa elimu kuhusu ugonjwa huu. Katika mwaka 2012/2013, wafanyakazi waliweza kupata mafunzo ya jinsi ya kijikinga na UKIMWI, matumizi ya dawa za kurefusha maisha na kuishi kwa matumaini. Aidha, Wizara imeendelea kuwahamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari na kwa walioathirika na virusi vya UKIMWI wameendelea kupatiwa huduma za dawa kwa magonjwa nyemelezi, dawa za kurefusha maisha (*ARVs*) na lishe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapambano dhidi ya rushwa. Kuhusu suala la rushwa, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuziba mianya ya rushwa kwenye maeneo yake. Maeneo hayo ni pamoja na utoaji wa huduma na usimamizi wa utekelezaji wa sheria ya manunuzi katika zabuni za ujenzi, ushauri na ununuzi wa vifaa. Aidha, Wizara imeliweka suala la rushwa kuwa moja ya agenda katika vikao vya Watendaji Wakuu, watumishi na wadau wa sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari, elimu na mawasiliano. Katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na kupitia vipindi mbalimbali vya televisheni, makala kwenye magazeti, tovuti ya Wizara na kushiriki matamasha mbalimbali ya kitaifa. Wizara ilitoa makala maalum ya kuelezea Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne ambayo ilirushwa kwenye televisheni na kutolewa kwenye magazeti mbalimbali. Aidha, katika mwaka 2012/2013, Wizara ilikuwa mshindi wa tatu katika maonyesho ya Siku ya

Wakulima (Nanenane) na kupata cheti maalum pamoja na kikombe. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea na mkakati wake wa kutengeneza vipindi maalum na kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati wote waliochangia kuiwezesha sekta ya uchukuzi na hali ya hewa kufanikisha malengo na majukumu yake. Nakiri kwamba mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2012/2013 ni kutokana na jitihada na ushirikiano wa pamoja kwa misaada ya kifedha na kitaalamu kutoka kwa wadau wa ndani na nje ya nchi. Natoa shukrani kwa wadau wote wa sekta ya Uchukuzi na Hali ya Hewa ikiwemo sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutimiza malengo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa washirika wa maendeleo ikiwa ni nchi hisani au Taasisi za fedha za Kimataifa. Washirika hao ni pamoja na Shirika la Bahari Duniani (*IMO*), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*ICAO*), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (*WMO*), *UNESCO*, Benki ya Dunia (*WB*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Kuwait *Fund*, Malaysia, Jamhuri ya Korea, *OPEC Fund*, Umoja wa Nchi za Ulaya, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, *Japan*, *European Investment Bank (EIB)*, India, China, *Denmark*, *Norway*, Ubelgiji, Ujerumani, Urusi, Sweden, Ufaransa, Finland, Singapore na wengine wengi. Naomba waendeleo na moyo huo ili tuweze kuendeleza sekta hii ambayo ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapofika mwisho wa hotuba hii, shukrani zangu hazitakuwa kamili bila kuwapongeza na kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba (Mb.), Katibu Mkuu Mhandisi Omar Abdallah Chambo, Naibu Katibu Mkuu, Ndg. John Thomas Mngodo, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti wa Bodi za

SUMATRA, TCAA, TGFA, KADCO, TAA, TPA, TRL, RAHCO, MSCL, TMA, SINOTASHIP, ATCL, DMI, NIT na TAZARA, viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na watumishi wote wa Wizara na Taasisi. Wote pamoja wamenipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu niliyonayo ya kusimamia sekta za uchukuzi na hali ya hewa. Naomba waendeleo kunipa ushirikiano huo katika kipindi kijacho ili tuweze kutekeleza malengo tuliyojiwekea kwenye sekta zetu za uchukuzi na hali ya hewa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 491,105,994,000 ili iweze kutekeleza majukumu na malengo yake. Kati ya fedha hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni Shilingi 100,584,774,000 na fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni Shilingi 390,521,220,000. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Shilingi 32,305,674,000 za Mishahara ya Watumishi na Shilingi 68,279,100,000 fedha za Matumizi Mengineyo (*OC*). Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha Shilingi 222,680,000,000 fedha za ndani na Shilingi 167,841,220,000 fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba, jedwali la miradi yote itakayotekelezwa katika mwaka 2013/2014 pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo imeoneshwa katika Kiambatisho Na.1. Naomba Kiambatisho hicho kichukuliwe kama sehemu ya hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: www.mot.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.
(*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

KIAMBATISHO NA.1

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 NA KIASI CHA
FEDHA KILICHOTENGWA KWA KILA MRADI

| Kasma | Jina La Mradi | Makisio ya Bajeti 2013/2014 | | | Anayegharamia |
|-------|---|-----------------------------|---------------|-----------------|---------------|
| | | (Sh. Mil.) | | | |
| | | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Jumla | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (3+4) | 6 |
| | SUBVOTE 1003: POLICY & PLANNING | | | e | |
| 6267 | Institutional Support | | | | |
| | i. Revamping ATCL | 1,000.00 | | 1,000.00 | GOT |
| | ii. Rehabilitation of MSCL vessels | 1,500.00 | - | 1,500.00 | GOT |
| | iii DMI Building | 2,871.00 | | 2,871.00 | GOT |
| | iv. MOT | 250.00 | 925.76 | 1,175.76 | GOT/EU |
| | SUBTOTAL | 5,621.00 | 925.76 | 6,546.76 | |
| | SUB VOTE 2005: TRANSPORT INFRASTRUCTURE DIVISION | | | | |
| 4158 | Construction of Kigoma Airport | 3,500.00 | 27,800.00 | 31,300.00 | GOT/IDA/EIB |
| 4158 | Construction of Mpanda Airport | ,800.00 | - | 1,800.00 | GOT |
| 4159 | Construction of Tabora Airport | 2,800.00 | 12,800.00 | 15,600.00 | GOT/IDA/EIB |
| 4206 | Construction of Songwe Airport | 8,500.00 | - | 8,500.00 | GOT |
| 4209 | Construction of Mwanza Airport | 8,000.00 | 3,482.79 | 11,482.79 | GOT/BADEA |
| 4210 | Construction of Arusha Airport | 500.00 | | 500.00 | GOT |

| Kasama | Jina La Mradi | Makisio ya Bajeti 2013/2014 | | | Anayegharamia |
|--------|---|-----------------------------|--------------|----------|---------------|
| | | (Sh. Mil.) | | | |
| | | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Jumla | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (3+4) | 6 |
| 4213 | Relaying of 197kms of TRC with 80 lbs/yards - RAHCO | | | | |
| | (i) Relaying with 80lbs/yard materials 197kms of track central line | 5,200.00 | | 5,200.00 | GOT |
| | (ii) Rehabilitation Tura Quarry | 3,200.00 | | 3,200.00 | GOT |
| 4215 | Rail Rehabilitation - Branch lines - RAHCO | 500.00 | | 500.00 | GOT |
| 4216 | Rail Rehabilitation - Main Line - RAHCO | | | | |
| | (i). Track repair and improvement of drainage Kilosa-Gulwe | 4,500.00 | | 4,500.00 | GOT |
| | (ii). Construction of bridge km 293 and km 303 | 5,415.00 | | 5,415.00 | GOT |
| | (iii). Construction of bridge km 517. Bahi - Kintinku Section | 2,640.00 | | 2,640.00 | GOT |
| | (iv) Realignment Study to avoid Floods (Kilosa - Gulwe) | 2,500.00 | | 2,500.00 | GOT |
| | (v). Rating and redesign of Bridges to 25 tons per axle load | 1,000.00 | 4,896.00 | 5,896.00 | GOT/IDA |
| 4217 | Tabora-Kigoma, Isaka - Mwanza Railway Project | 2,500.00 | | 2,500.00 | GOT |

| Kasma | Jina La Mradi | Makisio ya Bajeti 2013/2014 | | | Anaya-garamia |
|-------|---|-----------------------------|-------------------|-------------------|---------------|
| | | (Sh. Mil.) | | | |
| | | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Jumla | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (3+4) | 6 |
| 4218 | Mtwara - Mbambabay, Liganga and Mchuchuma Rail (FS) | 5,580.00 | - | 5,580.00 | GOT |
| 4220 | Construction of Mtwara Airport | 500.00 | - | 500.00 | GOT |
| 4221 | Construction of Sumbawanga Airport | 500.00 | 12,800.00 | 13,300.00 | GOT/EIB |
| 4222 | Construction of Shinyanga Airport | 500.00 | 16,840.00 | 17,340.00 | GOT/EIB |
| 4223 | Tanga(Mwambani)-Arusha-Musoma Railway Project | | | - | |
| | (i) Compensation | 4,900.00 | - | 4,900.00 | GOT |
| | (ii) Tanga - Arusha (DD) | 5,020.00 | - | 5,020.00 | GOT |
| | (iii) Arusha - Musoma (FS) | 5,580.00 | - | 5,580.00 | GOT |
| 4281 | DSM -Isaka -Kigali-Keza-Msongati | 200.00 | - | 200.00 | GOT |
| 4282 | Inland Container Depots. | 900.00 | - | 900.00 | GOT |
| 4287 | Construction of Bukoba Airport | 3,000.00 | 8,286.67 | 11,286.67 | GOT/IDA/EIB |
| 4289 | Construction of Terminal III JNIA | 9,000.00 | 80,000.00 | 89,000.00 | GOT/HSBC |
| 6520 | Dev. of Sea and Inland Berths | 500.00 | - | 500.00 | GOT |
| | SUB TOTAL | 88,735.00 | 166,915.48 | 255,650.48 | |
| | SUB VOTE 2006: TRANSPORT SERVICES DIVISION | | | | |
| 4219 | DSM City Commuter Train Project | | | - | GOT |
| | (i) Study of New railway lines | 1,500.00 | - | 1,500.00 | GOT |

| Kasma | Jina La Mradi | Makisio ya Bajeti 2013/2014 | | | Anaya-gharamia |
|-------|---|-----------------------------|-------------------|-------------------|----------------|
| | | (Sh. Mil.) | | | |
| | | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Jumla | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (3+4) | 6 |
| 4290 | TMA Radar, Equipment and Infrastructure | 4,000.00 | - | 4,000.00 | GOT |
| 4291 | Government Aircrafts maintenance | 8,200.00 | - | 8,200.00 | GOT |
| 4292 | Rolling Stock, Equipment, Track Maintenance and Contractual liabilities for TRL | | | | |
| | i) Procurement and repair of Rolling Stock, Equipment and track maintenance | 107,624.00 | - | 107,624.00 | GOT |
| | ii) Contractual Liabilities | 5,500.00 | - | 5,500.00 | GOT |
| 6377 | Construction and Rehab. of NIT buildings | 1,500.00 | - | 1,500.00 | GOT |
| | SUB TOTAL | 128,324.00 | - | 128,324.00 | |
| | TOTAL | 222,680.00 | 167,841.22 | 390,521.22 | |

16 MEI, 2013

na asilimia 30.88. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 22 Aprili, 2013 kiasi cha shilingi bilioni 80 kilitolewa na kuelekezwa kwenye reli ambapo *TRL* wametengewa shilingi bilioni 66.3 na *RAHCO* shilingi bilioni 13.7 na kufanya jumla ya Fedha zote za miradi ya maendeleo zilizotolewa hadi mwezi Aprili kuwa shilingi milioni 127,409.57.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hairidhishwi na utoaji huu wa fedha kinyume na Bunge liliyoidhinisha kwani inapelekea Wizara kushindwa kutimiza malengo iliyojipangia kwa wakati. Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha zote zilizokuwa zimeidhinishwa ili kusudi Wizara iweze kutimiza malengo yake yaliopangwa kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa bajeti na mpango wa bajeti kwa mwaka 2013/2014. Makadirio ya Matumizi ya Kawaida. Katika mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 100.584 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo shilingi bilioni 32.306 ni kwaajili ya kulipia mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake na shilingi bilioni 68.279 ni fedha kwa ajili ya Matumizi Mengine (*OC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya matumizi ya maendeleo. Kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka 2013/2014, Wizara imetengewa shilingi bilioni 390.521 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 222.680 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 167.841 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kupitia utekelezaji wa Wizara kwa mwaka 2012/2013 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2013/2014, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Wizara ya Uchukuzi. Kamati imekuwa ikiishauri Serikali mara kwa mara kuwa katika sekta ambayo Serikali ikiipa kipaumbe kwa kutenga fedha za kutosha, inaweza kuchochea ukuaji wa uchumi kwa haraka ni sekta ya uchukuzi na usafirishaji. Sekta hii inahusisha njia muhimu za kukua uchumi yaani usafirishaji wa nchi kavu, maji na anga. Pamoja na Serikali kuainisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji kuwa ni kati ya maeneo ya kipaumbele katika mwaka 2013/2014, bado Kamati

sehemu nyingine zinazofikika kiurahisi. Kwa mfano, mfuko wa Simenti Dar es Salaam unauzwa kwa wastani wa shilingi 14,000/= ikilinganishwa na Kigoma ambako mfuko huo huo unauzwa kwa wastani wa shilingi 21,500/=. Hali hii si nzuri kwa mustakabali wa nchi yetu kwa kuwa maendeleo ya kiuchumi hayapatikani kwa uwiano miongoni mwa kanda mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya kati yenye urefu wa kilometa 1252 ilijengwa mwaka 1905 – 1914 lakini pia reli ya Dar es Salaam –Moshi - Arusha na Dar es Salaam – Tanga – Moshi - Arusha zimatelekezwa na nyingine kung’olewa kabisa kama ilivyofanyika kwa reli ya Dar es Salaam - Mtwara na Manyoni -Singida ambayo ilifufuliwa na kufanya kazi kwa muda mfupi na kisha kutelekezwa tena. Vilevile reli ya Kaliuwa – Mpanda imekuwa ikisuasua na tumeshuhudia mlundikano wa mahindi kutoka katika Mikoa ya Rukwa na Katavi ambayo ilibidi kutumia malori ya Jeshi kuyaamisha ambayo yangeweza kuhamishwa kwa urahisi zaidi kwa kutumia reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba reli hizi ni za zamani sana hivyo zimekuwa zinaharibika mara kwa mara na hazikidhi mahitaji ya nchi. Kamati inaamini iwapo reli hizi zitafanyiwa ukarabati na kutumika, zitachochea kwa kasi uchumi wa maeneo zinakopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga mipango mbalimbali ya kujenga mitandao ya usafiri wa reli hapa nchini. Kati ya mipango hiyo ni pamoja na kuifanya reli ya kati iwe ya *Standard Gauge*, mradi wa reli kati ya Tabora, Kigoma, Isaka – Mwanza, kujenga reli ya Mtwara, Mbambabay, Mchuchuma hadi Liganga, pamoja na ukarabati wa reli kutoka Manyoni Singida na Kaliuwa Mpanda, kujenga reli ya kuunganisha bandari ya Mwambani jijini Tanga na Bandari ya Musoma Mkoani Mara. Hata hivyo, Kamati inaona kasi ya utekelezaji wa mipango hii ni ndogo kwani bajeti inayotengwa katika miradi hii hailingani na kazi kubwa inayohitajika. Kamati inashauri Serikali ichukue hatua mahsusi na za haraka kama ilivyofanya kwenye barabara kuhakikisha mradi huu unakuwa wa kipaumbele ili utafutiwe

na kutengewa fedha mahsusi ili uweze kukamilika kwa haraka na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifikapo mwaka 2015, reli ya kati itahitaji kusafirisha takriban tani milioni tatu za madini ya *Nike*/kutoka Msongati peke yake. Kwa kuzingatia hali na umuhimu wa reli kwa ujumla katika mpango wake unaoratibiwa chini ya *Performance Management Delivery Unit (PEMANDU)*, Serikali ilipanga kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2013/2014, Serikali itatenga shilingi trilioni tatu kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa reli. Kamati ilitaraji mwaka huu wa fedha ziwe zimetengwa shilingi trilioni moja kwa ajili ya reli peke yake. Hata hivyo, kiasi kilichotengwa ni shilingi bilioni 255.7 tu. Kamati inaomba Bunge lako Tukufu liambiwe kama Serikali bado ina nia ya kutekeleza mpango iliyojiwekea wa *PEMANDU*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kushauri Serikali izingatie umuhimu wa reli katika uchumi wa ushindani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa kufanya uamuzi wa makusudi wa kutafuta fedha nje ya utaratibu wa kawaida wa bajeti. Kwa kufanya hivyo zoezi la kujenga upya reli zetu na kuzifanya ziwe za kisasa (*modernization*) litafanyika mara moja na kwa muda mfupi. Kuendelea kusubiri wafadhili hatutafika. Kuendelea na zoezi la kufufua reli hizi za zamani halitusaidii sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa reli katika uchumi unafahamika duniani kote. Warren Buffett mwekezaji na bilionea maarufu nchini Marekani wakati ananunua kampuni kubwa ya reli duaniani, *BNSF* alisema, naomba kunukuu:-

“Railroads represent the future. They are best-positioned to haul the raw material and finished goods to a nation and economy. Unlike trucks, trains do not have to compete on congested highways. Nor do railroads depend on strapped governments to maintain infrastructure”. Mwisho wa kunukuu. Mwisho wa Kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri isiyo rasmi ya kauli hiyo ni kwamba njia ya reli ina maana katika mustakabali mzuri. Ni njia bora zaidi ya kusafirisha malighafi kwa ajili ya Taifa na uchumi wake. Kinyume na malori, usafiri wa garimoshi hauhitaji kushindana katika msongamano kwenye barabara kuu. Aidha, usafiri wa reli hautegemei sana ukarabati wa Serikali unaofanywa na Serikali yenye uwezo mdogo wa kifedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Uchukuzi alitoa maagizo safari za treni ya abiria kwenda Mwanza zianze ifikapo Mwezi Septemba, 2012. Kamati inapongeza Serikali kwa utekelezaji wa agizo hili kwani sasa treni inafanya safari zake mara mbili kwa wiki. Kamati inashauri Serikali ifanye mkakati ili idadi za safari za treni ziongezeke angalau kufika safari nne kwa wiki na kuongeza mabehewa ya daraja zote ikiwemo madaraja ya juu yaani la daraja la kwanza na la pili. Pia ni muhimu kuhakikisha kuwa mfumo wa taa, maji na vyoo ndani ya mabehewa unafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza Wizara kwa kuhakikisha uwepo wa Bodi mpya ya Wakurugenzi katika Shirika la Reli. Ni mategemeo ya Kamati kuwa bodi hii itamshauri vyema Waziri ili kuhakikisha malengo yaliowekwa na Serikali yanafikiwa, ikiwa ni pamoja na kuimarisha Chuo cha Reli Tabora ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji wa reli ya TAZARA. Kati ya majukumu ya msingi ya TAZARA ni kutoa huduma za usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo kati ya Tanzania na nchi jirani hasa za ukanda wa kusini mwa Afrika (*SADC*). Kamati imekuwa ikiainisha changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikikabili uendeshaji wa reli hii. Changamoto hizi zimekuwa zikisababishwa kwa kiasi kikubwa na Sheria iliyoanzisha TAZARA Na. 4 mwaka 1975. Kamati imefarijika kusikia mchakato wa kurekebisha Sheria hii umeanza. Kamati inashauri kasi ya mchakato huu iongezwe ili kupunguza kero mbalimbali katika uendeshaji wa reli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa treni ya kusafirisha abiria Jijini Dar es Salaam (*City Train*). Kuanzia mwezi Oktoba, 2012 Wizara ilianzisha usafiri wa treni. Abiria wengi wamekuwa wakisafiri kwa treni hiyo kutoka Dar es Salaam Stesheni, kwenda Ubungo Maziwa kupitia Buguruni na Tabata na kutoka Pugu, Mwakanga hadi Kurasini kwa kutumia treni ya TAZARA. Kamati ilifanya ziara ya kutembelea mradi huu wa kusafirisha abiria Jijini Dar es Salaam kwa treni kwa lengo la kuona namna usafiri huu unavyopunguza adha ya usafiri Jijini Dar es Salaam na pia kuona mafanikio na changamoto za mradi huo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuamua kuanzisha usafiri huu kwani sasa kutoka Ubungo hadi Stesheni ya Dar es Salaam abiria anatumia dakika arobaini tu badala ya masaa mawili mpaka matatu yaliokuwa yanapotea kwa kutumia usafiri wa mabasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa changamoto kubwa katika mradi huu ni gharama za uendeshaji kuwa juu zaidi ya mapato yatoananyo na tozo la nauli. Gharama hizi zinahusisha mafuta dizeli, mafuta mazito kwa ajili ya injini, mishahara na gharama za bima (*premium*) kwa abiria. Aidha, ili kufanikisha uwepo wa usafiri huu, Kampuni ya Reli Tanzania inatumia injini zilizokuwa za treni za safari ndefu ambazo zinatumia mafuta mengi sana na ili treni iweze kupandisha muinuko mdogo tu inalazimika kutumia injini mbili ili ziweze kusukuma mabehewa mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa kwa sababu zilizotajwa hapo juu mradi huu unaitetea Serikali hasara ya shilingi milioni mbili kwa siku. Hata hivyo, kufuatana na utafiti iliofanywa na JICA Mwaka 2009 ulibaini kuwa Dar es Salaam inapata hasara ya bilioni nne kwa siku kutokana na msongamano wa magari jijini Dar es Salaam. Kamati inashauri, ili mradi uweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuondokana na hasara, Serikali iharakishe kununua angalau treni mbili za kisasa na maalum kwa safari fupi ambazo gharama yake ni takribani shilingi bilioni nane kila moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Bandari Tanzania. Tanzania imezungukwa na nchi nane, sita kati ya hizo zinategemea kupitisha mizigo yao kupitia nchi zenye bandari ikiwemo bandari ya Dar es Salaam. Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuhusiana na umuhimu wa upanuzi wa bandari na ujenzi wa gati namba 13 na 14. Mchakato wa ujenzi wa gati hizi ulianza tangu mwaka 2009, ni takribani miaka mitano sasa bado mchakato huu haujakamilika. Kamati inaitaka Serikali kutoa maelezo katika Bunge lako Tukufu kuhusiana na hatua iliyofikiwa katika mchakato wa ujenzi wa gati hizo. Aidha, Kamati inaona wakati umefika kwa Serikali kuona umuhimu na kutoa kipaumbele katika ujenzi wa gati hizi katika bandari yetu ili kuiwezesha kushindana kwani nchi jirani zinakamilisha miradi yao kwa kasi ili kuongeza ufanisi kwa lengo la kukabili ushindani wa biashara kwa bandari yetu ya Dar es Salaam. Aidha, ili bandari ya Dar es salaam iweze kufanya kazi kwa kiwango kinachotakiwa ni muhimu kuhakikisha kuwa reli ya kati nayo inafanya kazi kwa ufanisi mkubwa. Kwa kufanya hivyo nchi yetu itakuwa ndiyo kitovu (*hub*) cha biashara ya usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kubwa kwa wasafirishaji wa mizigo kwa kutumia magari makubwa kwa kutokuwa na maegesho bandarini wala kwenye hifadhi za nchi kavu (*ICDS*). Kwa mujibu wa Sheria ya Forodha, Sheria Namba 85 ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004, magari ya mizigo inayosafirishwa nchi jirani kupitia bandari zetu yanapaswa kuwa katika barabara zilizoidhinishwa (*transit routes*) wakati wote wa safari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mkanganyiko mkubwa katika suala la sehemu ya maegesho ya magari makubwa. Mamlaka ya Mapato (*TRA*) inayo Sheria inayotaka magari ya mizigo ya (*transit*) kubakia kwenye njia mahsusi vinginevyo yanapigwa faini. Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ina Sheria na pia imeweka mabango yanayopiga marufuku kuegesha magari kandokando ya barabara. Vilevile Serikali za Mitaa nazo zimeanzisha Sheria

ndogo ndogo kuzuia uegeshaji wa magari barabarani. Magari hayo hutozwa faini kubwa na mamlaka hizo tatu za umma hivyo kuleta mkanganyiko mkubwa na usumbufu kwa wasafirishaji wa mizigo inayokwenda Mikoani na nje ya nchi. Kamati inashauri Serikali yenyewe au kwa kwa kuingia ubia ijenge maegesho makubwa ya magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini. Aidha, wakati hatua hizi zikiendelea kufanyiwa kazi, Serikali iruhusu magari haya kuegeshwa kwenye maeneo ya wenye mali iwapo itabidi. Vilevile Kamati inashauri *TRA*, *TANROADS* na Serikali za Mitaa zikutane ili kutafuta ufumbuzi wa haraka wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa hakuna utaratibu wa viwango vinavyowiana kwa mamlaka hizo tatu juu ya tozo la adhabu ya maegesho kwenye maeneo yasirohusiwa. Kamati inashauri Mamlaka zilizotajwa hapo juu zikae na kujadili suala hili na kufikia muafaka kwani ni usumbufu na chachu ya kukosesha uadilifu. Vilevile kuwe na viwango maalum vya tozo vinavyojulikana na kutolewe risiti za kieletroniki ili kudhibiti mapato na hatimaye Serikali kupata mapato halali yaliyolipwa na wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, makampuni yanayofanya kazi hii yamekuwa yakichukuwa fedha nyingi huku Serikali ikipata fedha kidogo sana kutokana na tozo hizi. Kamati inashauri Serikali na Mamlaka husika baada ya kuweka viwango maalum vya tozo kukaa pamoja na kuanisha upya kiwango cha mgao huo kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Boya la Mafuta (*Single Point Mooring*). Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kununua boya kubwa baharini ambalo litawezesha meli kubwa za tani 80,000 hadi 100,000 kushusha shehena ya mafuta kiasi cha tani 3000 kwa saa. Hii ni kutokana na uamuzi wa Serikali wa kununua mafuta kwa wingi na kwa pamoja (*Bulk Procurement System*) ili kupunguza bei ya mafuta kwa mtumiaji. Katika kuongeza ufanisi wa kuhudumia meli kubwa hapa nchini, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha mradi wa boya jipya tangu Novemba 2012. Kukamilika kwa mradi huu kumeiwezesha bandari

kuhudumia meli kubwa zenye uwezo wa kubeba mzigo wa tani 150,000 (*DWT*) kutoka 75,000 (*DWT*). Boya hili jipya linauwezo wa kushusha shehena ya mafuta ghafi (*crude oil*) tani 3,500 kwa saa na mafuta safi tani 2,500 kwa saa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati ina taarifa kuwa *flow meter* iliyokuwa imewekwa kwa ajili ya kupima kiasi halisi cha mafuta yanayoingia nchini matumizi yake jamesitishwa kwa sasa. Kamati inasikitishwa na maamuzi haya kwani badala ya kwenda na teknolojia tunarudi nyuma kwa kupima mafuta kwa kijiti (*deepstick*). Inawezekana huu ni mkakati mahsusi wa watu wasiowaaminifu kutengeneza mianya ya kunufaika na hali hii kwani ingekuwa kwa nia njema *flowmeter* hiyo ingefanyiwa ukarabati. Kamati inaitaka Serikali itoe maelezo kuhusu undani wa suala hili mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa biashara ya usafirishaji kati ya Tanzania na Zambia. Tangu Uhuru wa nchi hizi mbili, Tanganyika na Zambia tumekuwa na uhusiano wa kibiashara hasa ya uchukuzi wa mafuta kati ya Tanzania na Zambia mpaka tukafikia kujenga bomba la TAZAMA. Inashangaza kuona sasa Zambia inaweka masharti yasiyotekelezeka kuhusu matenki ya magari yanayopeleka mafuta Zambia kuwa yawe na vyumba (*compartments*) visivyopungua saba. Vigezo vya Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) vinaruhusu matenki ya magari ya mafuta yanayoingizwa Tanzania kuwa na vyumba vitatu hadi vinne. Kwa maana hiyo, kama magari haya yanataka kupeleka mafuta Zambia ni lazima yaongeze vyumba vya kuhifadhiya mafuta kama Shirika la Viwango la Zambia (*ZBS*) linavyotaka, vinginevyo hulipa faini ya dola 180 kila linapopeleka mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kero isiyovumilika na pia ni kinyume na Ibara ya 17(3) ya itifaki ya ya Biashara ya *SADC* ya mwaka 1996 inayozuia nchi moja kuilazimisha nchi nyingine kufuata viwango vyake. Ikumbukwe kuwa matanki haya haya pia hupeleka mafuta Kongo DRC ambako Shirika

la Viwango Kongo lina kigezo cha chumba (*compartment*) kimoja tu ili kupunguza muda wa kupakua mafuta. Aidha, malori yote yaliyosajiliwa Tanzania hupewa tozwa la dola 50 za Kimarekani kwa siku jambo linalopelekea kupanda kwa gharama za kufanya biashara. Kamati inashauri Wizara ya Uchukuzi kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kuzingatia Ibara ya 17(5) ya Itifaki hiyo, kuchukuwa hatua ya kuwasiliana na Serikali ya Zambia ili kupata ufumbuzi wa kero hizi na kuimarisha biashara ya kikanda kwa manufaa ya nchi zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, geti la kuingia na kutoka katika mpaka wa Tanzania na Zambia Mjini Tunduma ni moja tu hali inayosababisha msongamano mkubwa wa magari ya mizigo na hivyo kucheleweshwa kwa bidhaa na kuffisha ukuaji wa biashara baina ya nchi hizi mbili na kuwa moja ya sababu za kurundikana mizigo katika bandari ya Dar es Salaam kwani malori yanachukua muda mrefu kwenda na kurudi Zambia. Kamati inashauri, Serikali ya Tanzania na Zambia kuongeza mageti ili kupunguza msongamano na kuharakisha usafirishwaji wa mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vya ndege na usafiri wa anga. Hali ya uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius K. Nyerere Dar es Salaam si nzuri, madaraja (*aerobridges*) hayafanyi kazi na dari la jengo la kupokelea abiria limechakaa na maeneo mengi yanahitaji ukarabati mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka wa fedha wa 2012/2013 fedha iliyotengwa kwa ajili ya uwanja huu ilikuwa ni sh. 2,130,000,000/=, hata hivyo mpaka Wizara ya Uchukuzi ilipokutana na Kamati Mwezi Machi, 2013 hakuna kiasi chochote kilichokuwa kimetolewa kwa ajili ya Uwanja huu. Kamati inashauri fedha zilizotengwa zitolewe kwa haraka kabla ya mwaka wa fedha kuisha ili zikafanye kazi hizi kwa sababu muonekano wa uwanja wa ndege unatoa taswira ya nchi kwa wageni wanapoingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na mpango wa ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja cha

Kimataifa cha Julius Nyerere. Mpango huu ni muhimu kwani inakadiriwa kuwa kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi huu kutaongeza abiria kutoka abiria milioni 1.2 ya sasa kwa mwaka hadi abiria milioni 4.7 kwa mwaka. Hii itakuwa fursa nzuri ya kukuza uchumi wa nchi yetu hasa kwa kutoa ajira kwa watu wengi zaidi. Kamati inaitaka Serikali iliambie Bunge lako Tukufu hatua zilizofikiwa za ujenzi wa mradi huu kama ilivyoenezwa awali fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo kwa mwaka 2012/2013 hazikutolewa kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2013/2014 kiasi kilichotengwa kwa ajili ya uwanja huu ni Sh. 89,000,000,000/=. Kamati inashauri fedha hizo zitolewe mapema iwezekanavyo ili utekelezaji wa ukarabati wa uwanja huu uanze mara moja. Aidha, Kamati inashauri kuwa kupitia Kamati ya Bunge ya Bajeti, Bunge lako Tukufu liwe linapokea taarifa ya mwenendo wa bajeti ya Serikali kila baada ya miezi mitatu (*Quarterly Reports*) ili kujua uhalisia wa bajeti iliyopitishwa na Bunge ili liweze kushauri namna bora utekelezaji wa bajeti husika kwani kwa sasa Bunge linapitisha bajeti ya maendeleo lakini mwisho wa mwaka wa fedha bajeti inayotolewa ni wastani wa 50% au 60% tu. Hali hii inakwamisha miradi na hivyo kuendelea kuifanya nchi yetu iendelee kuwa maskini na tegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuongeza wigo wa safari za anga kwa kujenga kiwanja kikubwa cha Kimataifa kitakachotumiwa na ndege za ndani na zinazotoka nje katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini. Uwanja wa Songwe wa kimataifa ni kati ya viwanja vikubwa viwili kujengwa ukitanguliwa na uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Uwanja huu ni fursa muhimu kwa wakazi wa Mkoa wa Mbeya na Mikoa ya jirani kwani utaweza kuwasaidia kukuza uchumi kutokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi zitakazofanyika kutokana uwepo wa uwanja huo. Kamati inashauri Serikali iendelee kukamilisha maeneo yaliyobaki ili ndege kubwa za kimataifa zianze kutumia kiwanja hicho na kuvutia mashirika makubwa ya ndege kukitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati imebaini maendeleo ya ujenzi ya uwanja ndege wa Mwanza hayaridhishi kwa sababu ya fedha kutokutolewa. Kamati inashauri Serikali itoe fedha za kutosha kuhakikisha uwanja huu unajengwa kwa sababu ya umuhimu wake katika kukuza maendeleo ya ukanda wa Ziwa na Taifa kwa ujumla. Serikali itoe maelelezo kuhusu watu waliovamia maeneo ya kiwanja hicho na kama Serikali imepata hati ya kumiliki kiwanja hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL). Hali ya shirika hili ni mbaya ambapo kwa sasa lina ndege mbili tu ambazo ni *Dash 8 Q 300* na *Boeing 737-500*. Uendeshaji wa Shirika hili unakabiliwa na changamoto nyingi katika ngazi ya taifa na kimataifa. Changamoto hizo zinasababishwa na ufinyu wa bajeti inayotokana na kutokutolewa fedha za kutosha kwa ajili ya kulikwamua Shirika hili. Mwaka wa fedha wa 2012/2013, Shirika lilitengewa jumla ya shilingi bilioni tano ambapo mpaka kufika mwezi Februari, 2013 walikuwa wamepewa jumla ya 1,550,800,000. Mwaka wa fedha wa 2013/2014, Shirika limepangiwa jumla ya shilingi bilioni moja tu. Kamati inashauri fedha zitolewe za kutosha ili kuliwezesha Shirika hili kujimudu katika kutekeleza shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali ifanye uchambuzi wa kina ikiwa bado inalihitaji shirika hili iamue kuwekeza mtaji wa kutosha na kama hailihitaji iliuze kwa wanaoweza kuliendesha kuliko hali ilivyo sasa ambapo linaendelea kusuasua na kuitia hasara nchi yetu. Ni muhimu pia kwa Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu juu ya mkakati mahsusni uliopo sasa wa kulikwamua shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA). Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) ina majukumu ya kusimamia vyombo vya usafiri wa nchi kavu na majini. Kamati inashauri Wizara iendelee kuwa karibu na Mamlaka hii ili kufanikisha malengo na kupunguza ajali za barabarani zinazosababishwa na

uzembe wa madereva na kusababisha wananchi kupoteza maisha na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. Mamlaka hii ni muhimu sana hasa ukizingatia mabadiliko ya tabia nchi yanayojitokeza mara kwa mara na kuhitaji uchunguzi, utafiti na hata kutoa tahadhari kwa jamii. Katika miaka mitatu mfululizo bajeti ya mamlaka hii imekuwa ikiongezeka ambapo mwaka wa fedha 2011/2012 mamlaka ilipewa shilingi bilioni 3.4, mwaka wa fedha 2012/2013 mamlaka hii ilitengewe shilingi bilioni 3.8 na katika mwaka huu wa fedha mamlaka imetengewa bilioni nne. Kwa kuangalia mtiririko wa fedha, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuongeza bajeti ya mamlaka hii mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo hadi kufikia mwezi Machi mamlaka hii ilikuwa imepewa shilingi 531.38 ambayo sawa na 14%. Kwa mwenendo huu wa utoaji bajeti ni vigumu kwa mamlaka hii muhimu kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Katika mwaka huu fedha mamlaka imepanga kukamilisha ununuzi wa rada itakayofungwa Mwanza, vifaa vya hali ya hewa na matayarisho ya ujenzi wa jengo la utabiri wa hali ya hewa (*Central Forecasting Office*). Kamati inashauri Serikali kutoa fedha kwa wakati kwani pamoja na vipaumbele vingine, mamlaka hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za kilimo, usafiri wa anga na wamajini, pamoja na shughuli za kila siku za maisha ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 100.584 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo shilingi bilioni 32.306 kwa ajili ya mishahara ya Watumishi na shilingi bilioni 68.279 kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na shilingi bilioni 390.521 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kifungu kwa kifungu na kuipitisha. Kamati inaliomba Bunge

Iako Tukufu kukubali kuitisha maombi hayo ya fedha kwa Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Nawashukuru pia Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, Mb; Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba, Mb; Naibu Waziri wa Uchukuzi, *Eng.* Omary Abdallah Chambo; Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi pamoja na Wataalamu wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano, ushauri na utaalum wao ambao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge Iako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa kwa kupitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa napenda kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati ya Miundombinu, ambao ni Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba-Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya-Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha-Mjumbe, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee-Mjumbe, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka-Mjumbe, Mheshimiwa Said Ramadhani Bwanamdogo-Mjumbe, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida -Mjumbe, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris-Mjumbe, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo-Mjumbe, Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona-Mjumbe, Mheshimiwa Eng. Ramo M. Makani-Mjumbe, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad-Mjumbe, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby-Mjumbe, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe-Mjumbe, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo-Mjumbe, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura -Mjumbe, Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa-Mjumbe, Mheshimiwa

Elizabeth Nkunda Batenga-Mjumbe, Mheshimiwa Suleman Masoud Nchambi-Mjumbe, Mheshimiwa Said Amour Arfi-Mjumbe, Mheshimiwa Horoub Mohamed Shamis-Mjumbe na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati-Mjumbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashillilah, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na Katibu wa Kamati hii Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi na Ndugu Hosiana John kwa kuihudumia Kamati na kuandaa Taarifa hii. Nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba sasa kuwasilisha na ninaunga mkono Hoja hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, tunakushukuru kwa niaba ya Kamati yako kwa kutusomea maoni ya Kamati hiyo.

Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Paulina P. Gekul karibu sana. (*Makofi*)

MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niwasilishe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii ya Uchukuzi kuhusu Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Bajeti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9), Toleo la mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri na usafirishaji ni kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi na kuongeza pato la Taifa. Mchango wa sekta ya uchukuzi katika pato la Taifa

kwa mwaka 2010 pekee ulikuwa ni shilingi bilioni 853.53 sawa na asilimia 5.4 ya pato la Taifa. Kati ya mwaka 2005 na 2010 sekta ya uchukuzi imekua kwa wastani wa asilimia 6.4, mwaka 2011, shughuli za kiuchumi za uchukuzi zilikuwa kwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2010 na hivyo kuwa miongoni mwa sekta muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa letu. Hii ni kwa mujibu wa Kitabu cha Hali ya Uchumi kwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Uchukuzi ni Wizara yenye majukumu makubwa ya kusimamia yafuatayo: uandaaji wa sera za usafiri na usafirishaji na kusimamia utekelezaji wake; usafirishaji wa reli na bandari; usafiri na usafirishaji wa anga na viwanja vya ndege (vikubwa na vidogo); utoaji wa leseni za usafirishaji; usalama katika usafirishaji na hali ya hewa; kuongeza tija katika utendaji kazi pamoja na kuendeleza rasilmali watu na kusimamia Idara na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutimiza majukumu yake Wizara iliaweke malengo kwa kila idara na taasisi, miongoni mwa malengo hayo ni pamoja na kuwa na miundombinu na huduma za reli zinazokidhi mahitaji ya usafirishaji wa shehena na abiria nchini na nchi jirani, kuwa na bandari za mwambao wa Bahari na zile za maziwa makuu zinazokidhi mahitaji ya usafirishaji wa abiria na shehena ndani na nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 252.758 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, hadi kufikia mwezi Machi 2013 fedha zilizokuwa zimetolewa na hazina zilikuwa shilingi bilioni 47.409 sawa na asilimia 24.98 ya fedha za ndani zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya taasisi ambazo ziliathirika sana kutokana na kutokutolewa fedha kwa wakati (asilimia waliyokuwa wamepokea kwenye mabano)

ni pamoja na *RAHCO* (21.2), *TRL* (11.8), *NIT* (0), *TPA* (0) na *TMA* (14.0).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwenendo huo wa fedha ilisababisha kazi zifuatazo kushindwa kuanza kama ifuatavyo:-

(i) Kushindwa kuanza kazi za upembuzi na usanifu wa uboreshaji na ujenzi wa miradi kama ya reli Tanga - Arusha, Arusha-Musoma, Tabora -Kigoma/Kaliua-Mpanda na Isaka-Mwanza;

(ii) Kushindwa kutekeleza miradi kama ya kununua na kukarabati injini na mabehewa ya treni na vifaa vingine; na

(iii) Kulimbikiza madeni kutoka kwa wakandarasi mbalimbali kama vile miradi ya viwanja vya ndege vya Mwanza, Tabora, Kigoma, Bukoba na Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata majibu juu ya masuala yafuatayo:-

(i) Nini kilipelekea hazina kushindwa kutoa fedha kwa wakati kama zilivyokuwa zimepitishwa na Bunge;

(ii) Ni hasara gani imepatikana kwa Serikali kutokana na ucheleweshwaji huo wa fedha; na

(iii) Tutapaswa kulipa riba au tozo la ucheleweshaji malipo kiasi gani kwa wakandarasi baada ya Serikali kushindwa kutekeleza mkataba wa malipo kwa wakati.

16 MEI, 2013

16 MEI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utangulizi huu nilioutoa, ni wajibu wetu kama Bunge na Wabunge kujiuliza swali la msingi; ni kwa nini Serikali inashindwa kutekeleza mpango wake wa bajeti kama ilivyoomba na kuidhinishwa na kupewa uwezo na Bunge wa kukusanya mapato kama walivyotarajia? Kushindwa kupeleka fedha wakati Mamlaka ya Kukusanya Mapato (*TRA*) kila mwaka wanavuka lengo la makusanyo. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya kazi kwa baadhi ya sekta zilizofanyika; kama nchi ili tuweze kupiga hatua katika maendeleo. Tulijiwekea Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao uliidhinishwa na Bunge lako Tukufu; ni vyema sasa tukadurusu Mpango huo kama unatekelezwa na unatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa usafirishaji wa reli, Mpango wa Maendeleo unasema kuwa, kutengeneza reli ambayo itakuwa shindani kwa usafirishaji wa mizigo mikubwa ambayo inasafirishwa kwenda au kutoka maeneo yaliyo mbali na inakokusudiwa kufika. Katika hilo mkakati mahususi ulikuwa ni kubadilisha na kuweka reli ya uzito wa ratili 80(lbs) katika Reli ya Kati badala ya reli iliyopo ya uzito mdogo. Kwa kufanya hivyo, ungewezesha Reli ya Kati kufanya kazi kwa kiwango chake cha juu, tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukidhi hitaji hilo, Mpango ulitenga shilingi milioni 272.6 kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/13. Kwa mujibu wa Randama, inayoonesha kuwa, bajeti iliyotengwa kwa *RAHCO* ilikuwa shilingi bilioni 30.9 na hadi mwezi Machi zilitolewa shilingi bilioni 6.6, sawa na asilimia 21.4. Kwa upande wa *TRL* ziliidhinishwa shilingi 104,160,000, hadi Machi zilitolewa shilingi 12,291,000.32 tu, sawa na asilimia 11.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni kwa nini inashindwa kusimamia yale ambayo inapanga na kuliomba Bunge kuidhinisha, kwanza, kwa kutokufuata matakwa ya Mpango

wa Maendeleo na pili hata kile kiasi kinachopitishwa bado hakitolewi kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu hadithi ya Mtume Muhammad (*S.A.W.*), kuhusu alama za mtu mnafiki kuwa ni tatu: Moja, Akiongea anaongea uongo; pili, akitoa ahadi, hatimizi ahadi zake; na tatu, akiaminiwa haaminiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwa kauli hiyo, Serikali ya CCM haina pa kutokea; wameaminiwa, wanatoa ahadi na hawatimizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Reli kama lilivyojulikana toka enzi hizo na sasa linaitwa Kampuni ya Reli (*TRL*), limekumbwa na matatizo makubwa ya ukosefu wa mtaji, nyenzo za kufanyia kazi, uhaba na uchakavu wa injini na mabehewa ya abiria na mizigo, pia wakati mwingine mafuta ya kuendeshea mitambo na si kwamba lilikosa biashara. Kampuni hii ilikuwa ni uti wa mgongo kwa uchumi hasa usafirishaji wa mizigo kwenda na kutoka Mikoa ya Kanda ya Kati, Magharibi na Ziwa. Matokeo sasa mizigo inasafirishwa kwa barabara na kusababisha matengenezo ya mara kwa mara kwa barabara zetu kutokana na usafirishwaji wa mizigo mikubwa kwa kutumia malori kama ilivyo sasa na kuongeza mara dufu Bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Dar es Salaam inaunganishwa na masoko ya bara (*hinterland*) na nchi jirani kupitia mtandao wa reli na barabara. Reli ya *TRL* inayoanzia Bandari ya Dar es Salaam ni tegemeo kubwa katika usafirishaji wa mizigo ya nchi za DR Congo, Rwanda na Burundi. Aidha, Reli ya *TAZARA* inatumika kusafirisha mizigo ya Zambia na Malawi. Kutokana na utendaji hafifu wa reli, mizigo mingi inasafirishwa kwa njia ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha uondoshaji wa mizigo bandarini kwa njia ya reli kimeshuka na hivyo kuathiri uwezo wa bandari zetu kushindana kikamilifu na bandari jirani katika kufikia masoko ya nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi, Rwanda na Uganda. Kwa mfano, shehena

yote ya mafuta kuelekea nchi za Rwanda, Malawi na DRC Congo inasafirishwa kwa njia ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya barabara ambayo imekuwa ndiyo tegemeo kwa kusafirisha karibu asilimia 90 ya shehena bandarini, imeendelea kuathiriwa na gharama kubwa za uchukuzi, safari ndefu za njiani (*Transit Times*), uwezo mdogo wa kubeba mizigo mizito na pia vikwazo vya njiani (*Non Tariff Barriers*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wote huu wa reli katika Uchumi wa Taifa letu, bado Serikali haionekani ikitilia umaanani unaotakiwa katika kuwekeza kwenye sekta hii ambayo pia ingesaidia katika kuzifanya barabara zetu ziweze kudumu kwa muda mrefu, kwani mizigo mingi ingekuwa inasafirishwa kwa njia ya reli badala ya barabara kama hali ilivyo leo. Ikumbukwe kwamba, ndiyo usafiri wa gharama nafuu kwa Watanzania maskini ukilinganisha na usafiri mwingine wa barabara au anga.

Kambi Rasmi ya Upinzani, inashangazwa sana na Serikali kutenga kiasi cha shilingi bilioni 113.124 kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa vichwa vya treni, mabehewa, kulipa madeni na matengenezo ya kawaida ya njia ya reli yanayosimamiwa na *TRL*. Aidha, Serikali kutenga kiasi cha shilingi bilioni 51.135 kwa ajili ya Miradi ya Miundombinu ya Reli inayosimamiwa na *RAHCO*. Fedha hizi zitasosha kweli katika kuimarisha miundombinu ya reli? Wakati huo huo Serikali hii inakuwa na ndoto ya kusafirisha mizigo tani 800,000 ifikapo 2014 na tani milioni tatu ifikapo 2015. Kwa bajeti hii na ambayo haitolewi ipasavyo, ni ndoto ya saa sita mchana; vinginevyo, tupewe maelezo ya kina itafikiaje lengo hili na mtaji unatoka wapi na kwa masharti gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumiani ya Kambi ya Upinzani kuwepo kwa Bodi ya *TRL* itashughulikia kwa haraka, kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa reli, kuendeleza Chuo cha Reli Tabora, kulipa mafao na stahiki zao kwa wakati na waweze kukopesheka kama watumishi wengine. Aidha, Bodi itaharakisha mchakato wa kupata injini na mabehewa ya

abiria kwenda Mwanza, Kigoma na Mpanda. Pia kuimarisha karakana za Dar es Salaam, Morogoro na Tabora, pamoja na kufungua stesheni zilizofungwa ili kurahisisha na kuharakisha safari kwa ajili ya kupishana kwa gari moshi kwa uharaka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya wafanyakazi wengi wa Shirika la Reli Tanzania (*TRL*), wanapendekeza Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (*RAHCO*) ivunjwe, kwani kusudio la kuanzishwa kwake kwa sasa halipo kwa kuwa reli inamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, *RAHCO* wajibu wao ni kuhakikisha njia ya treni (reli) ipo katika hali nzuri kwa usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo. Wameshindwa kabisa kusimamia mali zilizokuwa za *TRC*, ikiwemo viwanja, majengo, mitambo, mabehewa na rasilimali zingine. Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya Uchunguzi Maalum (*Special Audit*) kwa mali zote zilizokuwa za *TRC* na mgawanyo wa mali na *TRL* na taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni.

Kwa kuwa zilizokuwa mali za *TRC* inonekana kuwa hazina msimamizi, viwanja vinaporwa, majengo yanauzwa, hati za umiliki kwa maeneo yao haijulikani ziko wapi. Mfano mzuri wa maeneo yaliyokuwa yanamilikiwa na *TRC* hapa Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na kadhalika, yamevamiwa na watu na kujimilikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha nyingi zimekuwa zikipelekwa *RAHCO* kwa ajili ya matengenezo ya reli ya dharura kati ya Stesheni ya Gulwe na Kilosa mwaka hadi mwaka, mvua zikinyesha kidogo usafiri unasimama au kuleta ucheleweshaji usio wa lazima kwa safari za treni.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku wakielewa kabisa kuwa, ufumbuzi wa tatizo hilo ni kujenga Bwawa la Kidete na mabwawa mengine manne. Kambi ya Upinzani inataka kujua mkakati wa Serikali kuhusiana na kumaliza tatizo hilo linalojirudia mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kaliua - Mpanda, kumekuwapo na malalamiko kuwa matengenezo yanayofanywa na Kampuni ya *R & A* yako chini ya kiwango, hayaridhishi na ni ya gharama, ukilinganisha na uwepo wa magenge kama ilivyokuwa hapo awali. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kurejesha magenge na kuajiri wafanyakazi waliofahamika kama pigilia na kuwepo kwa Wakaguzi wa Njia (*PWI*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania ni nchi ambayo kijiografia imekaa kuhudumia nchi ambazo hazikubahatika kuwa na ukanda wa bahari, hivyo basi fursa hiyo ndiyo ilipelekea kuundwa au kuanzishwa kwa Mamlaka itakayosimamia shughuli za usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*). Majukumu ya Mamlaka ni kuendeleza huduma za kibandari, kuweka viwango na masharti mengine kwa watoa huduma, kusimamia na kudhibiti huduma za bandari na kulinda mazingira ya usalama wa bandari kwa viwango vinavyokubalika kwa watumiaji wa Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutumiza majukumu yake, Mamlaka ya Bandari inawajibika kuishauri Serikali aina ya uwekezaji na maeneo ya uwekezaji ambayo yataongeza tija kwa watumiaji wote wa bandari na hivyo kuifanya bandari hiyo kuwa chanzo kikubwa cha uchumi wa nchi yetu kama ilivyokuwa kwa nchi ya Singapore.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba, kama Singapore ambayo miaka ya 70 kiwango cha maendeleo na ukuaji wa uchumi, tulikuwa tunalandana nayo na fursa tulizonazo hasa za kuhudumia nchi ambazo hazina bandari na hivyo bandari yetu kuwa mgodi katika uchangiaji wa mapato ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa bandari ni kwamba, Bandari ya Dar es Salaam, inashughulikia takribani asilimia 75 ya biashara zote za nje; na kwa kuwa mahitaji yanazidi kuwa makubwa, jambo linalopelekea msongamano mkubwa wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, jambo

hili limesababisha waagizaji wa mizigo kuhamia Bandari ya Mombasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Mpango wa Taifa wa Maendeleo lilikuwa ni kuongeza uwezo wa bandari kuhudumia shehena nyingi kwa muda mfupi ambapo ilikadiriwa kumudu shehena kutoka tani milioni 7.13 hadi tani milioni 9.87, kupunguza muda wa meli kufika na kuondoka bandarini kutoka siku 4.4 hadi siku mbili.

Bajeti iliyokuwa imepangwa kwa mwaka 2012/2013 ni shilingi 129,124,000 (Rejea Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano, ukurasa wa 81). Kwa mujibu wa Randama ya Utekelezaji ya Wizara ya mwaka 2012/13, inaonesha kwamba, Bandari ilitakiwa kuhudumia shehena tani milioni 12.65, lakini hadi Desemba ilihudumia shehena tani milioni 6.014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tofauti hizi za takwimu, inaonesha kuwa, hakukuwepo na mashauriano na uhakiki wa takwimu baina ya Tume ya Mipango, Wizara na Mamlaka ya Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina taarifa kuhusiana na meli kukaa siku 19 bila kuhudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam. Kwa mwaka 2012, Meli ya *Maersk Alabama* ilikaa kwa siku 19, Meli ya *E M ANDROS* ilikaa kwa siku 11 na Meli ya *SAFMARINE KURAMO* ilikaa siku 10 na nyinginezo nyingi. Hali ambayo iliwafanya mawakala wa meli kuiandikia barua *TPA* baada ya wamiliki wa meli hizo kutishia kutokufanya kazi na *TPA* na badala yake kuwa na mpango wa kuhamisha kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ucheleweshaji wa kupakua meli bandarini, bado lipo tatizo lingine la mamlaka kutokujibu barua kwa wakati na hivyo kuwafanya wenye meli kufikiria kuhamia Bandari ya Mombasa. Kwa mfano, meli zinazomilikiwa na *IGNAZIO MESSINA* kutoka Italy, zimekuwa zikitia nanga upande wa *TPA* kwa miaka mingi na kwa sababu ni meli za aina ya *RORO*, tofauti na meli nyingine za *containers*, huwa wanashusha na kupakua kwa vifaa vyao

wenyewe ambavyo huhifadhiwa kwenye eneo maalum bandarini na kwa mkataba maalum. Kutokana na kuwa Bandari hawatoi vifaa vyovyote katika kutoa huduma kwenye meli hizi zaidi ya *documentation* ya kawaida, huwa wanapewa *reduction* au *rebate* kutoka kwenye bandari husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na urasimu mkubwa katika utendaji wa Mamlaka ya Bandari, jambo linalopelekea kukosa biashara. Kutokana na kasoro hizo, baadhi ya wenye meli wameamua kuhamishia biashara zao katika Bandari ya Mombasa kama barua ya Kiambatanisho A, inavyoonesha. Kambi Rasmi ya Upinzani inajuliza ufanisi wa bandari yetu uko wapi kama hata kujibu barua au kufanya maamuzi inachukua zaidi ya miezi sita? Kwa nini hatujui kuwa biashara ni muda? Aidha, tunataka kujua tutapoteza mapato kiasi gani kama kampuni hii ikiondoka katika Bandari yetu ya Dar es Salaam na kuhamia Mombasa? Hii ni dhahiri kuwa, bado tuna safari ndefu sana katika kufikia malengo ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna haja ya kuiangalia Mamlaka ya Bandari na mipango yake ya maboresho kwa ukaribu zaidi na kuharakisha mchakato wa kupata watendaji wenye sifa na uwezo wa kuendesha biashara ya bandari na kuwathibitisha wale wote ambao wanakaimu kama wamekidhi sifa na vigezo vinavyotakiwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Bodi ya Mamlaka ya Bandari ishughulikie jambo hili kwa umuhimu na uharaka wa kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanisi mwema na wenye tija wa mamlaka kwa upande mmoja ni kukaribisha makampuni makubwa ya meli duniani kuleta meli zake hapa nchini. Kosa lililofanywa la kuuu Wakala wa Meli wa Taifa (*NASACO*) kwa maslahi ya watu wachache, kumeendelea kulipotezea Taifa mapato mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusambaratishwa kwa *NASACO* kumeendelea kuziletea sifa mbaya Bandari zetu

kwani mizigo haramu mingi inayokamatwa nje ya nchi inatokea Bandari za nchi yetu, ukiacha mbali kontena lililokamatwa mwaka 2009. Gazeti la kila wiki la *The East African* la *May 4 -10, 2013* linasema kuwa, kontena lingine limekamatwa Singapore likitokea Bandari ya Dar es Salaam likiwa limewekewa nembo kuwa *spare part* kutoka Burundi, wakati lilikuwa limesheheni meno ya tembo. Hivi ni kweli *spare part* zinaweza kusafirishwa kutoka nchi ya Burundi kwenda Singapore?

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mtandao unaotengenezwa kati ya wamiliki wa meli na makampuni yao ya uwakala, kwani sisi kama nchi, hatuna uwezo wa kukagua aina ya mizigo inayotoka au kuingia. Kazi hii hapo zamani ilikuwa inafanywa vyema na *NASACO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya kwa Serikali siyo mapya, kwani katika mkutano wa Mheshimiwa Waziri na Chama cha Wakala wa Forodha (*TAFFA*), alielezwa kwamba, kuna wamiliki wa meli ambao pia wanafanya kazi ya kuingiza na kutoa mizigo bandarini, jambo ambalo ni kinyume cha sheria. Kwa mujibu wa Sheria za Mamlaka ya Udhubiti wa Vyombo vya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (*SUMATRA*) ni marufuku Kampuni ya Wakala wa Meli kuwa na leseni ya kuingiza na kupakuwa mizigo bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushahidi huo ni kwamba, watendaji ndiyo wanaoshiriki kuikosesha mapato nchi; ni kwa vipi leseni ya kufanya uwakala zinatolewa kwa wamiliki wa meli? Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, Serikali hii ya CCM ndiyo inayohujumu uchumi wa nchi hii, kama Viongozi wa *TAFFA* walivyomweleza Mheshimiwa Waziri. Sasa ni muda mwafaka kwa Mheshimiwa Waziri kulieleza Bunge na Watanzania wote, ni vigogo wepi wanaomiliki Makampuni ya Uwakala wa Meli wakati umiliki wao kwenye Makampuni hayo hisa zao siyo zaidi ya asilimia 50? Hii ni kwa ajili ya Sheria ya *Shipping Agency Act, 2002*, kifungu cha (7). Kwa maana nyingine, wanatumika na wamiliki wa meli kuihujumu kwa wamiliki wa meli kumiliki pia Kampuni za Uwakala wa Meli

zao na hivyo fedha zinazobaki ndani kuwa kidogo kulinganisha na kusudio la sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kandarasi iliyotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa Kampuni ya China *Communication Construction Company Ltd (CCC)*, iliyoleta mtafaruku mkubwa hapa nchini ya kujenga Ghati 13 & 14 katika Bandari ya Dar es Salaam, mpango ambao ulitokana na mpango mkuu wa bandari nchini (*Port Master Plan 2009-2028*), mradi ambao ulikisiwa kutumia kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 323, sawa na shilingi bilioni 517 za Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi kuhusu uteuzi wa Mshauri Mwelekezi na mkandarasi katika Mradi huu iliyotolewa tarehe 9 Novemba, 2012 na *PPRA*, Kamati ya Uchunguzi kuhusu uteuzi wa Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa ujenzi wa Gati Namba 13 na 14 katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa, katika Mkutano wa Saba wa Bunge uliofanyika mwezi Aprili, kulikuwa na majadiliano ya kina kuhusiana na ujenzi wa gati hizi na Bunge liliagiza kuwa Mradi huu utekelezwe kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya Exim ya China kama ilivyokuwa imependekezwa na Mamlaka ya Bandari. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata majibu juu ya masuala yafuatayo:-

(i) Mchakato wa ujenzi wa Ghati 13 na 14 umefikia wapi mpaka sasa?

(ii) Je, mchakato wa kumpata mkandarasi mpya kwa ajili ya ujenzi huo umefanyika au bado?

(iii) Baada ya kusitishwa kwa mchakato wa mkataba wa awali ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali dhidi ya waliohusika na mchakato ambao ulikiuka sheria za nchi?

(iv) Je, ni lini ujenzi wa Gati hizi utakamilika ili kuweza kwendana na Mpango Mkuu wa Bandari Nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara ya Rais wa China hapa nchini mwezi Machi, 2013, miongoni mwa Mikataba ambayo ilisainiwa baina ya Serikali yetu na ile ya Watu wa China ni Makubaliano ya jumla ya Ushirikiano wa Kimkakati kuhusu uendelezaji wa Kanda Maalum ya Kiuchumi ya Bagamoyo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya *China Merchant Holding International (CMHI)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya ziara hiyo, Watanzania kupitia vyombo mbalimbali vya habari walitangaziwa kuwa miongoni mwa mikataba iliyosainiwa ni pamoja na ujenzi wa bandari mpya ya Mbegani – Bagamoyo. Aidha, kwenye Randama ya Wizara, ukurasa wa 17 inaonesha kuwa, moja ya majukumu yatakayotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ni ujenzi wa Bandari ya Mbegani (Bagamoyo).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusainiwa kwa Mkataba huu mkubwa wa kihistoria katika ujenzi wa bandari hii, pamekuwepo na usiri mkubwa kuhusiana na Mkataba wenyewe na hali hiyo imefanya uwepo wa maneno mengi sana kuhusiana na vipengele vya Mkataba huu. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata majibu kuhusiana na masuala yafuatayo juu ya Mkataba huu wa ujenzi wa bandari hii:-

(i) Ni kweli kuwa baadhi ya vipengele vya Mkataba huu vinakataza uendelezwaji wa bandari nyingine zilizoko karibu na Bagamoyo kwa miaka 50 ijayo?

(ii) Je, ni kweli kuwa sehemu ya Bandari hii itatumiwa na Wachina kwa ajili ya matumizi ya kijeshi kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara?

(iii) Je, uendeshaji na usimamizi wa Bandari hii utafanywa na Watanzania ama ni Wachina?

(iv) Kama ni Wachina, uendeshaji na usimamizi utakuwa ni kwa muda gani? Wahenga walisema rahisi ni ghali; Serikali ina hisa kiasi gani katika Mradi huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kuhakikisha usalama au kufanya ukaguzi wa miundombinu, vifaa na utoaji wa leseni kwa ajili ya vyombo vya usafirishaji wa majini, nchi kavu na angani, limewekwa chini ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri Majini na Nchi Kavu (*SUMATRA*). Kwa maana hiyo basi, ukaguzi wa treni, meli na magari yanayosafirisha abiria na mizigo yamekasimiwa kwa Mamlaka hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya kuhakiki ubora na usalama wa vyombo hivyo vya abiria na mizigo, pia mamlaka hii ina jukumu la kuhakiki sifa za wafanyakazi wanaohudumia vyombo hivyo na pia kutoa leseni kwa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu utendaji usioridhisha wa mamlaka hasa katika kufanya ukaguzi wa vyombo vinavyofanya kazi zake baharini, kwani ajali zinazotokea katika Maziwa na Baharini ni kutokana na kutokuwepo kwa usimamizi madhubuti wa Mamlaka hii. Msingi wa kutokuridhishwa huku ni kutokana na takwimu za ajali za majini zilizotokea kati ya Julai, 2012, na Januari 2013, zilitokea ajali 14 ambapo jumla ya watu 231 walipoteza maisha. Kwa kipindi kama hicho mwaka 2011/2012 zilikuwa ni ajali 10 na watu 218 walipoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya ni kwa jinsi gani Mamlaka hii itafanya kazi zake ili kukidhi matarajio ya uanzishwaji wake, kwani inaonesha kuwa mbinu zinazotumika kwa sasa zimeshindwa kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na matatizo hayo ya ajali, kuna tatizo lingine linalohusu viwango vya ada za leseni kwa usafirishaji wa abiria kwa pikipiki na pikipiki za magurudumu matatu (bajaji). Kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa na *SUMATRA* kwa mujibu wa Sheria ya Leseni za

Usafirishaji (Pikipiki na Bajaji) ya Mwaka 2010, zilizotolewa tarehe 12 Machi, 2010 na kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2011, inaonesha kuwa ada ya leseni kwa pikipiki ni shilingi 20,000 kwa mwaka na ada ya maombi ya leseni ya pikipiki ni shilingi 2,000 na hivyo kufanya ada kwa mwaka kuwa shilingi 22,000. Kwa upande wa bajaji (magurudumu matatu), ada ya leseni kwa mwaka ni shilingi 30,000 na ada ya maombi ya leseni ni shilingi 2,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya Utoaji Leseni za Usafirishaji Abiria Barabarani za Mwaka 2007, *The Transport Licensing (Road Passenger Vehicles) Regulation 2007*; ambazo ndiyo kanuni zinazoiongoza *SUMATRA* katika utoaji leseni za usafirishaji wa abiria barabarani. Kanuni ya Tatu inatamka kuwa, gari la abiria, maana yake ni gari la abiria, lenye uwezo wa kubeba watu zaidi ya saba na dereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia ada ya leseni kwa mwaka, gari inayobeba abiria hadi 15 ni shilingi 20,000, maana yake ni kuwa hii ni sawa na ada inayolipwa na pikipiki inayobeba abiria mmoja. Kwa upande wa bajaji, ada yake kwa mwaka ni sawa na gari la abiria linalobeba abiria 16 hadi 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia kwa makini viwango hivi wanavyotozwa wafanyabiashara wa bodaboda na bajaji kama kweli zina uhalisia kulinganisha na viwango vinavyolipwa na magari mengine ya abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, kumekuwepo na malalamiko na kunyanyaswa kwa wamiliki wa magari aina ya *Noah*. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni kwa nini Mamlaka ya Utoaji Leseni (*SUMATRA*), kinyume cha sheria inakataa kutoa leseni za usafirishaji abiria kwa magari aina ya *Noah*; wakati aina hiyo ya magari inao uwezo wa kubeba zaidi ya watu wanane na dereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sababu zinatolewa kuwa usalama wa magari hayo ni mdogo; je, ni kweli usalama

wa *Noah* ni mdogo kuliko wa pikipiki na bajaji ambazo zimepewa leseni kisheria? Kama kweli usalama wa magari hayo ni mdogo kiasi hicho, ni kwa nini mamlaka zinazohusika zimeruhusu uingizwaji wa magari nchini ambayo usalama wake ni mdogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia kitendo cha kunyima leseni za usafirishaji wa abiria magari aina ya *Noah* siyo tu kinaongeza ugumu wa usafiri maeneo mengi ya miji, lakini pia inanyima Wananchi fursa za ajira za kuwaongezea kipato na kuboresha maisha yao, pia kuna harufu ya rushwa na ufidadi na hasa ikizingatiwa kuwa hakuna ushahidi wa kisayansi kuwa magari hayo usalama wake ni mdogo, kama ambavyo mamlaka husika inataka Watanzania waelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka utaratibu ambao utasababisha kuwa shughuli za magari hayo uwe kwenye umbali fulani wa eneo husika na si kwa safari ndefu, lakini siyo kupiga marufuku kwa kunyimwa leseni za usafirishaji na huku tukijua wazi kuwa, nchi yetu ipo kwenye soko huria ambapo mlaji anakuwa na fursa ya kuchagua atumie usafiri wa aina gani na siyo kuchaguliwa na *SUMATRA* kuwa lazima watumie mabasi au daladala kwa ajili ya usafiri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata msimamo wa Kisera wa Serikali kuhusiana na Sekta ya Usafirishaji wa Nchi Kavu na Mamlaka ya *SUMATRA* katika kuamua ni magari ya aina gani yapewe leseni za usafishaji na yapi yasipewe ili Wananchi waweze kujua kama wayaingize magari haya kwa matumizi gani. Kumekuwepo pia malalamiko ya viwango vikubwa vya faini vinavyotozwa na *SUMATRA* kwa kuzingatia kanuni na siyo kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu (*Penal Code*) kwa makosa yale yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la usimamizi wa meli katika Maziwa. Kwa mujibu wa randama ya Wizara, ukurasa wa nane, iliyowasilishwa mbele ya Kamati ya Bunge, inaonesha kuwa kati ya changamoto zilizojitokeza katika

utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013 ilisema kuwa, nanukuu: Sehemu ya (iii): *“Kushindwa kufanya ukarabati wa meli katika Maziwa, yaani Ziwa Tanganyika, Ziwa Viktoria na Ziwa Nyasa, hii inaonesha wazi kuwa, Serikali imeshindwa kuzuia ajali ambazo zingeweza kuepukwa kwenye Maziwa haya kutokana na kushindwa kutimiza wajibu huu muhimu wa kukarabati meli zilizo na ambazo ni za muda mrefu sana na nyingine huzimika injini zikiwa katikati ya safari. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa ajali za mara kwa mara kwenye vyombo vya usafirishaji vya majini hasa meli hapa nchini na kusababisha maafa makubwa baharini, kwa mujibu wa takwimu za *SUMATRA* ni kuwa, vyombo vidogo huchangia asilimia 78.6 ya ajali zote. Taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (*SUMATRA*) inasema hali hii ilitokana na meli kuwa chache, wakati vyombo vidogo na ambavyo havitambuliwi na mamlaka hayo ni vingi na hubeba abiria na mizigo mingi kwa ujumla wake kuliko meli zilizo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali nyingi zimesababishwa na ama vyombo husika kutokidhi ubora unaohitajika kwa mujibu wa sheria, hali mbaya ya hewa, upakiaji wa abiria na mizigo kuzidi kiwango na uwezo wa chombo husika na vyombo kuendeshwa na wafanyakazi wasio na sifa au uzoefu unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa za *SUMATRA* ni kuwa, *SUMATRA* imesajili jumla ya meli 90, kati ya hizo 50 zipo Bahari ya Hindi, 34 Ziwa Viktoria, nne Ziwa Tanganyika na mbili Ziwa Nyasa. Aidha, *SUMATRA* inakadiria kuwa kuna vyombo vingine vipatavyo 50,000 vinavyofanya safari majini nchi nzima. Pia yapo maelfu mengine ya vyombo vya usafiri kwenye mialo na bandari ndogo na ambavyo vinabeba abiria maelfu kwa maelfu ambavyo viko nje ya orodha na Mamlaka ya *SUMATRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huu ni kuwa, *SUMATRA* hawana takwimu za kuthibitisha vyombo vilivyopo wala hakuna mpango mkakati wa kudhibiti ajali nje ya duara

lao la vyombo ambavyo wanavifahamu na au vile ambavyo vikipata ajali na kutangazwa na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari, 2006 hadi Desemba, 2010, kulikuwa na matukio 54 ya ajali zilizosababisha vifo vya watu 237 na 662 kuokolewa. Takwimu zinaonesha kuwa, mwaka 2006 kulikuwa na jumla ya ajali tano zilizoua watu 57; mwaka 2007 kulikuwa na ajali 11 zilizoua watu 20 na mwaka 2008 watu 71 walikufa katika ajali 12. Mwaka 2009 kulikuwa na ajali 13 zilizoua watu 35 na mwaka uliofuata, watu 54 walikufa katika ajali 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali 21 zilitokea Ziwa Viktoria, mbili katika Ziwa Tanganyika, moja katika Ziwa Rukwa na 28 katika Bahari ya Hindi. Ajali mbili zilitokea katika Mito ya Ruvuma na Rufiji. Kwa upande wa vifo vilivyotokana na ajali hizo, 126 vilitokea katika Ziwa Viktoria, 44 katika Ziwa Tanganyika, 40 katika Bahari ya Hindi na vinane katika Ziwa Rukwa. Vifo kumi vilitokea Mto Ruvuma na vingine tisa katika Mto Rufiji. Kwa ujumla, Ziwa Viktoria ndiko kumekuwa na matukio mengi ya vifo, ambapo katika kipindi cha tathmini ni asilimia 53 ya vifo vyote. Aidha, kwa mwaka 2012/2013 idadi ya ajali za majini kwa upande wa Tanzania Bara zilikuwa 14, ambapo jumla ya watu 231 walipoteza maisha na ongezeko hili la ajali ni sawa na asilimia 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kuhusiana na masuala yafuatayo:-

(i) Kuna mikakati gani ya kushughulikia ajali za majini zinazohusu meli na vyombo vidogo ambavyo ni vingi kama ambavyo takwimu zinaonesha?

(ii) *SUMATRA* ina mikakati gani ya kukagua vyombo vyote vya majini kabla ya safari ili kuhakikisha kuwa vina usalama wa kutosha kwa ajili ya abiria wanaovitumia vyombo hivyo ili kupunguza madhara ya ajali na vifo?

(iii) Kuna mpango gani wa kufanyia ukarabati meli zinazofanya safari kwenye Maziwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari za Maziwa na Kampuni ya Huduma za Meli (*MCCL*), ni kampuni ambayo kazi yake ni kutoa huduma katika Maziwa Makuu ya Tanganyika, Nyasa na Viktoria, kwa kuimarisha mawasiliano na kusimamia usalama kwa vyombo vinavyosafari katika Maziwa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za Taarifa ya Hali ya Uchumi iliyotolewa mwezi Juni, 2012, inaonesha kuwa; Mwaka 2011, Kampuni ya Huduma za Meli (*MSCL*), ilisafirisha jumla ya tani 63,682 za mizigo na abiria 297,763, ikilinganishwa na tani 78,639 za mizigo na abiria 328,234 waliosafirishwa mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 19 kwa mizigo, ukilinganisha na mizigo iliyosafirishwa kwa mwaka uliopita.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua yafuatayo:-

(i) Nini kilipelekea kupungua kwa shehena za mizigo zilizosafirishwa na kampuni hii ya huduma za meli nchini?

(ii) Kwa nini hadi sasa hajapatikana wakala wa kupakia na kupakua mizigo (*clearing & forwarding agency*) katika Bandari ya Kigoma na nini athari yake kwa uchumi na maendeleo ya Bandari hiyo?

(iii) Hatua zilizochukuliwa za kulinda, kuhifadhi na kusajili maeneo yanayomilikiwa na Mamlaka ya Bandari kwa Bandari za Mwanza na Kigoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwepo na tabia kwamba, wamiliki wa meli zinazofanya kazi katika Maziwa hayo ndiyo hao hao wanaoshughulika na utafutaji, upakiaji na upakuaji wa mizigo kwa meli hizo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, kutokana na uzoefu uliooneshwa na wamiliki wa meli zinazofanya kazi zake Bahari ya Hindi na hasa kwa Bandari za Dar es Salaam na Mtwara kuwa mapato ya nchi yamekuwa yakipotea ama yakiibiwa

na wamiliki wa meli. Hivyo basi, sasa ni muda mwafaka kwa Serikali kuanzisha rasmi wakala au kitengo maalum kwa ajili ya meli zinazofanya shughuli zake kwenye Maziwa tajwa hapo juu, kwa sababu zile zile zilizopelekea kuwepo kwa Sheria ya *Shipping Agency* ya Mwaka 2002, ambayo inasimamiwa na *SUMATRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (*TCAA*) ni pamoja na kudhibiti usafiri wa anga, kudhibiti huduma za viwanja vya ndege na kutoa huduma za uongozaji ndege hapa nchini katika viwango vya kimataifa. Pamoja na umuhimu wa mamlaka hii kwa Taifa, hatujawekeza vya kutosha katika kuiimarisha Mamlaka hii.

Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kujua Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi, kati na mrefu wa kuimarisha mamlaka hii kwa masilahi ya Taifa letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*), kuhakikisha wakandarasi wanaojenga viwanja vya ndege wanamaliza kazi zao kwa mujibu wa Mikataba waliyowekeana na Serikali. Aidha, Serikali nayo itimize wajibu wake wa kuchangia sehemu ya fedha kwa mujibu wa mikataba hiyo ili viwanja vya Mwanza, Tabora na Kigoma vikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Mamlaka inatakiwa ilipe fidia stahiki na kwa wakati, kwa maeneo yote ambayo yametwaliwa kwa ajili ya upanuzi wa viwanja vya ndege. Pia wawe tayari kushughulikia malalamiko ya mapunjo ya fidia toka kwa Wananchi ili kuepuka kesi zinazoweza kusimamisha Miradi ya Ujenzi wa viwanja hivyo.

Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata maelezo ya kina kuhusu ujenzi wa *Terminal III* kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Julius K. Nyerere Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ubia ya Meli Kati ya Tanzania na China (*SINOTASHIP*), ambayo hutoa

huduma za usafirishaji wa masafa marefu baharini kwa mizigo na bidhaa za kibiashara, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2012, ilisafirisha mizigo takribani tani 300,000. Watanzania wanataka kujua Kampuni hii ina meli ngapi na Serikali inapata kiasi gani kwa mwaka kama gawio na inalipa kodi kiasi gani? Pia Uongozi wa Kampuni hiyo na ikama ya Watumishi Watanzania ni wangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), limethibitika sasa kuwa haliwezi kufufuliwa tena kutokana na uzoefu wetu wa miaka mingi kuwa tumesikia kila mara kuwa kuna mpango wa kulifufua, huku likiwa lina ndege moja, lakini tukiendelea kulipa wafanyakazi wengi kila mwaka wakati hawana kazi za kufanya na huku wenzetu wa nchi ya Rwanda wakisonga mbele katika kununua ndege. Viwanja vya ndege tunavyojenga nchi nzima ni kwa ajili ya matumizi ya ndege zipi au tunajenga kwa ajili ya matumizi ya wenzetu katika Jumuiya ya Kanda ya Afrika ya Mashariki?

Kambi Rasmi ya Upinzani, inashauri kuwa sasa ni wakati mwafaka Shirika hili likafilisiwa na tukaanza upya, badala ya kuendelea kutenga fedha kila mwaka kwa Shirika ambalo halina tija. Ni vyema tukajua kuwa, fedha zinazotengwa si kwa ajili ya kufufua au kununua ndege bali ni kulipia ufisadi uliotangulia. Kuanza upya siyo ujinga ni kujiimarisha na kujisahihisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taasisi zingine zilizo chini ya Wizara hii ambazo ni muhimu sana kiutendaji, lakini zinaonekana kutokuwa na umuhimu kwa sababu ya kutokutengewa fedha za kutosha kutekeleza mipango yake. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Chuo cha Usafirishaji, Chuo cha Ubaharia, Chuo cha Usafiri wa Anga, Chuo cha Hali ya Hewa na Chuo cha Bandari.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuimarisha taasisi hizi na kuzijengea uwezo ili zitekeleze majukumu yake, ikiwa pamoja na kuendelea rasilimali watu katika taaluma mbalimbali zinazotolewa na vyuo hivyo. Aidha, Mamlaka ya

Usafiri wa Anga na Mamlaka ya Hali ya Hewa ni muhimu kwa Ustawi na Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul, kwa hotuba yaako.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia katika hatua ya uchangiaji. Naomba mchangiaji wetu wa kwanza awe Mheshimiwa Godfrey Zambi, Kamishna na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto atafuatia.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache kufuatia Hotuba ya Wizara ya Uchukuzi iliyowasilishwa hivi punde na Mheshimiwa Waziri Dkt. Harrison Mwakyembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, pamoja na msaidizi wake, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Tizeba, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara hii tangu wameingia. Hapana shaka kila Mtanzania anayeona na anayesikia, anaona kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara hii, tunawapongezeni sana na tunaomba mwendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza linahusiana na jambo ambalo Waziri amelisema, lakini na wasemaji wengine pia wamelisema. Ningeliomba sana, Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa sababu ni mambo muhimu sana haya pamoja na kwamba wameweka mwelekeo.

La kwanza, ambalo ningelipenda niseme na niseme tu kwamba, nataka niwasemee hawa Watanzania, wanyonge, wa chini, ambao hawana namna nyingine au mahali pa kukimbilia zaidi ya kukimbilia kwa wawakilishi wao

Wabunge na watu wengine kama vile Madiwani katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, gari za *Noah*, zimeingia nchini nyingi sana na vijana wengi wamekwenda kwenye Mabenki wamekopa kwa ajili ya kufanya biashara hiyo. Kwa bahati mbaya sana, wamekumbana na vikwazo vingi sana. Ninalisema hili kwa sababu nina uzoefu, kule Mkoa wa Mbeya, tumeyashughulikia malalamiko, misugvano ya wao na Polisi, misugvano ya wao na *SUMATRA*, wakaonekana hawana mahali pa kukimbilia. Ni faraja kwamba, Mheshimiwa Waziri amesema sasa ameiagiza *SUMATRA* ianze kutoa leseni baada ya wamiliki wa magari hayo kutimiza mashari fulani fulani.

Mheshimwa Naibu Spika, lakini masharti haya mengine yasije yakawa nayo ni kikwazo; kwa mfano, unasema lazima gari liwe na viyoyozi; magari mangapi ya abiria katika nchi hii yana viyoyozi maana hilo wanaweza wakaona kwamba kimekuwa kikwazo? Kama halina kiyoyozi maana yake usifanye kazi. Tuelezwe magari mangapi katika nchi hii, hata mabasi yanayokwenda safari ndefu hayana viyoyozi. Kama ni sharti, basi liwe kwa magari yote ya abiria ambayo yanafanya kazi katika nchi hii.

Sijaona, Dar es Salaam pale, ambapo pana magari mengi kama yana viyoyozi. Kwa hiyo, hilo ninaomba lisije likawa sharti. Pia tunaomba jambo hili, kwa wale wanaotimiza masharti waruhusiwe na waanze kufanya kazi mapema bila vikwazo vyovyote. Hivi ninavyosema, Watanzania wengi wanaomiliki magari haya, wawe Arusha, Mwanza, Mbozi, Mbeya, Kyela, Dar es Salaam, Morogoro na maeneo mengine ya nchi hii, wanasikiliza na bila shaka wamefualilia taarifa ya Waziri na tuone kwamba hili kwa kweli linatekelezwa mapema inavyowezekana.

Suala la pili, linahusu waendeshaji wa pikipiki na bajaji za miguu mitatu. Jambo hili Serikali ilishalitolea maelekezo mwaka jana. Mheshimiwa Waziri Muu mwenyewe, alitoa maelekezo na Waziri wa Fedha alitoa maelekezo,

inashangaza maelekezo yaliyotolewa na Serikali mpaka leo hayajatekelezwa na Serikali yenyewe na kwa maana hiyo, kupitia watu wa *TRA*.

Ninaomba nitoe mfano; kwanza, katika hili la bodaboda na pikipiki, ninaomba niseme watu wa Mbozi kwa ujumla ambao wanajihusha na biashara hii, ninazo karatasi zao hapa, wako zaidi ya 600. Wana Chama chao na wamejisailli, lakini wanasumbuliwa na kodi nyingi sana. Wana kodi, kwa mfano, *Motor Vehicle* wanalipa, Bima wanalipa, *sticker* za Halmashauri maegesho. Kodi nyingi sana wanazolipa watu hawa, ukizingatia biashara anayoifanya sijui inamwingizia shilingi ngapi kwa siku mpaka um-*subject* kwenye kodi nyingi za namna hii! Sasa ninaomba kwa sababu Serikali ilishaahidi na naomba nirejee, nimeshasema hapa Bungeni mara kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo *Hansard* ya tarehe 22 Juni, 2012, ambayo Waziri wa Fedha tulipokuwa tumekubaliana kwamba, tunaondoa kodi ya ushuru kwa watu wa pikipiki, imetangazwa hivyo lakini haijatangazwa na sasa kutoka ushuru wa Sh. 95,000 waliokuwa wanalipa wakati ambao Serikali ilisema itauondoa, sasa hivi wamepandishiwa wanalipa Sh.100,000. Sasa haya ni maajabu sana, Serikali inasema hivi halafu utekelezaji unakuwa vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niisome inasema hivi: "Mheshimiwa Naibu Spika, bada ya kusikiliza mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge walio wengi kuhusu suala la utozaji vijana wa bodaboda, Serikali inapendekeza kuwa tabaka la kwanza libadilishwe kutoka mapato yasiyozidi Sh. 3,000,000 na kuwa mapato yasiyozidi Sh. 4,000,000. Tukipandisha hilo, tabaka la kwanza kutoka Sh. 3,000,000 mpaka Sh. 4,000,000 kama mapato ghafi ya chini ya kiwango cha kutoza kodi, kiwango hiki cha chini kisichotozwa kodi kinapendekezwa kupandishwa ili kuwafanya vijana wetu wanaofanya biashara walio wengi, wadogo wadogo, kutotozwa kodi ya mapato ya Serikali Kuu."

Mheshimiwa Waziri wa Fedha hii ni kauli yake na aliposema hivyo alipigiwa makofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, akaendelea akasema; "Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ndivyo tunavyoamini kwamba, vijana wetu wa bodaboda na wengine wenye vipato hivyo vya chini watakidhi. Kwa hiyo, tumeskia kilio cha vijana wetu, tumesikiliza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, ni sikivu kwa Waheshimiwa Wabunge wote, tunawashukuru, akapigiwa makofi na kicheko."

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ilikuwa ni Kauli ya Waziri wa Fedha. Badala ya vijana hawa kuondolewa kodi hiyo ambayo tuliisema hapa Bungeni, sasa hivi wanalipa Sh. 95,000. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, wewe ndiye unayeshughulikia usafirishaji; nimesema nakala ya *Hansard* hii ninayo, utoleee maelekezo Serikali ziko ngapi katika nchi hii; Serikali moja inasema tunaondoa; na nyingine inasema tunatekeleza. Kwa hiyo, tunaomba mtutolee maelezo ili vijana wa bodaboda waweze kuridhika na waone Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyo sikivu inawasikiliza na inawaondolea kero hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo suala la ukamilishaji wa Kiwanja cha Ndege cha Mbeya. Kwanza, tunaishukuru sana Serikali na tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Benjamin Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu, pia tunamshukuru sana Mheshimiwa Mandosya, aliyekwua Waziri wakati huo, kwa wazo la kuja na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege pale Songwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo namshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na Naibu wake, kwa jitihada za kuendeleza na kuhakikisha kile kiwanja kinakamilika na sasa ndege zinatua pale. Wananchi wa Mbeya na Mikoa jirani ni mashahidi, wanajua namna ambavyo kiwanja hiki kimeondoa adha ya wasafiri wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, maana ulikuwa mpaka utembeee saa 15 uweze kufika Mbeya. Leo kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, unatumia dakika 90. Wakati unakamilisha

Kiwanja hiki, tunaomba Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, ukumbuke na fidia za Wananchi wa eneo lile.

Wananchi wa eneo lile, pamoja kwamba walilipwa, lakini mpaka leo wanalia. Mimi kama Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya, wazee zaidi ya 100 wametufuata pale kusema kwamba, wanaamini walipunjwa na hawakulipwa sawa sawa. Mheshimiwa Waziri, nimeshazungumza na wewe, unasema umeelekeza viwanja vya ndege waliangalie upya. Tunategemea hili lifanyike, isije ikawa Rais anakwenda kuzindua kile kiwanja halafu akakumbana na maandamano yanayosema tunadai, tumedhulumiwa, hatujalipwa sawa sawa. Tunategemea hilo utalitatusa mapema inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kama muda utaruhusu ninaomba niseme kwenye taasisi zako, Mheshimiwa Waziri, wapo Wakuu wa Taasisi wanaokaimu kwa muda mrefu sana. *SUMATRA* wanakaimu, *TAA* wanakimu, tunaomba mchukue hatua. Unapokaa kwenye nafasi ya kukaimu muda mrefu, maamuzi wakati mwingine yanakuwa magumu kuyachukua. Ninajua nimezungumza na wewe na umeniahidi kwamba, hili suala utalitatusa siyo muda mrefu sana, tunategemea tuone umelitatusa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niwasemee *TAZARA*. Mheshimiwa Waziri, *TAZARA* kuna matatizo kama ulivyobainisha na Kamati imebainisha. Ninaomba niwasemee wastaafu wa *TAZARA*. Jamani wale watu wametumika, wanahangaika sana, hawana pa kukimbilia. Nakuomba Mheshimiwa Mwakyembe, uwasikilize, hawalipwi pensheni sawa sawa, wanaodai mirathi hawalipwi sawa sawa, wataendelea kuhangaika katika nchi yao mpaka lini? Hii ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ninaamini inasikiliza, tuwaondolee matatizo.

Baada ya kusema hayo na kwa sababu najua muda hauko na mimi, ninaomba niseme naunga mkono Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi, kwa asilimia 100. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimwia Godfrey Zambi. Mheshimiwa Kabwe Zitto, atafuatiwa na Mheshimiwa Haroub Shamis.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011, Wabunge walichachamaa sana hapa kwa ajili ya kuongeza Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na zikaongezwa shilingi bilioni 93 zilizoondolewa kutoka kwenye Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, kwa ajili ya kununua vichwa, kufanya ukarabati wa reli na mabehewa. Mpaka sasa ripoti zilizopo ni kwamba, fedha ile haikwenda kabisa katika Wizara ya Uchukuzi.

Mwaka 2011, shilingi bilioni 130 ziliombwa na *TRL*, kwa ajili ya kutekeleza mpango wao wa biashara (*Business Plan*) yao. Shilingi bilioni 68 zikatolewa na kuidhinishwa na Bunge, lakini ni asilimia 37 ya fedha hizo ndizo zilizotoka kwenda *TRL*.

Mwaka 2012, shilingi bilioni 104, ziliombwa hapa Bungeni na Wizara ya Uchukuzi, kwa ajili ya kununua vichwa na mabehewa na ukarabati, lakini ni asilimia 25 tu ya fedha hizo ndizo zilizotoka kwenda Wizara ya Uchukuzi. Leo, Waziri wa Uchukuzi, mwalimu wangu, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, anaomba shilingi bilioni 113 kwa ajili ya reli, kwa vyovyote vile hata asilimia 30 haitafika kutokana na *trend* ambayo ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri; mwaka 2011, katika Bajeti ya 2012/2013, bajeti inayokwisha hivi sasa, alipokuja hapa kutuomba zile bilioni 104, alisema kwamba, iwapo fedha hizi zikitoka ni matumaini ya Wizara kuwa uwezeshaji huu wa kifedha utaongeza idadi ya treni za abiria kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kufikia tatu kwa wiki. Leo hii Mheshimwia Waziri, ametuletea ripoti ya utekelezaji wa Wizara yake na ameomba tena shilingi bilioni 113, lakini amekwepa kabisa kusema kama imefikia hizo treni tatu kwa wiki. Kamati ya Miundombinu, imempongeza Waziri kwa ku-*maintain* treni mbili kwa wiki. Napenda nimkumbushe Mheshimiwa Dkt.

Mwakyembe kwamba, mwaka 1920 kulikuwa kuna treni inatoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ninasoma Shule ya Msingi Kigoma, nilimaliza darasa la saba mwaka 1990. Nilikuwa ninakwenda stesheni ya reli, mara nne kwa wiki, kulikuwa kuna treni inatoka Dar es Salaam kwenda Kigoma na kulikuwa kuna treni inatoka Kigoma kwenda Dar es Salaam, mara nne kwa wiki. Leo hii tunapongezana kwa kwenda mara mbili kwa wiki. Kwa vyovyote vile ni dhahiri kwamba, Serikali haina nia ya dhati ya kuhakikisha usafiri wa reli hapa nchini unatimizwa kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumkumbusha tu Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na Naibu wake ni kwamba, mwaka wa fedha wa 2002/2003, treni ya Reli ya Kati iliweza kusafirisha tani 1,500,000 ya mzigo. Leo hii kwa taarifa yake yeje mwenyewe wamesafirisha tani 205,000 tu.

Mwaka 2012 walisafirisha tani 260,000, kwa maana hiyo ni kwamba, toka wameingia hawa ndugu zetu wawili, tani zinazosafirishwa kutoka Kigoma kwenda Dar es Salaam au kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma, zinazidi kupungua. Ninaelewa ya kwamba, kuna kazi kubwa iliyofanyika Dar es Salaam, lakini nina wasiwasi kwamba, mliamua kuhakikisha ya kwamba, Dar es Salaam inafanikiwa kwa sababu ndiyo kila mtu anaiona, *at the expense* ya sisi ambao tunategemea reli kwa maana ya Mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi, Shinyanga, Mwanza na kadhalika. Ninaomba nipate maelezo ya kina kabisa kuhusiana na mtiririko huu wa Bajeti na namna gani ambavyo Wizara inajipanga kuhakikisha ya kwamba, fedha zitakazotoka safari hii zitaweza kutekelezwa. Kambi ya Upinzani Bungeni imeeleza kwamba, tunalo tatizo kubwa sana la mahusiano kati ya *RAHCO* na *TRL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *RAHCO* kazi yake ni nini hasa? *RAHCO* ni *TANROAD* ya Reli, kwa hiyo, kama *RAHCO* ni *TANROAD* ya reli basi ibakie na mtandao wa Reli, isiwe na mabehewa, isiwe na Reli na isiwe na vichwa, kwa sababu hivi vinapaswa kuwa mali ya *TRL*, ili *TRL* iweze kuendesha. Hivi

sasa ukiangalia mizania ya hesabu za *TRL* na nimekutana nao kwenye Kamati, mizania ya hesabu za *TRL*, haina mali yoyote kwa sababu mali zote zipo *RAHCO*. Lazima tuamue ya kwamba, *RAHCO* wanabakia ni waendesaji na wajengaji na wakarabati wa mtandao wa reli. Makampuni mengine na siyo *TRL* peke yake, maana nimeona mmependekeza kwamba, sasa mnataka kubinafsisha usafiri wa reli Dar es Salaam, mnataka kutangaza zabuni ili usafiri wa reli Dar es Salaam uendeshe na watu binafsi; inaweza kuwa ni hatua nzuri lakini hao watu binafsi wataendesha kwa kutumia *engine* za nani? Wataendesha kwa kutumia *engine* zetu ambazo zimenunuliwa kwa fedha za walipa kodi au watanunua *engine* zao? Wataendesha kwa kutumia mabehewa yetu au watatumia mabehewa yao? Sasa ni vizuri kuwa wazi katika hili na kuhakikisha kuwa *RAHCO* inabakia kama msimamizi wa mtandao wa reli na watu binafsi hao na *TRL* wanaweza wakaendesha.

Nina mapendekezo yafuatayo: Moja, ni kwamba, lazima tuwe *serious* katika reli kwa kuwekeza vya kutosha kwenye reli, kwa sababu mabilioni ya fedha ambayo tunayataja hapa Bungeni hayaendi kweli kwenye utendaji wa kazi. Pili, *RAHCO* wabakie na *network*, *TRL* sasa waweze kuwa na hizo *engine* na mabehewa na kadhalika ili yaweze kwenda vizuri. Tatu, tungependa sana Serikali iweke uwazi wa kutosha katika mpango wake wa kubinafsisha uendesaji wa reli Dar es Salaam kama ambavyo imetajwa katika Hotuba ya Waziri wa Uchukuzi. Mwisho kabisa, tunaomba *Special Audit* kwenye ubinafsishaji mzima wa Shirika la Reli, iliyokuwa *TRC*, kwa sababu mali nyingi za *TRC* zimeuzwa hovyoy, viwanja, nyumba na kadhalika zimeuzwa hovyoy na tungependa kuhakikisha kwamba hilo linakuwa sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili na la mwisho ambalo ninapenda kulizungumzia ni bandari na hasa Bandari ya Kigoma. Sasa hivi tumeichukua Bandari ya Kigoma chini ya *TPA*. Wananchi wengi wa Kigoma wanalalamika sana hivi sasa kwa sababu huduma zimekuwa mbaya zaidi tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Kama mnavyofahamu ni kwamba, Kigoma ni Bandari, Mji wa Kigoma ni ile Bandari ya Kigoma.

Bandari ya Kigoma isipofanya kazi vizuri, hakuna kabisa uhai katika Mji wa Kigoma, kwa sababu mnyororo wa thamani katika uendeshaji wa Mji wa Kigoma unategemea sana Bandari ya Kigoma.

Kwa hiyo, tungependa Serikali itoe kauli rasmi kwamba, nini hatua inayofuata kuhusiana na Bandari ya Kigoma; tunakwenda kutafuta mwendeshaji mwingine au tunaendesha wenyewe na kwa namna gani ili kuweza kuhakikisha ya kwamba, tunakwenda vizuri. Watu wa Kigoma wangependa waone ANU anarudi Kigoma, kwa sababu ni watu ambao wamekaa naye miaka 85, wameendesha ile bandari vizuri. Vilevile ni vizuri taratibu za manunuzi zianganaliwe ili kuweza kuona namna ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, Wizara inamalizia ujenzi wa Bandari ya Kagunga katika Jimbo la Kigoma Kaskazini. Bahati mbaya ni kwamba, juzi Mheshimiwa Waziri Magufuli, tulipokuwa tunashukuru, yeye alitubeza sana. Anatomia vibaya kushukuru kwetu, sasa nashindwa kushukuru kwa sababu tumeshapewa amri kwamba, hakuna kushukuru tena. Watu wa Kagunga wamefurahishwa na hatua hiyo na Bandari ya Kagunga itaweza kuwa imekamilika muda ambao unatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ninaomba Wizara iangalie matumizi ya *electronic data interchange* katika Bandari ya Dar es Salaam ili kuongeza ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam na kuweza kushindana na bandari nyingine kutokana na ushindani ulivyo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na hayo ndiyo nilikuwa nimeomba kuyachangia katika Wizara hii ya Uchukuzi. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zitto Kabwe na ninakushukuru kwa mchango wako na hasa kwa kutoa ruhusa kwamba, shukrani zinaruhusiwa kuanzia sasa.

Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Keissy.

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mawazo yangu katika Bajeti hii ya Wizara ya Uchukuzi. Pamoja na shukrani hizo, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya ya kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Uchukuzi ni muhimu sana katika ku-*stimulate* uchumi wa nchi yetu. Mimi ni mmoja kati ya Wajumbe mahiri wa Kamati ya Miundombinu. Tumekuwa tukishauri sana Wizara hii namna ya kufanya kazi na kuweza kuboresha kwa haraka uchumi wa nchi yetu ili Watanzania walio wengi ambao ni wanyonge waweze kukwamuka na hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na kushauri kwetu huko, kwa sababu sisi kazi yetu ni kushauri na kutoa hoja na Sera ya Chama chetu ni kwamba, siasa itumikie uchumi na uchumi usitumikie siasa; lakini bado Serikali haijataka kusikia jambo hilo. Uthibitisho ni kwamba, mwaka jana hapa ilitengwa bajeti ambayo iliidhinishwa na Bunge lako Tukufu ya shilingi 189.7 bilioni, ambazo hizo ni fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo ya Wizara hii. Cha kustaajibisha sana, katika fedha hizo zilizotengwa ni shilingi bilioni 47 tu ambayo ni takribani asilimia 25 zilizotolewa, yaani robo. Hili ni jambo la kuhuzunisha na kusikitisha na la kuonesha kwamba, hakuna dhamira ya Wizara hii kufanya kazi ya kuinua uchumi wa nchi yetu.

Pamoja na kuunganisha hapo, fedha za nje zilikuwa ni takribani shilingi 63 bilioni, ambazo zilitengwa katika bajeti ya mwaka jana. Jambo la kufadhaisha zaidi ni kwamba, utaona bora wale wahisani au wafadhili au washirika wa maendeleo wanatuonea huruma kwa shida zetu kuliko tunavyojionea huruma sisi wenyewe, maana fedha zao zimetoka asilimia 31. Kwa hiyo, wao wana huruma zaidi na sisi kuliko sisi tulivyojihurumia wenyewe! Hili ni jambo la

kufadhaisha sana, kwa sababu binadamu unatakiwa kwanza ujihurumie mwenyewe nafsi yako halafu yule wa karibu ndiyo naye ataweza kukupa msaada wa kiasi cha juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Serikali itupe majibu kwamba; je, ni kweli ipo makini katika kutengeneza miundombinu ambayo itainua uchumi wa nchi hii au inapiga siasa tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kelele tunazozipiga ni nyingi, lakini hazisikilizwi na Serikali inasema ni Serikali sikivu, labda wametia pamba masikioni maana kuna aya inasema wana masikio lakini hawasikii, wana macho lakini hawaoni na wana nyoyo lakini hawafahamu. Sasa sijui wako katika kifungu hiki na hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kuongezea hapo ni Bajeti ya Maendeleo ya mwaka huu, zimetengwa takribani shilingi 390 bilioni, kwa ajili ya Wizara hii. Wasiwasi wangu ni uleule kwamba; utekelezaji utakuwaje? Fedha hizi zitatolewa kweli au tunakaa hapa kushauri, kuelekeza, kutoa nasaha na kufundisha mara nyingine, maana anayefundisha siyo lazima awe mkubwa au mwenye elimu ya juu, lakini hata yule mdogo anaweza akafundisha? Sasa sijui kama fedha hizi zitatolewa kiasi gani maana fedha zilizotengwa za bajeti ya maendeleo ya ndani ni shilingi 222 bilioni na za nje ni shilingi 167 bilioni. Vilevile ukiangalia umakini kwamba haupo ni kwa sababu bajeti ya ndani ya mwaka huu imeongezeka kwa takribani asilimia 13; huu ni mchezol! Wizara kama hii ambayo inategemea isafirishe kwa usafiri wa treni au reli mnaita ninyi huku.

Usafiri wa majini ambao unatumiwa katika nchi nyingi duniani kwa sababu ni rahisi, ambao unaweza kuwakomboa watu wanyonge, bidhaa zinakuwa rahisi, tunasema mfumko wa bei unapanda kila siku lakini hauwezi kushuka kama hakuna usafirishaji wa njia hizi. Tumeambiwa hapa kwamba, mfumko wa bei mwaka huu umeshuka kutoka asilimia 19 mpaka asilimia 11. Naambiwa lakini siyo bidhaa za chakula. Bidhaa za chakula au chakula kama hakijashuka bei, basi

bado hali inaendelea kuwa ngumu na tumeshuhudia hapa, mahindi yanayozalishwa katika Mikoa ya Kusini kwa kaka yangu Mheshimiwa Keissy kule Katavi, yamesafirishwa kwa malori ya Jeshi. Badala ya Jeshi kuliachia majukumu makubwa ya kufanya kazi nyingine za kulinda nchi, tunawapa kazi ya kusafirisha mahindi, wakati reli hii ipo, ingefungwa mabehewa.

Serikali ipeleke pesa za uhakika kutengeneza reli na mabehewa kwa haraka siyo kwa vipande vipande kama tunavyotia viraka. Kanzu imekwisha, tukate kitambaa kipya tushone kanzu mpya. Reli hii inategemewa itengenezwe kwa haraka siyo kwa fedha kidogokidogo kama hizi. Tutatengeneza hata miaka 20 hatuwezi kufika mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni ufanisi kwa bandari, bandari ndiyo lango kuu la uingizaji wa bidhaa za ndani ya nchi na nje ya nchi, lakini bado ufanisi wake haujatosheleza. Kitengo cha *TICTS* bado kinafanya kazi chini ya uwezo; sijui kwa nini? Nataka Mheshimiwa Waziri akija hapa, aniambie kwa nini *TICTS* wanafanya kazi chini ya uwezo. Habari tulizonazo ambazo sina takwimu nazo ni kwamba, hawana vifaa vinavyohitajika kama kwa mujibu wa mikataba kuboresha Bandari ya Dar es Salaam. Sisi kama Kamati, mara nyingi tunataka tukague hizi sehemu kujiridhisha zaidi, lakini nafasi ya kukagua inakuwa ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ni jambo jema, lakini pia lina usiri mkubwa sana. Sisi kama Wabunge, ambao kazi yetu kubwa ni pamoja na kutunga sheria na kuishauri Serikali na kuielekeza, hatujui lililopo katika ujenzi wa Bandari kuna nini? Tutashauri nini? Tutaelekeza nini kama mambo haya ni siri kiasi hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari hii tunavyosikia tu fununu kwamba, itajengwa na watakabidhiwa wajengaji waiendeshe kwa miaka 50. Je, hapo tutakuwa tena na bandari sisi ikiwa tulikataa ujenzi wa Bandari ya Dar es Salaam Gati 13 na 14 kwa miaka 45; sasa tutakuja kujenga ya

Bagamoyo kwa miaka 50? Tena Bandari ya Dar es Salaam ilijengwa zamani, kwa viwango madhubuti, leo tunataka kujengewa na kampuni za Kichina ambazo zina wasiwasi na utaalamu wao. Najua utaalamu wanao, lakini nia ya dhati ya wajengewa.

Nimetangulia kusema hapa kwamba, mimi ni Mjumbe makini wa Kamati ya Miundombinu. Pamoja na kwamba, mimi siyo *engineer* lakini najua hesabu. Kwa hiyo, nimekuwa nikiwaambia kwamba, miradi mingi inayojengwa inajengwa chini ya viwango, hawa *consultants* wetu wako wapi? Hawa *consultants* wa hii miradi wako wapi? *Engineers* wetu wako wapi na wanafanya kazi gani mpaka mradi unakwisha unasikia umejengwa chini ya viwango?

Nina wasiwasi kama bandari itajengwa chini ya viwango na kabla haujafika muda wa kumaliza na mjengaji kuondoka, bandari itakuwa imebomoka na tutaachiwa mavumbi matupu. Wasiwasi wangu ni huo! Kwa hiyo, naomba Serikali kupitia Wizara hii iniridhishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Dar es Salaam Airport*, ujenzi wa *Terminal Three* ni jambo jema kabisa. Nimeona mkataba ukisainiwa kwa Dola za Kimarekani 164 milioni kutoka Uholanzi kwa kaka zetu Wadachi. Jambo ambalo nataka kulisisitiza ni kwamba, umakini wa ujenzi pia wa uwanja huu, kwa sababu tumeona Jengo la *VIP* limejengwa pale halikidhi, wala halina sifa; kwa kweli ni aibu! Jengo lile jipya la *VIP*, ukienda sasa hivi ndiyo kwanza mwaka mmoja au miwili, lakini viwango vilivyopo ukiangalia kwa akili ya kupima tu, basi bila kutoka kwa *engineer* haliridhishi.

Kwa hiyo, sina wasiwasi na wataalamu waliopo katika Wizara, *especially*, hawa wa viwanja vya ndege. Nataka kutoa msisitizo kwamba, wawe makini, tusije tukapewa mbuzi ndani ya gunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ni mengi, lakini nataka nigusie kidogo msongamano na barabara za mabasi ya mwendokasi Dar es Salaam. Muda umekuwa mrefu, ujenzi

wa barabara hizi za kupunguza msongamano Dar es Salaam unachelewa na hauendi kwa kasi ya kuridhisha, umesababisha uchumi kukwama na kama mnavyojua, uchumi wa nchi hii asilimia kubwa upo Dar es Salaam, kazi hazifanyiki. Kwa hiyo, nataka Wizara iongeze mazungumzo na mkandarasi aongeze *speed*; tatizo ni nini?

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Haroub Shamis.

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Capt. John Komba.

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kabla ya yote, naunga mkono hoja kwani sababu ninazo. Hapa tumekuja Bungeni Wabunge wote walipigiwa kura na Wananchi wao wa Majimbo, hawakuja hapa kwa ajili ya kuja kupiga makofi au kumfurahisha mtu. Kila mtu anaona kwake kumeungua ndiyo anakuja kueleza hapa, ametumwa na Wananchi wake. Cha ajabu Wabunge hapa wanakuwa wanawajibia Mawaziri hoja na kujipendekeza kwa Mawaziri, tuache tabia hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namshukuru sana Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mkurugenzi wa *TPA*, Ndugu Kipande. Mara baada ya kuona tatizo la Bandari ya Kipili, Karema, Lagosa na Sigwesa, walikuwa wepesi, Waziri amekuja mara tatu na ananishirikisha moja kwa moja. Mkurugenzi wa *TPA* amekuja na kunishirikisha moja kwa moja na kuchukua hatua ya kumsimamisha Mkandarasi ambaye ni mwizi na walimpa ukandarasi kwa ajabuajabu na kufukuza baadhi ya wafanyakazi, lazima nimuunge mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza hapa kuhusu kufufua Reli na Shirika la Ndege, lakini ndugu zangu hata unapokwenda hospitali, daktari anakuuliza unaumwa tumbo umekula nini, hawezi kukupa dawa hivihivi halafu upimwe. Tunazungumza hapa ili tujue kwanza chanzo, waliofilisi mashirika, nimezungumza mara nyingi, tukifufua Reli na Shirika la Ndege watafilisi vilevile. Nilizungumza mapema kabisa kwamba, hata kama wamefariki tukaweke pingu kwenye makaburi yao tuoneshe hasira. Kama wapo bado na wana mali tuwafilisi. Wapo hapa, wameiba kwenye mashirika mpaka wameyafilisi, tunahangaika hapa tuliyafilisi mashirika tuyafufue kwa vipi mashirika haya wakati walioyafilisi wapo?

Mimi mwenyewe ni mfanyabiashara, unakwenda Shirika la Reli kuomba behewa hupewi, unakwenda kukata tikeki, miaka ya nyuma wakati bado nafanya biashara, unaambiwa hakuna tiketi. Ukihonga ukiingia ndani ya behewa hakuna abiria peke yako, unastahili kwenda Kigoma, mara mbili au tatu, nimekwenda Kigoma na behewa tupu. Shirika la Ndege vilevile unakwenda kukata tiketi unaambiwa hakuna tiketi, lakini pita mlango wa nyuma mtafute mtu unayejuana naye, unakuta ndege tupu Dar es Salaam mpaka Mwanza. Tuwatafute kwanza hawa waliotumalizia mashirika yetu, tukiwaadhibu hao basi watakaokuja watahika adabu, bila huruma. Huu ni ushauri wa bure kwa Mheshimiwa Mwakyembe, watakusumbua sana, hili Shirika unatakiwa uwe mkali kama wembe hakuna kumwonea mtu huruma. Kama tutaweka kwenye makaburi pingu hapo hapo mpaka tumalize nchi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwanja wa ndege Sumbawanga, kuna watu wanadai fidia yale majumba yapo pale ndugu zangu wamekaa nusu nje nusu ndani. Nakuomba kabla ya kutengeneza ule uwanja, kwanza, hawa Wananchi walipwe fidia zao, zile nyumba zivunjwe wakajenge kwingine walipwe fidia Wananchi wa Sumbawanga.

Kuhusu usafiri wa Ziwa Tanganyika, niliuliza swali la nyongeza siku moja nilidandia swali hapa. Mheshimiwa Naibu Waziri akasema kwamba, ni hasara kupeleka *trip* mbili za meli

katika Ziwa Tanganyika. Siyo kweli kwamba ni hasara, nilimwambia hata Waziri pembeni kwamba, watumishi wako, wafanyabiashara na wasafiri wote, wanakwenda bure. Wakitoka Kasanga kuna kijiji kimoja kinaitwa Kirando Kigoma, wanashukia pale wote hawalipi nauli. Mizigo yao inakwenda Burundi bure na wenyewe bure, zinaingia mifukoni mwao, nilikwambia!

Vilevile wanauza mpaka dizeli na vilainishi. Watumishi wa Shirika la Meli Liemba, kila kitu! Vijiji vyote vilivyo katika Mwambao wa Ziwa Tanganyika vyenye mashine za unga, dizeli hawanunui katika *petrol station* wananunua kwenye Meli ya Mv. Liemba. Sasa namna gani tutafika? Nimekwambia chunguza na usiende kama Waziri, vaa hata kanzu, utawakamata dhahiri shahiri! Tena wanaiba mchana kweupe, hakuna mtu anayelipa tiketi kule, wanachukua wanauliza wewe utateremka njiani? Wanachukua pesa wanaweka mfukoni, wana majumba Wafanyakazi wa Shirika la Meli. (*Kicheko*)

Vilevile ushauri wa bure, kwa upande wa Kongo kuna miji kama Moba, Kalemi na Uvinza, hawana meli ya abiria, peleka meli yetu tutaingiza fedha za geni.

Kuhusu Bandari ya Kipili, Lagosa, Karema na Sigwesa, kama yule Mkandarasi mnasema ameshindwa, nakuomba Meneja wa *TPA*, Ndugu Kipande na Mheshimiwa Waziri, harakisheni kutafuta Mkandarasi mwingine atumalizie bandari zetu. Vilevile niliomba bandari moja ya Kabwe na juzi nimekutana na Ndugu Kipande ofisini na wataalamu wake wakasema ipo, lakini naona kwenye bajeti hii hakuna kitu ni zilezile za zamani. Naomba Bandari ya Kabwe kwani Wananchi wanapata tabu.

Tuliwahi kwenda na Waziri mdogo zamani kabla yako alikuwa Ndugu Mfutakamba, alikubali kabisa, aliona kile kijiji kina haki ya kupewa bandari. Nilichokuwa nimekubali ni kwamba, Wananchi wa kule hawataki fidia kabisa, mtakapoamua ijengwe bandari pale kama kuna shamba au mti wa mwembe au mnazi, Wananchi hawataki fidia. Sisi

shida yetu ni bandari, haya mambo ya kudaidai fidia yamepitwa na wakati, tunataka maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, msinigongee bado dakika zangu msiwe na haraka! (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Hapohapo!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Hapohapo inagonga!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kusema kweli naeleza kwa ufundi, ufasaha na ufupi, sirudii hotuba kwani mambo yangu nimeshaeleza kwa ufasaha. Watu wa *Sumbawanga Airport* walipwe fidia. Shirika la Meli liongeze ratiba kwa watu wanaotaka kufika kule na uoneshe kwamba linaongozwa, kwa sababu nimeshakuhadithia kwamba ni wezi, wanaiba fedha zinakwenda mifukoni mwa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Ndugu Kipande, aendelee na uzi uleule wa kuwabana mafisadi wa Bandari ya Dar es Salaam. Huyu anafaa, ni mtumishi hodari, hata ukimpigia simu yupo imara, ukimwendea ofisini kwake anatekeleza. Sasa utakosa kumsifu mtu kama huyo hapa Bungeni? Anafanya kazi kwa ufasaha, amekuja Kipili kuangalia bandari, amemfukuza yule mkandarasi anaitwa Masanche, hafanyi chochote. Kwa hiyo, nampongeza na naona Mheshimiwa Waziri Mwakyembe ungempandisha moja kwa moja kuwa Mkurugenzi wa Bandari ili awabane watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ally Keissy. Sasa namwita Mheshimiwa Capt. John Komba na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, ajiandae.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nami nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na ndugu yake, Mheshimiwa

Dkt. Charles Tizeba, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache. Suala la meli tatu; meli ambali itakayokuwa katika Ziwa Victoria, itakayokuwa Ziwa Tanganyika na itakayokuwa Ziwa Nyasa. Hii habari imezungumzwa tangu mwaka 2010, lakini hadi leo ni ahadi tu. Ilikuwa ni Denmark, sasa leo tumesikia kitu kingine kwamba, Korea Kusini nao wanaleta meli. Sasa sijui kama mpango ni ule ule wa meli zile tatu, ama hii ni nyongeza ya meli zile tatu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri akisimama aniambie hawa Wakorea wamechukua nafasi ya Denmark au Denmark wanaendelea na kazi ile halafu na hawa Wakorea wanaleta kitu kingine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, katika Ziwa Nyasa hakuna meli, kuna meli moja ambayo inatembea kule ambayo inaitwa Mv. Ilala. Hii ni meli ya wenzetu wa Malawi, Tanzania hatuna meli, tuna boti tu. Tuna meli ndogo ndogo tu, meli ya kwanza Mv. Mbeya imezama muda mrefu tangu miaka ya 80, sijui ilizamia wapi? Ilizamia Makonde.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli nyingine ni Mv. Iringa, ambayo imekufa, haifanyi kazi. Hii ni boti kubwa tu siyo meli. Boti kubwa nyingine ambayo sisi huku tunaita meli ni Mv. Songea. Hii inazimika kila wakati inapokuwa katika safari. Kutoka Mbamba Bay kwenda Kyera, inachukua zaidi ya siku tatu au nne, mwendo wa saa nane mpaka kumi, inachukua siku tatu mpaka nne. Kwa hiyo, abiria hawana usalama wa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tegemea wakati wowote meli hii kuleta tanzia tena kama meli nyingine. Hata matengenezo ya meli hii ambayo inasuasua hayapo kabisa katika Hotuba hii ya Waziri! Siyo matengenezo, siyo *recognition* kwamba, haifanyi kazi, hamna kabisa. Sasa hili ni tatizo kubwa sana, wakati wowote tutasikia maafa katika meli ile. Mimi ndipo ninaposema kwamba, nafikiri lile Ziwa tumeshalitelekeza na ndiyo maana yule mama kila wakati anadai ni Ziwa lake, kwa sababu sisi huku hatujali kabisa

maendeleo ya wale watu ambao wanakaa upande huu.
(*Kicheko*)

Watu wale wanapigania meli ya kutoka Malawi, sasa hivi haitembe kabisa kwa sababu ya mgogoro, wakati ule ilikuwa inatembea. Kwa hiyo, Wananchi wa mwambao hawana chombo cha kufanyia biashara, kusafiria wala kufanyia nini. Wananchi hawa ni kama wametelekezwa kabisa. Naangalia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hakuna meli za Ziwa Nyasa zilizoelezwa humu, wameeleza meli za Maziwa mengine, lakini siyo meli yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona bandari nyingi tu zimewekwa katika Hotuba; Bandari za Ziwa Viktoria, Bahari, Ziwa Tanganyika hata Mheshimiwa Keissy pale amesifia bandari ambazo zimetengenezwa kule. Hakuna bandarai hata moja ambayo imewekwa kwenye Hotuba hii kwa miaka miwili mfululizo ambayo inatengenezwa. Bandari ya Mbamba Bay, Bandari ya Itungi, Bandari ya Makonde, Bandari ya Lupingu, bandari ya Ndumbi, Bandari ya Mlundu, Bandari katika Ziwa Nyasa, hakuna. Ukienda Mbamba Bay ukaangalia Bandari pale ni kichekesho tu, kwa hiyo, ni kama vile tumeitelekeza hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kinyume na agizo la Rais wetu, Mheshimiwa Rais alisema kipindi hiki ni cha kutazamia maendeleo katika Wilaya zilizoko pembezoni. Pembezoni ni pamoja na Ziwa hili Nyasa. Bahati nzuri mimi ninayezungumza na huyo anayetoa maelezo ya Wizara hapa tunatoka katika Ziwa hilohilo. Sasa tusiwe kama wale wazee wa zamani, akina Mzee Kawawa, ambao walikuwa wanatengeneza kule juu, kwetu walikuwa hawatengenezi kwani walikuwa wanajua ipo siku kutatengenezwa. Sasa ipo siku ndiyo tumbaki sisi.

Naomba Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe atambue yeye na mimi tuna wajibu wa kulifanya lile Ziwa nalo lionekane ni Ziwa kama Maziwa mengine; Tanganyika, Viktoria na Maziwa mengine. Sisi ni maskini kabisa kule, tusije tukasema aah, tuliwapeni watu hawa wafanye kazi hizo, hawakufanya

kazi ile. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ana muda wa miaka hii miwili kabla hajamaliza, tafadhali Ziwa lile lionekane kweli linaleta maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imesemwa hapa Reli ya Mtwara – Mbamba Bay – Liganga – Mchuchuma zimewekwa shilingi bilioni tano. Sasa sijui fedha hiyo ni kwa ajili ya kujenga tuta au mataluma? Sielewi shilingi bilioni tano itajenga kitu gani labda ni upembuzi yakinifu, *I don't know*. Nataka kushauri tu kwamba, ile reli ikifika Songea, pamoja na kwenda kule Mchuchuma, kuna kiwanda hiki kinachoitwa Ngaka, ambacho kinatoa makaa ya mawe sasa. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri reli ikitoka Songea wakati inaenda Mbamba Bay ikate *branch* ya kwenda Ngaka ili badala ya magari yale kuharibu barabara, maana magari yana uzito mkubwa, yanaharibu barabara, barabara siyo za lami ni za vumbi. Badal aya kuharibu, reli hii ingesaidia kutoa makaa yale kupeleka sehemu nyingine au Bandari ya Ndumbi kule Ziwa Nyasa ili barabara ibaki salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Songea nao ni mahututi na maskini. Uwanja huu ni mzuri, tunamshukuru sana Marehemu Mzee Gama, alifanya kazi kubwa ya kujenga uwanja ule, lakini uwanja ule ni kama *white elephant*, hakuna ndege inayotua pale. Kuna ndege moja inakuja kila siku, lakini siyo ndege hasa ya usafirishaji, ni *charter* ya kukodi. Kwenda Songea na kurudi ni shilingi 650,000, sasa hiyo siyo ndege ya abiria, ni ndege ya kukodi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana, uwanja ule ni wa lami na umekaa muda mrefu, kule kuna jua, baridi na mvua, lami ile wakati wa mvua inatoka, wakati wa jua inapauka, wakati wa baridi inapasuka. Kwa hiyo, tunaomba na sisi watu wa Songea, tupatiwe usafiri wa ndege, kwa sababu uwanja ni mzuri. Tunaomba sana, kama Mbeya wanavyofurahia na sisi watu wa Songea na lringa kwa maana ya Nduli pale, tupatiwe usafiri wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Naibu wa Wizara hii akiwa Mheshimiwa Mfutakamba, alifika Mbamba Bay,

tukamwitia Wananchi pale, akatangaza kwamba, katika meli hizo zinazojengwa, chelezo ya kujengea meli itajengwa Mbamba Bay. Wananchi walimchezea ngoma za Kihoda, Mganda, wakampa na mbuzi, eeh, wakafurahi kwelikweli, lakini sasa ninavyoona humu, chelezo hiyo haitajwi na wala haipo, sijui inapelekwa *Itungi Port*.

Sielewi kwa nini ipelekwe *Itungi Port* au Serikali ile ilikuwa ni nyingine? Maana ile Wizara ni Taasisi, huyu ametoka amekuja mwingine hivyo ni lazima aendeleze yale ya nyuma. Kama yale ya nyuma ni mufilisi, tuambiwe yale ya nyuma yalikuwa mufilisi, sasa ya kweli ni haya. Kwa hiyo, tunaomba tuambiwe, je, chelezo ya Mbamba Bay ambayo Serikali imeahidi itajengwa ama haijengwi na kwa nini ikajengwe kule *Itungi Port*? Watu watasema labda kwa sababu Waziri anatoka huko. Sasa naomba sana Waziri akisimama atuambie kwa nini chelezo ya Mbamba Bay imeondolewa haijengwi tena pale, inaenda kujengwa huko sehemu nyingine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni Mamlaka ya Hali ya Hewa. Ninaishangaa kweli Mamlaka hii, wanatoa utabiri wa Hali ya Hewa Dar es Salaam, sijui jua litatoka saa fulani, sijui litazama wapi muda huu, halafu wanakuja wanasema hali ya hewa ya Ziwa; hali ya hewa ya Ziwa ni ya Ziwa Viktoria peke yake. Sasa sisi wa Tanganyika, Nyasa, yale Maziwa wanakaa watu, ng'ombe au nani? Ukiangalia hakuna Ziwa ambalo linachafuka sana kama Nyasa. Mamlaka ya Hali ya Hewa inatakiwa iwaambie wale watu kwamba, wakati fulani kutakuwa na mawimbi makubwa, mchafuko wa upepo, lakini wanachozungumza ni hali ya hewa katika Ziwa Viktoria. Sasa sisi Ziwa Nyasa ni Ziwa la nani ni la yule mama au lenu? Hakuna habari ya Ziwa Nyasa, watu wanavua kule, wanakufa kwa sababu hawajui hali ya hewa. Naomba leo Waziri aniambie ni kwa nini hali ya hewa inatangazwa katika Ziwa Viktoria tu; *why?* (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja ikiwa haya ambayo nime-*pause* yatajibiwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kapteni John Damian Komba. Kwa kweli inabidi tuelewe ni yule mama au!

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyeniwezesha kusimama hapa, kwa uwezo wake nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sitakushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, uliyenipa fursa hii.

Vilevile nataka niwashukuru wachapakazi wa Wizara hii, ikiongozwa na Dkt. Mwakyembe, ambaye tunategemea atapata nafasi kubwa huko mbele kuliko aliyonayo panapo majaliwa kutokana na utendaji wake wa kazi. Vilevile, namshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, kwa utendaji wake wa kazi ambao ni makini. Naendelea kusema kila wakati kwamba, kutokana na utendaji wake ni mtu anayefuatilia mafaili na hasubiri hadi yafike juu ya meza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitakuwa sijamtendea haki *Port Manager* aliyepata nafasi juzi, Alhaji Awadhi Masawe kutoka Tanga, ambaye kwa muda mfupi tu alionyesha maendeleo makubwa katika *Port* ya Dar es Salaam, ambayo ni kiungo kikubwa cha uchumi wa Tanzania hii. Katika muda mfupi ameweza kuonesha maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sitampongeza *Security Officer* Mtwange, kwa kazi anayoifanya bandarini, ambayo ni mfano wa kuigwa. Yeye hukaa mpaka saa tano au sita ndipo huondoka pale katika Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, sasa nije na kilio cha bandari ambayo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu hili. Tatizo hili limekuwa sugu na halijapata ufumbuzi hadi hii leo. Upungufu wa *radio calls* kwa ajili ya mawasiliano ya kikazi umekuwa ni tishio katika bandari yetu kwani ni tatizo sugu na la muda mrefu. Pia kuna upungufu wa *operators* wa *folk lift* ndani ya bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kuvuja kulikokithiri kwenye maghala ya sheli na 1, 2, 3, 5, 6 na 7. Hali hii ni ya muda mrefu na haijapatiwa ufumbuzi. Upungufu mkubwa wa *pallets* kwa ajili ya shughuli za bandarini; hiki kimekuwa kilio kikubwa, mizigo ya wafanyabiashara inazidi na inaendelea kuharibika. Sifikiri kama yanahitaji gharama kubwa kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokuwepo kwa sehemu maalum za kuogea wafanyakazi wa bandari ambao wanafanya kazi nzito. Hawa ni wanyonge wa nchi hii ambao wanavuja jasho kwa nguvu zao baada ya kubeba mbolea na chumvi iliyomo mle ndani wanahitaji sehemu ya kujisitiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu wa makarani na udhaifu wa wale walioajiriwa. Baada ya hapo, niseme kwamba, matatizo yapo mengi na sitaweza kumaliza kuyazungumzia yote. Kuna karibia shida 50 ndani ya Bandari hii ambayo ndiyo kituo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nije katika sehemu ya *Malindi Wharf*. Hapa ningeomba hawa watu wakapimwe afya zao kwanza, kutokana na eneo lile kukithiri vumbi, haijulikani wakati wa mvua wala jua. Likija jua, upepo mkali, vumbi lote ni la wafanyakazi na linaathiri vifua vyao. Wakati wa mvua kuna tope jingi kiasi ambacho mtu hawezi kutia mguu pale na sijui hata panahitaji *interlock* kuwekwa katika eneo lile. Hapa hapa *Malindi Wharf*, kuna sehemu inaikosha mapato Serikali. Kuna *barge* karibu miaka miwili, halina kazi yoyote na limekaa tu. Ukiwauliza watendaji wanakwambia ni egesho la vyombo vyao, sababu ambayo si ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna meli zina mizigo zinataka kuja kushusha pale, lakini hazipati nafasi kutokana na *barge* lile. Wanakwambia ni egesho la vyombo vyao. Kuna sehemu ya chombo kinaitwa ndovu, nafikiri na huu umekuwa mzigo kwa Serikali kwa sababu sijui ina kazi gani ndovu hiyo, imekaa pale na hakuna kinachoendelea kwa muda huo.

Pia kuna meli za *local* ambazo zimesajiliwa hapa Tanzania, *charges* za meli hizi zinalipwa kwa dola. Benki Kuu wamekuwa wakipigia kelele suala hili kwamba, vitu vya ndani havitakiwi kuwa *charged* kwa dola. Naomba *charges* hizi zingebadilishwa watu waweze kulipa kwa kutumia *Tanzania Shillings*.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa wafanyabiashara wetu umekuwa hatarini baada ya kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Mwakyembe ya kuzuia kodi zisivuje bandarini, usalama wa wafanyabiashara umekuwa mdogo. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, kwa dharura, kabla jengo kubwa halijaisha, ni vyema wafanyabiashara wakawekewa benki ya muda mle ndani. Sasa hivi baada ya kupakia mizigo yao, inabidi watoke nje kwenda kulipa fedha. Hali hii inasababisha usalama mdogo kwa maisha yao. Mfanyabiashara yule anapokuja kwa lengo la kupakia mzigo, anakuta meli imeshaondoka, anajikuta hana pa kuweka mzigo wake, hifadhi ya ndani ni ndogo na mabanda yanavuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mwekezaji wa Kitanzania, ambaye anamiliki karibu meli nne mpaka tano. Huyu ni mlipa kodi mzuri sana kwenye bandari ile, nafikiri kwa mwezi hakosi kulipa kiasi cha milioni 100. Leo mfanyabiashara huyu amekuwa na kilio cha muda mrefu akitafuta ofisi ndani mle, hana sehemu hata ya kuweka hata bati akajificha.

Nimekwenda kwa Bwana Kipande mara tatu au nne nikimpeleka mhusika, lakini Bwana Kipande hana nafasi ya kuonana na mtu huyo. Juzi nilimhadithia *Port Manager*, Alhaji Awadhi Masawe, hili ombi amelichukua na ameomba apewe muda. Naona hiyo sehemu yenyewe imeshapatiwa ufumbuzi, lakini hadi hii leo hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, hapa ningeoomba maelezo kamili kwa mwekezaji huyu ili ikiwezekana angalau apatiwe eneo mle ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza na kusikitisha zaidi ni kwamba, mle ndani kuna watu wemepewa maduka wanauza nguo, simu, mikate, ambapo mwekezaji

anayetumia eneo lile hana haki ya kutumia eneo lile. Huu ni uwajibikaji wa aina gani? Kama Kampuni ya Coastal imo mle ndani inauza tiketi za ndege, wakati yeye anahusika na eneo la uwanja wa ndege yumo mle ndani, mwekezaji huyu anakosa nafasi. Hapa nitahitaji maelezo ya kina, hili suala nilishahangaika nalo muda mrefu, sina mahali pa kulisemea zaidi ya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu wachukuzi. Eneo la Uwanja wa Ndege, *Terminal Two*, wachukuzi wamekuwa wakipata shida sana pamoja na kuwa na vitambulisho vinavyowaruhusu kuingia ndani, *Security Officers* wananyanya watu wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, niseme nitaunga mkono hoja hii baada ya kupata maelezo yanayoridhisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, tunakushukuru sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea wakati wa jioni tutakaporejea. Ninao wachangiaji wengi, nitaomba wote ambao wako kwenye orodha wajitahidi kuwepo kwa wakati. Tutaanza na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na wengine mpo kwenye orodha tutaendelea na uchangiaji.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hiyo, naomba nitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni.

(Saa 6.58 Bunge lilifungwa hadi saa kumi na moja jioni)

16 MEI, 2013

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Tunaendelea na majadiliano yetu, mchangiaji wetu wa kwanza leo ni Mheshimiwa Haji Juma Sereweji na Mheshimiwa Andrew Chenge ajiandae.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muungwana yeyote mahalii pakiwa na tatizo, lakini tatizo lile likianza kuondoka kidogo kidogo basi lazima atoe shukrani. Tuishukuru Wizara hii na hasa tumshukuru Waziri na Naibu Waziri kwa jinsi wanavyokwenda kwa kasi kabisa kuleta maendeleo ndani ya Wizara hii. Nimshukuru kwa kuleta na kuboresha treni zetu ambazo zinafanya kazi vizuri sana, vile vile kuleta mabasi yaendayo kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tusifikie hapo tu, sasa hivi Dar es Salaam imekua sana na kila siku inakua. Kila mmoja anakuja Dar es Salaam, wako wafanyabiashara nadhani hawapungui wananchi milioni nne, wanaoishi pale kati ya hao si chini ya wananchi milioni moja au laki nane huwa wanataka usafiri wa mara kwa mara ndani ya Dar es Salaam na nje kidogo ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nimwombe tu Waziri sasa hivi aweke treni ambazo zitakuwa zinazunguka ndani ya Dar es Salaam ili kuondoa usumbufu wa usafiri ndani ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimshukuru vile vile na hasa kwa hotuba yake ya leo, lakini nadhani sasa hivi Serikali ijikite na ijue kwamba sasa hivi kuna biashara nyingi

na kuna uwekezaji. Baada ya mwaka mmoja au miwili, basi tuletewe treni za kileo zinazokwenda kwa umeme ili kazi zetu ziende haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi naingia kwenye kituo cha Mtoni Mtongani. Kituo cha Mtongani ni kituo kikubwa sana cha Daladala na mara ya kwanza kilikuwa kituo kamili ambacho Daladala zinasimama. Lakini hivi sasa kituo kile kimekuwa *transit*, pana mpito tu. Kituo kile cha Mtongani kuna wananchi wa Mashine ya Maji, Mbagala Kuu pamoja na Mtoni Kijichi ambao wote wanakuja pale na Wana-Mtongani wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utakuta kuanzia saa moja au saa 12.00 mpaka saa 6.00 pana vurugu kubwa sana wananchi bado hawajapata usafiri, kituo kiko Temeke Mwisho na kingine kiko Mbagala Juu ambako wananchi wanapata matatizo makubwa sana. Ningemwomba Waziri kupitia kwako kituo kile kirejeshewe Daladala zake na kianze kazi mara moja. Sisi Wabunge ndio wadhamini wa Mawaziri, tunalosikia sio tunung'unike tulilete hapa na tukishalileta lifanyiwe kazi ili wananchi wasinung'unike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumzia kuhusu Bodaboda. Bodaboda hivi sasa zina matatizo makubwa na vijana wetu ambao tunawategemea na ndio nguvu kazi wanapata matatizo makubwa sana na matatizo yenyewe ni ya ulemavu. Wengine wanavunjika miguu, wanaovunjika mikono, wanaopoteza maisha, wao pamoja na abiria wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ukiwaona vijana wengine ambao wanaoendesha Bodaboda hata miaka 14 au 15 hawajafikia vizuri. Hivi sasa waendeshaji wa Bodaboda wamekuwa kama waliojitolea. Kama unaendesha gari anaweza kukupitia pembeni kama hukuwa dhahiri kidogo tu unaweza kumpiga *booster*. Hivi sasa Jeshi la Polisi na wahusika wote wajitahidi sana kuwadhibiti Bodaboda wale ambao hawana leseni na hawajafikia kuendesha Bodaboda, kwa sababu tumekuwa tunapoteza vijana wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, India kulikuwa na Bodaboda, lakini wameziondoa, wameweka baiskeli za ringi tatu, wameweka na hivi vigari vyao vidogo vidogo ndio vichenge vile, sijui vinitwaje? Ndio vinavyofanya kazi baada ya kuona kwamba wananchi wao wanapata matatizo. Sasa kwa vyovyote vile vile Serikali wasifumbie macho mambo haya, mara moja wadhibitwi lakini vile vile itolewe taaluma yaani mafunzo, elimu kwa vijana wetu ili wasipoteze maisha hovyoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu boti zetu za Zanzibar. Nashukuru sana boti zetu za Zanzibar hivi sasa na namshukuru sana Waziri baada ya kufika pale na kutoa maelekezo ambayo sasa yanafuatwa, boti zinakwenda vizuri na hazina matatizo. Lakini hivi sasa nawaomba wale wafanyakazi kwenye boti wawadhibitwi abiria wao, kwa sababu kabla hatujafika utakuta abiria wote wakishaiona Zanzibar tu au wakishaiona Dar es Salaam tu kama bado dakika 10 kufika, wote wanasogea mlangoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake sehemu moja ya ile boti ina shehena na huku hakuna kitu. Jambo ambalo ilikuwa wasisimame mpaka boti lisimame, watoke nje kwa salama na amani lakini hawawezi kujizuia. Sasa hivi wafanyakazi ndani ya boti hizo wawazuie na watoe taaluma maalum kwamba, mpaka sasa tafadhalini mtu asisimame, asiende mlangoni mpaka itoke ruhusa, inakuwa hatari kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu huwa zinaharibika sana kutokana na magari makubwa. Kwa hivyo, nataka *SUMATRA* wawe wanasimamia vizuri sana, yale magari yasipakie *over tones* ili yakipita kwenye barabara zetu angalau ziwe zinachukua siku nyingi bila ya kuharibika. Utazikuta gari zingine zinapita huku mizigo imesheheni sana. Kwa hivyo, naomba tu wahusika wasimamie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Sereweji, sasa namwita Mheshimiwa Andrew John Chenge, kama hayupo nafasi yake inachukuliwa na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa na ajiandae Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nikushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo, ikiwa ni hotuba yangu ya pili tangu bajeti ianze. Nipende tu kuanza kwa kuwapongeza tena kwa dhati kabisa, Wizara hii ya Uchukuzi pamoja na jopo lao lote kwa kasi kwa nguvu na shughuli zote ambazo wanazifanya katika Wizara hii. Aliye na macho haambiwi tazama, wote tu mashuhuda wa uchapaji wa kazi wa Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwapongeza hivyo, nakumbuka bajeti ya mwaka jana katika waliosimama na kupinga bajeti hii ya Uchukuzi, bajeti ya mwaka jana na mimi nilikuwa mmojawapo. Tena nadhani ndiye niliyeanzisha na nikaungwa mkono na Wabunge wengi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kilichosababisha ilikuwa ni bajeti ndogo sana na wakati huo huo kulikuwa hakuna treni inayotembea kwenye reli zetu, hakuna kabisa ndege ya uzalendo wetu ya *ATCL* na kadhalika, halafu tunaambiwa kupitisha bajeti, hapana, nilikataa. Lakini kwa kipindi hiki pamoja na kidogo kinachojitokeza, lakini kwa ukasi kwa kutoka *zero*, leo tuna safari mbili za treni kwa wiki kwenda Mwanza, sina sababu ya kupinga bajeti hii hata kidogo pamoja na treni ya mizigo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanaobeza juhudi hizi na kusema haitoshi, lakini wakumbuke kwamba tulikuwa na *zero*, tulitoka kwenye treni ya kila siku tukawa tunashuka, tukawa na treni ya siku nne lakini mpaka tulifikia *zero*. Sasa leo tumeinuka tuna mbili. Jamani niombe tuone ku-*appreciate* hiki kwamba hawa wanaume wapo kazini. Ni kwamba wewe chukulia tu unakuwa na mtu mgonjwa, labda anaugua *Polio*, kwa mfano au mtu mmoja anakuwa na dhambi nyingi tu ambazo zilimwelemea akaamua kwenda kwa Anthony Lusekelo huko kupata upako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo anajikwamua katika ugonjwa ule, hivi utaamka uje umulize hivi wewe ulipougua *Polio* sasa hivi umepona, utamwuliza hivyo, unamwangalia, una-*appreciate*, unamwona huyu ni mzima na unamshauri afanye kazi. Vivyo hivyo na aliyeokoka usimfuatilie alikotoka ni mbali ili mradi sasa amempokea bwana unapaswa kushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nipende kuongelea suala la magari ya *Noah*. Kwa kweli ni ukombozi mkubwa mno kwa watu ambao wana vipato vya kati. Niombe kabisa Serikali kupitia *SUMARTA* iwasimamie hawa. Katika kitabu cha Waziri, ukurasa wake wa 30 anasema: “Wajipange vizuri ili waweze kukata leseni watengeneze madirisha, wafanye nini, lakini kitu ambacho kinanisibu kila leo ni ule muda (*timeframe*), ukiiacha inaning’inia hivi Mheshimiwa Mwakyembe sidhani kabisa kama watafanya kazi kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa *ALAT* Taifa kule kwenye Mkutano, baadhi ya mikoa walilalamika kwamba kuna mikoa iliruhusu *Noah* hizi na kuna mikoa walikatazwa. Walilalamika kweli kweli, lakini kwa nia ya kututuma sisi tuje tulisemee na bahati nzuri umelisemea wewe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa liwe na muda kama ni kufungua haya madirisha, kama ni kukata leseni, kama ni kurekebisha, kama ni kuwapa semina mbalimbali za kama walivyopewa watu wa pikipiki, kwamba muwape muda kabisa kwamba, aidha mwezi Juni au Julai kila *Noah* mshirikiane na vyombo vinavyokamata kamata huko barabarani, wawaambie waweke madirisha, wawe huru ili *Noah* hizi zisaidie wafanyabiashara wenye vipato vya kati. Ni ukombozi mkubwa mno vijijini. Nimwombe Mheshimiwa Waziri hilo aliwekee muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda niliongelee ni suala la ndege. Sijui niseme nini na huwa nashangaa kabisa. Mimi ni mzalendo wa kutupa, napenda kusafiri na ndege, nikienda Mwanza kuomba tiketi nakwenda

pale *ATCL*. Lakini Mungu wangu mara ya mwisho nilipokwenda nikaambiwa ndege imepasuka kioo kimoja cha mbele huko. Sasa naiomba Wizara, hakuna kitu kizuri kama uzalendo, hiyo ni mara ya pili napigia kelele hili, hakuna kitu kizuri kuwa na chako, cha kuazima ni cha kuazima tu. Ningewaambia msemo mmoja unasemwa kwa Kisukuma lakini ni mbaya, yaani hakistiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, tafadhali sana, jaribuni kwa kila njia, mpate fedha za kuweza kununua angalau moja au mbili tu. Mwanza kama Mwanza yaani kuna abiria wa kubaki, lakini tunabaki tunajenga viwanja vya kuruka Mashirika makubwa makubwa haya, kwa fedha yetu jamani, sisi hatuna kabisa. Niombe kabisa kila usiku na mchana Mheshimiwa Waziri awazie hilo, tunampongeza kwa yote, lakini hili bado baba mkwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lifuatalo lingine ni kuhusu viwanja hivi. Hivi viwanja ukitoka cha *KIA*, cha Dar es Salaam kinachofuata cha Mwanza. Bahati nzuri Naibu Waziri ni wa Mkoa wa Mwanza. Siku moja tulikuwa naye kwenye uwanja huo, mpaka ikafikia mahali nikaangalia wanabomoabomoa, lakini wanatengeneza nikawashawishi waweze kuwa na huu mkanda unaitwaje kwa Kiingereza *conveyer belt*. Sisi Mwanza ni *flyover* na sasa tunaomba *conveyer belt* kwa maana huu mkanda unaopokea mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi haiwezekani Mwanza, nikawauliza hivyo. Lakini nikawa naangalia yarabi hasa haka kajumba kenye ni kadogo, lakini walinikubalia, waseme nini wameona Mbunge, wakanikubalia. Kwa hiyo, niendeleo kusisitiza *if possible*, naomba uwanja wa ndege wa Mwanza, wale wanaoujenga huo uwanja, nadhani ni wazito na hawana vyombo vya kutosha, vile ambavyo wameandika kwenye mapatano yenu, kwenye mikataba au kwenye andiko, hivi ni nini, bado wako pale pale kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe nipate jibu katika hili, kama hawatoshi mna adhabu gani nao. Sisi tunataka kabisa uwanja wa ndege maana yake kila leo nikisikiliza

naupata wa Mbeya yaani unakwenda kwa kasi. Mwanza tuna *contractor* wa namna gani huyu mpaka tuweze kupata na hiyo mikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanza ina watu wengi, Mwanza ina mzunguko wa fedha, Mwanza ni kila kitu jamani, tunaomba huo uwanja anayeusimamia, hebu Mheshimiwa Tizeba, Mheshimiwa baba mkwe na nani mbaya kutaja kwa Kisukuma, muweze kutengeneza sasa *strategy* ya kuweza kukomboa kabisa viwanja hivi, viwe na matumizi ya kisasa yenye huduma za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba kuwasilisha na naunga mkono na Waheshimiwa Wabunge wote nawashawishi tafadhalini sana tutoe fedha kwenye Wizara hii inayokwenda kasi, inayofanya kazi usiku na mchana ili kazi yao isije ikarudi nyuma. Ahsanteni kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Mchangiaji anayekuja sasa ni Mheshimiwa Peter Serukamba ajiandae Mheshimiwa Mtutura M. Mtutura.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru, lakini nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Uchukuzi kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma, Waziri amesema asubuhi kwa ajili ya Kata ya Kibirizi, ningeoomba sana malipo ya watu yafanyike kwa haraka na maeneo ya Katosho, lakini pia niwashukuru kwa kiwanja cha ndege cha Kigoma, ningeoomba wale watu waliobaki nao walipwe stahili zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi bandari ndio wanaendesha pale Kigoma na kuna vijana wengi sana wamepata ajira pale, lakini kiasi wanacholipwa ni kidogo sana kuliko cha yule aliyekuwepo. Kwa hiyo, ningeoomba kupitia Wizara hii, tuwaombe watu wa *TPA*, waangalie zile

rate za vibarua wanaofanya kazi pale zimekuwa za chini mno kuliko mtu aliyekuwepo awali. Lakini *otherwise* nawashukuru sana kwa kazi inayoendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Uchukuzi ni kati ya Wizara ambazo kama tutawekeza vizuri na kwa kazi wanazofanya itatupeleka mbele kimaendeleo. Kwanza angalia jioografia ya nchi yetu, kuna watu wengi sana wanatuhitaji. Kwa hiyo, niombe, tuamue kuweka pesa kwenye reli na bandari. Ukiweka pesa kwenye reli na bandari ukamaliza, maana reli ukishajjenga vizuri, ukajenga *standard gage* hutohitaji kufanya *maintenance* kila wakati. Utakaa miaka mingine 50 mpaka miaka 100 na ukimaliza tu kujenga itaanza kuingia pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa, kuanzia mwaka 2015 *Nickel* wataleta mzigo karibu tani milioni tatu, hiyo ni ya Msongati bado Kabanga na hujasema nchi zingine zote zinazotuzunguka. Tutakachohitaji ni kuwa na reli na bandari na *efficiency*. Vitu vitatu hivi tukiwekeza nina hakika sekta ya uchukuzi itachangia kwa kiasi kikubwa kwenye *GDP* ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeangalia hapa, fedha inayowekwa kwenye reli shilingi bilioni 255/=, ni jambo jema lakini bado. Kwa reli yetu ilikofika na wenyewe Serikali mmesema kwamba angalau kwa mwaka wa kwanza kwa miaka hii mitatu tungeweka shilingi trilioni 1.6 au trilioni moja. Hatujaweka tumeweka bilioni 255/-. Sasa maana yake tuna-*solve* kazi za kila siku ili angalau twende. Lakini nadhani umefika wakati Wizara ya Uchukuzi isaidiwe na Wizara ya Fedha, make, mkubaliane tutafute pesa, tukope kokote duniani, tujenge bandari na reli zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanikiwa kujenga bandari na reli nchi hii tutapiga kasi kubwa ya kimaendeleo kuliko tunavyopiga sasa kwa sababu wenzetu wote wanatuhitaji. Kutoka hapa kwenda Rwanda ni karibu kuliko

Mombasa kwenda Rwanda. So, Rwanda kwetu sisi kwenye *economics geography*, wanatuhitaji sisi kuliko kwenda Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hatuna reli, bado na malori yenyewe tunayakamata kila baada ya dakika tano, hayafiki haraka hakuna ayakayekuja, *we are no longer efficient*. Kwa hiyo, ni lazima tu-*invest* kwenye *efficiency* ili angalau tutumie jiografia ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia maamuzi yetu, mazuri, lakini yanachelewa. Leo tumehangaika huu ni mwaka wa sita kujenga gati 13 na 14. Nashukuru Mheshimiwa Waziri amesema kwamba anaamini *by June* tutaanza. Waziri tunakuamini, tunaomba basi hiyo Juni kweli tuanze. Maana tumeshaambiwa Juni nyingi sana, basi hii iwe Juni ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi bado narudi kwenye reli. Reli sio tu kwa ajili ya biashara, itasaidia wananchi wetu, itasaidia kwenye kukuza uchumi. Leo hii Tanzania tunazalisha chumi mbili. Ukinunua bidhaa za viwandani Dar es Salaam na ukaenda Kigoma, Mpanda, Kagera au Kusini bei ni kubwa zaidi kwa sababu ya *transportation cost*. Lakini mazao yao kule yanauzwa kwa bei rahisi. Kwa hiyo, mama ambaye amezalisha mahindi kule Rukwa, mahindi yale inabidi ayauze bei rahisi, lakini yakifika Dar es Salaam yanauzwa bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *products* zinazotoka Dar es Salaam yule mama aliyeuza mahindi bei rahisi, inabidi azinunue kwa bei kubwa. Maana yake nini? Hapa *transportation cost* ndiyo inafanya biashara iwe ngumu. Kwa hiyo, tunaposema tuwekeze kwenye reli ni kwa sababu tunataka tusaidie uchumi wa nchi hii na tuwasaidie wananchi wetu, *inflation* itakwenda chini, bei za vitu zitakwenda chini na hii ndiyo kazi ambayo tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe sana Serikali na Wizara ya Fedha kwa kweli hapa lazima tusaidiane,

tuisaidie Wizara hii. Kama tumepanga fedha billioni 200 tujitahidi zifike 200. Tunapoanza kutofikisha zote ndiyo maana mambo hayaendi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia wenzetu South Africa, mwaka huu wameagiza *locomotive* 500, yes South Africa ina uchumi mkubwa, basi sisi tungeagiza 10, 20 basi au 50. Tulikuwa tumepanga mwaka huu vichwa 13, namshukuru Mheshimiwa Waziri, mwaka ujao walikuwa wamepanga vichwa 50, hakuna fedha. Maana yake hatuwezi ku-*compete* na dunia ya leo ni *competition*. Sisi tusipofanya, wenzetu watafanya na tukishapoteza hiyo treni hakuna atakayekuja kwetu tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo South Africa wanajenga reli mpaka Malawi, wanataka nchi zote za *SADC* kupeleka reli zao. Maana yake ni nini? Wanataka watumie bandari zao pamoja na reli zao, sisi tuna *drag*. Nawaombeni sana watu wa Serikali mtusaidie, mumsaidie Mheshimiwa Waziri tupate fedha nyingi, tukope. Twendeni China twende wapi, tujenge reli na bandari zetu. Tukimaliza nina hakika wataanza kuchangia maendeleo ya nchi na kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kuhusu suala la wasafirishaji. Tumekutana nao kwenye Kamati, mengi wanayoyasema wala sio ya kibajeti. Tunahitaji Serikali mkutane, muongee yale ambayo ni ya kutekeleza myatatue. Mengine ni kuamua wala hayahitaji fedha. Tunaomba sana na siku hiyo bahati nzuri Naibu Waziri wa Fedha alikuwepo na wa Uchukuzi. Nawaombeni yale tuliyokubaliana mkakae, yale tunayoweza kuyaamua tuyaamue kwa sababu hawa watu wanaleta fedha za kigeni nchini. Hawa watu wanatoa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima na sisi kama upande wa Serikali, tujue wana mchango, tusiwaone kama ni wafanyabiashara tu maana iko *scenario* hapa, wafanyabiashara ni kama watu wabaya hivi, ni watu

wanatuibia tu, wanania mbaya, hapana. Hawa ni *partner* wetu katika maendeleo. Kwa hiyo, lazima na sisi kama Serikali tuwa-*facilitate* ili wafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakifanya vizuri watapata pesa, tutapata kodi, wataajiri watu na nchi yetu itakuwa *competitive* na matokeo yake maendeleo yatapatikana maana hawa wana-*trade* kwa dola. Kwa hiyo, ukiangalia *current account* zao za dola ni kubwa, wanakusanya dola wanakuja kuchukua madafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Serukamba. Sasa nipate ya Mheshimiwa Mtutura na Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimuunge mkono sana kwa maneno mazuri ambayo Mwenyekiti wangu wa Kamati ameyazungumza. Labda niongeze tu kwamba, kama leo Mtukufu Rais angeniteua kuwa kwenye Tume ya Mipango na nikawa ndiye msemaji wa mwisho kwenye Tume ile, basi mwaka ujao wa bajeti fedha zote, narudia fedha zote za maendeleo ningezipeleka kwenye ujenzi wa reli na bandari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kabisa ndani ya miaka miwili basi tija ambayo ingeweza kupatikana, tungeweza kufanya mambo mengi ambayo tumeyasimamisha kwa miaka miwili tungeyafanya kwa kasi kubwa ya ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi jirani ya Kenya imethubutu na imefanya, imekopa fedha zaidi ya dola bilioni saba kwa ajili ya kujenga bandari ya Lamu, gati 13 zenye kina cha mita 13 kila moja. Vile vile wameamua kujenga reli ya kutoka Lamu kwenda South Sudan ambayo vile vile itahudumia mpaka Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sisi tunasuasua na shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kujenga reli. Nawaombeni Watanzania tuamue, tukwamue uchumi wa nchi hii kwa kufanya maamuzi magumu. Najua wengine watasema kila Wizara ina umuhimu wake, lakini ningeulizwa leo nini chenye umuhimu mkubwa ningesema ni miundombinu na si mingine isipokuwa ni reli na bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, katika kumuunga mkono Mwenyekiti wangu, nije kwenye hoja zangu ambazo nimeziandaa. Uanzishwaji wa Bodi ya Wataalam wa Usafiri pamoja na Usambazaji, kwa maana ya *Transport and Logistic*. Suala hili tumekuwa tukilizungumza mara kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiliangalia kasma za Wizara zote utakuta gharama kubwa sana imeelekeza kwenye maeneo ya usafirishaji, *repair and maintenance*, lakini haya yote yanashindwa kusimamiwa ipasavyo kwenye Idara mbalimbali za Serikali na Mashirika mbalimbali kwa sababu hatuna wataalam wa kusimamia masuala ya *transport and logistic*. Ni sekta nyeti sana, ni sekta ambayo si vizuri kumpa mtu ambaye hakusomea taaluma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote hapa tunafahamu kwamba, bila usafiri, hakuna ambacho kinaweza kikafanyika. Sasa sekta hii ambayo ndiyo *prime mover* ya kusimamia sekta zote imesahuliwa, inajiendesha kiholelaholela. Ofisi nyingi hazina ma-*transport officer*, mtu amesomea labda *administration* basi anakuwa *transport officer*. Matokeo yake vurugu zinakuwa nyingi, usimamizi wa vyombo hivi vya usafiri unakuwa hovyona gharama za uendeshaji za ofisi zinakuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano michache, kwa mfano sasa hivi, madreva ambao ndiyo wanaobeba roho zetu, haki zao nyingi hazisimamiwi ipasavyo. Matokeo yake wanafanya kazi hii bila kuwa na ridhaa, mpaka ndani

ya nafsi zao. Mishahara yao hasimamiwi vizuri, madereva hawa wamekuwa wakitoa mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu ya kukosekana chombo ambacho kinasimamia haki zao za msingi, inakuwa vigumu sana katika kusimamia mambo mengi ambayo ni ya msingi katika shughuli zao. Uwajibikaji unapungua, unaweza ukamwamboa aende akapeleke barua na yeye anatumbukiza mambo yake mengine. Lakini inashindikana kusimamiwa ipasavyo kwa sababu ya kukosekana viongozi. Si ajabu sasa hivi utakuta magari mengi madereva wengi wanafungua ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saa tatu dereva anaungurumisha gari, amefungua AC, amelala kwenye gari na hiyo yote ni kwa sababu hakuna *transport officer* ambaye anasimamia *fuel ratio* na *fuel consumption*. Lakini idara ile kama kungekuwa kuna *transport officer* angeweza kumbana dereva kwa nini mafuta yametumika mengi kuliko *consumption* ya gari ambayo ni *consumption ratio*. Kwa hiyo, naishauri Serikali iunde Bodi ya kusimamia sekta hii ya usafirishaji na usambazaji ambaye ni *transport and logistics*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye suala la bandari. Naipongeza Serikali, nampongeza sana Waziri pamoja na Naibu wake na timu nzima ya Wizara, kwa kuamua sasa kwamba, gati namba 13 na 14 lijengwe. Huu utakuwa ni ukombozi mkubwa kwa sababu tunasema tunataka mafanikio ya haraka sana. Hiyo miradi mingine mikubwamikubwa tunaiunga mkono, lakini ili tuweze kupata matokeo ya haraka sasa, ni lazima gati namba 13 na 14 lijengwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile bila kusahau bandari ya Mtwara na bandari ya Mbamba Bay, kwa sababu ndiyo itakayofungua na kupata mizigo ya kutoka nchi za wenzetu za Malawi. Nchi ya Malawi inapitisha mizigo yake Dar es Salaam, kwa sababu hawana namna nyingine yoyote. Lakini bandari ya Mtwara na bandari ya Bamba Bay

zikifunguka hawana sababu yoyote ya kupitisha mizigo yao Dar es Salaam kwa sababu njia hii ya Mtwara kwao ni fupi na mara nyingi wafanyabiashara wote wanapenda sana kutumia njia fupi ambayo itawaletea faida kubwa. Vile vile tutaweza kupata mizigo ya kaskazini mwa Msumbiji ambao sasa hivi wao wanatumia bandari ya Nakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana ndugu zangu wa *TPA*, Waswahili wanasema kwamba, ukimwona mwanaume anatoka kwenye nyumba ya mama yako amevaa kanga, basi huyo ndiyo baba yako; huna chaguo. Kwa nini nasema hivyo? Niliwahi kuwa Mkurugenzi wa Bodi ya Bandari siku za nyuma, nafahamu nini kinachoendelea *TPA* nawaombeni sana wafanyakazi wote wa *TPA* muunge mkono mabadiliko yote yaliyofanywa na Mheshimiwa Waziri na muunge mkono hao viongozi ambao wapo madarakani sasa hivi, ili muweze kupata tija ambayo nchi nzima inatarajia kutoka kwenu. Hao ndiyo viongozi wenu wa sasa na kama yatatokea mabadiliko mengine yoyote, naomba vile vile mfanye nao kazi ile ambayo wewe unawajibika nayo katika shirika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye viwanja vya ndege. Nashukuru sana kuna mabadiliko makubwa na mapinduzi makubwa katika ujenzi wa viwanja vya ndege. Lakini niseme tu kidogo, kiwanja chetu cha Mtwara na Songea, kiasi ambacho kinakusudiwa kufanywa mwaka huu, tunaomba, hatuwezi kubadilisha lakini msimu ujao, tunaomba mtukumbuke sana katika uwanja wa Mtwara na uwanja wa Songea, kwa sababu dhamira yetu, viwanja hivi vifanye kazi mpaka usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha Mtwara zamani kilikuwa kinatua ndege usiku, lakini sasa hivi taa zote zimeng'olewa tunaomba zile taa zote zirudishwe. Pia kiwanja kile cha Songea taa zifungwe ili wananchi waweze kusafiri muda wowote ambao wanaona kwamba unafaa. Sisi tuko mpakani na viwanja vya mpakani lazima viheshimike kwa kuwa ni viwanja vya ulinzi, viwanja ambavyo vitatuletea

usalama katika nchi yetu. Kesho na kesho kutwa tunalazimika labda ndege za kijeshi zitue usiku ili liweze kuwalinda wananchi hawa wa pembezoni hasa ukanda huu wa kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nisingependa kengele inigongee, nakushukuru sana kwa kunipa muda na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo muhimu, ni bora nilisome sasa hivi na nitalisoma tena wakati tunamaliza Bunge. Kwa sababu ya matishio ya kiulinzi na kiusalama yanayoendelea kujitokeza hivi sasa. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuanzia kesho tarehe 17 Mei, 2013 kutoegesha magari yenu pembezoni mwa uzio unaozunguka Ofisi ya Bunge hapa Dodoma. Badala yake magari hayo yaingizwe na kuegeshwa eneo la maegesho ya Waheshimiwa Wabunge ndani ya viwanja vya Bunge.

Kama Mheshimiwa Mbunge atapenda kuegesha gari lake nje ya ofisi, anaombwa kuegesha eneo la ng'ambo la upande wa kaskazini mwa barabara itokayo Dar es Salaam. Tunaomba ushirikiano wenu.

Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Arfi ajiandae.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niungane na Wabunge waliotangulia kumpongeza Waziri Mheshimiwa Mwakyembe na Naibu wake kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. Mbali ya kwamba miaka nenda, rudi wamekuwa wakipewa bajeti ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze hasa mbali na changamoto alizokuwa amezipata, aliweza kuisafisha bandari ambayo ilikuwa imekithiri rushwa na najua yeye na masuala ya rushwa ni vitu viwili tofauti. Nimwambie Mheshimiwa Mwakyembe wapo vijana ambao wanachukia vitu vya namna hiyo na tuko nyuma yako tunaku-*support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni dhahiri kwamba, ni kweli mwanzoni usafiri wa reli ya kati ulikuwepo, lakini kutokana na usimamizi mbovu ukasuasua, ukawa haupo kabisa kutokana na baadhi ya watu wenye uchu. Lakini leo hii wanatokea wazalendo kama akina Mheshimiwa Mwakyembe wanaamua kufufua, inabidi kusahau yale yaliyopita, wote kama viongozi tuwange mkono kuhakikisha mustakabali na uchumi wa Taifa letu unaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuna Wizara ambazo zimeshikilia maisha ya Watanzania. Lakini kuna Wizara ambazo zimeshikilia uchumi wa Taifa letu na uchumi wa Mtanzania mmoja mmoja. Miongoni mwa hizo Wizara ni Wizara ya Uchukuzi. Lakini cha kushangaza miaka nenda rudi Wizara hii ambayo ina-*deal* na usafiri wa anga, usafiri wa majini na bandari wamekuwa wakitengewa kiasi kidogo cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii kuwatangazia Watanzania mchapakazi Mheshimiwa Mwakyembe ana dhamira ya dhati, kwenye fedha za maendeleo tunampa bilioni 200 kati ya trilioni 1.6 ambazo anazihitaji. Naamini kabisa Serikali ina uwezo wa kumpa hizo fedha. Msimtengenezee mazingira ya kuonekana mwongo kwa wananchi. Msimtengenezee mazingira ya kushusha *credibility* yake, mpeni fedha afanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia reli ya kati unazungumzia uchumi wa Taifa letu, ukizungumzia bandari unazungumzia uchumi wa Taifa letu na kukuza ajira kwa vijana wenzangu, ukizungumzia reli ya kati unazungumzia kusaidia wakulima kusaidia wananchi wa vijijini wanaopata adha kubwa ya kusafirisha mazao yao na kusafiri wenyewe. Sisi kama Wabunge hatuwezi kukubali Wizara ambazo zinashikilia uchumi wa Taifa letu zikaendelea kutengewa fedha kidogo, hatutakuwa tunatimiza wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna jukumu la kuisimamia Serikali bila kuona haya, bila kutafuna maneno, waongezewe fedha. Tunaposema kuongeza fedha, hatusemi kuongeza

fedha kufurahisha tu, tunataka kuona fedha zinatoka na zinafanya kazi na suala la kufanya kazi sina mashaka nalo, tuna watendaji waadilifu, wazalendo watasimamia fedha hizo za walipa kodi kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali jaribuni kuwa na vipaumbele, chagueni Wizara ambazo tuna uhakika tukizipa fedha na kutenga fedha zetu za ndani, zinaweza kuleta mabadiliko, zinaweza kuwapa matumaini Watanzania na hilo linawezekana, lakini mbaya zaidi mbali na hizi bilioni 200 ambazo wanapewa na ambazo ni ndogo ni sawa na 20% ya fedha wanazozihitaji hawapati zote. Sasa hatuwezi kila siku tukija huku Bungeni Ester Bulaya ukisimama unaongea mambo yale yale haiwezekani, ninaomba tutimize wajibu wetu. Tulitumikie Taifa hili kwa vitendo na siyo kwa maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia kitabu cha Mheshimiwa Mwakyembe, najua hana hela, lakini naomba Bandari ya Musoma, nilikuwa kwenye Kamati ya Mashirika ya Umma, tumezungumzia huu mwaka wa tatu na tunajua ina umuhimu gani katika kukuza uchumi wa Mkoa wa Mara katika kuchangia kutoa ajira kwa vijana wanaoishi jirani na Mkoa wetu wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine najua mna *plan* ya kujenga uwanja wa Ndege wa Serengeti na naafiki ni jambo jema kwa sababu litaongeza uchumi wa Taifa letu na Watalii watakuja kwa wingi, lakini haiondoi maana ya kwamba Musoma kama Makao Makuu ya Mkoa, mshindwe kutengeneza Kiwanja cha Ndege kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii watu wa Mara wanapata tabu, leo ninapofikiria kwenda kwetu niwaze kushukia Mwanza. Hilo haliwezekani wakati kuna uwanja pale na tuna uwezo wa kuuboresha, tuna uwezo wa kukarabati na ukasaidia kutoa ajira kwa vijana wa Musoma na Mkoa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuzungumzia suala zima la kupanda kwa nauli. Bado hatujawatengenezea Watanzania njia za kuimarika kiuchumi, tunakuja kuwatwika mzigo wa kuwapandishia nauli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba SUMATRA, wamweleze Mheshimiwa Mwakyembe sababu za msingi za kupandisha naul. Mtanzania wa leo hii ambaye anashindwa kuhimili milo miwili kwa siku unamwongezea mzigo wa kumpandishia nauli. Wao wanatoa sababu za uendeshaji, tunajua mafuta hayajapanda. Tunaomba afanye utafiti, Watanzania wamelalamika, wadau wanalalamika, maisha ni magumu na hao ndiyo wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Mwakyembe anajali watu wa kipato cha chini naomba asikilize kilio cha Watanzania, wanalalamika, nauli za mabasi ya Mikoani, daladala na tozo za majini zimepanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo yalikuwa yangu. Naomba Mheshimiwa Mwakyembe aangalie wananchi wa kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kayombo, Mheshimiwa Kayombo hayupo, Mheshimiwa Arfi, jiandae Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. SAID M. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kusema kuwa, mara zote tumekuwa tukisikia kauli kwamba ka sungura ni kadogo, kwa hiyo, ni kauli ambayo imezoeleka katika Bunge hili na tumekuwa tukivumilia hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kama sasa tumeua tembo na kama tumeua tembo na nyama ni nyingi

sasa, tunaweza tukagawana kila mahali tukafanikiwa katika yale ambayo tunatarajia kufanikiwa, itakuwa ni faraja na habari njema sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua na nimefanya kazi kwa karibu sana na Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Mwakyembe na mwenzake, najua nia yao ya dhati ya kutaka kusukuma mbele sekta hii ya uchukuzi, lakini kama tulivyosema katika hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani, kikwazo kikubwa ni fedha na kama bajeti yetu ni ile ile, ni kale kale ka sungura, je, ni muujiza gani sasa utakaofanyika wa kuweza kuibadili hali hii ikaweza kuboreka na matumaini waliyokuwa nayo na matarajio ambayo wanayo Waheshimiwa Mawaziri hawa yakaweza kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bulaya amesema sasa hivi, Wizara hii ili iweze kutoa matokeo ya haraka ilikuwa inahitaji zaidi ya trilioni 1.3, leo wanapewa bilioni 200 na kidogo kwa vyovyote vile ni kwamba yale waliyokuwa wanatarajia kuyafanya hayataweza kufanyika, ni lazima sasa tuitazame Hazina watueleze ni kwa nini wanashindwa kupeleka fedha kama zinavyoidhinishwa na Bunge na inapobidi kuwawajibisha basi tuwawajibishe, kwani sisi hatuwezi kupoteza muda wetu hapa na kodi ya Watanzania, miezi mitatu tunaidhinisha fedha, halafu fedha haiendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka jana Shirika la Reli tu peke yake lilikuwa limetengewa bilioni 104, wamepelekewa wamepelekewa bilioni kumi na kidogo hivi sawasawa na 11% ya fedha ambazo walikuwa wametengewa. Huu ni utani, hatuwezi kwenda, hatuwezi kupata Injini, hatuwezi kupata mabehewa kama Hazina itaendelea kukumbatia fedha na ikashindwa kupeleka fedha katika Wizara kama zinavyoidhinishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasipobadilika Hazina, hizi hadithi tunazosisikia humu, zitaishia humuhumu na hakuna mabadiliko yoyote. Hazina ni lazima ijipange na iheshimu

maamuzi yanayofanywa na Bunge. Naamini kabisa mwisho wa mwaka wa fedha Wizara itakapokuja ituletee taarifa kuwa imepokea fedha zake zote na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie reli; wiki tatu zilizopita nimeonja adha ya usafiri wa treni. Nimesafiri na gari moshi kutoka Dodoma kwenda Tabora hadi Mpanda na kurudi, nilitakiwa nifike stesheni ya Dodoma saa saba na nusu mchana na nimefika wakati huo. Nimekaa ndani ya behewa mpaka saa kumi na moja ndiyo gari limeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofuatilia kuuliza naambiwa tatizo ni maji, wanachota maji kwa ndoo, wanajaza kwenye injini, Dodoma Mjini! Mfumo wa maji wanaotegemea ni Mamlaka ya Maji ya Dodoma, siku hiyo kwa bahati mbaya sana kulikuwa hakuna maji. Stesheni ya Dodoma yapo matenki (*Reservoirs tanks*) yako pale, lakini yametoboka, kinawashinda nini kuziba yale matenki ili kuwe na akiba ya maji Gari Moshi likifika, lisiweze kuchukua muda mrefu na kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuishia hapo injini zenyewe ili ziweze kufika Tabora, ni lazima zaidi ya mara tatu njiani zisimame ziongezewe maji, tena kwa kuchota kwa ndoo. Hii inasikitisha sana, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mabehewa halikadhalika hairidhishi, yako katika hali mbaya na yamechakaa, kusheni zimekwisha na ni hatari wakati mwingine. Nilikwenda katika chumba cha kulia chakula katika gari inayokwenda Mpanda, nikachana suruali yangu kwa sababu *springs* za kwenye viti zimeshatokeza nje, huwezi kuwasafirisha wananchi katika hali kama hii. Ni lazima mnapochukua fedha zetu kama nauli, mtupe huduma minayoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adha nyingine kubwa ni uchache wa mabehewa. Najua hali ngumu mliyo nayo, lakini wataalam wetu wa kizalendo kama wakipewa motisha,

wakapewa na vifaa (vipuri) vinavyohitajika wana uwezo mkubwa wa kukarabati mabehewa yaliyoko pale Dar es Salaam ili kupunguza tatizo la mabehewa ya abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabehewa ya daraja la tatu kwenda Mpanda hayatoshelezi hasa kipindi hiki cha mavuno, abiria ni wengi na msongamano ni mkubwa. Huwezi kupata nafasi kutoka mwanzo wa behewa hadi mwisho wa behewa kwa sababu mpaka watoto wanalazwa kwenye korido, hali ni mbaya sana. Niombe tu kama itawezekana, najua Mheshimiwa Mwakyembe ulishasafiri na treni kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma na nasikia kutoka Kigoma mpaka Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila nafahamu kuwa Mheshimiwa Tizeba amefika Mpanda mara kadhaa ila siyo kwa treni, nawaomba sasa mmoja kati yenu asafiri na gari moshi kutoka Tabora mpaka Mpanda, aweze kuona hali halisi ya reli ilivyo leo. Ni afadhali usafiri kwenye barabara yenye mashimo kuliko kusafiri kwenye treni inayokwenda Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kulala, huwezi kupumzika, inadunda utafikiri mpira wa tenisi, hali ni mbaya mno, huwezi kuweka kikombe cha chai ukanywa. Lakini yupo Mkandarasi pale na yako malalamiko kwa wananchi, ukipita katika reli ile ukaongea na wananchi pembezoni pale, wanamlalamikia Mkandarasi huyu, lakini Mkandarasi huyu bado anaendelea kukumbatiwa na Mamlaka kwa sababu wanazozijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe ndugu zangu kuwa, hebu mwangalie sasa namna ya kuisadia hii reli iweze kuwa na ufanisi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine, nizungumzie mtandao wa reli wa Afrika ya Mashariki. Hapo nyuma kulikuwa na mtandao wa reli wa kuunganisha nchi zote za Afrika ya Mashariki kwa maana ya Tanzania Bara, Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli inayotoka Mombasa kwenda Nairobi mpaka Kisumu na reli iliyokuwa inaunganisha reli ya kati kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma kwa maana ya *branch line* inayoanzia Ruvu kwenda mpaka Taveta, sasa hivi haifanyi kazi. Tuna mashirikiano na tuna Itifaki kadhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Je, kuna mpango gani mahususi sasa wa kuifufua hii reli iliyokuwa inaunganisha nchi zetu za Afrika ya Mashariki ili kuweza kurahisisha biashara kati ya nchi hizi jirani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ili kuweza kufanikiwa ni lazima tuziimarishe karakana zetu. Hali ya karakana ya Tabora ni mbaya sana, haina vipuri, haina wataalam wa kutosha, majengo ni machakavu. Hali kadhalika karakana ya Morogoro na Karakana ndogo ya Mwanza. Niwaombe ili tuweze kuwa na huduma ya uhakika, ni lazima tufanye kila tunachoweza, kuziimarisha hizi karakana zetu. Pia Wakaguzi wa mabehewa unapofika hapa Dodoma unakuta kuna wakaguzi wa mabehewa watatu na wana mabehewa 25 ya kukagua, kwa hiyo, muda wa kusubiri unakuwa mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niombe Serikali ijaribu kuangalia na kulishauri Shirika la Reli kufungua stesheni ambazo wamezifunga. Hizi zinasababisha pia magari kuchelewa kwa sababu ya kupishana. Stesheni hizi zilikuwa ni muhimu sana ili kurahisisha kupishana kwa magari moshi, sasa hivi inabidi wasubiri kwa muda mrefu sana kwa sababu stesheni nyingi zimefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa Mawasiliano, najua Shirika la Reli lilikuwa na Mkongo wa Mawasiliano na wenyewe uko katika hali mbaya sana, haufanyi kazi kwa ufanisi, ni lazima mwangalie ni namna gani sasa mnaweza kuurekebisha Mkongo huu wa Reli ili uunganishwe katika Mkongo wa Taifa ili tija iweze kupatikana na Shirika la Reli liweze kupata mapato kutokana na kuwepo kwa Mkongo huu ambao ni wa siku nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Kalema, Ndugu yangu Keissy ameizungumzia sana hapa na niwapongeze kwa hatua mlizochukua, lakini zisiishie katika hatua za kumsimamisha Mkandarasi tu, wananchi wanahitaji kuwa na Bandari pale Kalema itachukua muda gani ili kazi hiyo iweze kukamilika? Niiombe Wizara na Mamlaka ya Bandari iangalie kila itakavyoweza kuhakikisha kwamba, Bandari ya Kalema inakwisha katika muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo na malalamiko na matatizo ya wafanyakazi kwa maana ya mafao kupandishwa madaraja, mishahara, fedha zao za likizo na malimbikizo mengine mengi, ni eneo ambalo limesahauliwa. Pia wafanyakazi wengi sasa wanakaribia kustaafu, kuwepo na mpango mahususi wa kuweza kupata watumishi badala yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Arfi. Sasa namwita Mheshimiwa Ritta Kabati, ajiandae Mheshimiwa Mfutakamba na Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Uchukuzi. Nitoe pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya. Hii imethibitishwa leo, maana kila aliyesimama ameweza kutoa sifa zake na pongezi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pongezi hizi haziwezi kufika popote kama Wizara hii haitaongezewa pesa. Tumeona mikakati mikubwa sana katika kitabu chao ambayo wameionyesha. Tuna imani kuwa kama kweli wataongezewa fedha za kutosha, Serikali hii sasa tutaweza hata kuondoa umaskini na itaweza hata kusaidia barabara zetu kubeba mizigo mizito kwa kutumia reli hii. Tunajua reli inatumika katika

mambo mengi sana, hata usafiri, msongamano wa magari utapungua na kuhakikisha kuwa nchi yetu inafika pale tunapotakiwa kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kubwa kwa kaka yangu, Mheshimiwa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, katika ukurasa wa 47 ameelezea kuhusu maboresho ya kuchimba dawa. Nakumbuka mwaka jana nilichangia kwa uchungu mkubwa sana jinsi akinamama wanavyonyanyasika wakati ule wa kuchimba dawa. Yeye kwa kuwa anawaonea huruma akinamama na anajua jinsi tunavyopata shida kule barabarani, alilichukulia wakati ule ule akalitolea maamuzi kuwa lazima hilo jambo lifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kuwa ameleta mpango mzuri sana kuhakikisha kuwa maboresho yanafanyika, tunaomba yafanyike kwa haraka sana ili sisi akinamama tusiendele kuaibika, tunaiabika sana katika kuchimba dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nawaomba akinamama wachangamkie hizi fursa, hizi pia ni ajira maana amesema kuna ramani na kuna kila kitu kimewekwa sawa waende pale walipoambiwa leo kwenye hii taarifa, wakachangamkie ili watu waweze kupata ajira, tunajua hata vijana wetu sasa wataajirika na tunajua kuwa haya maeneo yako katika kila Halmashauri. Kwa hiyo, kila Halmashuri zinaweza pia kufanya huu mpango, wakaweza kujiongezea kipato katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie habari ya viwanja vya ndege, niendeleo kupongeza kazi nzuri ya uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini. Nimeona viwanja vya ndege vingi vimeanza kuboreshwa na mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, nakushukuru sana, endelea kushirikiana na Wanakamati na tunakushukuru, tukikuita tukikushauri unatusikia. Tunaomba hata Wizara zingine ziige mfano wa Wizara hii, ndiyo maana itakwenda kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendeleo kuomba Wizara hii wapo viongozi wazuri sana, wanafanya kazi zao kwa umakini, lakini wamekaimu muda mrefu sana. Hata huyu wa viwanja vya ndege kila siku tunamsema, anafanya kazi nzuri na inaonekana, kwa nini na yeye asithibitishwe? Maana ni sawasawa na mama kila siku unakuwa nyumba ndogo, mwisho unaanza kuiba, ni bora uhalalishwe ili uweze kufanya kazi yako ujiamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwatendee haki wananchi wa Iringa hasa Jimbo la Iringa Mjini, kuna kiwanja cha ndege cha Nduli, namshukuru Naibu Waziri alikuja, akaona changamoto zilizopo katika uwanja wetu wa ndege. Zile changamoto tunaomba sasa zitendewe haki, ule uwanja unahitaji maboresho kwenye njia za kurukia ndege, uwanja ule hauna fensi kiasi kwamba binadamu wanakatiza na wanyama wanakatiza pale. Leo hii ikitokea ajali, mtaanza kuunda Tume, Tume ya nini, wakati inaeleweka? Mtakuwa hamtutendei haki kuanza kuunda Tume wakati tatizo kila siku tunalisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile maboresho yanahitajika katika jengo la abiria, lile jengo halina hata vyoo, tunaona hata aibu. Jengo la abiria wa ndege halina vyoo, naomba mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja ule pia hauna kituo cha mafuta, kituo cha mafuta kinatakiwa kiwepo kwa sababu tulipozungumza na wanaoleta ndege, sasa hivi kuna abiria, wanasema kwamba bei ni kubwa kwa sababu ndege mpaka iende Mbeya ije Dodoma kujaza mafuta, ndiyo maana bei imekuwa kubwa sana. Tunaomba waweke hata kituo kidogo tu ambacho kitasaidia ndege ziweze kujaza mafuta, zikifika pale Iringa zikiwa zimeishiwa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo linguine, ningeomba ufafanuzi, kuna barabara inayopita pale tuelezwe kama ipo ndani ya uwanja wa ndege au itapelekwa nyuma ya uwanja wa ndege, maana yake wananchi wamekuwa na wasiwasi, kama utakuwa

umesogezwa, maana yake kuna wananchi watasogezwa. Sasa waondolewe wasiwasi ili wajue kwamba, fidia zao zitakuwaje. Vile vile hakuna leseni ya uendeshaji, ni lini tutaipata kwenye uwanja ule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasemee pia Wazee, wazee ni dawa, tunaendelea kwa ajili ya wazee. Kuna wazee ambao wana madai yao ya siku nyingi sana. Hata Kumbukumbu la Torati, mimi siyo Mchungaji, lakini ni Mzee wa Kanisa, linasema kwamba, waheshimu wazee uendeleo kuishi maisha marefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazee waliokuwa *East African Railways* wanadai madai yao muda mrefu sana, hayo madai yao yamefikia wapi? Nakumbuka hata wakati ule walifanya maandamano Dar es Salaam. Tunasikia aibu kuona wazee wanalalamikia nchi hii haiwalipi, wazee wananung'unika, wengine wamekufa, hata Mzee wangu zamani alikuwa anafanya kazi kwenye shirika hilo, alishakufa, hata sisi wenyewe tunashindwa kudai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wawekeeni utaratibu mzuri, hata Mheshimiwa Waziri atakapojibu kujibu kwa sababu wao walitaka niwalete kwa Mheshimiwa Waziri, waje waongee naye, maana yake hawajui kama ni Wizara ya Fedha au ni Wizara hii. Sasa tunaomba japo atakapokuwa anajibu Wazee wote wakiwepo wa Iringa na Tanzania nzima waelezwe madai yao yamefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu *SUMATRA*, nafikiri wao ndiyo wadhibiti wa usalama wa vyombo vya usafiri majini na nchi kavu. Tunaomba *SUMATRA* pamoja na kwamba, wamejitahidi hata kwenye ripoti yake amesema kwamba sasa hivi wameendelea kuboresha kwenye mikoa karibu yote, tunaomba watoe elimu ya kutosha kwa abiria na kwa madereva wa daladala au madereva wote wanaoendesha magari. Abiria wengi sana hawaelewi haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii gari likiharibika njiani abiria ananyanyasika kiasi kikubwa sana, analala pale, hapewi kitu chochote, hapewi malazi, hapewi chakula na anaweza asipewe nauli akakaa hata siku tatu. Tunaomba wenye magari wawe wanasema kama gari likiharibika abiria anafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, abiria leo hii gari likipata ajali likaungua hawaelewi hata *compensation* ya mizigo yao, hawajui watalipwa na nani. Pia abiria akipata ajali, akivunjika mguu ama akifa, hatujui hata kwenye haya magari ile bima kama inahusu na abiria yule ambaye yupo kwenye gari lile. Tunaomba *SUMATRA* waendeleo kutoa elimu hiyo ili abiria wajue kwamba ni nani anawajibika kwa ajili ya madai yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Waziri kuwa ana huruma sana, sisi wote humu ndani ni walemavu watarajiwa. Nakumbuka hata Mbunge wangu wa Iringa alikuja siku moja na magongo humu ndani, hatukutegemea kama angekuwa mlemavu. Lakini vyombo hivi si rafiki na walemavu, ni lini sheria itakuja ili tuwawekee sheria na wao vyombo viwe rafiki na walemavu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mimi nimegawa baiskeli Mkoa mzima, lakini hawawezi kwenda kupandisha kwenye daladala, hawezi kupandisha kwenye basi, hata kwenye vyoo mnavyojenga barabarani na wenyewe watengewe maeneo kwa ajili ya walemavu. Sisi wote hapa ni walemavu, unaweza ukaja leo ume- *paralyze*, tayari ni mlemavu, hebu tujiangalie na sisi wenyewe tuwatendee haki walemavu. Tulete sheria itakayowabana wenye vyombo vya usafiri wawatendee haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kulikuwa na mgomo Iringa, niwape pole sana wananchi wa Iringa walipata tabu kidogo, lakini tatizo ni hawa *SUMATRA*, hebu waendeleo kuwaelimisha vituo vya daladala, vipo wapi na wajaribu kukagua, wao wanapiga tu faini bila kuwapa elimu, si kitu

kizuri. Unawanyanyasa wenye daladala, unawanyanyasa abiria kwa sababu abiria wale wanapata matatizo. Pale Iringa kuna *route* zingine ni ndefu sana...

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Eeh! Dakika kumi tayari! (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Mfutakamba, wajiandae Mheshimiwa Amina Mwidau na Mheshimiwa Moshi Kasoko.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii na niipongeze Wizara ya Uchukuzi kwa hotuba nzuri na kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo kwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Dkt. Tizeba, Katibu Mkuu Injiniya Chambo, Naibu Katibu Mkuu, John Mgondo na timu yao wote, napenda nizungumzie suala la uwanja wa ndege wa Tabora. Tunaishukuru Serikali ya CCM, sasa tuna lami tangu tarehe 8 Januari, 2013. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alifungua ule uwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa ndege ile ya *ATCL* ianze kushuka pale. Nilipata dharura kubwa Jimboni kule, wacheza mpira walianguka na lori, mchezaji mmoja ikawa haiwezekani kutibiwa hospitali ya Mkoa wa Tabora, tukampeleka Mwanza, Mwanza hawakuwa na kifaa cha ku-*decompress spinal cord* (uti wa mgongo), kwa hiyo ikabidi tutafute ndege ya kumsafirisha kutoka Mwanza mpaka Dar es Salaam. Kama *ATCL* ingekuwa inashuka Tabora pale tungeweza kumsafirisha kwa shilingi aghalabu laki tatu, lakini ilibidi itugarimu shilingi milioni moja kumleta mpaka Dar es Salaam pale Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara nyingi zinachelewa, huduma nyingi wanazikosa wananchi kwa sababu ndege ya *ATCL* haishuki pale Tabora. Tunaomba

ikienda Kigoma ishuke pale ndio ije Dar es Salaam na ikiwezekana waangalie uwezekano wa safari za Dar es Salaam – Tabora, Tabora - Mpanda, Mpanda - Kigoma, Kigoma - Bujumbura, Bujumbura - Kigali, hii italipa, naamini kabisa wasafiri wapo wengi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ziada ambayo ni mbovu. Nilipokuwa katika nafasi kama Naibu Waziri, kweli nilikwenda mpaka *Mbamba Bay* na Mwekezaji kutoka Dubai, yule Mwekezaji alikubali kujenga Cherezo pale *Mbamba Bay* ili waweze kujenga meli za uvuvi, meli za mizigo na pia meli za abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ilifuatilie suala hili kwa sababu rekodi zipo kwenye faili na yule mwekezaji nafikiri alikutana na *SUMATRA* wakamwambia abadilishe zile meli badala ya meli *design* aliyokuwa nayo walimpa *design* nyingine inayokubalika. Naamini naye ameshakubali kufanya hivyo, tufuatilie hilo *Mbamba Bay* pamoja na Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, mwekezaji huyu alikubali kuwekeza meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishwaji wa Chuo cha Reli cha Tabora pamoja na karakana. Karakana ya Morogoro, naamini kama tukiunganisha nguvu za Mang'ula, ingawa Mang'ula jana Waziri wa Viwanda alisema kwamba kile kiwanda pia kitafufuliwa kwa vipuri, lakini ninavyoelewa kimeshabinafsishwa, sasa labda mazungumzo yafanyike ili yule aliyebinafsishiwa labda arejeshewe pesa, lakini naamini vipuri ni changamoto kubwa katika Shirika la Reli na mashirika mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuki-*mobilize* hizi karakana mbalimbali, vipuri vingi ambavyo haviwezi kupatikana kwa sababu haviko kwenye *shelf*, ni lazima ufanye *order* ya miezi sita, nane, ufufuaji wa Injini zetu unaweza kuwa changamoto kubwa. Lakini tukiwa na karakana hizi, tukatumia mafundi wetu wa ndani wana ujuzi kabisa na

naamini tuna rasilimali kubwa ya mafundi ambao wanaweza kutengeneza vipuri vingi ambavyo tungetegemea viagizwe kutoka nje, tunaweza kuvizalisha hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki Chuo cha Reli cha Tabora kina historia ndefu na wapo wanafunzi wanaweza kutoka hata nchi jirani. Kwa hiyo, naomba kiimarishwe ili kiweze kutoa mchango mkubwa kwa watalaam wetu wa reli na nchi jirani wanaweza kuja wakafundishwa pale Tabora kwa sababu kinaweza kutoa taaluma mbalimbali ambazo zinahitajika kwa kuboresha huduma zetu za usafiri wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi Aprili, 2013, Serikali ya Kenya imesaini mkataba wa ujenzi wa bandari ya Lamu, magati matatu. Kampuni inayojenga ni kampuni ya CCC ya China, wanakubali kuanza kujenga haya magati, wataanza kuchukua mizigo ya Ethiopia, mizigo ya Sudan, Sudan Kusini pamoja na Uganda pamoja na ile reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuangalie kwa sababu kuna kitu cha kujifunza hapa, wenzetu wamepata hiyo nafasi na wameweza kujengewa *fly overs* kwa mkopo wa *Exim Bank* ya China, sisi kidogo tuna tatizo, lakini naomba ku-*quote* kauli moja hapa inasema kwamba dunia hii inakwenda haraka sana, kwamba kuna baadhi ya siku wakati mtu mmoja anasema haiwezekani anashtuliwa na mwingine ambaye anafanya kitu kile kile ambacho yeye anasema hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe makini, fursa hii tunayo kubwa, sisi tuna mahusiano mazuri sana na Serikali ya China na historia ndefu kuliko hata Kenya na Uganda,, lakini wenzetu wametumia fursa hii vizuri sana kujineemesha katika miundombinu na maeneo mengine ya biashara. Tuchangamkie sana fursa hizi ili tuweze kusukuma gurudumu la maendeleo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya CCM, nimekwenda Kagunga kwa Mheshimiwa Zitto, nilikuta kuna mawe tu, nimepata faraja kubwa sana Mheshimiwa Dokta

Harrison Mwakyembe ananiambia sasa gati la Kagunga, Kagunga ni mpakani mwa Tanzania na Burundi, lile gati lipo tayari kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze sana maamuzi ya Wizara kwa bandari ya Kipiri, bandari ya Kalema, hata mimi niliona yule Mkandarasi hakuwa na vifaa vya kutosha. Utaratibu aliokuwa anafanya kujenga yale magati usingeweza kutoa tija na ufanisi wa kutosha. Kwa hiyo, napongeza sana jitihada na maamuzi ya *TPA* pamoja na Wizara ili kubadilisha Mkandarasi kwa sababu wananchi wanahitaji sana huduma ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na yapo maendeleo makubwa pia katika bandari ya Kasanga. Katika bandari ya Kasanga niliona pale godauni ziko tayari, lakini mahindi mengi yanayotoka Katavi na Sumbawanga meli ile ya *MV*. Liemba ikisimamiwa vizuri na kama Wajerumani wamekubali kuikarabati, inaweza kuchukua mizigo mingi na hasa mahindi kupeleka Kigoma, Rwanda mpaka Burundi ambako mahindi yetu wanayapenda na watalipa kwa pesa za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kupongeza jitihada kubwa za ujenzi wa viwanja vya ndege. Tabora tunashukuru sana kwa hizo mita zilizojengwa mpaka sasa, lakini ili kuweza kuongeza biashara, ningependa kwamba, urefu wa *runway* uongezwe ili kuwe na uwezekano wa ndege kubwa zaidi, kuweza kufika Tabora kwa sababu tumejipanga kibiashara na kutakuwa na baadhi ya mizigo iweze kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini si kwa umuhimu, pale Tabora tuna njia karibu nane zinazolingia Mkoa wa Tabora. Kwa hiyo, *ICD dry port* ni sehemu ambayo ni muhimu sana Tabora na itakuwa siyo *dry port* kwa ajili tu ya mikoa inayozunguka Tabora kwa sababu lami sasa zinakuja Tabora, lakini pia hata nchi jirani za Zambia, DRC, Rwanda, Burundi, wanaweza kuleta mizigo yao pale na tukapanua uwanja wa ndege utakuwa tayari, baadhi ya ndege ambazo zinabeba mizigo zinaweza kushusha mizigo yao pale, Guangzhou ya Tanzania ikawa Tabora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, Tabora itakuwa Guangzhou tu, tutake tusitake, nakushukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana mtalaam wa magati kumi na tatu, kumi na nne, namwita sasa Mheshimiwa Amina Mwidau, wajiandae Mheshimiwa Moshi Kakoso na Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na bandari, naweza kusema kuwa Tanzania ni nchi ambayo ina bahati sana, naweza kusema kuwa Mwenyezi Mungu kaipendelea, kijiografia imekaa vizuri sana ukilinganisha na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nchi chache duniani zenye jiografia nzuri kama ya Tanzania na ambao hawakuitumia nafasi hiyo ipasavyo, naweza kusema kuwa tuko *under utilized* kwa jinsi ambavyo tuna jiografia nzuri, lakini hatujaweza kuitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imepakana na mataifa sita ambayo ni tegemezi *Land Locked Country*, ambazo ni Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia na Congo na zinategemea sana Tanzania japokuwa tunao majirani zetu Kenya na Msumbiji, lakini Tanzania ina nafasi ya pekee kwa sababu Kenya imepakana tu na Uganda labda sasa hivi tunaweza kusema na *Southern Sudan*. Msumbiji imepakana tu na Zimbabwe, Swaziland na Malawi, lakini Tanzania tumepakana na nchi sita, bado hatujalionga hilo kwa sababu bado tupo *under utilized* ya jiografia ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli bandari zetu zilitakiwa ziwe na pilikapilika kubwa sana, pia kiwe chanzo kikubwa kabisa cha ajira na pato la nchi yetu. Lakini inasikitisha kwa sababu hali sivyo ilivyo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tukiangalia Uganda, Uganda ipo karibu zaidi na Tanzania kwa upande wa Tanga kwa kutumia bandari ya Tanga kuliko hata kuja Dar es Salaam au Mombasa. Wakija Dar es Salaam tutakuwa tumenufaika, bado pato litakuwa linaingia nchini, lakini wakienda Mombasa itakuwa ni nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonisikitisha zaidi kuliko yote ni pale Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilivyotukatisha tamaa watu wa Tanga. Nasema hivyo nina sababu za msingi, Awamu hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilitupa matumaini makubwa sana wakazi wa Tanga na tukapata imani kubwa sana kuwa sasa Tanga itarudi enzi zake au zaidi ya vile kwa kuwa na bandari sasa, reli zitarudi, kukawa na matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tanga wakahamasika, walitoa maeneo yao upande wa Mwambani, walishirikiana kwa kiasi kikubwa sana japokuwa Serikali imewalipa fidia, lakini kilichotokea huwezi kuamini. Kitu cha kushangaza zaidi ni pale ghafla bandari ile ilipoota mbawa na kupaa kuelekea Mbegani Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilianza kama fununu, lakini nikawa napata matumaini kuwa ahaa, haiwezekani kwa sababu tulimwamini sana Rais, tukasema safari hii Tanga ameamua, alipompa Mheshimiwa Nundu kuwa Waziri wa Wizara hiyo, tukasema safari hii Rais ameamua Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nundu akatoka, nikasema haiwezekani bandari itakuja tu Tanga. Mheshimiwa Wassira aliposoma Mipango hivi juzi, fununu zile nikazona kwenye mipango. Nikasema hii bado nina matumaini, namsubiri Waziri akija kusoma hotuba yake. Leo Waziri alipokuja na hotuba yake hii, nikaona kuwa kilichoandikwa humu *I am sorry* Waziri Dkt. Mwakyembe, kwa kweli *to be honesty, I am sorry to say this*, lakini kilichoandikwa humu ni kama vile funika kombe mwanaharamu apite. Kwa kweli ni changa la macho la waziwazi. (*Makofi*)

Ni siasa! Haiingii akili hata kidogo! Mimi sio kama nawaonea wivu watu wa Bagamoyo, lakini mkiwa na baba mmoja ambaye wewe ni mkubwa anaku-*promise* kuwa utapata hiki, anakuja kumnunulia mtoto wa mwisho, kwa kweli unajisikia vibaya. Maendeleo ni sehemu yoyote, lakini Tanga iko *position* nzuri sana. Iko kwenye sehemu ambayo ingeweza kuleta manufaa kwa wazi wa Tanga na kwa Tanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo ukiangalia sisi Tanga tumepakana pale na Mombasa, tuko pua na mdomo. Leo Kenya kama alivyosema Mheshimiwa Mfutakamba pale, amesema pia Mheshimiwa Mtutura, wanajenga bandari ya Lamu; na Lamu kwa miundombinu yao ilivyokaa vizuri, kwa kweli ni bandari kubwa na Kenya ni Watendaji, hawana mikakati na mipango yenye makabrasha kama sisi. Watalitenda hili. Lakini pia sasa hivi nakumbuka Kenya wana Magavana, na Gavana ni kama Rais kwenye eneo lake na Gavana wa Mombasa - Mheshimiwa Hassan Joho alisema hivi karibuni; Mombasa pale pana sehemu inaitwa Shimoni, akasema kuwa hapa ni sehemu ambapo panafaa kuwa na bandari nyingine.

Kwa hiyo, ukiwa na bandari ya Mombasa, Lamu, Shimoni, Tanga tuko katika nafasi gani? Sisi bado tunapiga *mark time*. Kwa kweli kwa hili hatujatendewa haki na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kweli Tanga ni watu wenye hekima na busara, na ni wapole, lakini mmetufikisha pasipo, kwa sababu hizi ndiyo shukrani zenu za kupewa Majimbo yote Chama cha Mapinduzi na mnajisifu kabisa kusema Tanga hakuna upinzani. (*Makofi/Kicheko*)

Mimi niwaambie *very friendly*, hii ni talaka yenu. Mna mtihani mzito sana ambao majibu yake mtayapata mwaka 2015. Kwa sababu hiki mlichotutendea hapa, sisi hatutaandamana, wala hatutapigana mapanga, siyo desturi yetu hiyo Tanga. Lakini majibu yake mtayapata mwaka 2015. Hii siyo haki hata kidogo! Leo watu wameathirika, mnawachanganya watu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili halitoshi. Kuna fununu nyingine mpya, na sasa naziogopa fununu. Kuna fununu mpya kwamba hii bandari inaweza kujengwa Kigombe. Sasa mnawachanganya watu Mheshimiwa Waziri! Unapokuja hapa tunaomba utuambie, huo mwaka mtakapoamua itajengwa pale pale Mwambani au itajengwa Kigombe? Kwa sababu fununu hizi zinakwenda zinakua mpaka zinakuja kuwa za kweli. Au kutakuwa na bandari mbili; Mwambani na Kigombe? Yote tunaomba utufafanulie ili tuweze kujua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye fidia. Bandari hii iliendelea kuathiri watu wengine wa Tanga. Kwa sababu kuna maeneo ambayo *RAHCO* waliona wajiandae. Walikuwa na mkakati wa kujiandaa kuwa bandari ikijengwa Mwambani wapate sehemu ya kuweka makontena.

Kwa hiyo, kuna ndugu zangu wa Magaoni *A, B*, Saru maeneo yao yalichukuliwa, kaya kama 660 hivi wakaahidiwa kulipwa fidia, miaka minne nyuma. Kwa taarifa nilizonazo, wamelipwa hivi juzi, sijui wiki mbili nyuma! Lakini fidia ile siyo! Kwa sababu miaka minne ni muda mrefu! Mtu akikupa Sh. 10,000/= leo na atakayepewa Sh. 10,000/= baada ya miaka minne ni tofauti. Thamani zinatofautiana jamani, hesabu mbona zinawatatiza! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu wamelipwa fidia ndogo, hawajatendewa haki. Pia waliahidiwa kupewa na viwanja. Kwa sababu kwa taarifa nilizonazo wengine wamekataa ile fidia. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, Daktari, watu wamekusifu sana hapa; watu wanakuamini. Nakuomba unapokuja hapa mbele uniambie ile fidia wanayolipwa watu wa Magaoni ni ile ile au wataongezwa? Hivi viwanja walivyoahidiwa, ni kweli au siyo kweli? Naomba utoe ufafanuzi katika maeneo haya tafadhali, kwa sababu watu wameathirika sana, walikuwa na nyumba zao, wengine walikuwa wameanza ujenzi, ujenzi ule wamesimamisha. Wengine walikuwa na misingi na ilikuwa ni kero kubwa, lakini bahati nzuri mmewapa japo kidogo, japokuwa wengine wamevikataa. Naomba uwape ufafanuzi katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekee kidogo kwenye *ATCL*. Shirika hili sasa limefikia tamati. Najua Daktari ni hodari, anajitahidi, anachapa kazi. Lakini kwa hali iliyopo *ATCL* hakuna dalili zozote ambazo zinaonyesha kuwa litafufuka kweli kweli. Mimi nahisi Daktari labda unapokuja hapa, utupe mikakati ambayo itatutia matumaini, siyo mikakati ile ya kisiasa, mikakati ambayo bado hivyo hivyo tunapiga hapo hapo *mark time*; utupe mikakati ambayo ni kweli kabisa hili Shirika litafufuka.

Mimi nakumbuka mwaka 2012 nilikuwa kwenye Kamati ya *POAC*, Hesabu za Mashirika ya Umma, tulitoa mapendekezo hapa tukasema kwamba jamani hali ni mbaya sana. Hili Shirika tulizike kabisa ili tuanze upya. Lakini bado mliona kuwa kwa utaalam wenu kuna matumaini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa Amina, nakushukuru sana.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Kakoso, ajiandaye Mheshimiwa Kikwembe, ajiandaye Mheshimiwa Silinde.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii na mimi nipate kuchangia katika Wizara hii muhimu. Awali nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mwakyambe na Msaidizi wake Mheshimiwa Charles Tizeba. Hawa wamefanya kazi kubwa sana na wametoa matumaini kwa Watanzania.

Niwapongeze kwa kazi kubwa sana walioifanya hasa pale bandarini Dar es Salaam. Ukiritimba uliokuwepo pale ulikuwa mkubwa sana. Lakini kwa jitihada za Mheshimiwa Waziri ameonyesha njia njema ambayo itawakomboa Watanzania. *(Makofi)*

Nizungumzie suala la reli. Reli ya Kati ni reli muhimu sana kwa ustawi wa Taifa hili la Jamhuri ya Tanzania. Reli hii ikiimarishwa itatoa fursa nyingi za kiuchumi na itatoa mdirororo wa kiuchumi na kupunguza mfumuko wa bei. Mimi nina imani kubwa sana kama reli hii itaimarishwa Watanzania wengi watanufaika na Taifa hili litasonga mbele kiuchumi. Naomba sana Wizara ifanye kila jitihada za dhati kuhakikisha inaboresha huduma za reli. Reli ya Kati ni kiungo muhimu kati ya Mataifa jirani. Mataifa ya Burundi, Congo kama watakuwa wameiboresha reli hii, itakuwa imeongeza uchumi na tutasafirisha mizigo mingi sana itakayoiongezea nchi yetu pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya Mpanda; wananchi wa Mpanda, wananchi wa Tabora wanahitaji sana huduma ya reli ya Mpanda. Reli hii ni muhimu wa usafirishaji wa mazao yanayozalishwa katika Mikoa ya Rukwa na Katavi. Hali ilivyo, hali ya reli ni mbaya sana, yaani hata maelezo yake hayaelezeki. Niiombe Wizara ifanye kila jitihada za dhati kuhakikisha inatenga fedha za kuboresha reli hii. Nina imani wenzangu walionitangulia wamezungumzia mengi sana juu ya reli ya Mpanda, Kaliua, lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri afanye jitihada za dhati kufika kukagua matatizo ya reli ya Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tumekuwa tukichangia Waheshimiwa Wabunge tunaotoka katika maeneo hayo, lakini Mheshimiwa Waziri hajafanya utafiti wa kina kwenda kufanya utafiti kwenye reli hii. Hali ya behewa za reli ya Mpanda au treni ya Mpanda ni mbaya, zina uwezo mdogo sana wa kuchukua abiria, lakini mabehewa yenyewe ni chakavu kupita maelezo. Ni reli ambayo kimsingi unaweza ukaandika historia. Katika reli hii unaposafiri na treni ya Mpanda ndiko pekee kunakopatikana mpaka kunguni kwenye mabehewa ya reli hii. Niiombe Serikali ihakikishe inaboresha huduma ya treni kwa wakazi wa Mkoa wa Katavi na Tabora kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usafiri wa majini Ziwa Tanganyika; tuna meli moja tu ya MV. Liemba ambayo ina

umri wa zaidi ya miaka 100. Meli hii ndiyo imekuwa ikitoa huduma katika mwambao mwa Ziwa Tanganyika kuanzia bandari ya Kasanga mpaka Kigoma. Wananchi walio wengi wanatamani kusafiri na meli hii, lakini inafanya safari mbili tu kwa wiki jambo ambalo haliwasaidii sana wananchi wa mwambao wa *Lake Tanganyika*. Niiombe Serikali wahakikishe wanaifanyia matengenezo meli hii ili iweze kukidhi mahitaji ya wananchi. Lakini napata shaka sana kwenye meli hii endapo Serikali haitaweka mipango thabiti ya kulfanyia ukarabati mapema. Inawezekana tukasababisha ajali nyingine kwa sababu meli hii imezeeka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya kina; tulikuwa na meli mbili katika Ziwa Tanganyika; meli ya MV. Mwongozo na meli ya MV. Liemba. Meli ya MV. Mwongozo imebadilishwa matumizi kiasi kwamba inafanya sasa kuwe na matatizo ya hali ya usafiri katika Ziwa Tanganyika. Ni kwa nini meli hii isirudishwe iweze kutoa huduma katika maeneo hayo? Naomba Serikali ije na maelezo ili tuweze kupata maelezo yatakayosaidia kutatua tatizo la usafiri katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa bandari. Bandari ya Karema, Kipili na Lagosa ni bandari muhimu sana katika maeneo haya. Nitoe pongezi za dhiti kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuchukua hatua za dharura kumfukuza Mkandarasi aliyekuwa amepewa kazi hizo. Lakini kumfukuza pekee haitoshelezi, tunaomba sasa mchukue hatua za kuweza kukamilisha ujenzi wa bandari hizi. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa majibu atuambie ni lini ujenzi wa bandari za Kipili, Karema na Lagosa upande wa Mkoa wa Kigoma zitakamilika? Lakini tukija na hadithi na ngonjera ambazo zimezoeleka, kwa kweli hatutakuwa tumewatendea haki wananchi. Naomba Mheshimiwa Waziri afanye kila linalowezekana kukamilisha tatizo la ujenzi wa bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi aliyekuwa amepewa nafasi ya kukarabati au kujenga bandari hizo,

nasikitika sana kwamba Serikali ilifanya makosa. Alipewa Kandarasi kwa maeneo yote matatu, kiasi kwamba uwezo wake ulikuwa mdogo na amesababisha hasara kubwa sana pale na ile hasara aliyokuwa amesababisha, naomba Serikali imchukulie hatua aweze kufidia fedha ambazo kazitumia za Serikali wakati hajafanya kazi ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni vituo vinavyotumiwa na meli ya MV. Liemba. Vituo ambavyo MV. Liemba inasimama ni vituo vichache sana katika ukanda wa Ziwa Tanganyika. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri aongeze safari zile za MV. Liemba na ahakikishe kunakuwa na vituo ambavyo vitatumiwa na wananchi kama kituo cha Msamba upande wa Mkoa wa Rukwa, Msamba Namansi na maeneo mengine ambayo ni ya kiuchumi katika Mkoa wa Kigoma ili waweze kupata nafasi ya kusafiri.

Mara nyingi meli zinapokuwa zinafanya safari zake, wananchi wanashindwa kupata nafasi ya kupanda meli hiyo kwa sababu baadhi ya maeneo hakuna vituo vya usafiri. Naiomba Serikali ifanye kila linalowezekana kuhakikisha huduma hii inatolewa katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie na eneo la usafiri wa anga. Mpanda tumebahatika kupata uwanja mzuri na wa kisasa, ambazo ni jitihada za Wizara. Nawapongeza sana. Lakini tuna tatizo moja, hatuna route za ndege kubwa.

Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atufanyie mpango mahususi kuhakikisha tunapata huduma ya usafiri wa anga kwa kupata ndege za ATC au Precision Air. Hii itajenga uchumi katika maeneo haya na kufanya wananchi wa Wilaya ya Mpanda na Mkoa wa Katavi kwa ujumla waanze kutumia usafiri wa anga. Lakini kama hatutakuwa tumefanya hivyo, hatutakuwa tumewasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Kakoso. Sasa namwita namwita Dkt. Kikwembe, ajiandaye Mheshimiwa David Silinde na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wote walioweza kuelezea umuhimu wa reli katika ukuaji wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza kabisa, naomba niongelee hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya mwaka 2012/2013. Ukienda ukurasa wa 12 na wa 13 mwaka jana nilichangia katika eneo hili na sikuweza kupata majibu ya uhakika. Ilikuwa ni kuhusu utengenezaji na ununuzi wa injini na mabehewa mapya.

Mheshimiwa Waziri aliongea kwamba kwa sababu teknolojia ya mabehewa na injini zilizokuwepo vilipitwa na wakati na inawezekana kabisa viwanda vile sasa hivi havitengenezi ama viko kwenye teknolojia nyingine, kwa hiyo, ni ngumu mpaka pale watakapoweza kubadilisha reli kwa kiwango cha ratili 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye hotuba ya mwaka huu 2013 katika ukurasa wa 14, 15 utaona kwamba pesa iliyotengwa ya Shilingi bilioni 104 ya mwaka 2012 ambayo ilikuwa ifanye ukarabati na kununua vichwa vipya vya treni 13, injini za treni hizo; mabeha mapya 22 na mabehewa 34 ya breki.

Katika mwaka *TRL* iliweza sasa kuingia mkataba kwa ajili ya kujenga upya vichwa vya treni nane, kununua mabehewa 22 ya abiria, mabehewa 34 ya *brake*, mashine moja ya kutandika reli na kadhalika, kwa maana kwamba hii kazi haikufanyika na mwaka 2012 katika hii bajeti tuliiongezea pesa. Sasa kama ile pesa haikwenda, tunataka tuelezwe, ile pesa tuliipitisha hapa kwa misingi ipi na kama tuliipitisha, kwa nini haikwenda kutumika kwa kazi ile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda moja kwa moja kwenye suala la reli ya Tabora – Kaliua - Mpanda. Katika bareti hiyo hiyo ya mwaka 2012 na mwaka 2013 anakwambia kilomita 5.5 mpaka ilipofika mwezi Mei ndiyo zilizokuwa zimekarabatiwa. Lakini kwenye bajeti hii tena 2012, limeongelewa hilo suala kilomita 5.5 kwa maana kwamba kilomita 3.5 zinasubiri sasa, hizo zinasubiri kukarabatiwa. Hazikukarabatiwa kwa sababu ya kutokana na kukosekana kwa vifungio vya reli mataruma.

Kwa maana hiyo basi, wananchi wa Mpanda wategemea kuendelea kuwa na tatizo la reli na usafiri wa reli mpaka pale hivyo vifungio na mataruma yatakapopatikana. Zitapatikana vipi? Vitapatikana baada ya kutekeleza mradi wa kutandika reli mpya ya uzito wa ratili 80 kwa *yard*. Kwa maana gani? Mnataka kuwaambia nini wananchi wa Mpanda? Mnataka kuwaambia nini wananchi wa Katavi? Wamekosa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara kutoka Tabora mpaka Mpanda, kupita Koga, Sikonge pale mpaka Inyonga kuingia Mpanda, imetengewa Shilingi bilioni mbili. Barabara ile sasa hivi haipitiki kwa amani. Mvua za Mpanda mnazifahamu, mvua za Tabora mnazifahamu, barabara ile haipitiki. Wananchi wanategemea treni ya kutoka Mpanda mpaka Tabora. Tuna wagonjwa kule wanakwenda *Referral Hospital*, Bugando, Muhimbili; nimeongea sana kuhusu hili suala, lakini sasa sielewi tatizo ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kilometa tatu Mheshimiwa Arfi kawaeleza hapa. Treni ya Mpanda ni sawa na Lori jamani! Ukipanda mle mjamzito wa miezi nane na nusu, utajifungua, kwa jinsi inavyoruka, inavyoyumba. Amesema Mheshimiwa Kakoso, ina kunguni. Siyo kunguni tu wala siyo misumari tu aliyosema Mheshimiwa Arfi; ina panya wale wakubwa, wale panya wakubwa hasa! Ukimwona kama sungura! Unaweza ukakimbia. Eeh! Halafu bado mnasema, Mungu wangu!

MBUNGE FULANI: Nyama choma hiyo! (*Kicheko*)

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Eeh, jamani! Wananchi wa Katavi wamekosa nini? Ni wazalishaji wakubwa, tunazalisha alizeti, tunazalisha mahindi, tunazalisha mpunga, mchele safi kabisa; eeh, leo hii kweli, namna hii? Haiwezekani hata kidogo! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwakyembe, naomba sana eneo la Kaliuwa pale mpaka Mpanda, lifanyiwe marekebisho mwaka huu kabla ya mvua za mwezi wa Tisa hazijaanza ili wananchi waweze kutumia hayo mabehewa. Niliongelea suala la kuongezwa mabehewa. Kuna behewa moja tu la *Second Class*, mabehewa ya *Third Class* ni machache ambayo kwanza hayatoshelezi, ameshasema pale Mheshimiwa Arfi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiografia ya Katavi, utatoka Mpingo, utatoka Karema, utatoka Mishama, utatoka Mwese, lazima ulale Mpanda pale. Nimeongelea pale majengo, *Station* ya Mpanda; sio kila abiria atatoka kule ana hela Sh. 20,000/=, Sh. 30,000/= ya kulala *guest*. Pale hakuna kituo cha abiria kupumzika, hakuna vyoo vya uhakika; eeh, lazima ulale pale kesho yake ndio uanze usafiri. Safari zenyewe sasa, bora hata ingekuwa inafika *on time*. Unaweza ukaambiwa treni inafika saa 7.00 mchana ikafika saa 10.00 usiku, kwa maana kwamba huwezi kuondoka, itabidi ukae pale *Station*. Utatoka pale unakwenda Tabora, unaweza ukashangaa mmefika Kaliuwa, ama mmefika kilometa 60 kabla ya kufika huko Tabora au kabla ya kufika Urambo, kichwa kimekufa na hapa tunaambiwa vinatengenezwa. Kwenye Bajeti humu tunaambiwa vinatengenezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi treni ya kutoka Tabora kuja Dodoma imekwama Zuzu hapo. Kichwa kimetoka Salanda, haya yanayovuta pale kwenye mlima ikikwama, ndiyo yamekuja kuingiza treni hapa Dodoma. Jamani! Mimi sikatai, kazi inafanywa vizuri, lakini tuwaangalie hawa wananchi wa Vijijini; tujiangalie sisi tunaotumia treni. Usafiri wa treni ni rahisi kuliko wa basi, ni rahisi kuliko wa gari. Mwananchi wa kawaida ndio anaoutegemea. Siyo wa

kawaida tu, kwanza mimi napenda kutumia treni kwa sababu najua ina raha yake tofauti na magari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kweli, najua juhudi za Mheshimiwa Mwakyembe, anavyofanya kazi kwa bidii. Sasa sijataka hii bidii yako iyumbeyumbe kwa wananchi wa Katavi; tafadhali endelea na juhudi yako, lakini hakikisha matatizo ya Kaliua pale, kutoka Tabora mpaka Mpanda, kupitia pale Kaliua mpaka Ugala pawe vizuri. Nilisema tunaomba mabehewa ya kutoka Mpanda ya *Second Class and First Class* ambayo wananchi watakata tiketi kutoka Mpanda mpaka Mwanza ama kutoka Mpanda mpaka Kigoma ama kutoka Mpanda mpaka Dar-es-Salaam, na siyo kukata tiketi za vipande vipande. Mbona zamani ilikuwa inawezekana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo ukienda kukata tiketi ya *Second Class*, unaambiwa lazima ufanye kwanza *booking Tabora*. Kwa hiyo, huwezi kukata tiketi Mpanda mpaka ufanye *booking Tabora*. Sasa sijui Tabora unafanyaje *booking* na wewe uko Mpanda, eeh! Hatutegemei kwamba, kila mtu ana ndugu Tabora pale ama kila mtu ana simu pale anaweza akapiga *Tabora Railway* pale akawekewa nafasi, sio rahisi. Kwa hiyo, naomba hilo nalo mlirekebishe. Kwamba, mwananchi anatoka Mpanda anakata tiketi yake moja kwa moja, *booking* inafanywa Tabora. Ndiyo kazi ya *Station Master*, ndiyo kazi ya Mkatisha Tiketi pale. Yeye ndio afanye mawasiliano kule, ili mwananchi awekewe nafasi, ili aweze kusafiri vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunabeba wagonjwa, tunabeba wazee, wameshatamka wenzangu Wabunge humu, watoto, lakini hali ya kwenye mabehewa siyo nzuri kabisa. Unaweza ukasafiri kutoka pale ukafika una *TB*; unatoka Mpanda mpaka Tabora, unafika kwanza umepunguza uzito kwa ile adha iliyoko mle ndani. Kwa hiyo, naomba hilo pia mliangalie na napenda pia nipate majibu mazuri tu, ambayo kwa wana-Mpanda, yatawapa matumaini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Karema, narudia, wenzangu wote wametamka. Wananchi wa Karema hawajafurahia tu kwa kumfukuza yule Mkandarasi, hapana. Wanachotaka kuona ni ile Bandari inafanya kazi. Miaka 50 ya uhuru, tunaimba, tunashangilia, tunachekelea, lakini pale siyo pazuri. Ziwa Tanganyika mnalifahamu liliyo, likichafuka lile ni kasheshe. Sasa tunaomba kwa kweli, hebu mtutengenezee pale. Karema ni mahali pazuri sana, pana *beach* nzuri mno! Nawakaribisha Waheshimiwa Wabunge mje Karema mtembee, ni pazuri mno. Pakitengenezwa pale ni kivutio kizuri sana cha watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kabisa, najua Mheshimiwa Waziri ananisikia, na Mheshimiwa Tizeba ulikwishafika pale, nakuomba upaangalie kwa jicho kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa ukataji tiketi. *(Makofi)*

(Hapa kengekele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Dokta Kikwembe. Sasa namwita Mheshimiwa David Silinde, ajiandae Mheshimiwa Mariam Kisangi na Mheshimiwa Kayombo.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 wakati tunapitisha Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano, moja ya mambo ambayo niliyazungumza, niliomba Serikali iwe na vipaumbele. Tatizo la Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni kukosa vipaumbele. Hilo limejirudia tena leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Uchukuzi, ukipitia Hotuba nzima, huwezi kujua kipaumbele ni kipi. Ni reli, ni bandari ama ni masuala ya ndege? Hakuna kipaumbele! Watwambie watueleze kwamba kipaumbele chetu namba moja mwaka huu ni bandari na tutahakikisha kabisa kwamba tunajua fedha zote zinazopatikana kwa kiwango kikubwa

zinakwenda kwenye bandari. Hatujapewa kipaumbele namba moja. Huo ndiyo ukweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia hotuba nzima imeelealelea tu, kila mahali inagusa. Ndio maana hata hako kasungura kadogo kanakopatikana kanashindwa kufanya kazi. Mwisho wa siku tutashindwa kupima weledi wa ufanyakazi. Tutampongeza kwa reli ya Dar-es-Salaam ya siku mbili, tatu, ambayo inahudumia watu wachache wa Dar-es-Salaam, haiwahudumii watu wa Tunduma na maeneo mengine. Sasa tunataka tuwe na kipaumbele kimoja ambacho kitalifaidisha Taifa. Tunataka mfanye kama ilivyofanya Wizara ya Nishati na Madini kwamba kipaumbele chetu mwaka huu ni kuhakikisha Bomba la Gesi linajengwa kwa ajili ya maslahi ya Taifa. Tukienda kwa mfumo huo, hii nchi itafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie msongamano katika eneo la Tunduma, mpaka wa Tunduma. Ni kwamba, ukipitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hili suala halipo kabisa na kiukweli wao wanalalamikia Wizara ya Fedha. Ukienda Wizara ya Fedha, wanalalamikia magari ya mizigo ambayo yako chini ya Wizara ya Uchukuzi. Sasa hapa zinakuwa ni Wizara mbili ndani ya Serikali moja ambazo kila moja inashindwa kujua wajibu wake ni nini. Sasa tukiendelea hivi, maana yake tunaendelea kupoteza mapato kwa ajili ya faida, kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Tunduma kila mwezi huwa linaiingizia mapato Serikali Shilingi bilioni 1.8 mpaka Shilingi bilioni mbili kila mwezi. Kwa mwaka siyo chini ya Shilingi bilioni 48 mpaka 50, eneo la Tunduma. Lakini pamoja na mapato hayo, bado eneo la Tunduma halipati hata mrahaba wala *Service Levy* wala kitu chochote. Hakuna tozo yoyote ambayo Mamlaka ya Mji wa Tunduma inaipata. Lakini jambo la pili, hatupati huduma ambazo tunazihitaji ikiwemo; maana nilipeleka mapendekezo na Mheshimiwa Naibu Waziri anajua. Safari moja tulikutana Mbeya, tukapeleka mapendekezo, ambayo hata Mheshimiwa Rais alishawahi kuahidi kwamba tujenge Bandari ya nchi kavu kwa sababu

eneo lile lina msongamano mkubwa wa watu, lina msongamano mkubwa wa masuala ya biashara, kwa hiyo, na magari msongamano wake ni mkubwa. Tutakapojenga Bandari Kavu maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja tutaongeza ajira; pili, tutapunguza msongamano wa magari; lakini tatu, tutawezesha Serikali kupata mapato zaidi. Lakini Serikali, bado haisikilizi mawazo mbadala kwa ajili ya faida ya hili Taifa. Sasa matokeo yake ni nini? Madhara yamekuwa mengi na kiwango cha ongezeko la ugonjwa wa *UKIMWI* katika eneo la Tunduma kimekuwa kikubwa zaidi ya kiwango cha *UKIMWI* cha Taifa, ile tunayosema *percentage ratio* ya Tunduma. Yote ni kwa sababu ya msongamano wa magari pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu ya migomo ya madereva waliyoitoa, ilikuwa ni pamoja na msongamano wa magari pale Tunduma. Kwamba wanatoka Dar-es-Salaam, wakishafika Tunduma wiki mbili, wiki tatu, magari hayaendi nchi yoyote ile. Ukiangalia mpaka wa Tunduma, ndiyo mpaka ambao unapitisha magari kwenda nchi zote za *SADC*. Leo tunapuuzua, tunauacha, tunakuwa na mipango isiyotekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiendelea na mfumo huu, tuieleweje Serikali hapo? Kwa sababu, tukiendelea kupongezana, maana yake tunapooza hoja na tutaendelea na mambo yale yale kila siku na hatutapata majibu juu ya hili Taifa. Kwa hiyo, tungependa tupatiwe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine, kulikuwa na madai ya madereva wa magari makubwa waliyatoa mbele ya Waziri wa Uchukuzi wa kipindi hicho, alikuwa Mheshimiwa Nundu. Naamini pamoja kwamba, Mheshimiwa Nundu alikuwa ni Waziri wakati huo, bado kuondoka kwake haina maana kwamba yale matatizo yameondoka, ameyaacha Ofisini kwa sababu, nafasi ya Waziri wa Uchukuzi bado iko pale pale, walidai Mikataba ya Ajira, bado wanalalamikia. Walitaka wawe na mishahara ya moja kwa moja, ambayo inakwenda kukatwa na *PSPF*, *NSSF* na

kwingineko, lakini mpaka leo bado hawakatiwi. Sasa hawa ni binadamu kama binadamu wengine, tunaomba Mheshimiwa Waziri, alifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni vizuizi vya magari makubwa ya mizigo kuwa vingi barabarani. Mheshimiwa Kagame alishawahi kuzungumzia hili kwamba, haiwezekani unatoka Dar-es-Salaam mpaka Kigali, kuna vizuizi 29. Hii ni Serikali ya namna gani ambayo mnashindwa kuaminiana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tumejenga mfumo wa kutokuaminiana na ndiyo maana tumejenga mfumo wa wizi kwa sababu hakuna mtu anayemwamini mwenzake. Vizuizi vimekuwa vingi, ndiyo maana imekuwa ni magendo magendo tu! Kila mtu anaficha! Magari yanabeba mizigo mingi, yakifika mahali shusha, na rushwa inaongezeka kwa sababu, tumekosa kuaminiana. Sasa haya tunahitaji tupatiwe majibu, lakini wakati huo Wizara ya Uchukuzi mkae na Wizara ya Fedha, tujue. Mheshimiwa Mwakyembe vilevile ulishawahi kwenda pale Tunduma, ukawaambia kwamba magari yapite saa 24. Siku moja tu yakapita, siku iliyofuatia hamna kitu. Sasa mkae upya, maana kila siku tumekuwa tukileta haya mawazo, hamsikii. Mnataka tuwaambie nini ili muweze kutusikiliza? Kwa hiyo, sasa tunataka mje na majibu ya msingi yatakayoweza kulisaidia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie masuala ya reli. Mwaka juzi huo huo 2011, nilisema Serikali ya Chama cha Mapinduzi, haijawahi kujenga hata kilometa moja ya reli kwa fedha zake za ndani. Hata kilometa moja ya reli kwa fedha zake za ndani! Nilizungumza hili na ninarudia tena kusema; jamani, tukienda kwa mfumo huu wa kutegemea fedha za Wahisani, wa kutegemea misaada, hatutafika mahali popote. Hakuna mtu anayeomba au anayetegemea nyumba ya mtu mwingine kumlisha mtu mwingine ukaendelea, haipo, ni aibu. Haiwezekani Taifa moja likategemea mawazo ya Taifa lingine kuhakikisha kwamba tunapata maendeleo. Kwa mfumo huu hatutaweza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya Kati, hakuna mtu ambaye hajui kwamba ilijengwa na Mjerumani. Reli ya TAZARA hakuna mtu ambaye hajui kwamba ilijengwa kwa msaada wa Mchina. Lakini mpaka leo reli hizo ndiyo zimekuwa mwendo mzima ni ukarabati, ukarabati, ukarabati. Hatuelewi tunakwendaje! Tuna-*invest* vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa nchi ya Thailand, wao Serikali imeamua, imekwenda kukopa Benki ya Dunia, yaani kwa maana ya *World Bank* pamoja na *IMF*, bilioni 600 *USD*, wanafumua reli za nchi nzima na kuweka reli katika nchi yao kwa manufaa ya nchi yao. Wao wanasema ile reli siyo huduma kama sisi tunavyoizungumzia, ni *investment*. Tunawekeza kwa ajili ya Taifa letu.

Mataifa yote yameendelea kwa sababu, wana miundombinu bora, wana-*infrastructure* bora na ndiyo maana leo tunakwenda kuiga kwao, lakini sisi tunakwenda tunaiga tunashangaa, tutafika lini, tumekosa uaminifu; hatuwezi kwenda kwa mfumo huu. Serikali, ichukue maamuzi magumu, tuamue kujenga reli zetu, tuamue kujenga bandari yetu; tukikopa fedha za kutosha kwa manufaa ya Taifa letu. Lakini kwa kuendelea hivi hivi na kasungura kadogo na fedha ambazo hazitekelezeki ni sawasawa na kazi bure. Tutawasifu kwa kuongea vizuri na kuweza kujibu hoja, lakini kwenye utekelezaji ni sifuri. Hatuwezi kwenda katika mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa tupewe ufafanuzi. Hizo gharama za ununuzi hata hivi vichwa tu vya reli ni kiasi gani? Kwa sababu, ukarabati umekuwa mwingi mno. Unaangalia kukarabati tu labda vichwa viwili vya treni dola laki nane, *almost 1.3 billion, a lot of money*, yaani ni hela nyingi. Sasa tupewe ufafanuzi tujue kama tutaendelea kukarabati. Maana kitu chakavu kitaendelea kuwa chakavu na ndiyo maana ilipitishwa ile Sheria humu ndani kwamba, tuendeleo kununua vitu chakavu ili tuendeleo kutumia gharama nyingi za kulipia matengenezo. Sasa huu ni mfumo wa kupoteza fedha za Serikali. Ni bora tukanunua kitu kipya kitakachokaa muda mrefu na kitakachosaidia kupunguza gharama zisizokuwa za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili lingependa tuweze kupatiwa ufafanuzi. Ukipitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameelezea Shirika la *TAZARA* kupata hasara; sasa tueleze ni hasara kiasi gani? Kwa sababu hapa unaona tu tunaunda Kamati kupitia mahesabu ya Mamlaka. Sasa mahesabu ya Mamlaka, kila siku mahesabu, tumeibiwa, hasara; tuelezwe hasara kiasi gani na nani amesababisha? Maana hizi Tume zimezidi, Kamati zimezidi. Tunaendelea kuliibia Taifa na tunaendelea kuliangamiza Taifa letu wenyewe. Tuwe wakali juu ya hili na tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nizungumzie Shirika la Ndege la Taifa, *ATCL*. Mwalimu Nyerere wakati anaondoka, wote tulikuwa tukijua na tumekuwa tukilirudia hili; ameondoka Taifa likiwa na ndege 11, Shirika la Ndege la Taifa. Leo tuna ndege moja tu na ndege yenyewe ndiyo hiyo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakieleza kwamba mara sijui imetoboka kioo, mara sijui hairuki, mara inafika masaa nane! Sasa tunauliza tunakwenda mbele ama tunarudi nyuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa mfumo huu, ndege yenyewe ikumbukwe ilikuwa ni msaada wa Wachina, kwa hiyo, ni vizuri tukaliweka vizuri hili na ikaeleweka. Serikali, mpo wapi? Hatuwezi kununua ndege zetu wenyewe na ninyi wenyewe mnajua utaratibu wa kununua ndege?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ni gharama na mtalalamika kwamba ni gharama. Sasa kama hamwezi, mnaona ni gharama kubwa, basi tupeni sisi ambao tunaona hizo gharama ni ndogo tuweze kuongoza ili tuweze kuwasaidia Watanzania kwa ajili ya kulifikisha kule tunakotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Silinde. Namwita Mheshimiwa Kisangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Kayombo na Mheshimiwa Juma Njwayo ajiandae.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa naanza kwa kuunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii tokea wamechaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema naunga mkono hoja, na sababu za kufanya hivyo ninazo. Sababu ziko nyingi za kuunga kwangu mkono hoja, lakini kuna mambo ambayo yamenigusa mimi na wananchi wa Mkoa wa Dar-es-Salaam, kwa yale ambayo wamefanyiwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo kwanza, kwa mara ya kwanza Serikali imerudisha shehena ya meli yenye mafuta yasiyo na viwango. Hilo siyo suala dogo. La pili, Serikali imefanya mabadiliko makubwa ya uongozi katika Mamlaka ya Bandari jambo ambalo limeleta tija kwa Serikali. Tatu, Serikali, Mheshimiwa Waziri na Naibu, wamesaidia sana kuibua na kuvumbua mtandao wa wizi ndani ya Bandari ya Dar-es-Salaam. Nne, kusimamia na kufuatilia kwa karibu mwenendo mzima wa Shirika la Reli ya TAZARA. Tano, kuanzishwa kwa usafiri wa treni jijini Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo siyo mambo madogo. Haya mambo yamekuwa yakisemwa sana mpaka tunaonekana Chama cha Mapinduzi, hakuna tunachokifanya, lakini Chama cha Mapinduzi, kimefungua njia Mkoa wa Dar-es-Salaam. Nashukuru sana Viongozi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono hoja, kutokana na sababu zangu nilizozitaja hapo japokuwa ziko nyingi, sasa naomba nielekeze mchango wangu katika maeneo yafutayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naanza na Bandari ya Dar-es-Salaam. Bandari ya Dar-es-Salaam nimesikia kwamba kwa utaratibu uliowekwa sasa hivi, imeweza kupata tija kubwa sana. Lakini bado nichangie

kwamba liko tatizo kwa wakazi wa Dar-es-Salaam maeneo yanayozunguka bandari hasa maeneo ya Kurasini magari yanajaa sana ya makontena kule hali ambayo ni hatari kwa wakazi wa maeneo hayo; yanaziba njia yote maeneo ya Kurasini mpaka unafika hapa Bendera tatu kila wakati. Ninashukuru tu juhudi za Jeshi la Polisi na *traffic* wanasaidia mara nyingine njia inapofungwa kutuweka sawa angalau wananchi wapite na daladala na magari madogo. Hilo ni tatizo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Waziri alipiga hodi Kontena *Terminal* Bandari, mimi nakwambia ingia, tena ingia uone na ukifika huko utuambie kulikoni? Juna nini? Kwa sababu ile shehena ya magari yanayojaa pale na makontena tatizo liko ndani ya Bandari. Kwa nini hawaingizi yale magari kwa muda yakatoka yakaendelea na safari zake? Sasa mimi kwa vile Mheshimiwa Waziri alishapiga hodi na akaingia sasa tunakusubiri majibu yako Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nichangie bandari hiyo hiyo. Bandari ya Dar-es-Salaam iko Dar-es-Salaam na ndiyo yenye jina hasa! Lakini hata ajira ndogo ndogo kwa vijana wa Dar-es-Salaam na hasa wale wanaokaa Temeke na Kurasini ndani ya Bandari ni tatizo. Mle amewekwa sijui *agent* gani, anawachukua vijana anawaambia sijui nendeni Serikali za Mitaa. Wakija huko anawalipa Sh. 5,000/= kutwa, yaani vitu havieleweki na mwisho vijana wale wanashindwa hayo masharti na vijana wa Temeke hawafaidiki. Tunaomba Mheshimiwa Waziri na Uongozi wako na mabadiliko uliyoyafanya, hebu sasa muiangalie Temeke ambayo ndiyo imebeba Bandari nzima kwa jicho la huruma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mamlaka ya Bandari imeajiri takribani wanawake 3,000, ninaishukuru Wizara na nashukuru Mamlaka siku ya sherehe yao ya wanawake inawapa vitenge. Lakini vitenge peke yake havitoshi. Naomba kuwepo Dawati la Wanawake katika Mamlaka ya Bandari nao wajengewe uwezo na ujasiliamali. Wanawake wale wa Bandari wanafanya kazi ndani ya

Mamlaka ya Bandari kwa masaa mengi. Wanapokuja kustaafu wanakuwa maskini, hawajui hata pa kuanzia wala pa kuishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeingia pale kuongea na akina mama wale, wanahitaji msaada wa elimu endelevu ya maisha yao. Kwa hiyo, Bandari inazalisha na akina mama wale wana mchango mkubwa sana wa kuzalisha ndani ya Bandari. Hivyo Serikali iwaangalie kwa kuwawekea Dawati lao na wapewe elimu ya ujasiriamali na pia iwatengee muda wa wanawake wale angalau wakutane na wabadilishane mawazo, wasifanye kazi kama utumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kwenda kwenye Bandari, sasa naomba nichangie kwenye eneo la uwanja wa ndege. Uwanja wa ndege wa Dar-es-Salaam ndiyo mama. Naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga viwanja vya ndege katika Mikoa mingi kweli ya Tanzania. Hayo ni maendeleo! Miaka 50 iliyopita uwanja ulikuwa Dar es Salaam na ule mdogo na *KIA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Maendeleo yapo, japokuwa hayaendi kwa kasi, lakini yapo. Uwanja wa ndege wa Dar-es-Salaam ndiyo mama, Uwanja ule tunategemea kwamba wanaotoka Kilimanjaro, wanaotoka Mwanza watani zetu, wanaotoka Tanga, wanaotoka Arusha, Wanaotoka Mikoa yote, Dodoma wote wanaleta wageni pale Dar es Salaam lakini pia ndege za Mataifa mbalimbali zinatua katika uwanja wa ndege wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja ule una changamoto nyingi ikiwepo ni uchakavu wa majengo. Hali ya majengo yale hayaridhishi, hayaendani na hadhi ya jiji la Dar-es-Salaam. Lakini pia uwanja wa ndege ni kioo na kitivo cha uchumi wa nchi. Mwonekano wa uwanja wetu unatushushia hadhi yetu hata kiuchumi. Hatuwezi kupata uwanja wa haraka kama wa Dubai, India au Taifa lingine lakini angalau Serikali ifanye juhudi za makusudi

kuutengeneza uwanja wa ndege wa Dar es Salaam, uwanja ule pia ni kivutio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona nchi za wenzetu zina maduka mazuri, unapofika *airport* kuna mambo mazuri. Lakini kwetu bado kuna vioski, vile vibanda, ile hali haifai! Dar es Salaam ni Jiji, tunaomba lipewe hadhi ya Jiji ikiwemo na uwanja wa ndege wenye hadhi ya Jiji! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie tena kwenye mwenendo mzima wa treni. Nimeipongeza sana Serikali kwa kuanzisha angalau ile treni ya Ubungo. Idadi ya watu Ubungo ni kubwa sana. Treni ile imesaidia sana kupunguza watu wanaotoka kila siku Ubungo, Kimara, Mbezi, Kibamba kuelekea Mjini *station*. Lakini pia katika juhudi hizo, niiombe Serikali, pamoja na mpango uliokuwepo sasa wa kuibua tena usafiri wa treni kutoka Pugu ambao utasaidia watu wa Chanika, Majohe mpaka Kisarawe nao kuja *station* pia. Mpango huo ni mzuri mimi nasema nawatakia kila la kheri mwendelee nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya hapo, niiombe Serikali sasa ifanye juhudi ya makusudi ya kuweka usafiri wa treni Mbagala. Mbagala wengine kwetu, sasa idadi ya watu Mbagala ni kubwa katika Dar-es-Salaam nzima. Watu kule ni wengi, tena Mbagala inapokea wanachi wengi wanaotoka katika Mikoa ya Kusini, kuna kituo pale. Sasa tukiweka hiyo treni itasaidia kwa wale wakazi wa Temeke, Mbagala, Mbande na wale wanaotokea Mikoa ya Kusini.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya, nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Kayombo, na Mheshimiwa Njwayo ajiandae na msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Kandege.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kutokana na kazi ambazo zimefanywa na Wizara hii Mheshimiwa Mwakyembe na Naibu Waziri wake, pamoja na haya ambayo yameandikwa humu leo, mimi siyo tu kwamba nataka kuunga mkono, isipokuwa nalazimika kuunga mkono hoja hii. Maana mambo yaliyoelezwa humu yanatoa matumaini makubwa na kazi ambayo imekwisha kufanyika inathibitisha kuwa matumaini ambayo yanaonyeshwa hapa yatatekelezeka. Wasiwasi wangu ni mmoja tu, pengine Mheshimiwa Waziri wa fedha, ndugu yetu Mheshimiwa Mgimwa atusaidie kupata fedha za kutosha ili kutekeleza ambayo yameandikwa hapa. Hii ndiyo changamoto ambayo naiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nilibahatika kuwa kwenye Kamati ndogo iliyoundwa na Mheshimiwa Spika ya kuishauri Serikali juu ya kutafuta mapato na taarifa ile ipo Serikalini. Taarifa ile imesheheni mambo mengi sana mazuri. Mimi nataka kuiasa Serikali hapa ikayatafakari yale mambo na kuyatekeleza. Ningependa pia kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi aiangalie ile taarifa. Mambo ya Bandari yamezungumzwa kwa kina pale na mambo ya reli. Bandari ya Dar-es-Salaam sisi wanauchumi tunasema, *transport* ni *key* katika *economics*. Uchumi wowote wa nchi hauwezi kwenda bila uchukuzi na kwa hiyo, uchukuzi wanapaswa wapewe fedha nyingi lakini pia uchukuzi inaweza ikaingiza fedha nyingi Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Dar-es-Salaam wengi tunaamini kwamba ni *gold mine*, ni eneo lingine la machimbo ya dhahabu, isipokuwa limelala, halijatumika kikamilifu. Lakini kwa kazi ambazo zimeonekana kwa siku chache ambazo hawa Waheshimiwa wawili wamekaa pale pamoja na wenzao huko maofisini, nina matumaini kwamba dhahabu imeanza kuchimbwa pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii ya kati tunayoongelea, kwa taarifa zilizopo naambiwa ilijengwa mwaka 1918 sasa ni miaka 95 toka ilivyojengwa; na ukiachilia

reli ya Singida - Itigi ambayo iling'olewa na baadaye ikarudishwa, nchi hii hatujajenga tena reli nyingine ukiacha ile ambayo tulisaidiwa na ndugu zetu wa Kichina reli ya TAZARA. Ukiangalia mtandao wa reli ambao ni muhimu sana katika usafirishaji, kwa sababu ni nafuu lakini pia unasafirisha kwa wingi utakuta iko hapa katikati na kwenda Mwanza. Lakini ukiangalia chakula katika nchi yetu kinatoka Mikoa ile ambayo ina matatizo makubwa ya usafiri, na usafiri mkubwa unaotumika ni malori ambayo yana gharama kubwa mno lakini pia yanaharibu mno barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi ni barabara ya Dar-es-Salaam – Dodoma. Angalia inavyoharibika kwa sababu tu reli ya kati haifanyi kazi vizuri. Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa ni kuomba kwamba Wizara hii iangalie uwezekano wa kuweka reli kutoka pale Makambako kwenda Songea, Mbinga, mpaka Mbambabay. Imeandikwa hapa juu ya reli hii ya Mtwara - Songea – Mbambabay. Ni jambo zuri sana, na likitekelezwa, ndugu yangu Mheshimiwa Mwakyembe tunakutakia baraka nyingi sana za Mwenyezi Mungu ili uweze kufanikiwa zaidi katika maisha yako. Lakini hiyo reli hiyo, mapendekezo yangu, kuna eneo fulani ukitoka Songea pale unafika Kitai na tunayo machimbo ya makaa ya mawe kule Ngaka kijiji cha Tunduwalo Kata ya Ruanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale jamaa wanasafirisha ule mkaa kwa malori pengine 100 kwa siku, yanatimua vumbi, watu wanapata mafua, sasa mkombozi wao ni wewe Mheshimiwa Mwakyembe kwa kuweka reli pale. Reli hii inaweza kwenda mpaka Ndumbi kwa sababu wakati mwingine yale makaa ya mawe yanasafirishwa pale yanakwenda kutokea kwenye Jimbo lako pale Kyela ili yaweze kwenda kukilisha kile kiwanda cha saruji kule Mbeya. Kwa hiyo, yatanufaisha Jimbo lako na Jimbo langu na Jimbo la Mheshimiwa Kapteni Komba, gari kubwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lingine ni kiwanda cha ndege pale Mbinga. Halmashauri inayo sehemu ambayo inaweza ikatoa, tunakosa tu ushauri na uwezeshaji kidogo ili tuweze kuanza. Naomba sana Mheshimiwa Waziri

atufikirie kwa hilo. Mbinga ni wazalishaji wakubwa sana wa kahawa, theluthi moja ya kahawa ya *Arabica* nchi hii inatoka Jimboni kwangu.

MBUNGE FULANI: Eh!

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Wakati wa miaka ya themanini wakati uchumi wetu ulipokuwa hoi, ilibidi Serikali iangalie *stock* za kahawa za Mbinga na za Kilimanjaro na Mbeya ili tuweze kupata mafuta ya kuendesha mitambo na magari katika nchi yetu. Huo ndiyo ulikuwa mchango mkubwa sana wa wana Mbinga katika uchumi wa nchi hii. Lakini wale watu wa Mbinga wameachwa hivi hivi, hata kiwanja cha ndege hakipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna wawekezaji wengi wanatamani kwenda kule lakini wanaulizia namna ya usafiri. Upo uwanja pale wa Songea, lakini pia tunaomba angalau ile *runway* pia iwekwe lami ili iboreshwe iweze kuwa inafanya kazi vizuri zaidi. Hili la ndege pia linahusika na nauli. Sasa hivi kutoka Dar-es-Salaam kwenda Songea ni Sh. 325,000/= *single trip* kwenda tu kwa ndege, watu wachache sana wanaweza wakalipia usafiri huu. Watu wale wa Mbinga ni watu wa Mungu kama walivyo watu wa Dodoma, kama walivyo watu wa Mpanda, kama walivyo watu wa Mbeya, wanahitaji huduma iliyo bora kama wana wa Mungu. Kwa sababu Mheshimiwa Mwakyembe nakujua wewe unampenda sana Mungu, ombi hili nitashangaa kama hutatusaidia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili niungane na Wabunge wenzangu kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza naomba kutangaza maslahi binafsi kwamba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake ni rafiki zangu wa karibu na ninapenda sana uchapakazi wao. Kutokana na hilo, sina sababu ya kutounga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza Mtanzania mwenzetu mwenye Kampuni ya SS Bakharesa, maana Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ukurasa wa 17 ametamka wazi kwamba amechangia dola za Kimarekani 800,000 kwa ajili ya kuhakikisha treni zinakarabatiwa. Mtanzania huyu pamoja na kuwa ana kampuni, ana magari mengi lakini ameonyesha moyo wa kizalendo ambao pengine uzalendo wake ndiyo umemfanya kuchangia. Kwa sababu kuwa na magari wala siyo sababu wapo wengine ambao hawajaonyesha *interest* ya namna hiyo. Mimi naomba Wizara impe cheti cha *appreciation* Mtanzania huyu kwa kutuunga mkono kwenye jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba niishauri Serikali katika maenoyo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nchi yetu ina mpango mkakati unaotufikisha mwaka 2025 wa kuwa na uchumi wa kati; na mpango huu utafanikiwa tu kama tutaamua kuwekeza kwa makusudi kwenye reli, bandari, nishati, utalii na mambo mengine. Lakini kwa sababu leo tuko na Wizara ya Uchukuzi, naomba kuchukua nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Daktari Mwakyembe na Watendaji wake kwamba waamue kabisa kuweka mipango mkakati kwa ajili ya reli na bandari. Haya ndiyo yanayoweza kutuokoa kwa muda mfupi sana kama yatawekezwa sawasawa.

Kwa maana hiyo, naomba sana mtambue mpango ule wa reli ya Mtwara – Songea – Mbambabay, ni miongoni mwa mambo yatakayotusaidia sana kama tukiamua kwenda nayo kasi. Kwa sababu makaa ya mawe, bandari yenyewe iliyoko Mtwara, gesi, Mchuchuma yatatusaidia sana kwenda haraka. Vile vile tuna nchi za jirani kule ambazo zinatamia reli hiyo na bandari ya Mtwara kwa ajili ya kutusaidia sisi kusonga mbele na uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuishauri Serikali kwamba huko nyuma tulikuwa na kitu kinachoitwa *TACOSHIRI*, sitaki kusema *TACOSHIRI* irudi hapa, lakini wakati

wa *TACOSHIRI* tulikuwa na meli ya MS Mtwara, MV. Lindi zilizokuwa zinabeba shehena za mizigo kupeleka Mikoa ya Kusini. Hivi leo kuna mpango wa ujenzi wa barabara unaoendelea kukamilika pale, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi asubuhi hapa ametuahidi kwamba katika muda siyo mrefu sana barabara ile itakuwa imekwisha. Sasa inapokwisha na magari yanayopitisha *tonnage* kubwa ya mizigo inayopita ikiendelea kutumika kule ni kwamba barabara hiyo itaharibika katika muda si mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuamue sasa kuwekeza kwenye bandari, tuwekeze, tununue meli za uhakika mbili tatu ili isaidie kupeleka mizigo kwenye Mikoa ya Mtwara na Lindi jambo ambalo litasaidia sana kuimarisha na kuboresha barabara zetu. Sambamba na hilo, kuna kitu kidogo nataka niseme hapa. Sikuona mpango wowote wa kuiendeleza Bandari ya Lindi. Bandari hii ikiwekwa sawasawa itasaidia sana kuboresha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mtwara kwa sasa unawawekezaji wengi na wakubwa wanaotaka kuwekeza kwenye Mkoa ule. Lakini mambo haya hayaendani na hali ya uwanja wa ndege uliopo Mtwara. Watu wanataka watue usiku kule kukamilisha mambo yao uwanja hauna taa. Mimi naomba Wizara tuuangalie ule uwanja ufanane na hali ya uwekezaji uliopo Mtwara. Ukitaka kutua usiku, unatua; ukitaka kuruka usiku, uruke; siyo mchana tu. Huku kuzubaa kwetu katika mambo haya ndiyo kunakotuzidishia uchumi wetu kubaki ukiwa haundelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kusema kidogo kuhusu *National carrier* yetu *ATCL*. Ziko jitihada nazitambua za kurejesha huduma, lakini ndugu zangu *ATCL* ina madeni mengi kweli! Hasara iliyoko pale ni kubwa! Mizania ya *ATCL* haisafishiki kwa sasa, itatuchukua muda mrefu kuisafisha. Mimi natoa rai, tuachane na hii kitu, tuifute kwanza, halafu tuanze upya. Madeni yale kirahisi rahisi hayatakwisha pale na gharama za kuziendesha hizi ndege ni kubwa mno. Leo tuna ndege moja tu ya uhakika hapa, lakini kwa nini tusiwe na ndege tano tuanze upya tuwe na ndege tano, ndege

zitakazokuwa zinafanya *performance* nzuri, ndege ambazo zitasaidia kuitangaza Tanzania. Maana tukiwa na *National carrier* ya uhakika, Tanzania itatangazika pia, na kwa hiyo, kuongeza uchumi wetu. Mimi ningeshauri tuachane na hii hali iliyoko sasa, tuanze *fresh*. Siyo vibaya na itatusaidia sana kusonga mbele kuliko hali ilivyo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa na hayo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nashukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Josephat Kandege!

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi jioni ya leo niweze kuchangia. Nimepata taarifa nikiwa kwenye Kamati ya Bajeti ni kalazimika kukimbia kuja kwa ajili ya umuhimu wa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, naomba niunge mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Nina kila sababu ya kuunga mkono bajeti hii. Naona fahari sana Wizara hii kupata Mawaziri wachapa kazi, naona fahari kwamba Mawaziri hawa ni hazina kutoka Chama cha Mapinduzi, ndiyo raha ya kuwa ndani ya Chama cha Mapinduzi. Hata hivyo, nafarijika sana kwa nia ya dhati ambayo nimeiona ya Serikali kuhakikisha kwamba reli ya kati inafanya kazi ili ndugu zangu na marafiki zangu wa Kigoma waweze kwenda Dar-es-Salaam, lakini ikiwezekana wafike na Mpanda. Juhudi ambazo zinafanywa na Wizara ni kubwa sana, mtu yeyote mwenye kuona anapaswa kuipongeza Wizara hii kwa dhati kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo mazuri yanayotoka kwenye Wizara hii huishii kuyaona kwenye *Central Line* peke yake; unaona jinsi ambavyo wanahangaika kuhakikisha kwamba msongamano kwenye Jiji la Dar-es-Salaam unapungua. Hawasemi kwa maneno, wanatenda, watu waliopo Dar-es-Salaam ni mashahidi. Mambo kama haya hayakuwahi kutokea, lakini yametokea chini ya Uongozi wa

Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe na ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba. Hongereni sana na nadhani mnapata *support* kubwa sana kutoka kwa Watanzania. Hivyo hamhitaji kusema, acheni wengine tuseme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhati unaiyona jinsi ambavyo nimefarijika sana. Ukisoma kwenye kitabu cha bajeti unaona hawa watu wanavyofikiria na uzalendo wa hali ya juu. Leo hii kwenye kitabu cha bajeti inaonekana kwamba reli ya TAZARA *extension* inaanzia Tunduma kwenda mpaka Bandari ya Kasanga. Wazo jema sana hili. Mnastahili pongezi kwa mtu yeyote anayefahamu *potential* iliyopo kwenda Bandari ya Kasanga. Lakini haikuishia hapo, hata ujenzi wa Bandari ya Kasanga unatajwa na unafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, matumaini ni makubwa sana. Yale maisha bora ambayo tunasema yanawezekana ndani ya Chama cha Mapinduzi yanaonekana kwa vitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najjuliza kwamba, hivi Wizara hii yenye viongozi mahiri wanasemaje kuhusiana na kuwa na Shirika la Ndege la Tanzania ambalo linafanya kazi vizuri? Ukienda kwenye kitabu chao kuna mawazo mazuri kabisa. Naamini ambacho mnapaswa kufanya ni kuhakikisha kama kuna uozo wowote *ATCL* muuondoe. Maana wale ambao hawawezi kuiga utendaji kazi wenu bora msikae nao. Hali kadhalika, ukienda Bandari yetu, watu walikuwa wanalalamika sana, lakini hadi leo malalamiko yamepungua sana. Naomba niendeleo kuwapongeza. (*Makofi*)

Hata hivyo, naamini pongezi hizi kwenu nyie ni chachu ya kwenda kufanya mambo mazuri zaidi. Tunajua mnaweza kufanya mazuri zaidi kuliko haya. Ongezeni kasi na kuhakikisha kwamba uwanja wa ndege wa Sumbawanga ambao mara ya mwisho niliongelea, nafarijika kwamba leo umeweka bajeti, nadhani iko Shilingi bilioni 13 ambazo zinakwenda kufanya kazi. Ie adha ambayo tulikuwa tunakutana nayo, kwamba Uwanja wa Ndege Sumbawanga ni vumbi, haitakuwepo tena, itakuwa historia. Bahati nzuri Naibu Waziri tulifanya naye Mkutano Sumbawanga pale na akawaahidi

kwamba, ili uwanja uweze kujengwa, hebu tupeni muda kidogo. Naamini Kandarasi itachukua muda siyo mrefu.

Ni rai yangu kwenu, itakuwa busara tukatumia Wakandarasi ambao wako *site* maeneo ya kule, maana na jambo hili nalo lisije likachukua muda mrefu. Tumekula vumbi, muda unatoshia, tunataka na sisi ndege iruke kwenye Kiwanja kilichokuwa kizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoongelea reli ya TAZARA kufika Kasanga, maana yake nini? Unategemea makaa ya mawe ambayo yanapatikana kule Nkomoro, yatakwenda kusombwa, makaa ya mawe ya kule Namwele yatakwenda kusombwa. Hali hiyo inaleta mapinduzi katika uchumi wa Tanzania. Ninachoomba, haya mawazo mazuri, nitafarijika sana nikiambiwa baada ya miaka miwili tayari kazi hii itakuwa ilishaanza. Lakini haishii Kasanga, reli hii inakwenda Kilomea 700 mpaka Kigoma, maana yake tutakuwa tumeshaunganisha nchi kwa kila namna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru sana. Msingi ukiwa na mazuri hupaswi kusema sana, maana unaweza ukaharibu. Naomba kwa namna nyingine tena niunge mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo naomba niishie hapo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru. Bado muda tunao, sasa namwiita Mheshimiwa Moza.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii ya Uchukuzi. Nilikuwa nataka nichangie Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Msalato. Kwa kuwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyozungumza kuanzia mwanzo hajataja kabisa eneo hili la Kiwanja cha ndege cha Msalato, nitapenda nijue kwamba, kuanzia mwaka 2011/2012 Serikali ilishaeleza Bunge na Taifa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu kuwa umekamilika toka mwaka 2007/2008, hotuba ya Bajeti ya

mwaka wa fedha unaoishia, kiwanja kitakuwa kimekamilika. Cha ajabu na cha kushangaza hakuna sehemu yoyote ambapo Msalato imetajwa katika orodha ya viwanja vilivyotajwa.

Kuanzia ukurasa wa 59 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, naomba ninikuu: kwenye viwanja alivyovitaja Mheshimiwa Waziri, ametaja kukamilisha Kiwanja cha Songwe Mbeya ambacho kimetengewa Shilingi bilioni 8.5, kuendeleza uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege Mwanza Shilingi bilioni 11.483, kukamilisha ukarabati wa kiwanja cha ndege Bukomba, zimetengwa Shilingi bilioni 11.297, kukamilisha ukurasa wa kiwanja cha ndege Kigoma zimetengwa Shilingi bilioni 31.3, kukamilisha ukarabati wa kiwanja cha ndege Tabora zimetegwa Shilingi bilioni 15.6, kuanzisha ukarabati wa kiwanja cha ndege Shinyanga Shilingi bilioni 17.34, kuanza ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Sumbawanga Shilingi bilioni 13.3 zimetengwa, ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege Mtwara zimetengwa Shilingi milioni 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoweza kunishangaza sana, nafikiri huu mwenendo unaonyesha dhahiri kuunyanyapaa Mkoa wa Dodoma katika masuala mbalimbali ya maendeleo. Hii inaonyesha dhahiri kuwa kumbe hakuna dalili yoyote ya kuifanya Dodoma iwe Makao Makuu ya nchi kama inavyosemekana kwa maneno ya mdomoni. Kwa kweli, ni jambo la kusikitisha sana. Ni kitu gani kinachoifanya Serikali isiweze kujenga eneo hili la kiwanja cha Ndege hapa Dodoma wakati tayari watu mmeshakwishawapora maeneo yao na mmeshawalipa fidia, na kila kitu kimeshakamilika? Sasa naomba kujua uwanja huu utakuwa umekamilika lini au hata kuanza kujengwa tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la Bandari. Pamoja na jitihada kubwa za Waziri za kuubadilisha mfumo, Mheshimiwa Waziri nakupa hongera kwa kazi kubwa ambayo unaifanya, lakini huna wenzako ambao wangeweza kukusaidia na kukuunga mkono ili bandari iweze kuboreka zaidi. Mfumo wa bandari ni muhimu kwa uchumi wa Taifa. Bado hali halisi siyo nzuri katika bandari, kushindwa kubadili

ushindani wa kibiashara ukanda wa Afrika Mashariki. Tanzania iko katika nafasi kubwa na nzuri zaidi. Hivi Mheshimiwa Waziri ni kitu gani ambacho kinaonyesha ubadhirifu kiasi kwamba bandari inakuwa yenye msongamano mkubwa ambao haihitaji kubadilika pamoja na utaratibu wako na mfumo mzima wa kubadili. Tanzania ipo na nafasi kubwa ya kupata faida na bandari hii kuliko bandari nyingine yoyote Afrika, hii ni kutokana na Jografia yake. Hili tatizo limekuwa likurudiwa kila mwaka na kila Mbunge anayekaa anaongelea suala hili.

Mheshimiwa Mwakyembe ni mchapakazi, unajulikana kwa uhakika. Tafadhali tunakuomba, katika adha hii Wabunge wasiendeleo kurudia kila leo jambo hili naomba libadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye usafiri wa Reli. Kitendo cha kufufua usafiri wa reli katika Jiji la Dar-es-Salaam ni ishara tosha ya kutufanya tuamini kuwa kumbe hakuna linaloshindikana endapo tu nia ya dhati ipo. Mheshimiwa Waziri ni mfano mzuri sana. Upo usafiri wa treni ambao umekuwa ukilalamikiwa katika Reli ya Kati. Ni wakati muafaka wa kutumia uzoefu wa Jiji la Dar-es-Salaam katika maeneo mengine. Chonde, chonde, wale wote wanaokwamisha maendeleo haya, wanaokwamisha reli hii, wanaotoa mataruma, Mheshimiwa Waziri nakuomba uzingatie suala hili ili wachukuliwe hatua za sheria haraka sana, kwani imekuwa ni msongamano mkubwa na imekuwa adha kubwa katika chombo hiki. Ili ionekane huruma inatendeka, bila kufanya hivi, kila mwaka Wabunge watakuwa wanaongelea suala la usafiri wa Reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kwamba katika kipindi kilichopita vichwa vya treni vilikwenda kutengenezwa huko nje, sina hakika vilirudi au havijarudi. Sasa Mheshimiwa Waziri tunachotaka ni kwamba badala ya vichwa hivyo vya treni kwenda kutengenezwa nje, na sisi tunataka tupate wataalamu hapa hapa katika nchini yetu vitengenezwe hapa hapa ili tuone ufanisi unavyokwenda na kama kuna makosa yoyote yanayojitokeza na kusababisha ajali kubwa kila mara katika nchi yetu naomba sasa ubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, kwa kweli hoja hii moja kwa moja nasema kwamba sitaiunga mkono Mheshimiwa Mwakyembe na natoa Shilingi yako kwa sababu ya kiwanja cha ndege kilichopo Mkoa wa Dodoma ambapo mnasema ni dhana ya Makao Makuu ya nchi ya Tanzania. Naomba kama ni dhana kweli, basi iwe na mabadiliko ya dhana kweli tuone na wala siyo kejeli za mdomoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Moza. Sasa namwita Mheshimiwa Chilolo mchangiaji wetu wa mwisho.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mheshimiwa Mwakyembe Waziri mwenye dhamana wa Wizara hii nina imani naye sana, hata Naibu wake sina mashaka naye, pia Watendaji vilevile. Hata hivyo, kwa leo napata kigugumizi kutokana na baadhi ya mambo kutokutiliwa maanani katika Mkoa wa Singida. Nimesikiliza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijapata maelezo yanayotosheleza kuhusu treni ya Dodoma kwenda Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika treni za Tanzania hii, hii ndiyo treni pekee iliyojengwa na fedha ya Serikali hii ya Tanzania. Marahemu Baba wa Taifa alifanya kazi kuhusu treni hii, mpaka wananchi wa Singida wanasema kulikoni? Au kwa kuwa mwenye kuianzisha treni hiyo ni Marehemu, basi na barabara ndiyo ife?

Jamani, nawaomba msiwafikishe watu wa Singida huko. Mheshimiwa Mwakyembe tuna imani sana na wewe, nakupenda sana kaka yangu, lakini leo napata kigugumizi kwa sababu wananchi ndio walionipa hizi habari. Wananchi wanasema hebu tuulizie; treni hii, Serikali inataka nini? Tumfufue aliyeianzisha? Hivi kweli inawezekana? Kama binadamu anafufuka, basi tungepata matumaini. Lakini hakuna binadamu anayefufuka akifa. Tunaomba sana Mheshimiwa Mwakyembe uifikirie treni hii ya Singida mpaka Dodoma.

Kumbuka utajiri wa Singida! Tanzania hii kuku tunalishwa kutoka Singida, tunasafirisha kuku na watu humo, uliona wapi? Ng'ombe tunafuga Singida, Mbuzi wengi wanatoka Singida. Katika Mikoa mitano ya Tanzania inayofuga mifugo mingi, Singida ipo. Mifugo hii yote inasafiri kwa barabara, ndiyo maana barabara zinaharibika mapema, kwa sababu tunapitisha mizigo mizito kuliko kawaida. Ninakuomba kwa niaba ya wana-Singida, uifikirie treni ya Dodoma Singida ili tuweze kusafirisha mali nyingi za kutoka Singida.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri Kigoda, amesema sasa kiwanda cha mafuta cha *Mount Meru* kinaongezeka kinakuwa kikubwa zaidi, hivyo mafuta yatazalishwa zaidi. Hebu niambie, mafuta haya yatapita wapi? Tutayasafirisha kwa usafiri upi? Wakati treni haipo na hata maelezo hatujui yanasema nini. (*Makofi*)

Umeeleza treni ya kati tumekusikiliza, ufinyu wa bajeti tunajua, lakini basi tupe hata maelezo ambayo angalau watu wangeweza kupumua. Nakuomba sana Mheshimiwa Mwakyembe kesho utakaposimama, hebu waambie wana-Singida, treni hii ya Dodoma – Manyoni – Singida itafufuliwa lini? Mifugo yetu tusafirishe humo, mafuta ya Alizeti tusafairishe humo, kuku zetu zisafiri humo na mizigo mbalimbali tusafirishe humo ili tuinusuru barabara ya Magufuli. Barabara nzuri zimejengwa na Serikali hii, lakini usishangae hata kesho zikiharibika kwa sababu ya mizigo mizito inayopita kwenye barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwakyembe, naendelea kupata kigugumizi pale nilipoona hata vile vituo vya waangalizi wa treni hii, zile nyumba zimebomolewa. Sasa kama nyumba zimebomolewa, kuna dalili za treni kurudi kweli! Mpaka nyumba za kuangalia treni zimebomolewa Mheshimiwa! Ninakuomba sana kesho utueleze vizuri wana-Singida ili imani ambayo tunayo kwako tuendelee kuwa nayo. Tunaanza kupata mashaka. Wabunge wa Majimbo wanaulizwa kila siku, jamani vipi treni? Mimi mwenyewe swali ni hilo hilo! Tunaomba sana mtuhurumie wana-Singida, na siyo watu

wa Singida tu, hata watu wa Mikoa jirani, zipo Wilaya ambazo zilikuwa zinatamia treni hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu uwanja wa ndege wa Singida. Ama kweli Waswahili wanasema kutangulia siyo kufika. Uwanja wa ndege wa Singida tumeanza kuambiwa upembuzi yakinifu toka enzi ya kaka yetu Mheshimiwa Prof. Mwandosya bado ni Waziri mwenye dhamana wakiwa na Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari, upembuzi yakinifu mpaka leo, mpaka kesho! Hata Mikoa ambayo haikuwa kwenye upembuzi sasa wanajenga viwanja vya ndege. Singida tumeachwa, sijui tumekosa nini maskini yarabi! Ungejua ndiyo Mkoa ulio katikati ya Tanzania, tena ungetoa kipaumbele cha kujenga kiwanja cha ndege. Dodoma wamepata upendeleo tu, siyo katikati ya nchi. Katikati ya nchi ni Singida! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mingi tangu naingia Bungeni hapa tunaalezwa habari ya upembuzi yakinifu mpaka leo! Sasa wameanza kujenga Tabora, Singida tumo tu, tunapigishwa *mark time*, sawa. Mimi sina shida na jirani zangu, maana Sungura ndiyo huyo huyo. Lakini basi yule aliyetangulia kufikiriwa, si anaendelezewa! Lakini ndiyo tumepigishwa *mark times* tunaambiwa sisi ni katika bajeti ya 2014 sijui kumi na ngapi! Niambie wananchi wanakaa wanasema, jamani mmekuwa wapole sana au mmekuwa vip ninyi Wabunge wa Singida? Mnataka tusirudi humu kwa sababu ya uwanja wa ndege tu! Bado tuna nguvu sana jamani! Hakuna Mbunge mzee hata mmoja wa Singida, watu wote bado wananguvu. Yaani *airport* tu ndiyo ituletee matatizo Wabunge wa Singida jamani! (*Kicheko/Makofi*)

Kaka yangu Mheshimiwa Mwakyembe na Naibu Waziri - Mheshimiwa Tizeba, chonde chonde, hapa naongea kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Singida, kwamba tunakupigia magoti baba, tufikirie hiyo *Airport* ya Singida, kwa sababu, toka tumeanza kusema kiwanja hicho kipanuliwe, lakini mpaka leo tunaambia upembuzi, upembuzi! Tena mbaya zaidi kile Kiwanja hata nyumba ya wageni hakina. Jamani hata Mheshimiwa Rais akija Singida, hivi akishuka na

helicopter pale au ndege ndogo mvua inanyesha, inakuwaje? Hata nyumba ya kumpumzikia hakuna! Si muanze kidogo kidogo hata kujenga nyumba ya wageni wakati mnafikiria jambo lingine jamani? Nyumba ya kufikia wasafiri hakuna, Kiwanja cha Ndege ndiyo hicho; haya, huku mnatujengea viwanda vikubwa; hata hao wawekezaji watakujaje? Siku hizi watu wanapenda usafiri wa mkato, wenye kulinda hata na fedha zao. *(Makofi)*

Naomba sana, mambo haya makubwa mawili ndiyo yamenifanya nisimame jioni hii ya leo. Tena watu wamenikazia kweli kweli kwamba Mheshimiwa waeleze kwamba huu ndiyo ujumbe wa watu wa Singida, na wanakuita wewe jembe! Sasa jembe tena jamani, unanza kusahau watu wanaokuthamni kwa kiwango hicho? Jembe! Ndugu yangu unataka watu wa Singida walie au wafanyeje kaka yangu? Wafanye nini? Waseme lugha gani? Wenzetu wameongea lugha gani baba na sisi tutumie hiyo hiyo ili utufikirie. *(Makofi)*

Yaani hatuna ubaya na wewe ati! Yaani ni watu tunakupenda na kukuthamini kweli kweli na tuna imani na wewe. Lakini sasa tunaanza kufikiria, inakuwaje? Tatizo ni wapi? Sisi tumeteleza wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekit, nakushukuru sana, kesho nasubiri majibu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na wachangiaji wetu wote wamekwisha.

Hili tangazo nililisema mapema na sasa nalisema mara ya pili kulingana na umuhimu wake na kwa wale ambao hawajasikia basi waweze kuzingatia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu za matishio ya kiulinzi na usalama yanayoendelea kujitokeza hivi sasa, Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuanzia kesho tarehe 17 mwezi huu mwaka 2013, kutoegesha magari yenu pembezoni mwa uzio wa mzunguko wa Ofisi ya Bunge hapa

16 MEI, 2013

Dodoma. Badala yeke magari hayo yaingizwe na kuegeshwa ndani ya maegesho ya Waheshimiwa Wabunge, ndani ya Viwanja vya Bunge. Ikiwa Mheshimiwa Mbunge atapenda kuegesha gari lake nje ya Ofisi, anaombwa iwe katika eneo la ng'ambo upande wa Kaskazini wa barabara itokayo Dar es Salaam. Tunaomba ushirikiano wenu.

Baada ya maneno hayo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.42 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 17 Mei, 2013 saa Tatu Asubuhi)